Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 13 Julai, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mne Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. TUNDU A. LISSU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 188

### Maendeleo Yatokanayo na Mfuko wa TASAF

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Mfuko wa *TASAF* umesaidia sana maendeleo ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani:

(a) Je, mfuko huo umesaidia miradi mingapi Tanzania Bara na mingapi Tanzania Visiwani?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotolewa kwa miradi ya Tanzania Bara na ni kiasi gani kilitolewa kwa miradi ya Tanzania Visiwani?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Mahusiano na Uratibu) napenda kumjibu Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, Pemba kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia Machi 2012, Mfuko wa *TASAF* Awamu ya Pili, jumla ya miradi 11,333 imepatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya wananchi, ambapo miradi 10,571 iko Tanzania Bara na miradi 762 iko Tanzania Visiwani.

(b) Miradi hiyo ina thamani ya Tshs. 200,358,411,836/= ambapo kiasi cha Tshs. 191,273,453,642.17 ni kwa miradi inayotekelezwa Tanzania Bara na Tshs. 9,084,958,193.83 ni kwa ajili ya miradi ya Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mfuko wa TASAF umekuwa na mafanikio makubwa kwani jamii zimeelewa malengo ya miradi inayochangiwa na *TASAF.*

Hii imewafanya kuwa na moyo na ari ya kuomba miradi ili kutatua kero zao na kupunguza umaskini katika jamii zao. Tafiti zilizofanyika hivi karibuni zimeonyesha kwamba wananchi wanaridhika na fedha zinazotolewa na mfuko huu katika kuboresha hali zao za maisha na kuwapa uwezo wa kusimamia shughuli zao za maendeleo. *(Makofi)*

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *TASAF* umewasaidia Watanzania kwa kiasi kikubwa. Lakini kupitia majibu ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri nilipokuwa nikipitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, niliona kwamba miradi iliyotekelezwa kupitia Halmashauri zote za Tanzania Bara na Visiwani ni miradi 878 kutoka mwaka 2011/2012 hii miradi iliyozidi mpaka ikifika 11,333 imeongezeka kwa kipindi gani?

(b) Kwa kuwa Benki ya Dunia imepitisha kiasi cha bilioni 345.4 kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya tatu ya mpango huu kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na kwa kuwa Benki ya Dunia imepitisha bilioni 18 x 18 na *point* zaidi ya bilioni 18.6 za mwaka 2011. Je, zitakapoingizwa fedha hizi zitatolewa kwa kutumia kigezo kipi baini ya Tanzania Bara na Visiwani?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu maswali yake ya nyongeza Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kombo ana wasiwasi kwamba miradi iliyoonyeshwa kwenye kitabu ni michache kuliko miradi ambayo nimeonyesha katika jibu langu. Miradi ambayo nimezungumzia kwenye Jimbo langu ni miradi kwa ujumla wake kutoka awamu ya kwanza na ya pili.

Swali lake la pili ni kwamba vigezo ambavyo vimekuwa vikitumika siku zote na ambavyo vimeonekana ni vigezo vilivyosaidia sana vitaendelea kutumika. Lakini kwa sasa vigezo vya awamu ya kwanza na ya pili ilikuwa kwanza asilimia 20 ya fedha zote ziligawiwa kwa kila Wilaya. Zilizobakia zikatumia kigezo cha kwanza umaskini wa ile Wilaya, kigezo cha pili ilikuwa ukubwa wa eneo la ile Wilaya na kigezo kingine kilikuwa idadi ya watu wa Wilaya ile.

Kwa hiyo, kila Wilaya ilipata katika lile fungu la kwanza la *percent 20.* Tumeona kwamba vigezo hivyo vimefanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, katika hii awamu ya tatu vigezo hivyo vitatumika na tutaangalia vigezo vingine zaidi hasa kigezo ambacho kilichotumika cha ziada cha kuangalia Wilaya zile ambazo zilipatikana na uhaba wa chakula. *(Makofi)*

Na. 189

**Kutofikiwa kwa Malengo ya Millenia**

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY** aliuliza:-

Kuna kila dalili za kutofikiwa kwa malengo ya Millenia (2015). Je, Serikali inawaeleza nini Watanzania juu ya

kushindwa kwa malengo hayo kama dalili zinavyoonekana?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), napenda kumjibu Mheshimiwa Salumu Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni miongoni mwa mataifa 189 yaliyoridhia malengo ya maendeleo ya *millennia (MDGs – 2015)* Septemba 2000 katika Mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa. Malengo hayo yalijumuishwa katika Mipango ya Maendeleo ya Muda wa Kati kwa kuanzia na mkakati wa awali wa kuondoa umaskini *Poverty Reduction Strategy Paper* wa mwaka 2000/2001 hadi 2003/2004 na hatimaye utekelezaji wake kuendelezwa na mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini – MKUKUTA I (2005/2006 – 2009/2010 na MKUKUTA wa II 2010/2011 – 2014/2015. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar MKUZA I (2007 – 2010) na MKUZA II (2010/2011 – 2014/2015).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inaelekea kufikia malengo ya Millenia yanayohusiana na Elimu ya Msingi *(MDG 2),* usawa na jinsia *(MDG 3),* baadhi ya shabaha za lengo la kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI *(MDG 6)* na baadhi ya viashiria vilivyopo chini ya malengo kuhusu mazingira endelevu *(MDG 7).* Hata hivyo Tanzania ipo nyuma katika baadhi ya viashiria vya malengo ya

millennia hasa kwa shabaha zinazohusu malengo Na. 1, Na. 5 na Na. 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika malengo 8 ya millennia, kila lengo lina shabaha zaidi ya moja na katika lengo moja baadhi ya shabaha zinaweza kufikiwa wakati huo huo shabaha nyingine zisifikiwe kutokana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na ukuaji mdogo wa sekta ya kilimo 4.2% mabadiliko ya tabia nchi, uchache wa watumishi wa sekta za afya na elimu, kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu 2.9% na kupungua kwa misaada kutoka kwa wahisani wa maendeleo ambayo ilikuwa imeahidiwa kwa ajili ya malengo ya millennia pamoja na kuchelewa kutimiza ahadi zao.

Serikali imejipanga kutatua changamoto hizi kupitia kilimo kwanza na mpango wa maendeleo wa miaka mitano (2011/12 – 2015/2016).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo ya Serikali kuwa mafanikio yatakayopatikana katika utekelezaji wa mikakati iliyotajwa katika mipango ya Serikali itachangia kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa malengo ya millennia katika kipindi kilichosalia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Bajeti ambayo tunapitisha hapa kila mwaka katika miradi ya maendeleo ni Bajeti ambayo inategemea zaidi wahisani na bado wahisani

wanaendelea kusuasua katika kuchangia Bajeti yetu kwa asilimia kubwa.

(a) Je, huoni ni dalili ya kushindwa kukamilisha au kufikiwa kwa malengo hayo?

(b) Katika jumla ya malengo ya millennia ni kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano na akina mama wajawazito na idadi kubwa ya hao wanaishi huko vijijini na huduma za afya bado ni duni.

Je, katika jumla ya malengo hayo Serikali inaweza kutuambia sasa, ni kwa kiasi gani imepunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano na pia imepunguza vifo vya akina mama wajawazito? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Salum Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Bajeti yetu bado ni tegemezi lakini kama inavyofahamika kwa sasa hivi kuna mikakati ya zaidi ambayo itakayochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kuwa tunapata fedha za kujitegemea kutokana na mikopo kwa rasilimali tulizonazo ili kuangalia zaidi maeneo ambayo yanahitaji maendeleo kwa mfano masuala ya afya, masuala ya elimu, masuala ya maji, masuala ya miundimbonu. Kwa hiyo, huu ni mkakati mmojawapo ambao Serikali itauchukua ili kupunguza utegemezi ambao unatucheleweshea kufikia malengo ya millennia. *(Makofi)*

Kuhusiana na hatua zinazochukuliwa kupunguza vifo vya watoto wa chini ya miaka mitano pamoja na vifo vya akina mama wanapojifungua, hiyo pia ni katika mikakati tunayozungumzia katika mipango yetu ya miaka 15. Kuna mkakati vile wa kuboresha huduma hizi za kiafya na za maji na sekta zingine za kijamii kufuatia taratibu ambazo nimeziainisha.

Kwa hiyo, tunategemea kuwa kwa kipindi ambacho kimesalia Serikali itajipanga vizuri kutafuta vyanzo vyake yenyewe kwa ajili ya kukamilisha haya malengo ya millennia kama ambavyo inategemewa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Jana Wizara ya Fedha walijibu maswali mengi sana. Tuendelee na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Na. 190

**Ubadhirifu na Wizi wa Fedha za Umma**

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. MARY PIUS CHATANDA)** aliuliza:-

Wabunge wengi wamekuwa wakilalamikia sana ubadhirifu na wizi wa fedha na matumizi mabaya ya kodi za wananchi:-

(a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watendaji wa Serikali ambao wamehusika na wizi/ubadhirifu huo katika maeneo mbalimbali?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kubadili baadhi ya sheria zinazowapa na kuweka nidhamu badala ya kuhamishiwa vituo vingine vya kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** ajilibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa ufafanuzi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hutekeleza kazi na majukuu yake kwa kuzingatia Katiba, Sheria na Kanuni mbalimbali. Katika masuala ya fedha zipo Sheria mbalimbali kama vile Sheria ya Fedha za Umma Namba 6 ya mwaka 2001, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 na Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004.

Sheria hizi zimeweka utaratibu wa matumizi ya fedha. Hivyo vitendo vya ubadhirifu na wizi ni ukiukwaji wa sheria hizi. Watendaji wanaothibitika kuhusiana na ubadhirifu na wizi wanapaswa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria tajwa hapo juu pamoja na Sheria na Kanuni za Adhabu, Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi Na. 13 ya mwaka 1984, Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 pamoja na sheria nyingine za Utumishi wa makundi mbalimbali ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali dhidi ya watendaji wake ambao wamethibitika kuhusika na wizi/ubadhirifu wa fedha za Umma katika maeneo mbalimbali.

Hatua hizo ni pamoja kuwasimamisha kazi watumishi ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za nidhamu au jinai dhidi yao, kuwafungulia mashtaka ya jinai Mahakamani watumishi ambao hutuhumiwa kwa makosa ya jinai na pia kuwafungulia mashtaka ya nidhamu watumishi wenye tuhuma za ubadhirifu na wizi wa fedha za Umma.

Kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kuwa kati ya mwezi Desemba, 2008 hadi mwezi Machi, 2012 jumla ya watumishi wa Umma 231 walikuwa wamefikishwa Mahakamani kwa makosa yanayohusiana na ubadhirifu na wizi wa fedha za Umma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikirekebisha sheria zake mbalimbali ikiwemo kuzibadili sheria hizo pale inapoonekana inafaa ili kukidhi malengo yaliyokusudiwa kwa manufaa ya Umma.

Kwa mantiki hiyo ni dhahiri kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kubadili sheria zitakazoonekana kuwapa kinga isiyostahili watumishi kuchukuliwa hatua haraka ili waweze kuwajibishwa na kuweka nidhamu.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini malalamiko mengi sana ya Wabunge humu ndani yanatokana na Serikali kushindwa kuchukua hatua mathubuti kwa baadhi ya watendaji wanaoharibu kutoka kituo kingine na matokeo yake wamekuwa wakiwahamishia katika maeneo mengine.

(a) Sasa je, mtindo huu, Serikali haioni kwamba inaendelea kuwapa kichwa watu ambao wanaharibu kwa ajili ya kwenda kuharibu kwenye maeneo mengine?

(b) Lakini swali swali langu la pili, nashukuru kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kusema kuna baadhi ya watendaji wamechukuliwa hatua, lakini malalamko mengi ni kwamba wanaochukuliwa hatua ni wale dagaa na sio mapapa. Sasa je, Serikali mmejipanga vipi kuhakikisha wote wanaofanya ubadhilifu wa fedha za Umma bila kujali vyeo vyao wanafikishwa Mahakamani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani wiki iliyopita wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu analeta Bajeti yake hapa na wakati alipokuwa anajumuisha, tulizungumza hapa, tukakubaliana, tukasema mtumishi yeyote, mahali popote

akifanya mambo ya ajabu ajabu haya anayosema Mheshimiwa Bulaya na ambayo ameuliza Mheshimwa Chatanda hapa, anabaki pale pale hatoki. Tulitoa mfano hapa, tulimpeleka mtu hapa akaenda Tanga, tukamwambia rudi Songea nenda kajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulimpeleka mtu Babati pale alikuwa Mkurugenzi Mtendaji tukamwambia utarudi mpaka Kichapu uende ukajibu maswali na kama mnafahamu mtu yeyote ambaye amepelekwa mahali, tuambieni tutamrudisha pale pale aende akajibu maswali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nataka niwaambie wala hatutanii, hata hapa kama unaye mtu wewe unamjua huyu ametuhumiwa ni mwizi, mwizi mahali pake Polisi unampeleka pale unamaliza, unampeleka Mahakamani basi hakuna haja yaku-*debate* hapa. Leo unakaa hapa unabishana na Mbunge unamwambia unajua mwanawaye tumwache kidogo pale akae kidogo nanii. Huyu amefanya hujuma kama amefanya wizi peleka Mahakamani. Itia Polisi sukuama, halafu watu wengine watajifunzia hapo, watajua kwamba kuna matatizo hapo.

Hili la pili hili, analozungumza la dagaa kama nimemwelewa vizuri, *concept* ya dagaa naona kama kidogo kwa maana yake dagaa ni wadogo. Sasa maana yake labda ni wale wadogowadogo ndiyo wanashughulikiwa, wale wakubwa wanaachwa.

Mimi nataka niseme kama ifuatavyo. *This is abit hypothetical*, yeye kama ana mahali popote anapojua, juzi tumekaa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tumewasimamisha hapa Wakurugenzi Watendaji, ni dagaa hao? Hao ni dagaa? Wakurugenzi Watendaji tumewasimamisha kazi na wengine tumewafukuza kazi. Ni dagaa hao? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mkuchika alipokuja hapa, alitaja majina 33, yale majina 33 walikuwa watu wakubwa katika Halmashauri, wale ni dagaa wale? (*Kicheko*)

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie tu Mheshimiwa Bulaya, wewe kama unafahamu watu wakubwa wameachwa kwenye *system* hii, tutashuka nao, tuletee hayo majina sisi tushughulike nao. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, ni dagaa hao? Mheshimiwa Moses Machali, swali fupi sana la nyongeza.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu wapo baadhi ya watumishi ambao wamethibitika kwa matumizi mabaya ya fedha hasa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya na nimeiandikia Serikali. Lakini bado sijaweza kuona majibu yake kwa muda mrefu na kwa kuwa ninao ushahidi wa barua kwamba pesa za *basket fund* ambazo ni fedha za Umma hazijapelekwa katika hospitali kama za *Diocese of Force in Tanganyika* ndani ya Wilaya ya Kasulu na fedha hizi ni nyingi sana pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Kabanga takribani shilingi milioni kama 70 kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Serikali inachukua hatua gani dhidi ya Mganga Mkuu na wengine wote ambao wanahusika kwa matumizi hayo ya fedha ambayo ni mabaya ya toka mwaka 2010/2011? Kwa kuwa jambo hili sio jambo la kawaida, wananchi wamekosa huduma na mwaka jana hospitali Fulani zilifunga kutoa huduma kwa wananchi wa Jimbo la Kasulu Mjini na matokeo yake wakapata shida. Naomba majibu na kauli ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu swali ya nyongeza la Mheshimiwa la Mheshimiwa Moses Machali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikiri mbele yako kwamba Mheshimiwa Moses Machali amekuwa karibu sana na ofisi yetu, yako mambo mengi ambayo ametuletea pale ofisini. Hili la Daktari analozungumza nakiri kwamba limeletwa na haya mengine ambayo ameyasema hapa, nakiri kwamba yameletwa.

Nimezungumza na Mheshimiwa Dan Makanga alikuwa *DC* wetu kule Kibondo sasa hivi tumemhamishia pale Kasulu, Mheshimiwa Rais amemhamishia pale. Nimetaka waniletee taarifa ya kina juu ya mambo yote ambayo tumezungumza ikiwepo hili la Daktari ambaye anazungumzwa hapa. Sasa kama nilivyoeleza hapa ziko taratibu kwa maana yake hii nchi inaendeshwa kwa

Taratibu, Katiba na Sheria pamoja na kusema sukuma lakini lazima ufuate Sheria za nchi zinavyosema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa niendelee kukukaribisha ofisini, tuzungumze vizuri zaidi, tufuatilie kwa karibu jambo hili, nakiri kwamba tumelipokea na tutampatia majibu. *(Makofi)*

Na. 191

**Matatizo ya Maji Kata ya Mikocheni Eneo la TPDC**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. RITA L. MLAKI)** aliuliza:-

Mradi wa miundombinu ya maji uliofanywa na Wachina katika maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam hususan Wilaya ya Knondoni:-

Je, Serikali inaweza kueleza ni kwa nini Kata ya Mikocheni eneo la TPDC karibu na viwanja vya mitambo ya *TTCL* halipati maji mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mikocheni iko katika eneo linalopata maji kutoka mtambo wa Ruvu Chini. Kutokana na mahitaji ya maji kuwa makubwa ukilinganisha na uwezoo wa uzalishaji wa mtambo, huduma ya maji katika maeneo mengi Jijini hutolewa kwa mgao, hii ni pamoja na eneo karibu na viwanja vyenye mitambo ya *TTCL* Kata ya Mikocheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji katika Kata ya Mikocheni na maeneo yote yanayopata maji kutoka mtambo wa Ruvu Chini itakuwa ya uhakika zaidi baada ya kukamilika kwa mradi unaoendelea hivi sasa wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini. Mkandarasi anaendelea na upanuzi wa kuongeza uzalishaji kwa asilimia 50, kutoka lita milioni 180 kwa siku za sasa hadi kufikia lita milioni 270 kwa siku. Kazi hiyo itakamilika mwezi Machi 2013.

Sambamba na upanuzi huo, bomba kubwa litajengwa kuyatoa maji hayo kutoka eneo la mtambo kuyaleta Jijini. Serikali imetenga shilingi bilioni 116.4 katika mwaka wa fedha 2012/2013 kwa ajili ya kazi hiyo. Mhandisi Mshauri wa kusimamia kazi ameteuliwa na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi ziko katika hatua za mwisho na anatajiriwa mwezi huu wa Julai, 2012. Ujenzi utafanyika kwa miezi kumi na tano (15).

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa niaba ya Mheshimiwa Rita Louis Mlaki ni kweli kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri anatuonyesha hapa kwamba mipango hiyo ya kuweza kutatua tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam iko na inafanyiwa kazi. Lakini ningependa kufahamu, hivi Mheshimiwa Naibu Waziri yukotayari kutuambia hivi ni kwa

nini mabomba haya yaliyowekwa katika Jiji la Dar es Salaam maarufu kama Mabomba ya Mradi wa Maji ya Wachina yamechukua muda mrefu, maji hayo hayatoki na wakazi wa Jiji wengi wanapata shida kila siku.

(a) Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kutuambia sababu kubwa ya kimsingi ya mabomba hayo ya mradi wa Wachina kutokufanya kazi ni nini? (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba tatizo la maji katika nchi yetu ni tatizo kubwa sana ikiwemo hata kule katika Jimbo langu la Peramiho shida ya maji ni kubwa sana. Uko mradi wa maji ambao ulikuwa umefanyiwa tathmini chini ya mpango wa Benki ya Dunia katika Kijiji cha Mgongotema ambao una thamani ya shilingi milioni 600, lakini wataalamu wamefanya mradi tena kwa mara ya pili tathmini ya mradi ule kwa mara ya pili, mradi ule una thamani ya shilingi milioni 350 tu.

Sasa baada ya kuona tofauti hiyo kubwa. Je, Serikali haiku tayari sasa kutoa hiyo fedha milioni 350 kufanya mradi huo na kuachana na hiyo milioni 600 ambayo ilifanyiwa utafiti wa awali na mradi haujafanyika mpaka sasa kule Peramiho Mkongotema?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

(a) Swali la kwanza kuhusu ya mabomba ya Mchina kama vile Dar es Salaam. Kwanza yanaitwa ni ya Mchina kwa sababu Wakandarasi wengi waliokuwa wamefanya ile

kazi walikuwa wametoka kwenye kampuni za Kichina. Lakini lengo la ule mradi ilikuwa ni kuongeza mtandao wa mabomba pale Dar es Salaam na ilikadiriwa kuongeza mtandao wa kilomita 970. Lakini vile vile ilikuwa ni kuongeza vioski vya maji ilikadiriwa kufika 250 na vile vile ilikadiriwa kuongeza idadi ya watumiaji maji kwa maana watu mpaka 8000. hiyo ndiyo ilikuwa ni kazi kubwa. Lakini kazi ya tatu, ilikuwa ni kukarabati vyanzo vya maji vya Ruvu Chini ili viweze kuzalisha maji kulingana na uwezo wake. Sasa kilichojitokeza sasa hivi ni kwamba kama tunavyojua idadi ya watu imeongezeka na uzalishaji haujaongezeka. Kwa hiyo ni wazi kwamba mabomba yale yapo, lakini maji ya kwenda kusambazwa kwenye hayo mabomba hayatoshi.

Ndiyo maana kwenye vitu vya msingi tumesema kwamba huu mradi wa Ruvu Chini ambao unaongeza maji kutoka milioni 180 lita kwenda 270 ukikamilika yale mabomba sasa yataanza kutumika ukichukua na ule mradi wa Ruvu Juu yataanza kutumika na kusambaza maji katika sehemu zote ambazo zitakuwa sasa hivi hazipati maji kwa sababu ule mtandao tayari upo.

(b) Kuhusu swali la pili, kuhusu Peramiho, kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa namna kipekee anavyofuatilia mendeleo ya Jimbo lake la Peramiho kwa sababu swali alilouliza tayari ameshatukabidhi barua inayoelezea huo mradi kwamba ulipangiwa milioni 900 lakini wataalamu baadae wakausanifu wakagundua kwamba gharama zinaweza zikapungua hadi 350 milioni. Tumeshalipokea na nimeanza kulifanyia kazi na tutampa taarifa kulingana na fedha zitakazopatikana na namna gani utaweza kulitekeleza. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, kwa mujibu wa hotuba ya Wizara ya Maji hapa Bungeni. Mipango hiyo ya kuongeza uzalishaji utakamilika mwaka 2014 mwezi Disemba. Sasa kwa kuwa mabomba ya Wachina yanazidi kuharibika hivi sasa kutokana na kuwa hakuna maji na mabomba yapo. Ni hatua zipi za dharura ambazo Serikali inachukua kurekebisha hali hii ikiwemo kuwachukulia hatua waliohusika na kusababisha uzembe huu wa kuwekeza mradi mkubwa bila maji na miundombinu kuharibika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli haya mabomba sehemu ambazo hazipati maji maana yake inawezekana kukawa na uharibifu na kuzeeka kwa yale mabomba.

Lakini kwanza tuna mkakati, ule mradi wa Wachina, ulifanyikakwa awamu tatu. Kulikuwa na awamu ya kwanza, ya pili na tatu. Awamu ya nne itahusisha sasa mpango wa kuboresha usambazaji maji Dar es Salaam baada ya mpango huu wa kutoa maji Ruvu Chini kupeleka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tutakapokuwa na uhakika wa maji ndipo tunapoweza tukajua kwamba yale mabomba au ule mtandao uliokuwa umelazwa una mapungufu kiasi gani na tutatumia uzoefu ambao tumeupata sasa kutokana na lile zoezi zima ambalo lilileta matatizo ni namna gani tuboreshe usambazaji wa maji pale Dar es Salaam.

Kwa hiyo, la msingi ni kwamba tunao mkakati tayari ambao sasa utakuwa ni wa vitendo zaidi kwa sababu maji yatakuwa yanazalishwa kutoka Ruvu Chini na Ruvu Juu na vile vyanzo vya Mpira na Kimbira kwamba maji yatakuwa ni mengi kufikia lita milioni 710. Kwa hiyo, *definetly* tutaweza kujua sasa uwezo wa ule mtandao uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu sana saa hizi kusema kwamba ule mtandao umeharibika au hautafanya kazi bila kuruhusu maji yaweze kupita.

Kuhusu kwamba kuna ubadhirifu ulifanyika, mimi sina taarifa hizo za uhakika lakini tunalichukua kama changamoto ili tuweze kujifunza kama ni kweli na kama itajulikana hivyo, basi hatua za msingi za Kisheria zitachukuliwa. (*Makofi*)

Na. 192

## Ajira kwa Watoto

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za dhati katika kupunguza au kukomesha kabisa tatizo la ajira kwa watoto linaloongezeka kwa kasi nchini, licha ya athari zake?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Bunge lako Tukufu imetunga Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ambazo zinazuia utumikishwaji wa watoto katika kazi hatarishi kama vile kazi za migodini, viwandani, ukahaba, uvuvi na mashambani, hasa mashamba makubwa ya chai, tumbaku, katani, maua na kadhalika.

Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Ajira kinakataza kabisa ajira ya watoto walio chini ya miaka 14. Kifungu 5(2) kinatoa mazingira ya mtoto wa umri wa kati ya miaka 14 na 17 kuajiriwa katika kazi nyepesi na ambazo hazina madhara kwa afya na maendeleo ya mtoto na kwamba kazi hiyo haitaathiri mahudhurio ya mtoto shuleni, au ushiriki wake katika mafunzo ya ufundi au programu nyingine za kielimu.

Vile vile Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 inakataza ajira mbaya ambazo ni za kinyonyaji kwa mtoto. Sheria zote mbili hizi zimetoa adhabu kwa mtu yeyote atakayepatikana na hatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu juhudi mbalimbali za kukomesha utumikishwaji wa watoto katika ajira hatarishi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Kwa kipindi cha kuanzia Juni, 2011 hadi Juni 2012 jumla ya watoto 22, 2243 wametolewa katika utumikishwaji na kupatiwa mafunzo mbalimbali ikiwemo elimu ya msingi 8,402, elimu ya msingi kwa walioikosa (MEMKWA) 1,428 na elimu ya ufundi na kilimo 12,413.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa kukomesha utumikishwaji wa watoto ambao umebainisha majukumu ya wadau mbalimbali.

Katika utekelezaji wa mpango huo Wizara imepanga kutembelea Wilaya 128 kwa lengo la kuhamasisha watendaji wa Wilaya juu ya masuala ya kukomesha utumikishwaji wa watoto na kuunda Kamati za Wilaya za kuratibu masuala ya kutokomeza utumikishwaji wa watoto na pia kuhuisha masuala ya kutokomeza utumikishwaji wa watoto katika mipango na Bajeti za Wilaya zao. Mpaka sasa Wizara imeshatembelea Wilaya 7 za Lindi Mjini, Lindi Vijijini, Liwale, Ruangwa, Masasi, Mtwara Mjini na Mtwara Vijijini.

Aidha, tumeandaa orodha ya kazi hatarishi (*List of Hazardous Work*) ambazo hazistahili kufanywa na watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na nane. *(Makofi)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa hali duni ya maisha na umasikini uliotawala katika nchi yetu ni chimbuko linalosababisha watoto wengi kukosa matunzo ya familia na kujikuta wakihangaika hususani Mijini. Wakati zamani dunia ambapo ilikuwa bado ni tunu, jukumu la kulea familia hizi lilibaki kwa wanafamilia.

Lakini sasa, hata baadhi ya watu walio hai wanashindwa kuwamudu watoto wao. Hii inasababisha washindwe kuwachukua watoto wanaoachwa na ndugu zao, pindi inapotokea bahati mbaya kati yao amefariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kama jamii imeshindwa, yaani ndugu wameshindwa kuwatunza watoto hao na Serikali, nayo imeshindwa kuwatunza watoto hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, imeelezwa hapa Serikali, imeweka Sheria ya kuwachukulia hatua wale wote wanaowatumikisha watoto katika kazi ngumu, kama ukahaba na mambo mengine kwenye migodi na kadhalika.

Je, ni kesi ngapi ambazo ziko Mahakamani, ambazo wameshitakiwa watu hawa wanaoajiri watoto katika kazi hizo ngumu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema ni kwamba, sababu ambazo zinasababisha watoto kuajiriwa wakiwa bado wako chini ya umri ambao unahitajika waajiriwe, ni umasikini, ni uyatima, ndoa kuvunjika, malezi mabaya ambayo yanafanya watoto wanakuwa na tabia ya kutoka na kufanya kazi hizi. Kwa hiyo, nakubaliana na yeye kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni lazima tukubaliane kwamba, mambo yote haya ni mambo ambayo hatuwezi kuachia jamii kama jamii au familia kama familia. Ndio maana yeye mwenyewe anafahamu hapa Bungeni, tumekuwa tukizungumza mipango mbalimbali ya kuondoa umasikini wa watu wetu.

Sasa tukifanya mipango hii ambayo imekuwepo ya kuongeza uzalishaji, kuwepo na mipango kama ya ujasiriamali, watu kujiajiri, umasikini ukipungua basi, tatizo hilo na lenyewe litakuwa linapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishirikiana kutunza yatima na Serikali ina mipango mbalimbali ya kuhakikisha kwamba, yatima hawaachwi peke yao Serikali na jamii inajihusisha katika kuwatunza, basi na suala hili litakuwa limepungua. Ndoa kuvunjika, tumekuwa tukizungumza hapa, malezi bora na ni kwa nini ndoa zisivunjike na wanafamilia wajiweke katika ndoa zinazoaminika kwa namna nyingi na ndio maana kuna Wizara kabisa ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote haya yanafanywa na Serikali, lakini jamii vilevile inatakiwa ifanye. Kwa hiyo, mimi nakubaliana na wewe kwamba, ni lazima kama jamii kama Serikali, wote tushirikiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili kwamba, ni kesi ngapi? Kama nilivyosema, Sheria hizi mbili zote zinatoa adhabu. Kwa sasa sina takwimu hizo hapa. Lakini nataka nimhakikishie kwamba, watu ambao wanapatikana na kosa hili, sio tu kwamba, wale watoto wanaondolewa kama ambavyo nimeeleza, lakini vilevile hatua zinachukuliwa. Kesi ngapi ziko Mahakamani, naweza nikamtafutia takwimu baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, swali hili linahusu masuala ya ajira, na mimi niwape uzoefu mdogodogo. Kama mnavyofahamu Sheria, Katiba, Taratibu zinakataza ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa jinsia, kumbagua mtu

kutegemeana na dini yake, kumbagua mtu kutegemeana na kabila lake au rangi yake ya ngozi.

Sasa katika mambo haya ya ajira, tumejifunza hivi karibuni kwamba, katika baadhi ya nchi za Ulaya na hususan Uingereza, sasa hivi imepigwa marufuku kumbagua mtu kwa sababu, ya umri wake, huo nao ni ubaguzi.

Kwa hiyo, mtu akifikia kama Sheria za Nchi yetu, miaka 60 kwa hiyo, anaandikiwa barua ya kustaafishwa au kustaafu, kule sasa ni marufuku kwa sababu, kumwandikia barua ya namna hiyo ni kumbagua kwa umri wake. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay.

Na. 193

**Ukosefu wa Nyumba za Watumishi wa Serikali**

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY** aliuliza:-

Mwaka 2002- 2005 Serikali iliuza nyumba zake kwa watumishi waliokuwa wakiishi kwenye nyumba hizo, kutokana na zoezi hilo watumishi wa Serikali wanaohamishwa katika vituo mbalimbali nchini wanakosa nyumba za kuishi;-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupitia upya uamuzi huo *review* na kurejesha nyumba zilizokuwa za Serikali, Serikalini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliuza baadhi ya nyumba zake kwa watumishi wa Umma kwa lengo la kupunguza gharama za kuhudumia nyumba zilizokuwa za siku nyingi, kuwawezesha watumishi waliotumikia Serikali, kuishi katika nyumba hizo zilizo bora wakati wa utumishi na baada ya utumishi wao Serikalini. Na kuijengea *TBA* uwezo wa kujenga nyumba zaidi kwa ajili ya kuishi na kuwauzia watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuuza nyumba hizo lilifanyika baada ya uchambuzi wa kina uliojumuisha kuangalia uzoefu wa nchi nyingine. Katika kufanya uchambuzi huo, Serikali iliunda Tume ambazo zilitoa ushauri wa kitaalamu, kuhusu namna bora ya kupunguza tatizo la nyumba za Serikali. Tume hizo ni pamoja na:-

- Tume ya *ADU* ya mwaka 1963.
- Tume ya Nsekela ya mwaka 1975.
- Tume ya Mramba ya mwaka 1984.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kuuza nyumba *(TBA)*, ulifikiwa kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume nilizozitaja na hivyo Serikali, haina mpango wa kupitia upya uamuzi wake ili kurejesha nyumba zilizouzwa kwa watumishi wake.

Aidha, Serikali, kwa kupitia Wakala wa Majengo, ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Namba 30, mwaka 1997, itaendelea kujenga nyumba nyingine katika Mikoa yote na Wilaya zake, kwa kutumia fedha iliyopatikana kutokana na mauzo ya nyumba na mikopo nafuu kutoka kwenye mabenki mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, majengo yaliyo chini ya *TBA,* hadi sasa ni 2,713. Kati ya nyumba hizo 1,353 zimepangishwa kibiashara, nyumba 748 zinapangishwa watumishi wa umma, nyumba 416 wanakaa Viongozi, nyumba 103 ni nyumba za wageni *(Rest Houses),* 37 ni nyumba za Ikulu Ndogo *(State Lodges)* na nyumba 56 ni Majengo ya Ofisi.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwa kuwa, nyumba zilizouzwa zilikuwa katika maeneo ya *low density,* maeneo yaliyokuwa yanajulikana kwa majina rahisi “Maeneo ya Uzunguni”, ambayo yalikuwa yana ukubwa wa eka 1 mpaka eka 6 na yalipandwa miti. Na kwa kuwa, walionunua sasa wanakata miti mjini. Na kwa kuwa, wanamiliki ardhi yenye eka hadi 6 Mjini. Je, Serikali haioni kwamba, ni jambo la busara, kuja kutambua upya kwamba, iliuzwa nyumba au pamoja na ardhi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, katika Mji Mdogo wa Mbulu, ziliuzwa nyumba 6 zenye eka 60. Na kwa kuwa, walionunua sasa wanakata miti na wamezuwia ujenzi wa Hospitali na *MCH.* Je, Serikali, iko tayari sasa kufuta umiliki wa ardhi hiyo, ili wafidiwe watu hao, tuweze kujenga Hospitali na *MCH?*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Akunaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, nyumba iliuzwa pamoja na kiwanja kwa hiyo, hatuwezi kutenganisha. Kwa hiyo, unapewa nyumba pamoja na kiwanja chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika la pili kwamba, anashauri nyumba zilizouzwa katika Mji wa Mbulu zifutwe. Kama nilivyosema kwamba, nyumba hizo haziwezi kufutwa kwa sababu, walipewa vibali vya kuzinunua zile nyumba, sasa haiwezekani kuzifuta. Waheshimiwa Wabunge, labda niwarejeshe kwamba, suala la kurudisha nyumba za Serikali, lilishawahi kujadiliwa ndani ya Bunge hili, kulikuwa na hoja binafsi ya Mheshimiwa Aloyce Kimaro, likajadiliwa na Bunge liliridhia kwa hiyo, hatuwezi kurudi nyuma. Kwa sasa hivi tuiachie *TBA,* iendelee na utaratibu wa kujenga nyumba za Serikali. Watumishi wanaweza kupata nyumba kwa utaratibu huu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa, nyumba hizi za Serikali, ziliuzwa bei ya kutupa. Na Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema kwamba, uchambuzi yakinifu ulifanyika. Siyo kweli uchambuzi yakinifu ulifanyika kwa sababu, nyumba ziliuzwa kwenye maeneo ambayo ni *strategic areas.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, kupanga ni kuchagua. Bado Watanzania tunaona kuna umuhimu mkubwa wa nyumba hizi za Serikali, kurudi kwenye mikono ya Serikali. Je, Serikali, sasa iko tayari ku-*review* kama Swali la Msingi linavyouliza, ili Watanzania na wafanyakazi wa Serikali, wanufaike na nyumba hizi na sio kuwanufaisha watu binafsi na watu wachache? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kwamba, nyumba ziliuzwa kwa bei ya kutupwa, sidhani kama ndio hoja ambayo tunaizungumza hapa. Hoja ya msingi ni kwamba, kama alivyouliza ni kwamba, nyumba zirudishwe au zisirudishwe.

Lakini nimesema kwamba, Bunge hili, lilijadili suala hili kwa kina kwa kuweka Tume. Na ninayo *Hansard* hapa ya tarehe 29/08/2008 ambayo inaonesha ni nini Serikali, ilitakiwa ifanye. Ninayo Taarifa ambayo ilitolewa na Kamati, Maazimio ya Wizara ya Ujenzi, kupitia Kamati ya Miundombinu, iliyotolewa tarehe 1 Julai, 2009, kuhusu suala hili la nyumba za serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la kuhoji kama zilikuwa zimeuzwa kwa bei hii, halipo tena kwa sababu, lilishajadiliwa na Bunge, na tukafikia muafaka. Sasa kama kuna hoja nyingine mpya, basi liletwe tuweze kuijadili. *(Makofi)*

Na. 194

**Barabara ya Kilolo – Iringa**

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA** aliuliza:-

Ni azma ya Serikali, kujenga barabara kwa kiwango cha lami kufikia Makao Makuu ya kila Wilaya:-

Je, ni lini Serikali, itajenga barabara za Iringa – Kilolo na Ilula – Mlafu – Isagwa – Kising'a – Lulanzi – Kilolo, kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudi Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Iringa – Kilolo na Ilula – Mlafu – Isagwa – Kising'a – Lulanzi – Kilolo, ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara yangu, kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inatambua umuhimu wa barabara hizi za Iringa – Kilolo (Km 33) na Ilula – Mlafu – Isagwa – Kising'a – Lulanzi hadi Kilolo (Km 89) kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali, imeanza kuijenga barabara ya Iringa – Kilolo, kwa kiwango cha lami kwa awamu. Hadi sasa jumla ya Kilometa 5.8 zimekamilika.

Aidha, barabara ya Ilula – Mlafu – Isagwa – Kising'a – Lulanzi hadi Kilolo, itaendelea kuimarishwa kwa kiwango cha changarawe, ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza; ni kweli kwamba, kilometa 5.8 zimejengwa kutoka Iringa kwenda Kilolo, katika kipindi cha miaka 3. Kwa maana hiyo, ni wastani wa kilometa 1.9 kwa mwaka. Kwa hiyo, kwa sehemu iliyobakia, itachukua miaka 14, 15, kabla ya kukamilisha barabara hii.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, je, huu ndio utekelezaji wa falsafa ya Ari Zaidi, Nguvu Zaidi na Kasi Zaidi ya kujenga kilometa 1.9 kwa mwaka? Kwa barabara ya lami?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Ilula kupitia Mlafu – Isagwa – Makungu – Kising'a – Isele – Lulanzi mpaka Kilolo, ndio barabara pekee ambayo inaingia katika Wilaya ya Kilolo moja kwa moja, kuliko hii nyingine ambayo inajengwa, ambayo inapitia Iringa Manispaa, inapita katika Jimbo la Kalenga na hatimaye kupita Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali, itaanza ujenzi wa barabara hii ya kuanzia Ilula mpaka Kilolo, kwanza kwa kuanzia kwa changarawe na hatimaye kujenga kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Msola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Profesa, kwa namna anavyofuatilia Kilolo, iweze kupata barabara za lami. Lakini, niseme tu kwamba, ndio tumejenga katika muda huo, lakini kila kitu tunapanga.

Tumesema kwamba, tuanze kwanza na barabara zinazounganisha Mikoa na Mikoa na ndio tunayoendanayo sasa hivi. Baada ya pale, tutaingia kuja kujenga barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa, kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Profesa, atukubalie tu kwamba, kwa sasa, tutakwenda kwa hatua hiyo, lakini tunaangalia uwezo jinsi tunavyojenga. Hatutatumia miaka 15 kufika Kilolo, kwa kiwango cha lami, tutaiharakisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hiyo barabara ya pili ni kwamba, tunafanya vipaumbele, tuanze na hii moja inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya na baadaye tukijenga uwezo, tutaenda na hiyo nyingine ambayo Mheshimiwa Profesa Msolla, anashauri. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa, ukosefu wa barabara ya lami ya kuunganisha Makao Mkuu ya Wilaya ya Kilolo na Ilula na Vijiji alivyovitaja ni sawa na matatizo yaliyoko katika Wilaya ya Kasulu, Kibondo, Kakonko, ambapo Wilaya hizo ni

Makao Makuu ya Wilaya, lakini hazina barabara inayoziunganisha kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali, itajenga barabara ya kiwango cha lami ya kuunganisha Wilaya hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngenzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama nilivyosema Mheshimiwa Ngenzabuke, kwamba, tutaanza kwanza na Barabara Kuu zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa. Namna tunavyojenga uwezo wetu wa Taifa wa kimapato, tutaingia kwenye kuunganisha barabara zinazokwenda kwenye Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mipango ile na Tume ya Mipango, imeshaainisha barabara hizi. Kwa mfano, mwaka wa kwanza tutaingia zipi, mwaka wa pili, kila tunavyoweza kujenga uwezo ndivyo tutakavyoweza kufanya suala la kujenga barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Kasulu.

Na. 195

**Chuo cha Rungemba**

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini, mafunzo yaliyokuwa yanatolewa katika Chuo cha Rungemba, yamesitishwa?

(b) Je, hivi sasa Chuo hicho kinafanya nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba uniruhusu nitumie Bunge lako Tukufu, kuipongeza Timu ya Mkoa wa Tanga ya vijana, Umri wa Chini ya Miaka 17, kwa kuifunga Dodoma, Timu ya Naibu Spika, katika Mashindano ya *Coper Cocacola,* yanayoendelea.

Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga, tunaitakia heri timu yetu katika mchezo wa leo dhidi ya Morogoro. Morogoro, tutawachapa, hawaiwezi Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Elizabeth Batenga, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya ngazi ya Cheti, yaliyokuwa yanatolewa na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba, yalisitishwa mwaka 2008 kwa madhumuni ya kupandisha chuo hiki hadhi, ili kutoa mafunzo ngazi ya Diploma.

Wizara, ilifanya maamuzi hayo kwa lengo la kuwapata Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wenye upeo mkubwa zaidi wa kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo yao katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo hiki kwa sasa kina wanachuo 390. Aidha, wanachuo 295 wameshahitimu mafunzo yao toka kozi hii ya *Diploma*, ilipoanzishwa mwaka 2008.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru niulize maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kumbukumbu nilizonazo, maana mimi nilikuwa Afisa Maendeleo ya Jamii wakati ule.

Kabla ya mafunzo haya ya Cheti na *Diploma* kuanzishwa, chuo hiki kilitumika kutoa mafunzo kwa Viongozi wa Vikundi mbalimbali vya wanawake nchi nzima, walikutana pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo yaliyokuwa yakitolewa yalikuwa ni mafunzo ya uongozi, ni mafunzo ya *study* mbalimbali, lakini mafunzo haya pia yalisadia kujenga umoja wa kitaifa kwa sababu wanawake walitoka sehemu zote za nchi. Sasa kwa maoni yangu na maoni ya wengi mafunzo kama haya ni muhimu sana kuendelea kutolewa kwa wanawake. Sasa je, Mheshimiwa Serikali iko tayari kuandaa chuo ambacho kinaweza kuendelea kutoa mafunzo kama haya ili kuzidi kuimarisha umoja katika nchi yetu, maana wanawake ni chimbuko la umoja katika Taifa lolote.

Je, wakati Serikali ikifikiria kuanzisha chuo kama hicho ambacho ni muhimu sana. Je, yuko tayari chuo hicho kukiweka kanda ya ziwa na hususan mkoa wa Kagera?

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba licha ya kwamba Lungemba sasa hivi inatoa mafunzo ya *Diploma* lakini bado tuna vyuo vinne ambavyo vinatoa elimu ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya cheti, vyuo hivyo ni Uyole, Ruaha, Mlale na Mabugai, Lushoto katika Mkoa wa Tanga.

Lakini pia niseme tu kwamba tayari tuna vyuo 55 ambavyo tunaviita Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* katika wilaya mbalimbali na vyuo hivi ndiyo tunavitumia kwa ajili ya kutoa mafunzo yanayohusu maendeleo ya wanawake, jinsia ujasiliamali kazi mbalimbali za mikono, masuala ya afya ya ujana katika afya mbalimbali. Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge tuna vyuo vingi ambavyo vinaweza kufanya kazi hii.

Lakini suala la kwamba je, tuko tayari kufanya chuo cha Maendeleo ya Jamii katika kanda ya Ziwa nikuthibitishie tu kwamba wakati tutakapowasilisha Bajeti yetu tarehe 23 utaona kwamba katika kanda ya ziwa tuna vyuo ambavyo vinatumika katika kutoa mafunzo mbalimbali kuhusu Wanawake na Maendeleo ya Watoto. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umeisha na kama mtakavyoona kama kuna siku ambayo inabidi tuwe makini sana katika suala la muda ni leo kwa sababu ya hali iliyojitokeza jana

imesabibisha leo pawe na msongamano wa mambo mengi zaidi.

Tatizo lililojitokeza jana la kukatika umeme humu kwenye ukumbi wa Bunge, inatokana na kitu kidogo tu kinachoitwa *circuit breaker.* Kwa hiyo mafundi wetu wa *TBA* na *TANESCO* kwa pamoja wanashirikiana kufanikisha majukumu yao.

Aidha ni kuhakikisha kwamba hili tatizo la kukatika umeme mara kwa mara saa za jioni wakati matumizi ya umeme yanapoongezeka katika mji wa Dodoma, suala hili halijirudii tena. Tuhakikishe kwamb a umeme haukatiki tena katika ukumbi huu wa Bunge pamoja na maeneo yote ya Bunge. Tunajitahidi sana na wamefanya kazi usiku kucha na tunatumaini tatizo hili litakuwa limeondoka moja kwa moja. *(Makofi)*

Wageni, wako wageni wangu kutoka Kongwa, ambao ni ndugu Bahati Mfundo Njemeni na ndugu Chrispine Daniel Mguli, msimame pale mlipo karibuni sana, Bungeni hawa ni vijana ambao wanajishughulisha kweli kweli kwenye soko la Kitaifa pale Kibaigwa na wanaendelea vizuri sana. karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni kutoka mahakama na Wizara ya Katiba na Sheria ni kama wafuatao. Jaji Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Mohamed Chande Athuman, ahsante sana Mheshimiwa Jaji Mkuu tunakukaribisha sana hapa Bungeni na nikuhakikishie Bunge hili liko tayari kutoa kila aina ya ushirikiano kwa mahakama yetu ya Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye ndugu Faki Jundu, Jaji Kiongozi Mahakama Kuu ya Tanzania, Mheshimiwa Kipenka Musa, Jaji wa Mahakama ya Rufaa. Huyu Mheshimiwa Kipenka Musa amewahi kuwa Katibu wetu wa Bunge la Tanzania, kwa miaka michache iliyopita na alifanya kazi nzuri sana katika Bunge letu hili. Mheshimiwa Kipenka karibu sana na tunakushukuru sana na tunaikumbuka kazi yako nzuri uliyotufanyia. Tunakuombea kila la heri huko uliko. *(Makofi)*

Tunaye Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Ndugu Fanuel Bonde, karibu sana Katibu Mkuu. Tuna Ndugu George Masaju, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia yuko Mheshimiwa Mary Shangali, Jaji wa Mahakama Kuu kanda ya dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Makamu wa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Mheshimiwa Mahafudha Hamid, tunaye Jaji wa Mahakama Kuuu wa Tanzania na Mkuu wa Chuo cha Mahakama Lushoto, Mheshimiwa Aloyce Mjulisi, tunaye Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Jaji Prof. Ibrahim Juma.

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Jaji wa Mahakama Kuu kanda ya Dodoma Mheshimiwa Mwanaisha Kwaliko, lakini pia nichukue fursa hii kumtambulisha mkurugenzi wa Mashitaka Dkt. Elieza Fereshi. *(Makofi)*

Tunaye Jaji Mfawidhi *Division* ya Kazi, Mheshimiwa Regina Rweyemamu, *Division* ya Biashara Jaji Mfawidhi, Mheshimiwa Robert Makaraba, Jaji Mfadhiwi *Division* ya Ardhi, Mheshimiwa Richard Mziray, Jaji wa Mahakama Kuu

Mheshimiwa Francis Mtungi na pia Jaji wa Mahakama Kuu Gerad Lika. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Mawaziri ni kama wafuatao, wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Martin Chikawe ambao ni familia yake ikiongozwa na mkewe ni Prof. Amandina Lihamba. *(Makofi)*

Sijamwona Prof. Lihamba, sijui yuko wapi? Yuko njiani anakuja, Prof. Lihamba, amefundisha wanafunzi wengi tu humu ndani. Pia wako wageni wa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Angellah Kairuki ambao ni familia yakei ikiongozwa na mumewe Bwana Mbelwa Kairuki. *(Makofi)*

Ahsante sana bwana Mbelwa, naona wako na Waheshimiwa hapo karibuni sana Bungeni. Mama anafanya kazi nzuri kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Martini Chikawe.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, ana wageni watano ambao ni wachungaji wakiongozwa na Mchungaji Titus Julius, wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mahanga, wanaongozwa na Mchungaji Titus huenda watakuwa *basement* karibuni sana.

Lakini pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Eustace Katagira, kutoka jimbo la Kyerwa, mgeni wake ni Ndugu Sevelini Katabalo, karibu sana mahali popote pale ulipo. Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi tisini kutoka shule ya sekondari Wilavya ya Kigoma,

pamoja na walimu wao wanne na mwandishi wa habari mmoja.

Wanafunzi wa Sekondari ya Wilavya toka Kigoma, karibuni sana sana, wako pande zote za *Gallery* tunafurahi sana kuwa nanyi hapa Bungeni nyie wanafunzi. Safari ya kutoka Kigoma mpaka hapa siyo safari fupi, mmeonyesha kwamba inawezekana kabisa na wanafunzi wa Sekondari nyingine katika mikoa mbalimbali ya nchi yetu wanaweza kabisa wakalitembelea Bunge letu Tukufu. Karibuni sana na niwahakikishie Wabunge wenu wa Kigoma wanafanya kazi nzuri humu ndani ya Bunge hili.

Wanafunzi 50 na walimu wao kutoka shule ya Sekondari ya Msalato, ahsanteni sana. Hii ni shule ya wasichana na ni wasichana ambao wanakuwa wamechaguliwa wenye *marks* za juu, wana vipaji maalum, hongereni sana. Vijana wetu kutoka Msalato pamoja na walimu karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wanafunzi 39 kutoka kitivo cha Sayansi ya Afya ya Chuo Kikuu cha Dodoma, *UDOM* wako pale na kwa wale wasiofahamu na wengine wako huku *UDOM* nayo sasa ina Kitivo cha Sayansi ya Afya. Kwa hiyo muda si mrefu tutaanza kupata madaktari na manesi kutoka kwenye chuo kikuu hicho cha Dodoma. *(Makofi)*

Lakini pia tuna timu ya mpira ya *Albino United Sport Club* wakiongozwa na Ndugu Joseph Kulindwa, Mwenyekiti wa Timu, karibuni sana. *(Makofi)*

Karibu sana Dodoma, karibuni sana Bungeni. Inatutia hamasa kuona kwamba mmeweza kuunda timu ya mpira na niwahakikishie timu ya *Bunge Sports Club* ipo wakati wowote mkitaka kucheza nayo kupimana nayo nguvu basi mtutaarifu hata kwa muda mfupi tu tutaandaa mechi lakini muwe mmejiandaa maana yake timu ya Bunge yenyewe kila timu inayokaa mbele yake basi huwa inafungwa tu. *(Kicheko/Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, upande wa wageni wetu ni hao kama kuna ambaye nimemsahau mtanikumbusha. Tangazo kwamba Chuo Kikuu Huria watakuwepo hapa ukumbi wa Msekwa anaadhimisha miaka 20 na wana mambo ya kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge. Kikao cha Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria na Utawala saa saba mchana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti Paul Lwanji, anawaomba wajumbe wake ukumbi 231.

Waheshimiwa Wabunge sasa naomba tuendelee niwaambie tu kwamba tutakapoingia katika Kamati ya Bunge zima, Kamati ya Matumizi tutaendelea pale tulipoachia jana. Kwa hiyo wale ambao walisimama jana majina yao bado ninayo, tutaendelea. Kwa kuwa tutakuwa tunamalizia muda wetu ule wa jana, tutatumia si zaidi ya saa moja tutakuwa tumefikia mahali itabidi tuhitimishe Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili tuendelee na ratiba yetu ya leo. Katibu tuendelee na kinachofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013**

**Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

*(Majadikliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Katibu saa hizi ni saa 4.15 Asubuhi, hatutazidi saa moja tunaendelea Mheshimiwa Zarina Madabida.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi na kuzungumza niliomba kauli ya Serikali kuhusu ushiriki wa nchi ambao wanamiliki ardhi wakati Serikali inapochukua ardhi ile kupima aidha viwanja au kuweka mradi.

Je, hawa wananchi wanakuwa na wenyewe *part* ya mradi ule au ni umiliki wa ubia au ni kwamba wakilipwa fidia bado ndiyo inakuwa imeishia hapo. Kwa sababu wanapolipwa fidia wananchi wanakuwa wametumbukia katika dibwi la umaskini, sasa nilitaka kupata kauli ya Serikali . Je, wananchi hawa watashirikishwa kama na wao wabia?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nimjibu Mheshimiwa Madabida kwamba utaratibu tunapokuwa tunapima viwanja au miji kimsingi Serikali inakuwa imetwaa ile ardhi. Kwa hiyo kwa mujibu wa sheria ya utoaji wa ardhi ya mwaka 1967 ardhi ile inatwaliwa.

Lakini kwa mujibu wa sheria namba nne ya mwaka 1999 ya ardhi tunatoa fidia na taratibu za kutoa fidia tunatoa ya soko, lakini kama nilivyofafanua jana tunahakikisha kwamba tunatoa fidia kwa mujibu wa sheria, ni bei ya soko na tunalipa pia gharama za usumbufu unaoweza kupatikana kwa sababu mtu ardhi yake imetwaliwa.

Lakini katika hali ya mijini jana nimezungumzia *resettlement* tunahakikisha kwamba mwananchi anapewa pia na eneo lenyewe pale mbadala.

Sasa kama utaratibu huo ulikuwa haujafuatwa nihakikishie tu kwamba kuanzia sasa hivi hakuna tatizo kama lile. Fidia kitu kinachogomba ni kwamba wananchi wengi wakishapata fidia wengine kusema kweli inapokuwa ya kutosha inapomalizika migogoro mingine inayoibuka haimanishi kwamba fidia haikutolewa lakini wakati mwingine matumizi yake yamekuwa mabaya, ndiyo maana sasa hivi tutaingia kwenye hiyo *resettlement* kuhakikisha kwamba mtu anapewa kiwanja mbadala.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru maeneo mengi ambayo yanapakana na mbuga za wanyama, maeneo ambayo yana mapori au yana vitalu, yamekuwa na migogoro mbalimbali ambayo inaendelea na baadhi ya Wabunge tumekuwa tunaleta maswali mengi kuhusu mipaka hii kwa sababu ilipimwa zamani na Mheshimiwa Waziri jana ulituonyesha ramani ya moja ya hifadhi hizi.

Sasa ni lini Serikali itapitia maeneo yote ikiwemo kule Kibondo, Kasulu, Tabora na maeneo mengine ya nchi hii kupitia upya mipaka ili migogoro hii ya wananchi na watu wa maliasili isijirudie tena na tusiendelee kuuliza maswali haya.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tumelipokea na kusema kweli kama mimi mwenyewe nilivyoanisha kwamba hakuna mamlaka yoyote Tanzania yenye haki ya kujipimia eneo.

Kwa hiyo kama tunahakiki mipaka wakati mwingine tuna bikoni *recovery* kwa sababu wakati mwingine mipaka imetea hata kama ilikuwepo nyingine ya zamani toka enzi ya mkoloni. Kwa hiyo bikoni *recovery* upimaji wa ardhi uko chini ya Mkurugenzi wa upimaji wa ramani ambaye yuko Wizara ya Ardhi. Sasa kuhusu migogoro mingi.

Sasa nisisitize tu kwamba hii ni migogoro ambayo siyo ya lazima. Sasa hivi tayari tumeshakubaliana na Wizara ya Ulinzi na Kujenga Taifa kuwa tutaweka zoezi au mkakati wa kuhakikisha kwamba maeneo ya jeshi yanapimwa na tunayafahamu na tunaweka *demarcations* lakini hakuna

mamlaka yoyote yenye ruhusa ya kuyatumia ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, suala langu linafanana na alilililoliuliza Mheshimiwa Felix Mkosamali linahusu *game reserve* ya Rwafi, ambayo sasa hivi, karibuni ilitolewa kwa mamlaka ya hifadhi kutoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *game reserve* hii ilikuwa haijawekewa mipaka na bado kuna sintofahamu kubwa kati ya mipaka ambayo ilikuwekwa zamani na mipaka ya vijiji ambapo vijiji vyote vinavyozunguka vina malalamiko ya kataka kujua kama katika utaratibu huu mpya je, watazingatia kujua kama katika utaratibu huu mpya

Je, watazingatia kuweka mipaka ambayo itazingatia vijiji vyote vinavyozunguka *game reserve* ya Rwafi kuzingatia maoni ya wananchi kuwaongezea eneo ili kuepuka usumbufu wa kukosa ardhi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mipata tulikubaliana kwamba katika masuala ya sera hatutashughulika na mradi mmoja peke yake, kwa hiyo, utaniwia radhi sana.

Mheshimiwa Sakaya! Ametoka. Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa jana nilizungumza mambo mengi, lakini suala zima lilikuwa ni ukubwa wa tatizo la wawekezaji wanaochukua maeneo ambayo ukija kuangalia wamechukua kinyume cha utaratibu. Nikatolea mfano hata suala zima la uwekezaji wa *bio-fuel* katika zao

la jiotrofa katika Wilaya ya Kisarawe ambapo ukija kuangalia ni kwamba mtu amepata hati miliki, matatizo yamekuwa makubwa, lakini sikupata *clarification*. Lakini unaposema kisera mtu anakiuka utaratibu na kupewa hati je, Serikali inasema vipi katika utaratibu wa kufuta hati hizo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee tu kwamba, ni kweli kuna mgogoro huo wa *sun bio-fuel* na tayari tunaushughulikia Wizarani, lakini sasa kwa sababu tunashirikiana pia na Kituo cha Uwekezaji *(TIC),* kama kuna wawekezaji ambao wamechukua maeneo na inabainika kwamba hawayatumii kama ipasavyo, hakuna kinachozuia maeneo hayo kuangalia upya. Sasa kwa mfano, mtu ameomba, maana yake sisi tunaangalia matumizi ya ardhi, ardhi kama ile tunaitoa kwa Kituo cha Uwekezaji wenyewe. Sasa ndiyo wanamilikisha yule mwekezaji, lakini pia sisi kama *administrators* wa ardhi, kama kuna uthibitisho kwamba yule aliyepewa ardhi ameihodhi tu haitumii ipasavyo inaweza ikatwaliwa na kurudishwa kwa wananchi. (*Makofi*)

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nazungumzia sera na Sera ya kwanza ya Ardhi ya Taifa nchini Tanzania ilipitishwa mwaka 1995 na ni kwa sababu mbalimbali; ongezeko la idadi ya watu, kulikuwa na migogoro mingi kati ya wakulima na wafugaji ambayo inaendelea mpaka sasa hivi na matatizo mengineyo ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika mchango wangu niliainisha migogoro ya ardhi mbalimbali. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuweza kuiangalia upya Sera hii pamoja na Sheria

zake? Japokuwa jana ilikusikia ukigusia kuwa kuna *just a portion* ambayo mnaifanyia kazi, kwa hiyo, nataka kujua kwa kauli kwamba mnaifanyia *as a whole or just a portion*?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sera yetu ya ardhi nzuri sana inaendana na *foundation* ya Taifa letu, utekelezaji wa sheria kidogo ndiyo umekuwa na matatizo na mwaka 2004 katika marekebisho yaliyofanyika, kwa mfano, ilionekana kwamba sasa hivi wageni wanaweza wakamiliki ardhi kinyume cha misingi ya sera na sheria mama. Kwa hiyo, nimezungumzia marekebisho ambayo yataondoa matatizo yaliyokuja kuibuka katika utekelezaji, lakini kimsingi sera yenyewe iko imara na katika mchakato wa Katiba mpya hapo pia tuna nafasi kisera na kimsingi kuangalia namna ya kumiliki ardhi ya Taifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi inatamka bayana ardhi ni nini na mipaka ya matumizi ya ardhi na inaeleza bayana kwamba inajumuisha vitu vyovyote juu na chini isipokuwa madini na mafuta.

Lakini hivi karibuni tumeshuhudia kuna mkataba wa kampuni ya uwindaji ambayo imeingia na kampuni ya nje kwa madhumuni ya kufanya *exploration* ya madini ya *Uranium*. Sasa nataka kwa tafsiri ya Sheria ya Ardhi ilivyo na hiki ambacho kimefanyika kwa mtu binafsi ambaye ana leseni tu kuwinda kutumia ardhi ile kwa matumizi mengine, Serikali inasema nini kuhusiana na hili?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, ardhi ya Tanzania 70% iko chini ni ardhi ya vijiji, 287% ipo chini ya Hifadhi za Taifa mbalimbali ikiwemo madini, maliasili na kadhalika, lakini 2% tu ndiyo tunasema ni *public land* yaani ile ambayo ipo chini inayotwaliwa na Serikali na kuwekwa chini ya himaya yake hususan ardhi za mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mtu ana leseni ya kuwinda, kwa hiyo ana *surface right*, sasa akaingia yeye mkataba na mtu wa kuchimba kama nimeelewa swali la Mheshimiwa Mdee. Sasa suala hilo linajadilika na kwa upande wangu nitarejea kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atuelekeze, lakini sisi tunavyojua *land use* inayo *prevail* pale ni kuwinda. Kwa hiyo, sasa kama tunaingia kwenye uchimbaji hata hivyo jana nilifafanua kwamba kifungu cha 7, Ibara ya 97 ya Sheria ya Madini kwa mfano, inasema bayana kwamba, huwezi kuanza kuchimba madini kabla hujafidia wale wenye *surface rights*, maana yake kuwinda *the surface right* au siyo, ni sheria anatumia ardhi wanyama wako juu, hawapo chini ya ardhi. Sasa kama ameamua yeye kwamba anatakiwa yule afidiwe aondoke kwa mujibu wa sheria ile, aachie wale wanaochimba.

Sasa kama utaratibu huo umekiukwa hapo Sheria ya Madini kifungu cha 7 ibara ya 97 kitakuwa hakijafuatwa. Lakini suala hili *competent authority* ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Niseme tu kwa sababu Wizara ya Nishati na Madini itakuja mbele kidogo, wajiandae vizuri ili waje watoe ufafanuzi wa jambo kama hili, kwa sababu wengi wetu hatulielewi linakuwaje kuwaje.

Mheshimiwa Nassari!

**MHE. JOSHUA SAMWEL NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Issue* yangu kubwa ambayo niliizungumza wakati nachangia ilikuwa ni ile idadi ya mashamba ambayo niliyataja na wakati wa majumuisho Mheshimiwa Naibu Waziri ndiye aliyajibu, lakini ningependa kujua kwamba ni lini sasa ile Tume ya matumizi bora ya ardhi itakuja Arumeru kwa ajili ya kuondoa ile sintofahamu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Joshua Nassari Mbunge wa Arumeru Mashariki kwamba kwanza tunampongeza sana kwamba, mara baada ya kuingia amejitahidi kuwashughulikia wananchi wake.

Tume ya matumizi bora ya ardhi itakuwa tayari kwenda Arumeru mara mawasiliano pamoja na Halmashauri na Meru yatakapokuwa yamekamilika kwa sababu zipo gharama ambazo zinapaswa kubebwa na Halmashauri inayohusika na sehemu nyingine itabebwa na Tume yenyewe.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sera ya Chama cha Mapinduzi ni kuondoa kero za wananchi, Tunduru ina umbali wa kilomita 276 mpaka Makao Makuu ya Wilaya. Wananchi wa Tunduru bado ni wale ambao wako katika kaliba ile ya umaskini na migogoro ya ardhi Wilaya ya Tunduru ni mingi na ukichukua hotuba ya bajeti ya mwaka jana Wizara ilisema kwamba Wilaya ya Tunduru ni Wilaya miongoni mwa Wilaya zile 10 ambazo zitakuwa zimefunguliwa ofisi za Baraza la Ardhi. Je, Waziri anasema nini kuhusu sera hii ya kuondoa kero za wananchi kwa kuifungulia Wilaya ya Tunduru Ofisi ya Baraza la Ardhi haraka iwezekanavyo hasa ukizingatia kwamba ni Wilaya pekee ambayo ipo mbali sana na Makao Makuu ya Mkoa?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la Baraza la Ardhi, Tunduru ni kitu ambacho na sisi tunaona ni muhimu. Ufinyu wa bajeti ndiyo unatufanya tuwe katika hali tuliyonayo, kwa hiyo, niwe na matumaini kwamba bajeti yetu ikiongezwa na uwezo wetu ukaboreshwa na hapa naamini kwamba Waziri wa Fedha analisikia hili, tutaweza na hatuna sababu ya kutoweka Baraza la Ardhi, Tunduru kwa sababu ya sababu ambazo Mheshimiwa ametoa na ni za msingi.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati Mheshimiwa Waziri anatoa taarifa yake hapa alizungumzia suala la *City Park* hususan katika bonde la Msimbazi.

Mheshimiwa Waziri akumbuke kwamba katika bonde hili kulitokea maafa na Serikali ilitaka kuhamisha watu ili waende sehemu nyingine. Juzi baada ya taarifa yake hii ya kutaka eneo hili kulitenga kwa ajili ya *City Park* baadhi ya wananchi wameanza kupatwa tena na wasiwasi, tunataka tupate ufafanuzi wake, hii *City Park* itakuwaje? Itagusa maeneo gani na je, mradi huu utaanza lini? Ahsante.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba bonde la Msimbazi limetengwa kuwa *City Park* tangu mwaka 1979 kwa *Master Plan* ya Jiji la Dar es Salaam ya mwaka 1979 kuanzia *Surrender Bridge* mpaka Pugu, Bonde lote lile limetengwa kama *City Part* kwa sababu ndiyo eneo oevu na hakuna njia ya maji kuingia kwenye bahari isipokuwa kupitia mto wa Msimbazi. Kwa hiyo, makazi yoyote na maendelezo yoyote yaliyomo na mengine yapo pale kwa kupewa vibali, yote kusema kweli hayana mustakabali itabidi yaondolewe kwa sababu tunalinda lile eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaratibu wa kuendeleza *City Park* hapo nifafanue kwamba ni mradi mkubwa tunajipanga na utaratibu ambao tutautumia ni wa *concession. Concession* ni uratatibu ambapo maeneo fulani unawapa watu wenye uwezo wa kuyatunza kama *park* kwa sababu sasa hivi Halmashauri zetu husika katika Jiji la Dar es Salaam ni lazima nikiri kwamba si Wizara ya Ardhi kutunza sisi *Beaches*, siyo kazi yetu bali iko chini ya Halmashauri husika ila hali halisi ni kwamba Halmashauri husika zipo katika hali mnayoifahamu, hazijaweza kutunza maeneo hayo yote ya wazi. Watu wote katika bonde lile walio wengi kusema kweli wavamizi au *squatters* lakini

wamekuwepo pale kwa muda mrefu tunawaangalia kwa jicho la *understanding,* la huruma kama unataka lakini tangu mwaka 1979 enzi za Mwalimu tayari eneo lote lile lilishatangazwa kama *City Park*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ule mradi ndiyo tuna *catch up,* tunauendeleza, lakini wananchi walio mle nichukue nafasi hii kuhimiza kwamba walio wengi tumeshaanza polepole kuwaondoa kwa mfano wengine baada ya maafa ambayo yaliwapata watu wakapoteza maisha, kitu cha kusikitisha sana. Kwa mara nyingine tena natoa rambirambi zangu, lakini pia nahimiza kwamba tusingoje mvua ndiyo ituondoe kwa sababu lile ni eneo hatarishi hata kwa wenye viwanda kama mnavyofahamu sehemu za Tabata mvua inaponyesha pana *plot* sasa hivi ina *damming effect*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na muda kuwa mfupi nielezee tu kwamba, haya maeneo oevu kazi yake kubwa huwa ni kunyonya maji, bonde la Msimbazi linanyonya maji kusudi yasiende kwa kasi baharini. Sasa kilichotokea pale *Surrender Bridge* kwa mfano katika nyumba ya Mheshimiwa Mengi palikuwa na Sunami kwa sababu tairi ilikuwa inaingia ndani, maji yanakuja, kwa hiyo, kilichotokea ikaenda makaburini na Umoja wa Mataifa na sehemu nyingine zilizoathirika.

Kwa hiyo, maeneo oefu yana *absorptive function* yaani yananyonya maji ili kusudi mto mto unatema maji polepole. Tunapoyapiga *cement* na kuyajenga tunajitakia maafa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wasiwasi wangu ni mmoja tu, katika kujibu hoja Naibu Waziri na katika hoja za baadhi ya Wabunge walipendekeza kwamba Shirika la Nyumba la Taifa lisamehewe *VAT*. Sasa nakuwa na wasiwasi kwamba hapo likisamehewa *VAT* je, wananchi wanaokaa vijijini Tanzania kule ambao hawawezi kusaidiwa na Shirika la Nyumba na wanajenga nyumba kwa fedha zao binafsi na wenyewe vile vile wasamehewe *VAT* kwa vifaa vya ujenzi kama *cement*, saruji, nondo na mabati?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Keissy anagusia suala la msingi na nadhani wachangiaji wengi mawazo yenu tumeyapokea mmezungumzia tu siyo *VAT* kwa ajili ya nyumba za *National Housing*, lakini tunazungumzia pia kodi katika *building materials.* Kwa hiyo, njia ya kumsaidia mwananchi wa kawaida ni kupunguza *VAT* katika vifaa vya ujenzi. Kwa hiyo, suala la vifaa vya ujenzi na mimi ningependa kujua, mimi ni Waziri wa Nyumba na siyo Waziri wa *National Housing, National Housing* inaendeshwa na Mkurugenzi wake machachari Bwana Nehemia Mchechu na kazi anayoifanya mnaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi kama Waziri wa nyumba ni lazima nikiri kwamba, sasa hivi bado tuna changamoto za kuboresha makazi katika vijiji vyetu. Nilipotembelea Mkinga lazima niseme kwamba nilishtuka kuangalia hali ya nyumba, ilikuwa hairidhisha lakini umezungumzia mambo ya Mkonge, ambayo yamekuwepo miaka mingi *but there was nothing to show for it*. Nilipokwenda Mkinga niliona nyumba za wananchi zilikuwa bado zipo katika hali mbaya. Kwa hiyo, niombe tu tena

sasa Bunge Tukufu hapa naomba mnipeleke kwa Waziri wa Fedha aniangalie kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunikumbuka, lakini nazungumzia sera ya uchukuaji ardhi na ulipaji fidia na sheria kwenye ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu niliulizia juu ya ulipaji wa fidia Kurasini na Mtoni Kijiji cha wavuvi. Lakini pia nilizungumzia kuhusu utaratibu wa miradi, miradi inakuwa hai kwa muda gani? Sisi tunajua ni miaka miwili, Kurasini na Kigamboni. Kwa hiyo, ningefurahi sana Mheshimiwa Waziri angejibu hayo na suala la *National Housing* pia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Umechomekea kweli kweli, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja za Mheshimiwa Mtemvu kuhusu fidia kule Kurasini ni za msingi kulikuwa na ucheleweshwaji. Lakini labda niseme matatizo yanayotukumba sisi maana yake sisi kama nilivyosema hatuna shughuli na ardhi na kuigawa kwa watumiaji. Sasa eneo la Kurasini ni eneo la Bandari, ni Wizara ya Usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna deni kule Wizara ya Ardhi ilitumia bilioni 2.3 katika mradi ule ambao mpaka sasa hivi ni lazima nikiri kwamba haujarudishwa na Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, ndiyo maana unaona kwamba mradi wa Kurasini kidogo umeathirika. Sasa niseme tu baada ya hapa, mimi mwenyewe sasa hivi utaratibu ambao nimeuweka ni kwamba, kama mtu huna fedha ya kufidia

mradi, tafadhali usije Wizara ya Ardhi kwa sababu hawatakuja hao wathamini. Tutaweka utaratibu wa kudai *escrow account* lazima tuone kwamba mwenye mradi kweli ana fedha kwa sababu kumbuka kwamba tatizo ni kwamba, wenye miradi walio wengi wanataka walipe wao fidia lakini lawama zinaiangukia Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo lingine ambalo nitawaambia wenzangu ni kwamba tuweke utaratibu kwamba Mthamini Mkuu wa Serikali hatafanya tu *evaluation* lakini atafanya pia malipo atayasimamia ili kusudi sisi tuache kuwa *shock absorbers* wa matatizo yanayotokea katika sehemu nyingine.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa hotuba yake aligusia suala zima la kufanya mazungumzo baina ya Burundi na Kenya kurejesha alama za mipaka yaani *beacons*. Lakini mara nyingi karibu miaka saba sasa au nane Mawaziri wenzake waliopita walikuwa wakieleza maelezo haya haya. *Beacons* baina ya Tanzania, Tarime na Migori Kenya kwenye Vijiji vya Panyankore, Ikoma, Ronce na Kirongwe zimeondolewa, kuna tatizo la mpaka baina ya Tanzania pamoja na Malawi, nafikiri unaelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, Waziri wa Ulinzi na Mambo ya Nje, Mawaziri wawili hawa wamekuwa wakifanya bidii kubwa katika miaka mbalimbali, lakini lawama zimekuja kwa Mawaziri ambao wana dhamana ya Wizara hii, yeye mwaka huu kama ambavyo mwenyewe ametuambia jana...

**MBUNGE FULANI:** Profesa!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Profesa! Je, anasema juu ya mpango huu? Nashukuru!

**MWENYEKITI:** Umegusa pale pale. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifafanue, kama nilivyosema ni kweli kwamba, suala la mipaka ya Kimataifa sisi ni *technical authority,* tunapima na kubaini, lakini sasa inapokuja kwenye suala la *negotiation* tunafanya kazi pia na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje.

Suala la mipaka, niseme kwa kweli watu wanaharibu hizi *beacons*. Wengine siku hizi wanafikiria kwamba tunapima maeneo yao kuyachukua. Kwa hiyo, unakuta kwamba tunapoweka *beacons* wananchi wanaziondoa. Nichukue nafasi hii kuwaomba wananchi kwamba waheshimu hizi *beacons* zinapowekwa. Lakini sasa hizi *beacons recovery* na *delimitation* inavyokuwa ni lazima wataalam wanakuwepo na hatua nyingi zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la mpaka wetu katika Ziwa Nyasa au mpaka na Malawi. Hapa kuna mgogoro ambao naweza kusema kwamba ni tatizo, nisiite mgogoro, lakini kidogo kuna kutokuelewana. Wizara yangu imeshaandika *technical report* kupeleka kwa mwenzangu wa Wizara ya Mambo ya Nje. Hapo mambo yalipofikia sasa inabidi tukae na watu wa *Foreign Affairs* na kusema kweli ngazi za juu za Serikali kukubaliana kwamba mpaka kati ya Lake Nyasa tunachukua na sisi nusu ya Ziwa kwa

mujibu wa ramani ya Mjerumani au sisi tunakuwa hatuna Ziwa kwa mujibu wa ramani ya Mwingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya nchi hii kukabidhiwa kwa Umoja wa Mataifa (*League of Nations*) na mipaka yake mingine ikawa imebadilishwa. Sasa msimamo wa muasisi wa Taifa hili ilikuwa ni kwamba yeye anakwenda kwenye mipaka ya Mjerumani. Kwa hiyo, uelewa wetu sisi ni kwamba, tuko katikati ya Ziwa. Sasa tumeshaandika ripoti na iko kwa Waziri wa Mambo ya Nje, kusudi hatua zinazofuata ziendelee.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sera za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hasa kuhusu watu ambao tayari mmekwishawapa hati halali mnazozitambua, halafu wanavamiwa na watu wasiokuwa na uhalali wowote na mfano mzuri ni wale *Holy Spirits Sisters* wa Rawia, Marangu. Mheshimiwa Waziri ametuelimisha kama amekwishampa mtu ardhi na hati sio kazi yao kulinda ile ardhi. Ni kama mtu amenunua kitanda dukani, akakuta mtu amekilalia kile kitanda pale nje, kurudi kwa mwenye duka kumwambia bwana kitanda chake kinalaliwa na mtu fulani, unakwenda Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale Ma-*sister* wamefanya kazi mbili, naomba huruma yenu. Kwanza wamekwenda Mahakamani, naomba niipongeze Mahakama Kuu, Kanda ya Kaskazini, wakazungumza lile shauri wakaamua kwamba wale watu 11 waliokuwa na Ma-*sister* pale tangu wakinunua shamba hili wasihusike na hiyo amri ya muda iliyotolewa. Kwa sababu sasa hivi kuna watu wamepandikizwa pale watu 600, Mahakama

ikaamuru ni marufuku mtu yeyote na Mwenyekiti wa Kijiji ndio alikuwa anauza lile shamba, ni marufuku kuuza lile shamba, ni marufuku kuzika watu pale ni marufuku kufanya shughuli zozote pale, lakini wale watu wamekaidi na wapo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamwendea Mwanasheria hapa, namshukuru sana Mwanasheria akanipa barua nirudi Mahakamani Moshi. Ndio! Mahakama ikaniambia sasa wewe sisi tumekwishakufanyia maamuzi tekelezeni. Haya nikamwandikia barua Waziri wa Mambo ya Ndani kumwambia jamani tusaidieni kwenda kuondoa wale wavamizi. Waziri wa Mambo ya Ndani hata hakujibu. Mwisho wake nikamjia tena Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, sasa tunafanyaje, yeye ndio ametupa. Sasa tunataka kujua sera zenu katika mazingira haya, maana yake tunawadanganya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahangaika, Mbunge anahangaika, hajui aende kwa nani apate msaada. Kwa nini watu wanawapa kichwa pale kwamba kaeni hapa haondoki mtu. Leo tuna Ma-*sister* wanatoka Moshi, wanakuja kuhamia hapa Bungeni nataka wawaambie waende wapi kwa sababu wale watu wanawatukana matusi ya nguoni, wanawazingira. Sasa saidieni hawa watu wa dini, haya Makanisa mnaachia tu, haya madaraka mmepewa ya kufanya kazi gani kama mnashindwa hata watu wa Makanisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Mrema anafahamu kwamba kweli Ma-*sister* walikuja, anafahamu kwamba tulikuwa na kikao kizuri. Hili ni tatizo, katika migogoro ya ardhi, pamoja na matatizo mengine Mahakamani, lakini kuna tatizo, sasa tunaposhindwa kukaza hukumu migogoro inarejea. Niseme hali halisi kwa Waziri wa Ardhi, watu wanakuja, kwa hiyo, najikuta nina shida ya kusaidia kukaza hukumu. Lakini bahati nzuri nifafanue kwamba tayari sasa Waziri wa Mambo ya Ndani tumekubaliana tunakwenda kuunda kikosi cha *Land Police* hawataangalia mtu usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pale ni *squatters* wanatakiwa waondolewe. Mahakama imetoa amri kwamba wale ni *squatters* waondolewe na wenyewe wameng’ang’ania mle. Nina kesi nyingine kama hiyo hiyo pale Wazo Hill Dar es Salaam kwa mfano. Pale Kiwanda cha Sementi kina mgogoro kama huo na wenyewe wana *ruling* ya *Court of Appeal*. *Court of Appeal* wamesema kwamba wale ni *squatters* inabidi wahamishwe. Lakini sasa hali halisi inayotukabili pale tunaposhindwa kukaza hukumu, kitu ambacho nimejifunza katika *International System* pia kuna *mediation* wakati mwingine kukaza hukumu inakuwa *practically impossible*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hali hiyo unaingia kwenye *mediation* na Ma-*sister* niliwaambia kwamba nitakuja kuangalia, nitaangalia kama tufanye *mediation* au kama tukaze hukumu maana yake lazima pia uangalie hali halisi. Kwa mfano kule Dar es Salaam Wazo Hill, nimemwambia yule Meneja wa Kiwanda na amekubali atoe *ex-grace* ya *payment* halazimiki kulipa kitu chochote.

Lakini hakuna njia yoyote ya kumaliza ule mgogoro bila ya kuzungumza na wale wananchi labda kama Amri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Rais akiamua kuleta Majeshi yake kuondoa watu. Kwa hiyo, suluhu niliyonayo kimsingi sio juu yangu, lakini *techniques* ninazo na hizi ni *mediation* na *ex-grace ya payment* na Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda ameshasema, migogoro yote ya namna hii ya *mediation* irudi chini ya Wizara ya Ardhi kwa sababu tuna *skills* za kujaribu kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi Mheshimiwa Mrema kwamba na mimi nahitaji hizo sala na rozali za Ma-*sister* nitakuja kushughulika.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia tabia ya Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kuvamia maeneo ya ardhi ya vijiji katika nchi yetu. Vile vile Mheshimiwa Waziri atambue kwamba migogoro ya ardhi kati ya Wanajeshi na wananchi ipo ya aina mbili. Eneo la kwanza ni pale ambapo Wanajeshi wanakuwa na eneo lao wanaishi, lakini wanakuwa jirani na wananchi, kwa hiyo, wanagombea mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini aina ya pili ni pale ambapo Wanajeshi wanatoka sehemu yao wanasafiri kilomita na kilomita, tena mkoa kwa mkoa wanakwenda wanafika wanavamia ardhi ya kijiji fulani na kuikalia kwa mabavu. Nikatoa mfano ili aweze kunielezea sera hii kwamba Jeshi la Wananchi kutoka Mkoa wa Mwanza lilisafiri likaenda Mkoa wa Mara kwenye Kijiji cha Bunere, Jimbo la Mwibara na kuvamia ardhi katikati ya kijiji kwa vile tu kuna dalili za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua katika mazingira ambayo Jeshi la Wananchi, chombo cha Serikali linaposafiri kilomita na kwenda kuchukua ardhi ya wanavijiji, wanavijiji watatumia utaratibu gani wa kupata haki yao dhidi ya chombo muhimu kama Jeshi? Pia katika mazingira ambayo anazungumzia *Land Police* kama kweli Polisi hawa katika migogoro inayoendelea watakuwa na uwezo wa kwenda kuwafukuza Wanajeshi kutoka kwenye maeneo waliyovamia. Kwa hiyo, nataka kujua wananchi wa Tanzania katika maeneo kama haya watachukua hatua gani katika kuchukua ardhi yao iliyochukuliwa na Jeshi la Ulinzi wa Tanzania?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjulishe Mheshimiwa Lugola kwamba suala hili analolisema nadhani narudia. Maana yake nimeshasema kwamba tayari Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Mkuu wa Majeshi Meja Jenerali Mwamunyange tumeshakuwa na majadiliano ya awali kusudi tukubaliane namna ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu linatambua kwamba matumizi ya kijeshi ni maslahi ya umma au sio maana yake wanatulinda sisi. Kwa hiyo, wanapohitaji eneo na wenyewe wanaomba maana yake Sheria ya Ardhi iko wazi, ardhi zile ni ardhi ya kijiji lazima ihaulishwe na Mheshimiwa Rais ndiye Amiri Jeshi Mkuu, kwa hiyo Wanajeshi wanapohitaji ardhi hawawezi kujitwalia wenyewe. Tunaomba, Mheshimiwa Rais anahaulisha ile ardhi, inakuwa ardhi ya kawaida tunawamilikisha Wanajeshi. Labda niombe kwamba jamani kupunguza hii migogoro kusudi tufanye kazi maana yake tutakuja kuzama

katika *business of discussing work instead of doing it*, yaani biashara ya kuzungumzia kazi badala ya kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, matatizo haya yapo ni saikoloji moja ya matatizo tuliyonayo, lakini ndani ya Serikali tunalifanyia kazi. Sasa nimhakikishie tu Mheshimiwa Lugola kwamba hiyo kesi anayoitaja na yenyewe tutahakiki na tutaangalia na vyombo husika, Waziri wa Ulinzi lakini pia na Mwanajeshi wetu Mkuu ambao analifahamu tatizo. Nimeshazungumza kwamba tuna program rasmi ya ku-*demarcate* maeneo ya Jeshi. Yale ambayo yametwaliwa kinyemela kama yapo itabidi yapate ridhaa ya Mheshimiwa Rais kwa sababu maeneo ya Jeshi na yenyewe yanagawiwa kama watumiaji wengine wale.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa napenda nimfikishie pongezi zake Mheshimiwa Waziri na shukrani kutoka kwa vijana mbalimbali ambao wamenitumia *message* wakisema kwamba ameonesha dhamira ya dhati kuhakikisha vijana wa Tanzania na wenyewe wananufaika na ardhi yao, naomba nimfikishie salamu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyochangia kwenye mchango wangu wa maandishi kwamba miaka mitatu mfululizo Wizara imekuwa ikiomba fedha takribani shilingi bilioni 13 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuchukulia picha cha *satellite*. Kwa msisitizo kituo hicho kitajengwa hapa Dodoma na kitasaidia sana kupunguza migogoro ya ardhi katika mikoa mbalimbali pamoja na maeneo mbalimbali na hata kuhakikisha ramani zinakua vizuri pamoja na hati kupatikana kwa Watanzania.

Sasa nahitaji *commitment* ya Serikali na kituo hiki kwa kweli kitamsaidia sana mama Tibaijuka na Wizara kutimiza majukumu yao ipasavyo. Naomba *commitment* ya Serikali kwa nini katika mwaka ujao wa fedha zisitengwe hizi fedha ili tumalize matatizo na migogoro ambayo inalikabili Taifa letu.

**MWENYEKITI:** Ni kweli Mheshimiwa Ester kituo hiki kilikuwa kijengwe *UDOM*. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Bulaya kwa kuliona hili na kwa kulisema na mimi mwenyewe ningependa sana niwe na bajeti ambayo ingekuwa na takribani shilingi bilioni 14 kwa ajili ya kituo hiki ambacho kitajengwa hapa hapa Makao Makuu, Dodoma (*Satelite Receiving Station).* Sasa teknolojia hii haina tija, ukifanya *incremental funding* ni sawasawa na kununua gari ambayo haina matairi, kwanza unanunua halafu unasema matairi nitafunga baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunahitaji shilingi bilioni 14 kununua mitambo kusudi tufunge kituo chetu na kitatusaidia sana. Lakini sasa hivi hali halisi na kusema kweli kwa fani yangu kama Mchumi, sioni kama ina tija yoyote kuwa na *incremental funding* kusema kwamba mwaka huu wa fedha unapewa nusu baadaye na teknolojia hii inabadilika haraka sana. Kwa sababu unaweza ukanunua mtambo leo ukija kutafuta kifaa cha kuongezea unakuta kwamba teknolojia kule kwa wenzetu imeshabadilika. Kwa hiyo, kusema kweli hili lik mikononi mwa Bunge Tukufu kuniangalia kwenye bajeti inayokuja, mniwezeshe muone kazi itakavyokwenda.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Vile vile najielekeza moja kwa moja kwenye kasma 221000 kuhusiana na *travelling in country* kwenye *sub vote* hiyo ya 1001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilijadili sana matatizo ambayo yanaonekana kusababishwa na ukosefu wa utawala bora katika sekta ya ardhi na tunajua kwamba ni sera ya Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na nidhamu miongoni mwa watumishi wa Serikali wakiwemo watumishi wa ardhi kwa maana Maafisa Ardhi nchi nzima katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Sasa nimeeleza kwamba, kumekuwa na matatizo makubwa sana hasa katika Wilaya mbalimbali ikiwemo Kasulu Mjini. Sasa kwa kuwa katika kasma hii ya 221000 ina-*state* wazi kwamba kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Waziri kwamba ataweza kuzungukia katika maeneo mbalimbali. Nataka kupata *commitment* ya Mheshimiwa Waziri iwapo atakuwa tayari baada ya Bunge kufanya ziara katika Wilaya ya Kasulu ili kusudi tuweze kuangalia jinsi gani tutatatua matatizo haya ambayo yamekuwa ni makubwa kwa kuwa yamekuwa ni ya muda mrefu. Bila kuja sioni matumaini ya kwamba, wananchi wale matatizo yao yanaweza yakatatuliwa. Nini *commitment* ya Serikali katika kutatua matatizo ambayo ni ya utawala bora ambayo bila ya kuja hatuwezi tukaya-*solve* na tukaweza kupata muafaka wa kudumu?

**MWENYEKITI:** Fupi sana Mheshimiwa Profesa, safari ya Kasulu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Machali basi aniandalie angalau chakula kizuri maana niko safarini kwenda Kasulu. (*Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kupata ufafanuzi kuhusu jambo moja la kisera linalowagusa wananchi wa Jimbo la Ubungo na Watanzania kwa ujumla. Natambua kwamba wananchi kumiliki hatimiliki za ardhi ni nyenzo muhimu ya kupatia mikopo kwa maana ya dhamana, ni nyenzo ya kuhakikisha mipangomiji na ni nyenzo ya kuondoa vilevile migogoro ya ardhi kwa urahisi. Sasa kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya wananchi kuhusu kuchelewa kupata hati pale wanapowasilisha maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wanachukua miaka miwili, mwaka mmoja na wengine mwaka mmoja na nusu wakizungushwa kwenye Mamlaka mbalimbali. Kwa kuwa naamini Wizara inapaswa kuendeshwa na sera ya mkataba wa huduma bora kwa wateja (*Clients Service Chatter*). Ningeomba kauli ya kisera kwa Waziri, inachukua muda gani toka mtu anapowasilisha na kukamilisha vielelezo vyote vya maombi ya hatimiliki ya ardhi mpaka kupatiwa hati husika?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuhusu suala la Mheshimiwa Mnyika ni suala la utendaji na kuboresha ufanisi. Sasa hivi tuna kanda zetu sita ambazo zinatoa hati Mwanza, Mbeya, Mtwara, Dar es Salaam na Moshi kwa Kanda ya Kaskazini na Tabora ambayo nimeshasema

kwamba tumeanzisha Kanda mpya tunajaribu kusogeza huduma hizi za kutoa hatimiliki karibu na wananchi kama tunazungumza kisera.

Sasa nikijikita kwa Dar es Salaam ambapo Mheshimiwa Mnyika yeye ni Mbunge wetu hapo Ubungo ni kwamba, pale tuna Kanda yetu ya Pwani ambayo iko pale Wizarani. Mtaona kwamba hali halisi kuwa kweli *Customer care* na *Customer Service* jambo ambalo mimi mwenyewe linanipa tabu. Mbinu zetu pale *facilities* ziko finyu, kwa hiyo zinaboreshwa. Kwa hiyo, siko katika hali ya kukwambia sasa hivi inachukua siku nne au tano, labda nikwambie *normatively* kwamba inatakiwa kuchukua siku ngapi, ukiniuliza katika utendaji bora haitakiwi ichukue zaidi ya miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima nikiri kwamba hiyo sasa ni *normative,* maana yake sasa *realistically* bado sina jibu hilo. Hapo labda niseme tu lakini wananchi wenyewe pia kama nilivyozungumzia jana nilizungumzia kulalamika lalamika. Kuna watu wengi wamekuja mbele yangu unapotaka sasa kumpa hati yeye mwenyewe hajawa tayari, kwa hiyo unakuta kwamba kama tunataka kuwa *efficient particularly* watu wenye Makampuni lazima uwe na *seal* ya Kampuni au kwenye taasisi kama *NGO's* unakuta huko tayari sasa kwenye kuandika hati unasema leta *seal* hajawahi kuchonga *seal,* mambo kama hayo nayo yanatukwaza, lakini miezi sita ndio *the ideal time.*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Katika mchango wangu nilielezea sana suala la makazi holela. Nilitaka kujua ni nini sera ya Wizara katika kubadilisha mandhari ambayo

yamekuwa kwenye maeneo ya *squatters* au ya wazi. Kama kuna uwezekano vile vile ambao naamini kwamba upo katika kuyabadilisha maeneo haya kuwekeza ili yawe ya kisasa kwa ajili ya wananchi. Nasema hivyo nikitolea mfano katika eneo la Uyole kwenye Chuo cha Kilimo, kama kuna uwezekano wa Shirika la Nyumba la Taifa kufanya mazungumzo na chuo hiki cha Kilimo kwa ajili ya kujenga majengo ya kisasa kabisa kwa ajili ya wananchi. Nashukuru sana, naomba sera ya Wizara.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu tu Mheshimiwa Mary Mwanjelwa kwamba, kwa kweli hotuba yangu imeonesha kwamba, suala la mipangomiji ni muhimu sana. Sasa miji yetu mingi mpaka sasa hivi haina *master plan* na nilizungumzia dhana nzima ya kupima viwanja bila ya kuwa na *master plan,* tutakuja kuitolea *administrative order* kuzuia kwamba kama unataka kupima viwanja kwanza wekeza kwenye *master plan.*

Mji wa Mbeya ni mji mzuri sana na ni mji ambao inabidi tuulinde na ni mojawapo ya miji ambao tuna-*project* kwamba utakua na kuwa kitovu cha uchumi Tanzania. Sasa Shirika letu la *National Housing* linajitahidi, lakini pia nichukue nafasi hii kuelezea kwamba kama tunataka ku-*prevail over urban disorder* ni lazima pia na Halmashauri zianze na zenyewe kupima viwanja, sio kuviuza na kujenga nyumba. Ukienda Ulaya kila mahali kuna nyumba zinaitwa *Canso Housing* za kima cha chini, huwezi kuwasaidia watu wa kima cha chini kama Halmashauri zenyewe hazijengi nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika semina ya *ALART* nilitoa kauli na wito kwamba, naomba Halmashauri zenyewe tuwaone na wenyewe wanajali makazi, kutegemea kwamba *National Housing* ndiyo ataweza ku-*prevail over informality* na *squatting* wakati Halmashauri zenyewe hazijengi nyumba hasa za kawaida itakuwa vigumu. Lakini nimesikia wito kuja Mbeya na *National Housing* walikuja ila naomba wakija kwako na wewe uwasaidie kupunguza gharama na kodi za juu ambazo wanabambikiwa na Halmashauri ya Mbeya.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Wakati wa kuchangia kwa maandishi nilisema kuna tatizo kubwa la maeneo ya kilimo na hasa maeneo yenye rutuba na yenye maji kugeuzwa matumizi na kuwa maeneo ya makazi viwanda na matumizi ya mengineyo. Hili tatizo limetokea sehemu nyingi sana hapa Tanzania. Sasa itafika mahali ambapo hatutakuwa na maeneo mazuri kwa ajili ya kilimo. Je, ni lini sasa Serikali italeta Sheria ya kudhibiti na kuhakikisha kwamba maeneo ya kilimo na ufugaji yanalindwa na tuwe na kilimo endelevu na hasa ukizingatia kuwa wale ambao wanafanya maamuzi ya hayo matumizi ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa mara nyingi wakitoa mapendekezo unakuta si wakulima na si wafugaji na maeneo ya wakulima yanaendelea kupotea?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifafanue kwamba kwanza Sheria ipo, matumizi yanapangwa na Mkurugenzi wa Mipango Miji na Makazi chini ya Wizara ya Ardhi ndiye pekee wenye mamlaka ya kubadilisha matumizi ya ardhi. Kwa hiyo nifafanue pia jambo hili, watu wamefikiria kwamba Wilaya na Mikoa wana madaraka

haya, hawana. Wenyewe wanapendekeza, wakipendekeza tunaangalia, jana nilizungumzia kwamba tuna utaratibu tu Kamati ya Kitaifa ambayo inahusisha vyombo vingi kwa mfano ikiwemo ulinzi, Wizara ya Kilimo lazima tuwe nayo wakati tunabadilisha. Kwa hiyo, niseme kwamba Halmashauri nyingi kusema kweli tukitaka kuwakomalia wamejihusisha katika vitendo vya kubadilisha matumizi ya ardhi visivyo bila kuwa na ridhaa ya Mkurugenzi wa Mipango Miji. Kwa hiyo, suala hili kuanzia sasa hivi lisiwe tatizo tutarekebisha pale ambapo matatizo haya yamejitokeza.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia pamoja na mambo mengi ambayo nilizungumza kuhusu migogoro ya ardhi Babati na ripoti nzima ambayo Wizara ya Ardhi mpaka sasa hawajatupatia, kikubwa zaidi nilizungumza suala zima la Sheria ya Ardhi kuletwa hapa Bungeni kuifanyia marekebisho kipengele cha fidia. Nasema hili kwa sababu riba ya asilimia sita katika *fix deposit* kwenye *commercial banks* kwa sasa haikidhi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kwamba ardhi ya mwananchi imechukuliwa takriban miaka minne anakuja kulipa riba ya asilimia sita *of which*, inakuwa haimsaidii yule mwananchi. Nikaiomba Serikali watuletee ile Sheria tuifanyie marekebisho. Nahitaji kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri, ni lini sasa Muswada huo utaletwa Bungeni?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba suala la Mheshimiwa Gekul na lenyewe ni zuri na wachangiaji wengi Waheshimiwa Wabunge mliligusia. Labda tu niseme

kwamba, kwa misingi ya uchumi na katika kupigana na umaskini tatizo sio asilimia sita. Asilimia sita si haba, tatizo ni kuchelewa kutoa fidia. Kwa kuwa nimesema kwamba, sisi hatutajihusisha na kupima viwanja kama anayetaka tumpimie hana pesa.

Kwanza hilo tatizo litakuwa historia, lakini mimi mwenyewe nimechukua uamuzi kwa mamlaka niliyonayo chini ya sekta kwamba fidia zote ambazo zimeshavuka miaka mitatu, watu hawajalipwa itabidi wapime upya kusudi wapate bei ya soko. Kwa sababu nakubali kabisa hatuko kwenye biashara ya maendeleo sio kuwafilisi wale ambao inabidi tutwae ardhi zao. Kwa hiyo, huo ndiyo msimamo sio tatizo la kisheria na asilimia sita ya *savings account* si haba. Tatizo si asilimia, tatizo ni kuchelewa.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Watumishi wengi wanaofanya kazi kwenye miji midogo ukiwemo Mji wa Ngudu hawana nyumba za kuishi wananyanyasika, matokeo yake hawana ufanisi maofisini kwa sababu ya tatizo hili la nyumba. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa, wafikirie sasa kujenga nyumba ambazo zitakuwa *affordable* kwa watumishi ambao mishahara yao ni midogo, jambo ambalo linawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukijenga *one bedroom apartments* ambazo zitakuwa *self contained* mtaweza ku-*solve* tatizo hili la nyumba. Wananchi wa Ngudu wangependa pia wathibitishe ukweli wa usemi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, unaosema kwamba Tumethubutu, Tumeweza na Tunazidi Kusonga mbele, badala ya kurudi nyuma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia hiyo *one bedroom* halafu itakuaje? Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Leticia Nyerere kwamba kama nilivyosema suala la nyumba ni muhimu hasa nyumba ambazo ni za bei nafuu. Labda niseme tu kwamba, katika mikakati yangu ya kupigana umaskini hasa kuhusisha vijana nitapita sehemu mbalimbali za Halmashauri za kuweka kitu kinaitwa *Youth Construction Brigades*. Hawa ni vijana ambao wanafundishwa dhana ya teknolojia ya haraka sana. Kwa mfano kule Muleba kazi hii imeshaanza, vijana wanafundishwa na teknolojia ya *stabilized sold blocks* kutumia *cement* kidogo, kutengeneza tofali hapo hapo na kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa teknolojia hii ipo na napenda Waheshimiwa Wabunge tuwe wote katika Halmashauri zenu, tuweke kila Halmashauri iwe na *Youth Construction Brigade*. Itasaidia vijana wetu kupata ajira, lakini pia itasaidia wananchi kupata nyumba za bei nafuu. Teknolojia hii inaweza ikafanya nyumba badala ya kutumia shilingi milioni 15, ukatumia milioni tano tu na nyumba ikaonekana iko safi. Kwa hiyo, nafikiri kwamba, kwa hiyo hili linatekelezeka na tunalipokea na wanaotaka mjiorodheshe tulifanyie kazi bila kuchelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakushukuru. Bado nina majina kadhaa, lakini kwa kweli muda wetu kama nilivyoeleza wakati ule hauko upande wetu kabisa. Sasa ni wakati wa kuendelea, Katibu!

Kif. 1002 - *Finance and Accounts... ... ... ... ...* ...Shs 792,974,100/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning ... ... ... ... ... ...*Shs 2,769,783,600/=
Kif. 1004 - *Management Info System ... ... ... ...*Shs 585,183,000/=
Kif. 1005 - *Internal Auditor Unit ... ... ... ... ... ...*Shs 323,612,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit ... ...*Shs 412,555,300/=
Kif. 1007 - *Government Communication Unit ...* Shs 200,000,000/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit ... ... ... ... ... ...* Shs 200,000,000/=
Kif. 2001 - *Land Administration Division ... ...* Shs 2,605,688,000/=
Kif. 2002 - *Survey and Mapping Division ... ...* ...Shs 3,751,554,400/=
Kif. 2003 - *Registration of Titles Unit ... ... ... ...* Shs 1,114,545,600/=
Kif. 2004 - *Valuation Unit ... ... ... ... ... ... ... ...*Shs 944,800,800/=
Kif. 3001 - *Physical Planning Division ... ... ... ...* Shs 4,163,476,920/=
Kif. 3002 - *Housing Division ... ... ... ... ... ... ...*Shs 2,196,042,160/=
Kif. 3003 - *District and Housing Tribunal Unit ...* Shs 4,253,011,020/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 48 – WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management … … … …* Shs 0/=

Kif. 2001 - *Land Admin Division … … … … …*Shs 10,100,000,000/=

Kif. 2002 - *Survey and Mapping Div … … … …* Shs 300,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Physical Planning Div … …* **... ... ... ..**Shs 60,600,000,000/=

**MWENYEKITI:** Kabla ya kufika popote tumsikilize Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwanza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba urekodiwe kwamba tupo kwenye *guillotine*, hujasema hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Bunge halijakusikia, kama unaweza kurudia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo ulisema tunaendelea lakini ukweli ni kwamba, tunapitisha vifungu vyote kwa pamoja sasa. Naomba iwe hivyo ili rekodi ya *Hansard* irekebishwe.

**MWENYEKITI:** Tuko katika *Guillotine*, hebu Katibu tuweke vizuri, uirudie tena ili twende pamoja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taariFa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia makadirio ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2012/2013, mafungu kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2012/2013 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Bunge kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na Watumishi wengine wote wa Wizara hii muhimu sana kwa maisha ya Watanzania. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa Bajeti hii kwa mwaka unaokuja wa fedha, tunaamini kabisa kwamba sisi Wabunge tutakaporudi mwakani hapa baadhi ya malalamiko ambayo yamezungumzwa sana safari hii yatakuwa yamepungua kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri. Ahsante sana.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwenye orodha yangu haikuwa imewekwa vizuri, lakini tuna wageni zaidi ambapo ningeomba kuwatambulisha ndugu zetu wa Jukwaa la Katiba wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Deus Kibamba. Sijui wamekaa upande gani. Naomba wasimame. Ahsanteni sana na karibuni sana Dodoma. Lakini pia yupo binti wa Waziri Tamica Chikawe. Karibu sana. *(Makofi)*

Sasa moja kwa moja nimwite Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Moja kwa moja nitambue uwepo wa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Mohamed Chande, Kiongozi wa Mhimili wa Mahakama na Viongozi Waandamizi wa Sekta ya Sheria wote. Huwa inatupa faraja kila mara mnapokuwa mmekuja Bungeni kutupa *support*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kusoma hotuba yangu rasmi ya bajeti niruhusu nitoe pole zangu kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa msiba uliokupata hivi karibuni wa kufiwa na dada yako na pia kwa Mheshimiwa Stephen Masato Wasira kwa kumpoteza mama yake mzazi. Haya yote ni mapenzi ya Mungu. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Daktari Jakaya Mrisho Kikwete kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kuniteua kwa mara ya pili kuongoza Wizara ya Katiba na Sheria na kwa kumteua Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa imani aliyoionesha kwetu na tunamhakikishia kwamba tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa kwa kushirikiana na watumishi wenzetu na wadau wengine wote ndani na nje ya Serikali kufanikisha malengo ya Wizara aliyotukabidhi ili kuleta maendeleo ya Taifa letu. Natoa pongezi kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri

walioteuliwa, tunaahidi kushirikiana nao katika ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Nachingwea kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyonayo. Naahidi kuendelea kushirikiana nao katika azma ya kuleta maendeleo kwa ujenzi wa Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Vile vile naishukuru familia yangu kwa imani na uvumilivu wanaouonesha wakati wote ambao nakuwa mbali nao nikiwa katika shughuli za ujenzi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum (CCM); Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri wao ambao umetuwezesha katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na umetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni Hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe pongezi za dhati kwa Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Mbunge wa Mpanda Mashariki; Waziri Ofisi ya Rais, Uratibu na Mahusiano, Mheshimiwa Steven Masatu Wasira na Mbunge wa Bunda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Daktari William Augustano Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Waheshimiwa Mawaziri wengine wote walionitangulia kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa dira katika kutekeleza masuala ya Mipango na Uchumi na

kusimamia Mapato, Matumizi na shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao waliyoitoa wakati wakijadili hotuba za Mawaziri walionitangulia. Maoni na Ushauri wao ni chachu kwetu sote katika jitihada za kuliletea maendeleo Taifa letu. Pongezi kwa Spika na Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna wanavyoliongoza Bunge kwa Busara na Hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii pia kutoa salamu za pole kwa ndugu na familia za Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine wote wa kisiasa na kijamii ambao wamefiwa na ndugu jamaa na marafiki. Kwa wale ambao ni wagonjwa tunawaombea Mungu wapone haraka na warejee kwenye shughuli za ujenzi wa Taifa letu na kwa waliotangulia mbele ya haki tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuiwezesha Wizara yangu kusimamia mchakato wa mabadiliko ya Katiba, Muundo wa Wizara yangu umerejewa ili kukidhi zoezi la uratibu wa mabadiliko ya Katiba. Muundo huu umehuishwa kwa kuanzisha Idara mpya ya Katiba na Usimamizi wa Utoaji Haki *(Constitution and Justice Monitoring Division).* Vile vile, ili kulipa msukumo eneo la uchambuzi wa Mikataba, Muundo wa Ofisi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali umehuishwa kwa kuongezewa Idara kamili ya Mikataba *(Contracts and Treaties Division)* na Idara ya Uendeshaji wa Kesi na Uendeshaji wa Majadiliano *(Litigation and*

*Arbitration).* Marekebisho haya yanalenga kuboresha Mfumo wa Utoaji Haki na Utawala wa Sheria nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Wizara; Wizara yangu kwa mujibu wa Muundo wake inatekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kusimamia Mambo ya Katiba;

(b) Kuiwezesha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kukusanya na Kuratibu maoni ya wananchi kwa ajili ya kuandaa Katiba mpya;

(c) Kuandaa, kufuatilia na kutathmini sera za utawala wa kisheria na kusimamia masuala ya haki za binadamu nchini;

(d) Kusimamia uendeshaji na kufuatilia mfumo wa Utoaji wa Haki;

(e) Kusimamia uandishi na marekebisho ya Sheria;

(f) Kuandaa, kutoa ushauri katika majadiliano kwenye masuala ya Mikataba;

(g) Kusimamia uendeshaji wa Mashtaka ya Jinai na Mashauri ya Daawa nchini na Mashauri ya Kikatiba;

(h) Kuitetea Serikali inaposhtaki au kushtakiwa katika Mahakama za nchini na nje ya nchi;

(i) Kusimamia Sheria inayohusika Ubadilishanaji wa wahalifu wa Mashtaka ya jinai;

(j) Kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa jamii;

(k) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara;

(l) Kusimamia Shughuli zinazohusu masuala ya Sera; Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Kurekebisha Sheria, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Chuo cha Uongozi wa Mahakama na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini yaani *(RITA)*; na

(m) Kusimamia ufanisi na uendelezaji wa watumishi walioko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na malengo kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendesha Mfuko wa Mahakama kwa ajili ya usikilizaji wa mashauri yaliyoko Mahakamani katika ngazi zote;

(b) Kuimarisha na kujenga uwezo wa Divisheni ya Huduma za Kisheria kwa Umma;

(c) Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Mapambano dhidi ya Rushwa;

(d) Kusimamia usikilizaji na uendeshaji wa mashauri ya jinai na daawa nchini katika Mahakama za ngazi zote;

(e) Kuimarisha utoaji wa ushauri wa kisheria nchini katika masuala ya Mikataba, Katiba na haki za binadamu, Uandishi na urekebu wa sheria na kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya jinai na madai ndani na nje ya nchi;

(f) Kufanya tafiti na mapitio ya sheria mbalimbali;

(g) Kusimamia haki za binadamu na utawala bora;

(h) Kuviimarisha na kuviboresha vyuo vya Mafunzo cha Uongozi wa Mahakama *(IJA)* na Chuo cha Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(Law School);*

(i) Kuratibu Mchakato wa Katiba Mpya;

(j) Kutoa elimu kwa Umma juu ya Katiba na Haki za Kikatiba;

(k) Kuimarisha shughuli za Usajili, Ufilisi na Udhamini;

(l) Kupata Ufumbuzi wa Mlundikano wa Mahabusu Magerezani;

(m) Kuboresha mazingira ya kazi na maendeleo ya watumishi; na

(n) Kutekeleza masuala mtambuka ya UKIMWI, jinsia na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia malengo tuliyojiwekea, Wizara yangu imeendelea kutekeleza

majukumu yake ya Sera, Uratibu, Usimamizi na Tathmini za utekelezaji wa majukumu haya kupitia taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza mlundikano wa kesi. Mfuko wa Mahakama, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mfuko wa Mahakama ulioanzishwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011 umeanza kuonesha mafanikio katika Mahakama zetu. Mfuko huu umepokea kiasi cha Sh. 14,735,835,097.97 kati ya Sh. 20,000,000,000/= zilizokuwa zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Fedha hizi zimetumika katika kuwezesha uendeshaji wa mashauri katika Mahakama za ngazi zote kulingana na uwiano wa majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mahakama ya Rufani ilikuwa na jumla ya mashauri 2,786 ambayo yalijumuishwa pamoja na mashauri ya mwaka 2010/2011. Kati ya hayo mashauri 2,059 yalikuwa ya mwaka wa fedha 2010/2011 na mashauri 727 yalipokelewa kwa mwaka 2011/2012. Kati ya haya, mashauri 1,043 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi, hii ni sawa na asilimia 143 ya mashauri yote yaliyopokelewa. Hii ina maana kuwa Mahakama hiyo imedhibiti uzalishwaji wa mlundikano wa mashauri kwa asilimia 100 na kupunguza mlundikano wa mashauri uliokuwepo kwa asilimia 43. Kupungua kwa mlundikano wa mashauri kumetokana na kuwepo kwa fedha za Mfuko wa Mahakama zilizowezesha kufanyika kwa vikao 26 ikilinganishwa na vikao 21 vilivyofanyika mwaka 2010/2011. Mashauri yanayoendelea kusikilizwa ni 1,743.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu ilikuwa na Mashauri 14,935, kati ya hayo 10,718 yalikuwa bakaa ya mwaka wa fedha 2010/2011 na mashauri 4,217 yalipokelewa kwa mwaka 2011/2012. Kati ya haya, mashauri 5,198 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi sawa na asilimia 142 ya mashauri yote yaliyopokelewa. Kati ya Mashauri 6,024 yaliyosikilizwa, Mashauri 826 yalisikilizwa kwa kutumia fedha ya Mfuko wa Mahakama. Hii inaonesha kuwa Mahakama hiyo imedhibiti ongezeko la mlundikano wa mashauri kwa asilimia 100 na kupunguza mlundikano wa mashauri uliokuwepo kwa asilimia 42. Mashauri 8,911 yamebaki na yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi ilianza mwaka wa fedha 2011/2012 ikiwa na Mashauri 1,507 yaliyobaki kutoka mwaka wa fedha 2010/2011 na ilipokea mashauri mapya 669 na kufanya jumla ya mashauri kuwa 2,176. Mashauri 938 yalisikilizwa na kuhitimishwa sawa na asilimia 140 ya mashauri yote yaliyopokelewa mwaka jana. Kati ya Mashauri 938 yaliyosikilizwa, Mashauri 400 yalisikilizwa kwa kutumia fedha ya Mfuko wa Mahakama. Mahakama hiyo imedhibiti ongezeko la mlundikano wa mashauri kwa asilimia 100 na kupunguza mlundikano wa mashauri uliokuwepo kwa asilimia 40. Mashauri 1,238 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mahakama Kuu, Divisheni ya Ardhi ilikuwa na mashauri 5,083 yaliyosalia mwaka wa fedha 2010/2011 na ilipokea mashauri mapya 1,788 na kufanya jumla ya mashauri kuwa 6,871. Mashauri 1,328 yalisikilizwa sawa na asilimia 74.2 ya mashauri yote yaliyopokelewa mwaka jana. Mashauri 5,543 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu, Divisheni ya Biashara, ilianza mwaka wa fedha 2011/2012 ikiwa na mashauri 268 yaliyobaki kutoka mwaka 2010/2011 na kupokea mashauri mapya 189 hivyo kuwa na jumla ya mashauri 457. Kati ya hayo, mashauri 172 yalitolewa uamuzi sawa na asilimia 91 ya mashauri mapya yaliyopokelewa mwaka jana. Mashauri 285 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kwa kutumia fedha za Mfuko wa Mahakama, Mahakama ya Biashara imeendelea kuboresha miundombinu ya kusikiliza mashauri kwa kununua kompyuta za kurekodi mienendo ya usikilizaji wa Mashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa kurekodi mashauri umeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza uaminifu *(integrity)* na uwazi *(transparency)* katika mwenendo wa mashauri kwani hakuna malalamiko kuhusu uhalisi wa kilichotokea Mahakamani. Pia utaratibu huu umesaidia kuharakisha upatikanaji wa nakala za mwenendo wa mashauri na hukumu pamoja na kuwarahisisishia kazi Majaji wanaosikiliza kesi katika Mahakama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama imeendeleza matumizi ya Teknolojia, Elimu, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa kuanzisha kibanda cha kutoa taarifa kwa wadau au wateja wanabofya kompyuta *(touch screen)* na kupata taarifa zote za kesi bila kuonana na wafanyakazi wa Mahakama. Mpango huu umewezesha watumishi kufanya shughuli zingine badala ya kujibu maswali ya wateja kuhusu taarifa za kesi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara ilianzisha mchakato wa kutayarisha Kanuni za Mwenendo wa Usikilizaji wa Mashauri ya Kibiashara za mwaka 2012, ambazo zimejadiliwa na Wadau na kuwasilishwa kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuzipitia na baadaye kuzichapisha ili zianze kutumika. Sambamba na Kanuni za Mwenendo wa usikilizaji wa mashauri, Mahakama Kuu, Divisheni ya Biashara ilipitia upya Kanuni za Ada ya Kufungua Mashauri kwa nia ya kuondoa malalamiko ya wadau na tayari Kanuni zilizopitiwa zimewasilishwa kwa Jaji Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa na zitaanza kutumika katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama za Hakimu Mkazi, katika mwaka 2011/2012, Mahakama za Hakimu Mkazi zilikuwa na jumla ya mashauri 42,783 kati ya hayo, mashauri 28,592 yalikuwa ya mwaka 2010/2011 na mashauri 14,191 ni ya mwaka wa fedha 2011/2012. Kati ya haya, mashauri 17,781 yalisikilizwa na kuhitimishwa sawa na asilimia 125.2 ya mashauri yote yaliyopokelewa mwaka jana. Hii ina maana kuwa Mahakama hizo zimedhibiti uzalishwaji wa mlundikano wa mashauri kwa asilimia mia moja *(Clearance rate)* na kupunguza mlundikano wa mashauri uliokuwepo kwa asilimia 25.2.(*Clearance rate)*. Ongezeko la kasi hii limetokana na kuwepo kwa fedha za Mfuko wa Mahakama zilizowezesha upatikanaji wa mashahidi pindi walipohitajika. Mashauri 25,002 yaliyobaki, yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama za Wilaya, zilikuwa na mashauri 114,107 mwaka 2011/2012 yakiwemo mashauri 36,612 yaliyobaki mwaka wa fedha 2010/2011 na mashauri mapya 77,495 yalifunguliwa. Mashauri 83,082 yalihitimishwa sawa na asilimia 107 ya mashauri yote

yaliyopokelewa mwaka jana. Mahakama hizo zimedhibiti ongezeko la mlundikano wa Mashauri kwa asilimia 100 *(Clearance rate)* na kupunguza mlundikano wa Mashauri uliokuwepo kwa asilimia saba *(Clearance rate)*. Ongezeko la kasi hii limesababishwa na kuwepo kwa fedha za Mfuko zilizowezesha kusikilizwa kwa mashauri, pamoja na kupatikana kwa mashahidi pindi walipohitajika. Mashauri 31,025 yaliyobakia yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mahakama za Mwanzo zilianza na salio la mashauri 123,647 na kupokea Mashauri mapya 512,308 na kuwa na jumla ya mashauri 635,955. Kati ya hayo, mashauri 510,996 yamesikilizwa sawa na asilimia 99.7 ya mashauri yaliyopokelewa. Hii ina maana kuwa Mahakama hizo zimedhibiti ongezeko la mlundikano wa mashauri kwa asilimia 99.7 *(Clearance rate).* Ongezeko hili la kasi hii limesababishwa na upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Mahakama zilizowezesha kusikilizwa kwa mashauri, pamoja na kutembelea Mahakama za Mwanzo zisizokuwa na Mahakimu. Aidha, ongezeko hilo katika kusikiliza kesi limesababishwa na ajira ya Mkataba ya Mahakimu wastaafu 31 wa Mahakama za Mwanzo. Mashauri 124,959 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusogeza huduma karibu na wananchi, Wizara yangu kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama imefanikiwa kukamilisha ajira 300 za Mahakimu Wakazi, ambao ni wahitimu wa Shahada ya Kwanza ya Sheria na kuwasambaza katika vituo vya Mahakama za Mwanzo katika Wilaya 102. Hatua hii inakusudia kuongeza kasi ya kupunguza mlundikano wa Mashauri katika

Mahakama hizo na kutoa fursa kwa wenye mashauri kuwakilishwa kisheria kwenye Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo waliopo sasa wasiokuwa na shahada wataendelea kutoa huduma kwenye Mahakama hadi hapo watakapokuwa wamejiendeleza zaidi na kupata shahada ya sheria au kustaafu. Aidha, imewapandisha vyeo Mahakimu 73 wa Mahakama za Mwanzo waliopata sifa ya kuwa na Shahada ya Kwanza ya Sheria kuwa Mahakimu Wakazi na Mahakimu hawa watapangiwa katika Mahakama za Wilaya zenye upungufu wa Mahakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Magerezani; katika kushughulikia tatizo la Msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani, Mahakimu pamoja na viongozi mbalimbali wa Mahakama wameendelea kufanya ziara katika Magereza kwa nia ya kufahamu na kuzipatia ufumbuzi shida za mahabusu na wafungwa, ikiwemo kuwapatia dhamana Mahabusu na kutoa adhabu mbadala badala ya kifungo kwa mujibu wa sheria kwa washtakiwa wanaotiwa hatiani, kutoa nakala za hukumu, kufanyia masahihisho na kuhitimisha rufaa za wafungwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni katika kutekeleza dhumuni la Serikali la kupunguza msongamano unaoweza kuepukika, hivyo kuipunguzia Serikali mzigo usiokuwa wa lazima wa kuwahudumia wafungwa pamoja na kuwapa fursa wanaoachiwa huru kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuongeza kipato cha familia zao na Taifa kwa

ujumla. Aidha, kauli mbiu ya Siku ya Sheria mwaka 2012 ilikuwa "Adhabu Mbadala katika Mashauri ya Jinai: Faida zake" Majaji na Mahakimu walikumbushwa umuhimu wa kutumia adhabu za namna hii kwa lengo la kupunguza mlundikano wa wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kurugenzi ya Mashtaka kupitia ziara zake Magerezani kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka ya Mwaka 2008, Sura 430 zimepunguza msongamano wa Mahabusu na wafungwa kutoka 42,832 mwaka 2007 hadi kufikia 35,520 mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kupitia Kurugenzi ya Mashtaka katika mwaka 2011/2012 iliendelea kushiriki katika shughuli za Jukwaa la Taifa la Haki Jinai *(The National Criminal Justice Forum)* kwa kushirikiana na wadau wengine. Lengo ni kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizopo na kuboresha mfumo wa utoaji wa haki – jinai hapa nchini ili haki iweze kupatikana kwa wakati na kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa jambo hili katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kamati Maalum ya Jukwaa la Taifa la Haki – Jinai ilishirikisha Wadau wa Haki – Jinai na kuwahusisha Mawaziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mambo ya Ndani ya Nchi na Ofisi ya Rais, Utawala Bora na kuunda timu ndogo iliyotembelea baadhi ya magereza nchini kutatua baadhi ya kero zilizowahusu wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, izara kupitia Divisheni ya Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea kutekeleza jukumu lake la kuendesha mashtaka ya jinai. Jumla ya Mashauri ya Jinai 174,611 yaliendelea kuendeshwa Mahakamani. Kati ya hayo mashauri 77,981 yalikuwa ni salio la mwaka wa fedha 2010/2011 na Mashauri mapya 96,630 yalipokelewa. Mashauri 107,104 yalihitimishwa sawa na asilimia 61 ya mashauri yote yaliyopokelewa. Mashauri 67,507 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mashauri ya Madai; Kurugenzi ya Madai na Usuluhishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya jitihada kubwa katika kuendesha mashauri ya madai katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na Mahakama za Hakimu Mkazi. Vile vile, Kurugenzi hii iliendesha mashauri ya usuluhishi *(arbitration).* Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mashauri mapya 246 yalipokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kulikuwepo na salio la mashauri 756 ya madai na maombi ya madai 248, hivyo kufanya mashauri ya madai kufikia 1,002. Kati ya hayo, mashauri 73 yalihitimishwa sawa na asilimia 29.67 ya mashauri yaliyopokelewa. Mashauri 929 na maombi ya madai 248 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Katika Mahakama ya Afrika Mashariki yapo Mashauri mawili yanayoendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mashauri ya Kikatiba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Kurugenzi ya Katiba na Haki za Binadamu iliendelea na uendeshaji wa mashauri hayo. Katika mwaka wa fedha 2011/2012,

mashauri 43 ya Kikatiba na yanayohusu Haki za Binadamu yalikuwepo katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani na lilikuwapo shauri moja (1) katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu. Aidha, katika mwaka huu, mashauri matano yamehitimishwa na kubakia mashauri 38. Hii ni sawa na asilimia 11 ya mashauri yote ya Kikatiba yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashauri ya uchaguzi; katika kuimarisha demokrasia nchini, nchi yetu ilifanya Uchaguzi Mkuu mwaka 2010. Kufuatia uchaguzi huo, matokeo ya Ubunge kwenye Majimbo ya uchaguzi 44 yalipingwa, hivyo kusababisha uwepo wa mashauri 44 ya kupinga matokeo ya uchaguzi. Katika Mashauri hayo, Mashauri 20 yalikwisha katika hatua za awali na kubaki mashauri 24. Katika Mashauri hayo, 24 yaliyobakia, mashauri mawili (2) yalifutwa na wadai wenyewe na mashauri nane (8) wadai wake walishindwa kulipa dhamana *(Security for Costs),* hivyo kubaki na mashauri 14 yaliyoendelea kusikilizwa na kuhitimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mashauri 14 yaliyohitimishwa, mashauri mawili (2) matokeo yake yalitenguliwa katika Majimbo ya Arusha Mjini na Sumbawanga Mjini. Serikali imeshinda mashauri 32 na kuokoa kiasi cha fedha cha shilingi bilioni 96 ambazo zingetumika kufanya uchaguzi mdogo wa marudio. Sambamba na mashauri 44 ya uchaguzi mkuu yaliyokuwa yamefunguliwa pia kuna shauri moja (1) lililotokana na uchaguzi mdogo wa Jimbo la Igunga ambalo limefikia katika hatua ya utetezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uratibu wa upelelezi wa makosa ya jinai na uendeshaji wa mashauri makubwa; Divisheni ya Mashtaka iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai, kufungua, kuendesha na kusimamia mienendo ya mashauri mbalimbali Mahakamani. Kati ya mashauri yaliyofunguliwa yapo mashauri makubwa yakiwemo ya uhujumu uchumi *(economic and high profile criminal cases).* Miongoni mwa mashauri hayo makubwa na yenye maslahi kwa umma ni:-

(a) Kuendelea kusikilizwa kwa kesi 14 zinazohusisha wizi wa fedha kutoka katika akaunti ya *EPA* ya Benki Kuu ya Tanzania *(BoT)*. Mashauri hayo yanahusisha wizi wa fedha za Kitanzania zenye thamani ya Shilingi bilioni 36.2 na kati ya mashauri hayo shauri moja (1) limekwishaamuliwa na tunategemea shauri lingine litaamuliwa hivi karibuni;

Mashauri manne yalichelewa kuanza kusikilizwa na hii ilitokana na wahusika waliweka pingamizi kwa kufungua mashauri ya kikatiba. Pia kumekuwa na upungufu wa fedha wa kuendeshea mashauri hasa kwa mashahidi kutoka nje ya nchi. Hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 1.7 kimeokolewa kwa mashauri yaliyokamilika. Vile vile tunatarajia kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 1.36 kwa mashauri yaliyobaki;

(b) Kuendelea kusikilizwa kwa kesi 10 zilizofunguliwa Mahakamani kati ya mwaka 2007 na 2010 zikihusisha wizi au hasara ya Shilingi 323 bilioni;

(c) Kuendelea kusikilizwa kwa kesi 20 za jinai zilizofunguliwa mwaka 2010 na 2011 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu na Arusha kuhusiana na makosa ya

kutakatisha fedha, kula njama ya kutenda makosa na kugushi. Kesi hizi zinahusisha kiasi cha takribani Shilingi bilioni 48.8;

(d) Kusimamia na kuendesha mashauri yanayohusu watu wenye ulemavu wa ngozi *(albino)*. Hadi sasa jumla ya mashauri tisa (9) yameshasikilizwa na Mahakama Kuu na kati ya hayo mashauri nane (8) yamepata uamuzi. Aidha, Wizara yangu ina taarifa ya matukio 57 yaliyoripotiwa na Jeshi la Polisi nchi nzima katika vipindi tofauti. Ni matarajio yangu kwamba upelelezi wa matukio haya utakamilishwa mapema ili sheria iweze kuchukua mkondo wake; na

(e) Kuongeza kasi ya kushiriki katika vita vya kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na Polisi, Usalama wa Taifa, Tume ya Kudhibiti Biashara Haramu ya Dawa za kulevya na vyombo vingine. Ushirikiano huu wa vyombo vya dola umeongeza uwezo wa kukamata shehena kubwa ya dawa za kulevya kuanzia mwaka 2010 hadi mwezi Mei 2012, umeboresha mbinu za kipelelezi na mikakati ya kimashtaka lengo ikiwa ni kuzuia na kutowapa fursa wahalifu wa biashara hii kuendeleza vitendo vyao.

Matukio makubwa yaliyotokea yanahusisha dawa za kulevya zenye thamani ya kiasi cha takribani Shilingi 26.5 bilioni na kuna kesi zinaendelea katika Mahakama za Dar es Salaam, Tanga, Mbeya na Lindi. Lengo la kufunguliwa mashauri haya ni kuwaadhibu washtakiwa na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa *(asset forfeiture and recovery).*

Mheshimiwa Naibu Spika, utenganishaji shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka katika kuongeza jitihada

za upatikanaji wa haki kwa wote na kwa wakati pamoja na hatua zilizochukuliwa za kuanzisha ofisi za mikoa katika mikoa mbalimbali, Kurugenzi ya Mashtaka iliendesha Mashtaka katika Mahakama 17 za Hakimu Mkazi katika mikoa ambayo tayari kuna Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, hadi kufikia sasa, Kurugenzi ya Mashtaka imekuwa ikiendesha mashauri katika Mahakama 18 za Wilaya zilizopo katika Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika jitihada za kuendeleza Mpango huu ofisi imekwishaandaa utaratibu wa kuajiri Mawakili wa Serikali 115 ambao watapangwa kwenye ofisi za mikoa mbalimbali. Mpango huu wa Kutenganisha Shughuli za Upelelezi na uendeshaji wa Mashtaka umeonesha mafanikio makubwa na kusaidia kupunguza idadi ya kesi zinazofunguliwa Mahakamani ambapo mashauri hufunguliwa tu pale panapokuwepo na ushahidi wa kutosha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu, mwaka 2007, jumla ya mashtaka 2,055 yalifunguliwa kabla ya kuanza mpango huu ikilinganishwa na mashtaka 301 yaliyofunguliwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uimarishaji wa utoaji wa ushauri wa Kisheria nchini; Wizara imeendelea kuimarisha uandaaji wa mikataba yenye manufaa kwa maendeleo ya Taifa, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Taasisi, Serikali za nchi nyingine na mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa mikataba iliyohusisha maeneo ya kiuchumi na kijamii. Jumla ya mikataba 583 ilishughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ofisi hii ilihusika katika majadiliano ya moja kwa moja kwa kutoa ushauri wa kisheria kuhusu mikataba ya ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kushiriki katika mikutano ya majadiliano yanayohusu shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East Africa Community),* Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*, Umoja wa Afrika *(AU)*, Jumuiya ya Madola, Umoja wa Mataifa *(UN)* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utayarishaji wa Miswada ya Sheria, Hati za Serikali na Tafsiri ya Sheria, katika lengo la kuhakikisha kuwa Sheria zinazokuwepo zinakidhi mahitaji ya sasa ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitekeleza kazi zake za kuandaa Miswada ya Sheria na kuwasilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kupitishwa kuwa Sheria za nchi. Vile vile, kwa kushirikiana na Wizara, Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine, ofisi hii iliendelea kutayarisha sheria ndogo ndogo na maazimio yanayotokana na mikataba ya Kimataifa ambayo Serikali imeingia. Jumla ya Miswada ya Sheria 18 ya Serikali iliandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Miswada hiyo, Miswada tisa ilipitishwa na Bunge kuwa Sheria za nchi na Miswada tisa iliyobaki inaendelea kufanyiwa kazi ukiwemo Muswada wa fedha utakaowasilishwa Bungeni mwezi Agosti, 2012. Kati ya sheria zilizopitishwa, sheria 29 zilifanyiwa marekebisho. Aidha, Sheria ndogo ndogo 501 ikiwa ni pamoja na hati za Serikali zimeandaliwa, kuhakikiwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. Vile vile, Sheria tisa zimetafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili. Aidha, kazi ya kuzipatia Sheria namba za Sura

imeendelea kufanyika ambapo mpaka sasa idadi ya Sura za Sheria za nchi imefikia Sura 433.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa masuala ya Haki za Binadamu yanapewa umuhimu, Ofisi iliandaa na kuwasilisha taarifa ya nchi ya utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu nchini kwenye Baraza la Umoja wa Mataifa nchini Uswisi ambayo ilijadiliwa mwezi Oktoba, 2011. Taarifa hii inatoa taswira ya jinsi gani Serikali imekuwa ikiendesha shughuli zake kwa kuzingatia masuala ya haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo, Baraza lilitoa mapendekezo 24 ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji ifikapo mwaka 2016. Aidha, rasimu ya Mpango Kazi wa utekelezaji wa mapendekekezo hayo 24 yaliyotolewa na Baraza la Umoja wa Mataifa, Haki za Binadamu *(Universal Periodic Review Mechanism (UPR)* imeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia haki za binadamu na utawala bora, Serikali kupitia Kurugenzi ya Katiba na Haki za Binadamu, ilishiriki katika maandalizi ya taarifa ya nchi ya utekelezaji wa masuala ya utawala bora na Haki za Binadamu Kitaifa ambao ulisimamiwa na Umoja wa Afrika (*African Peer Review Mechanism)* na kuhakikiwa na Timu iliyoteuliwa na Umoja huo mwezi Machi, 2012. Taarifa hiyo inatarajiwa kujadiliwa tena kwenye kikao cha Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika kitakachofanyika mwezi Julai, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliendelea kushughulikia kero za wananchi kwa kupokea na kufuatilia malalamiko, kutoa ushauri wa kisheria kuhusu haki za binadamu, kufanya uchunguzi na utafiti juu ya masuala yanayohusu Haki za Binadamu na Utawala Bora. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ilishughulikia malalamiko 7,833 yaliyobaki mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ilipokea malalamiko 886 na kufanya jumla ya Mashauri kuwa 8,719. Kati ya hayo, malalamiko 372 yanahusu ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, malalamiko 112 yanahusu uvunjwaji wa haki za binadamu na malalamiko 402 yalikuwa nje ya mamlaka ya Tume. Jumla ya malalamiko 1,554 yalifanyiwa uchunguzi na kuhitimishwa na kubaki Mashauri 7,165 yanayoendelea kusikilizwa. Idadi hii ni sawa na asilimia 18% ya malalamiko yote yaliyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Tume kwa kushirikiana na *UNICEF* ilikamilisha taarifa ya uchunguzi wa hali za watoto walio katika vizuizi (magereza, vituo vya polisi, mahabusu za watoto na shule ya maadilisho) uliofanyika katika mwaka wa fedha 2010/2011 kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria *(LSRP)*. Katika taarifa hiyo ilibainika kwamba kuna uvunjifu wa haki za watoto ikiwa ni pamoja na watoto kuchanganywa na watu wazima na kukosa huduma muhimu za kijamii na kisheria. Taarifa hii ilijadiliwa na wadau na kupanga mkakati wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitoa huduma ya ushauri wa kisheria kuhusu haki za binadamu kwa wananchi wapatao 700 na inasimamia malalamiko 14 Mahakamani. Aidha, Tume kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya Kiserikali ijulikanayo kama *SAJEA* imetoa msaada wa kisheria kwa watu 300 wanaoishi na virusi vya UKIMWI katika Wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii pia imefanya uchunguzi wa wazi kuhusu uhamishaji wa wananchi katika makazi au ardhi yao uliofanyika katika Wilaya 42 nchini. Kati ya hizo Wilaya sita ni za Zanzibar. Uchunguzi huu ulilenga kubaini athari za uhamishaji wananchi katika maeneo yao na utaratibu wa malipo ya fidia ili kuishauri Serikali njia bora za kumaliza matatizo hayo. Taarifa ya uchunguzi huo itawasilishwa katika mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wadau mbalimbali imekamilisha Rasimu ya Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu *(The National Human Rights Action Plan for the Promotion and Protection of Human Rights).* Aidha, rasimu hiyo inatarajiwa kuwasilishwa kwa njia ya Waraka kwenye Baraza la Mawaziri. Mpango huu utaweka dira na kuainisha mikakati ya kukuza, kulinda na kutetea haki za binadamu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Kimataifa, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imefanikiwa

kupata daraja ‘A’ miongoni mwa Taasisi za Kitaifa za haki za binadamu katika tathmini inayofanywa na Kamati ya Kuratibu Ukuzaji na Kamati ya Kimataifa ya Kuratibu Ukuzaji na Utetezi wa Haki za Binadamu *(The International Coordinating Committee on the Promotion and Protection of Human Rights).* Hii imeipa nchi heshima mbele ya Jumuiya ya Kimataifa katika kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mpango wa Serikali Wazi; Tarehe 20 Septemba 2011 huko New York Marekani, ulizinduliwa Mpango wa Dunia wa Serikali Wazi *(Open Government Partnership*) ambapo nchi yetu ikiongozwa na Rais Daktari Jakaya Mrisho Kikwete ilionesha nia ya kujiunga na mpango huo. Mwezi Desemba mwaka jana Tanzania ilijiunga rasmi na mpango huu na Machi 2012 katika mkutano wake mkuu wa kwanza, Tanzania ilipata fursa ya kuingia katika Kamati Tendaji ya mpango huu wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano huu Rais wetu alipewa heshima ya pekee ya kutoa hotuba elekezi. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya bajeti, mpango wa Serikali wazi unahimiza uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa uwazi, uadilifu, utawala bora, kupambana na rushwa na kuzingatia ushirikishwaji mpana wa wananchi, ubunifu na matumizi ya TEHAMA ili kuwa na usimamizi bora wa matumizi ya rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya upangaji na uanzishwaji mpango huu hapa nchini, ulikuwa unasimamiwa na Ofisi ya Rais, Ikulu. Katika hatua ya utekelezaji, usimamizi wa mpango huu umehamishiwa

katika Wizara yangu. Aidha, katika mwaka huu wa fedha Serikali imeamua kuzipa kipaumbele sekta tatu muhimu na kuzifanya ziweke miundombinu muhimu ya uendeshaji wa sekta hizo kwa uwazi zaidi na kutoa taarifa zote muhimu kwa wananchi ili ziweze kuwasaidia kujiletea maendeleo yao wenyewe. Sekta hizi ni Afya, Maji na Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Kazi wa Kitaifa ambao tayari umekubaliwa na washirika wenzetu wa mpango huu utaanza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha hususan katika sekta hizo tatu. Katika mwaka unaofuata wa fedha tutateua sekta zingine tatu ambazo tutaziundia miundo mbinu itakayozifanya zitoe taarifa nyingi na wazi zaidi kwa wananchi. Makusudio yetu ni kuwa, baada ya muda wa miaka minne, tutaweka mfumo huu wa Serikali wazi katika sekta zote ili hatimaye mfumo wa Serikali wazi uwe ndiyo utaratibu wa kawaida wa kuendesha Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha tunakusudia kuleta ndani ya Bunge lako Tukufu, Sheria ya Uhuru wa Habari *(Freedom of Information law).* Sheria hii itakuwa katika viwango vya Kimataifa na itakuwa ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa mfumo mzima wa Serikali wazi nchini. Msingi wa sheria hii si uhuru wa kupata habari kwa magazeti au vyombo vya habari peke yao, bali ni uhuru wa wananchi wao wenyewe kupata habari muhimu zinazohusu maendeleo yao katika ngazi zote kuanzia katika Serikali Kuu ambako ndiko kuna habari nyingi sana hadi kufikia vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mabadiliko ya Katiba, kabla sijaelezea zaidi kuhusu Tume ya Mabadiliko ya Katiba, niruhusu nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais, Daktari Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kusikiliza kilio cha Watanzania cha kutaka Katiba mpya na kuchukua uamuzi wa kuanzisha mchakato madhubuti ili kufikia lengo hili. Uamuzi wake huu unaendelea kuthibitisha ni jinsi gani Rais Kikwete anavyowapenda na kuwathamini Watanzania na mawazo yao. Kwa hakika Mheshimiwa Rais Kikwete ni mtu wa watu.

Mheshimiwa Spika napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Tume ya Mabadiliko ya Katiba, imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 kwa madhumuni ya kukusanya na Kuratibu maoni ya wananchi juu ya Katiba mpya. Tume hii ilianza kutekeleza majukumu yake rasmi tarehe 1/5/2012 baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya uteuzi wa Wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Katibu na Naibu Katibu wa Tume na vilevile kuundwa kwa Sekretarieti ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu imefanya maandalizi yenye lengo la kuhakikisha kuwa mchakato mzima unatekelezwa kama ilivyokusudiwa na kwamba Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapatikana ifikapo tarehe 26 Aprili 2014 siku tutakapokuwa tunasherehekea miaka 50 ya muungano wetu mtukufu. Natambua kwamba jukumu tulilokabidhiwa ni zito, muhimu na nyeti sana kwa Watanzania wote na sisi tunaahidi kulitekeleza jukumu hili kwa wakati na kwa nguvu na uwezo wetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Tume imeshaanza Awamu ya Kwanza ya kazi yake, yaani kukusanya na kuratibu maoni ya wananchi. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mpaka leo hii kazi hii inaendelea vizuri katika mikoa yote minane ambako zoezi hili linaendelea. Baada ya kumaliza kukusanya maoni katika nchi nzima, hapo itafuata Awamu ya Pili ya kuandaa taarifa, mapendekezo na Rasimu ya Katiba. Aidha, Tume itakutana na Mabaraza ya wananchi katika nchi nzima ili kuweza kuijadili Rasimu ya Katiba ambayo hatimaye itawasilishwa kwenye Bunge Maalum kwa lengo la kuijadili na kuipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo na majukumu ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imepewa Fungu namba 8 (*Vote* 8) kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku na pia imegawanywa katika vitengo saba ili kufanikisha utendaji wa shughuli zake. Vitengo hivyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kitengo cha Utawala na Rasilimali Watu;
(b) Kitengo cha Fedha na Uhasibu;

(c) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;

(d) Kitengo cha Huduma za Ugavi na Manunuzi;

(e) Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;

(f) Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma; na

(g) Kitengo cha Kuratibu Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majukumu Tume hii imepewa Majukumu yafuatayo:-

(a) Kuandaa na kuendesha programu za kuelimisha jamii juu ya madhumuni na majukumu ya Tume;

(b) Kukusanya na Kuratibu maoni ya wananchi;

(c) Kuitisha na kusimamia mikutano au mabaraza katika sehemu na nyakati mbalimbali kama ambavyo itaamua;

(d) Kutathmini na kuchambua kwa kutofautisha maoni ya wananchi yanayokubaliana na yale yasiyokubaliana;

(e) Kupitia na kuchambua michango, mawazo, maoni, taarifa na mapendekezo yaliyokusanywa na kufanyiwa tathmini siku za nyuma;

(f) Kupitia na kutafiti usahihi na ulinganifu wa masharti ya kikatiba yanayohusu mamlaka ya wananchi, mifumo ya kisiasa, demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora;

(g) Kuruhusu mtu yeyote kufika mbele ya Tume kufanya majadiliano, kwa mazungumzo au kuwasilisha nyaraka, kuhusu jambo lolote la kikatiba ambalo Tume inaona ni muhimu na linahusiana na mchakato wa mapitio ya Katiba;

(h) Kushughulikia jambo lolote kama itakavyoona inafaa katika kutekeleza majukumu yake;

(i) Kuchapisha Rasimu ya Katiba katika Gazeti la Serikali na magazeti mengine ili kutoa fursa kwa wananchi kusoma na kutoa maoni zaidi kwa Tume kupitia Mabaraza ya Katiba;

(j) Kutayarisha na kuwasilisha ripoti itakayojumuisha:-

(i) Muhtasari wa maoni ya wananchi kwa kila hadidu ya rejea;

(ii) Mapendekezo ya Tume kwa kila hadidu ya rejea;

(iii) Ripoti za wataalamu/washauri waelekezi ambao Tume iliwatumia;

(iv) Rasimu ya Katiba; na

(v) Taarifa nyingine muhimu.

(k) Kuwasilisha ripoti ya Tume kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar; na

(l) Kuwasilisha Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Katiba na Sheria kwa niaba ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliandaa Bajeti ya Tume ya miezi mitatu ambayo ilijumuishwa katika vifungu vya Wizara. Serikali imetoa jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani lililopo Mtaa wa Ohio, mkabala na Hoteli ya Serena kwa ajili ya Ofisi ya Tume. Kwa upande wa Zanzibar, Tume ya

Mabadiliko ya Katiba imepata Ofisi katika jengo la Mfuko wa Barabara lililopo Mtaa wa Kikwajuni/Gofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya ufanyaji kazi, tulitambua umuhimu wa elimu kwa umma kuhusu mambo yatakayozingatiwa katika Katiba. Ni wazi kuwa wananchi hawawezi kutoa maoni yao kwa ukamilifu bila ya kuwa na elimu ya kutosha. Kwa hiyo, kwa kuzingatia umuhimu huo, Tume imetumia muda wa kutosha kuandaa na kupata nyaraka muhimu kwa ajili ya elimu kwa umma. Nyaraka hizo ni pamoja na nakala 500,000 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977, nakala 10,000 za Katiba ya Zanzibar ya 1984 na nakala 500,000 za Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83. Aidha, Tume inaendelea kuandaa Katiba za vidutu nakala 500 ili kuwashirikisha wananchi ambao ni walemavu wa macho nao watoe maoni yao katika mchakato huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kwamba nyaraka hizi hazitoshi na hata kama zikipatikana kwa wingi ni vigumu kwa wananchi kuzisoma na kuzielewa kwa urahisi, Tume imeandaa vijitabu na vipeperushi ambavyo vimeandikwa kwa lugha rahisi kwa ajili ya kuvisoma na kuvielewa. Nyaraka hizi zimeanza kusambazwa mikoani na leo hii Waheshimiwa Wabunge nanyi mtakabidhiwa nyaraka zote hizi ili msaidie kuwaelimisha wananchi katika Majimbo yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Tume imeendelea kuweka mazingira mazuri yatakayowawezesha wenye ulemavu wa kusikia kushiriki katika mchakato wa kutoa maoni yao kuhusu Katiba mpya kwa kuanzisha matumizi ya lugha ya alama katika mikutano itakayofanywa na Tume.

Tume imejenga mahusiano mazuri na Chama cha Walemavu hawa na wamekubaliana kufanya kazi kwa karibu ili kufanikisha ushiriki wa wanachama hao katika mchakato wa kupata Katiba mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti na Mapitio ya Sheria za Nchi, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ilipanga kuendelea kukamilisha miradi ya utafiti wa Sheria za Kilimo, Mifugo, Mfumo wa Haki za Madai, Sheria ya Mfumo wa Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na kupitia hukumu za Mahakama ya Rufani na za Mahakama Kuu ili kubainisha hoja za kisheria zilizojadiliwa na kuziweka katika Tovuti ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Hali halisi ya utekelezaji wa maeneo hayo ilikuwa ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imefanikiwa kuandaa ufupisho wa Sheria za Kilimo zipatazo 22 *(Compendium)* kwa ajili ya kuwarahisishia watumiaji wa sheria hizo na pia kuwajengea uwezo wadau katika kuchangia kutoa maoni ya maboresho ya sheria. Aidha, Tume inaendelea kuandaa ufupisho wa Sheria za Mifugo *(Compendium)* kwa ajili ya kuwarahisishia uelewa na rejea watumiaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Tume imeendelea kufanya mapitio na utafiti kuhusiana na sheria zinazosimamia sekta ya mifugo katika Mikoa ya Arusha (Wilaya ya Arusha Mjini, Ngorongoro, Longido na Monduli), Manyara (Wilaya ya Babati na Hanang), Dodoma (Wilaya ya Dodoma Mjini na Kongwa) na Mwanza (Wilaya ya Kwimba). Utafiti huo utatengeneza mfumo wa sheria utakaoongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Utatuzi na Usuluhishi wa Migogoro ya Ardhi uliopo sasa unashughulikiwa na Wizara tatu, ambazo ni Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Katiba na Sheria. Mfumo huu umeonekana una mapungufu katika kusuluhisha migogoro ya ardhi. Kutokana na mapungufu hayo, Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya utafiti wa Sheria za Ardhi katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Arusha, Mwanza, Kagera, Dar es Salaam, Morogoro na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kuzifanyia mapitio Sheria zinazohusu mfumo wa madai *(Civil Justice System)*kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wote na kuwepo kwa mfumo wa haki ya madai kwa mujibu wa Ibara ya 107A(2)(a)-(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inatoa msisitizo katika utoaji wa haki kwa wote bila ya kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi na kutochelewesha haki bila sababu ya msingi, kutoa fidia ipasayo kwa watu walioathirika kutokana na makosa ya watu wengine, kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro na kutoa haki bila ya ugumu wa utekelezaji. Sheria hizo ziko nane (8) zikiambatana na kanuni nane (8). Tume imekwishaandaa taarifa ambazo wadau mbalimbali wa sheria wamezipitia na kutoa maoni yao juu ya sheria zilizoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria, Tanzania imeweza kuchambua hukumu za mashauri ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania ili kubainisha misingi ya kisheria *(legal principles)* iliyoainishwa kwenye hukumu hizo

na kuziweka katika tovuti ya Tume ya Kurekebisha Sheria ili kuwarahisishia wadau mbalimbali katika masuala ya kisheria. Tume imeweza pia kutafsiri rasimu za sheria tano (5) kwa Kiswahili ili kuwarahisishia watumiaji walio wengi kuelewa sheria za nchi na ili waweze kuzitumia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Tume imetafsiri sheria 13. Kwa mwaka huu wa fedha, Tume imetafsiri; Sheria ya Polisi na Huduma Saidizi (Sura ya 322, Toleo la mwaka 2002), Sheria ya Huduma za Jamii (Sura 291, Toleo la 2002) na Sheria ya Magazeti (Sura 229, Toleo la 2002), Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Sheria ya Ukomo wa Mashauri ya Mwaka 1971.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, (*RITA*), imeendelea kuimarisha shughuli za usajili, ufilisi na udhamini. Wakala umeendelea kusogeza huduma za usajili kwa wananchi hususan walioko vijijini na kuendesha kampeni za uhamasishaji ambapo ulifanikiwa kusajili vizazi 403,850, vifo 48,997, ndoa 13,631, talaka 51 na watoto wa kuasili 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wakala umefanikiwa kusajili miunganisho ya wadhamini ipatayo 204, kuandika na kuhifadhi wosia zipatazo 33. Sambamba na hilo, Wakala ulifunga mirathi miwili na kupokea mirathi moja. Hali kadhalika, Wakala umeanza kutekeleza mradi wa kuandikisha watoto walio na umri chini ya miaka mitano ambao utatekelezwa kwa awamu tatu. Mradi huu umeanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa ufadhili wa *UNICEF*.

Kwa kuanzia, Wakala umeanza kuandikisha watoto katika Wilaya ya Temeke kwa majaribio katika Kata 14, zoezi linalotarajiwa kukamilika mwezi wa Julai, 2012. Awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi itahusisha Mikoa mitano ambayo ni Mbeya, Mwanza, Geita, Shinyanga na Simiyu pamoja na Kata 16 zilizobaki katika Wilaya ya Temeke. Awamu ya tatu ya mradi, itahusisha Mikoa yote ya Tanzania Bara. Wakala unaendelea kutekeleza mpango huo ambao ni mkakati wa kupunguza mlundikano wa vizazi ambavyo havijasajiliwa kwa kusajili na kutoa vyeti kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano na waliomo shuleni kupitia mradi wa *U5BRI – Under five birth registration initiatives.* Mradi wa Majaribio umetekelezwa Wilaya ya Temeke na unakamilika leo hii. Lakini mradi wenyewe unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa jukumu la ufilisi wa mali za *IPTL* uliendelea kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria na Taratibu. Hata hivyo, shughuli ya ufilisi ilisitishwa kwa amri ya Mahakama Kuu ili kusubiri maamuzi ya pingamizi zilizowasilishwa na wadeni wa kampuni ya *IPTL*. Wakala pia ulifanya mapitio ya Sheria mbalimbali zinazohusu masuala ya ufilisi wa mali za makampuni kwa lengo la kuwa na sheria moja itakayosimamia masuala ya ufilisi katika mazingira ya sasa ya kibiashara ambapo rasimu ya awali ya taarifa ya mapitio ya sheria hizo imekamilishwa kwa ajili ya kujadiliwa na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia wakala *(RITA)* kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* unaendelea na zoezi la usimamizi wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi za Wakala ambao unatarajiwa

kumalizika mwaka 2013. Ujenzi huo utakapokamilika, utaboresha utoaji huduma za Wakala kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha na kuiwezesha Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(Law School of Tanzania)*, Wizara yangu kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria nchini (*LSRP*), imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa majengo ya kudumu ya Taasisi hiyo katika kiwanja Na. 2005/2/1 mkabala na Barabara ya Sam Nujoma, Dar es Salaam. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group Company* kwa gharama ya Shilingi bilioni 16.1 ambapo hadi sasa Shilingi bilioni 10.8 zimekwishalipwa na ujenzi umekamilika kwa asilimia 95.

Ni matumaini yangu kuwa, ujenzi huu utakapokamilika, utaiwezesha Taasisi hii kuwa na majengo ya kisasa kwa ajili ya madarasa, kumbi za mihadhara, maktaba, utawala, ukumbi wa mikutano na chakula na Mahakama ya Mazoezi. Hivyo basi, Taasisi hii itakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi wasiopungua 2,000 kila mwaka na kuweza kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa ubora na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania ilipozindua mafunzo yake mwezi Machi, 2008, imedahili wanafunzi 2,570 katika Makundi *(cohorts)* 11. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Taasisi imesajili wanafunzi 486 ikilinganishwa na lengo la kusajili wanafunzi 600. Wanafunzi 321 waliokuwa wanaendelea na mafunzo walihudhuria mafunzo kwa vitendo *(field placement)* katika sehemu mbalimbali za kazi nchini.

Aidha, Taasisi ilianza kutumia Mtaala mpya wa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo baada ya kuhuishwa sambamba na Kanuni mpya za kuendesha mafunzo. Kanuni hizo zilipitishwa kwa nia ya kuboresha mfumo wa utoaji mafunzo na upimaji wa wanafunzi katika mitihani. Pia, Taasisi iliendeleza ushirikiano na Shirika la Mawakili la Uingereza liitwalo *International Senior Lawyers,* ambapo mawakili wa kujitegemea *(solicitors and barristers)* kutoka nchi za Marekanai na Uingereza na kwingineko walitoa mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mawakili Wahadhiri wa hapa nchini. Ushirikiano huu uliwezesha kutoa mafunzo kwa viwango vya Kimataifa hususan kwenye maeneo ya Uandishi wa Mikataba na Hati za Kisheria (*Legal Drafting Skills*), Mwenendo wa Mashauri ya Jinai *(Criminal Procedure and Practice),* Mbinu za Uwakili *(Advocacy skills)* na Mwenendo wa Mashauri ya Madai *(Civil Procedure and Practice).* Aidha, chini ya ushirikiano huu, wahadhiri 22 wa Taasisi hii walipata mafunzo ya ufundishaji *(Trainer Training)* mwezi Aprili, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa baadhi ya wanafunzi wengi wanaojiunga na Taasisi hii hawana uwezo wa kugharamia mafunzo yao na kwamba Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya mwaka 2004 hairuhusu wanafunzi hao kupata mikopo kwa ajili ya kugharamia mafunzo, Serikali imekuwa ikitoa fedha kupitia Wizara yangu kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi wahitaji. Mikopo hii inasimamiwa na Bodi ya Uendeshaji wa Taasisi hii. Tangu Taasisi ianze kutoa mafunzo hadi sasa, wanafunzi 1,609 wa Taasisi hii wamepewa mikopo yenye jumla ya Shilingi bilioni 4.1.

Aidha, Serikali bado inaendelea kutafuta utaratibu wa kudumu wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa Taasisi hii sambamba na kuboresha mfumo na uratibu wa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imeanza mchakato wa kurejea Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Mwaka 2004 na Sheria iliyoanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ya mwaka 2007 kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kinaendesha kozi za Cheti na Diploma ya Sheria, na kutoa elimu endelevu ya sheria kwa wanasheria pamoja na kozi fupi, warsha na semina kwa jamii ya Tanzania. Katika Mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kimeendelea kutekeleza majukumu ya msingi. Aidha, Chuo hiki kimeendelea na ujenzi wa mabweni ya kulala wanafunzi wa Chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha utendaji katika Utumishi wa Mahakama, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara yangu kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama imeratibu ajira za watumishi katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni wakiwemo Mahakimu 40 ambapo kati yao wanaume ni 35 na wanawake ni watano; kuthibitisha katika cheo Mahakimu 68 ambapo kati yao, wanaume ni 48 na wanawake ni 20; kuthibitisha katika vyeo Mahakimu 142 ambapo kati yao wanaume ni 89 na wanawake ni 53; na kupandisha cheo Mahakimu 71ambapo wanaume ni 37 na wanawake ni 34.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Tume ilishughulikia masuala manne (4) ya nidhamu. Kati ya masuala hayo, watumishi watatu walirejeshwa kazini na mmoja, suala lake bado linaendelea. Vile vile Tume ilipokea na kushughulikia malalamiko 12 kutoka kwa wananchi yaliyohusu nidhamu na utendaji wa Mahakimu na Majaji katika Mahakama. Aidha, mchakato umefanyika na tayari Mtawala Mkuu wa Mahakama ameteuliwa na Watawala wengine wa kujaza nafasi za Uongozi wa Mahakama *(Court Administrator)* kwa kuzingatia Sheria mpya ya Uongozi wa Mahakama Na. 4 ya 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Taasisi zake iliendelea na jukumu la kutoa elimu kwa umma ili wananchi wapate kuelewa masuala mbalimbali ya kisheria. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara iliandaa vipindi vinne vya Runinga kupitia *TBC-1* kuhusu miaka 50 ya Uhuru, mchakato wa Katiba na haki za msingi za binadamu. Pia ilichapisha na kusambaza nakala 18,000 za toleo la Jarida la Sheria *News* wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya uhuru kupitia Gazeti la *Daily News*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ilishiriki katika maonesho ya kitaifa ya kutoa elimu katika maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Wiki ya Wizara ya Katiba na Sheria, Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara na Maadhimisho ya siku ya Nane Nane (Maonesho ya Nane Nane).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba masuala ya teknolojia yanatiliwa mkazo kama eneo muhimu la kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake.

Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzisha mtandao wa *LAN* na pia mtandao usiotumia nyaya *(WIFI).* Wizara, Makao Makuu pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tayari zimeunganishwa na mkongo wa Taifa. Vile vile Tovuti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imezinduliwa pamoja na kuandaa Sera ya *Information Communication Technology*, (*ICT*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shughuli za utekelezaji wa *Case Docket Management System* unaosimamiwa na Kurugenzi ya Mashtaka zinaendelea. Utaratibu wa kuanzisha mfumo wa File *Management System* kwa ajili ya Masjala na mfumo wa *Library Management System* kwa ajili ya Maktaba unaendelea. Pamoja na mafanikio hayo, umeanzishwa utaratibu wa kuunganisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Makao Makuu, Kurugenzi ya Mashtaka na Kanda ya Dar es Salaam kwenye mfumo wa *Voice, Video*, *Data Local Area Network – LAN, na Wide Area Network – WAN.* Mpango huu uko katika hatua ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitoa mafunzo kwa Watendaji Wakuu 34 wa Mahakama wakiwemo Majaji 31 na Mahakimu Wakazi watatu. Pia mafunzo ya uzingatiaji wa misingi ya utawala bora yalitolewa kwa Viongozi na Watendaji wa Serikali za Mitaa katika Kata 21 za Manispaa mbili za Temeke na Kinondoni na kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Kata, katika Kata 16 za Manispaa ya Ilala na Kinondoni. Mafunzo hayo pia yanajumuisha Mpango Maalum wa kutoa elimu katika Shule za Sekondari zipatazo 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dhana ya kuboresha Mazingira ya Kazi na Ujenzi wa Majengo, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Jengo la Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(Law School of Tanzania)* ambao upo hatua za mwisho ili kukamilika;

(b) Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya *RITA* kwa kushirikiana na Shirika la *NSSF* bado unaendelea;

(c) Ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu Dar es Salaam na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu unaendelea;

(d) Ujenzi wa Awamu ya Pili wa Mahakama Kuu Shinyanga unaendelea;

(e) Mchakato wa kumaliza ujenzi wa mabweni ya Chuo cha Mahakama Lushoto unaendelea;

(f) Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kisarawe umekamilika;

(g) Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Magoma (Kongwa), Ngorongoro(Ngorongoro) na Korekelo (Bukoba) pamoja na Ujenzi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi uko katika hatua ya mwisho;

(h) Awamu ya Pili ya ujenzi wa Mahakama Kuu ya Bukoba ambapo ujenzi umekamilika;

(i) Basi moja la watumishi wa Mahakama na magari sita ya Majaji yalinunuliwa; na

(j) Kuendelea kutafuta majengo ya ofisi kwa ajili ya upanuzi wa uendeshaji wa shughuli za utenganishaji wa upelelezi na uendeshaji wa mashtaka katika Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria ambayo inajumuisha taasisi Nane. Kati ya Taasisi hizo, tano ni za Wizara yangu, Taasisi mbili za Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, na Taasisi moja ya sekta binafsi zinazoshugulikia uboreshaji wa huduma za kisheria, usimamizi na utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa, programu inafikia mwisho ambapo inatarajiwa kumalizika katika mwaka ujao wa fedha 2012/2013. Taasisi zinazotekeleza programu hii zinaingiza shughuli zao katika mipango yao ya kila mwaka kama sehemu ya utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za maboresho zinazotekelezwa zimelenga kufanikisha malengo makuu manne kama ifuatavyo:-

(i) Kuboresha na kuimarisha mifumo ya usimamizi na utoaji wa haki;

(ii) Kuimarisha taaluma na uweledi wa wahitimu wanasheria *(Law graduates);*

(iii) Kuongeza na kuimarisha mazingira na fursa ya upatikanaji wa haki kwa wote *(increased access to justice);* na

(iv) Kuimarisha kazi ya Uratibu, Usimamizi na Tathimini ya Programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria imefanya tathmini ya mwenendo wa mashauri katika Mahakama, ili kufahamisha wadau hali halisi ya wastani wa muda unaotumiwa katika hatua zote tangu shauri (Madai na Jinai) linaposajiliwa, kisha kusikilizwa na hatimaye kuamuliwa. Umuhimu wa kazi hii ni kuiwezesha Serikali kufahamu kwa undani changamoto zinazoukabili mfumo wa utoaji haki ili kushughulikia changamoto zilizopo kwa lengo la kupunguza muda ambao mashauri yanachukua tangu kusajiliwa hadi kuamuliwa kwake. Aidha, hatua hii ina lengo la kupunguza mlundikano wa mashauri yanayokaa muda mrefu bila kuamuliwa na pia itasaidia kuondoa mazingira na viashiria vya rushwa Mahakamani. Mapendekezo ya Ripoti iliyotolewa yamekwishaanza kutekelezwa hususan yasiyohitaji mabadiliko ya Sera au Sheria *(Non Policy Issues).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha na kuimarisha kazi za upelelezi na uendeshaji wa mashtaka nchini, Programu imeliwezesha Jeshi la Polisi kuendelea na kazi yake ya kuimarisha Idara yake ya upelelezi kwa kutoa mafunzo ya mbinu za kisasa za upelelezi zinazozingatia na kulinda haki za binadamu. Jumla ya Maofisa Waandamizi 277 wa Jeshi hilo toka katika ngazi za Wilaya wamepatiwa mafunzo.

Kwa upande wa uimarishaji wa mfumo wa uendeshaji wa mashtaka, programu iliwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kupitia Kurungenzi ya Uendeshaji wa Mashtaka kuimarisha kazi hii ya uendeshaji wa Mashtaka kwa kusogeza huduma hii karibu na wananchi. Aidha, kupitia Programu hii mabasi mawili makubwa, matano ya kati *(min bus)* na magari matano ya kusindikiza Mahabusu yamenunuliwa ili kuliwezesha Jeshi la Magereza kuboresha mfumo wa usafirishaji wa Mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha taaluma na uweledi wa wahitimu, wanasheria *(Law graduates),* Wizara kupitia Programu ya Maboresho iko katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa majengo ya kudumu ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (*Laws School of Tanzania).* Programu imefanikiwa kuboresha mazingira ya kuhifadhi watoto wanaoingia kwenye mgogoro na sheria kwa kujenga mahabusu za watoto na walemavu katika vituo vya Polisi vilivyoteuliwa vya Tunduma na Kituo Kikuu cha Polisi cha Mkoa wa Mbeya. Kazi hiyo inaendelea pia kwa Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria ilifanya tathmini ya utekelezaji wa masuala ya jinsia kwa taasisi zote zinazotekeleza programu hii na kupata changamoto zinazoendana na utekelezaji katika eneo hili. Kazi hiyo ilikamilika, taarifa na mpango wa namna ya kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanafanyiwa kazi katika utaratibu unaofaa uliandaliwa na kupitishwa na wadau wa programu.

Wizara pia imewezesha Jeshi la Polisi kuimarisha madawati ya Jinsia na watoto kwa kuanzisha madawati haya katika vituo vyote vya Polisi nchini na kufanya ukarabati wa madawati ya Jinsia na Watoto katika vituo vya Polisi katika Wilaya za Temeke - Chango'mbe, Hai na Magu. Ofisi za Dawati la Jinsia na watoto zilifunguliwa rasmi Mkoani Kilimanjaro na Wilayani Hai mwishoni mwa mwezi Mei, 2012. Aidha, tumeweza kusaidia katika utayarishaji wa Mwongozo wa uundaji wa madawati haya na nyenzo za kutumia katika utekelezaji wa *(Standard Operating Procedures for the operationalization of the gender and Children's desks)* ambapo mafunzo kwa askari katika Mikoa ya Mwanza, Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Zanzibar na Pemba yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (*LSRP*) unakamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha 2012/2013. Wizara yangu imeanzisha mchakato wa kufanya tathmini ya hali halisi ya sasa ya Sekta ya Sheria kwa lengo la kuiwezesha Serikali hii kutayarisha programu na miradi mingine ya kuendelea kuziboresha Taasisi za Kisheria na kuhakikisha huduma bora zinatolewa katika Sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hiyo, Programu itaendelea kukamilisha utekelezaji wa shughuli za maboresho kwa kuzijumuisha na majukumu ya kila siku ya Taasisi husika kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imefanya juhudi kubwa katika kuwaendeleza watumishi wake wa ngazi mbalimbali katika taaluma zao. Jumla ya Watumishi

524 wa fani mbalimbali waliweza kupata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi wakiwemo, wanaume 258 na wanawake 266. Kati ya hao, jumla ya Mawakili wa Serikali ni 242. Pia, jumla ya Mawakili wa Serikali 14 na mtumishi mmoja walihudhuria mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi. Mawakili wawili wa Serikali walihudhuria mafunzo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwateua Majaji wapya 10 wa Mahakama Kuu. Kati ya hao, wanawake watatu na wanaume saba. Majaji hawa wamepangiwa kuanza kufanya kazi Dar es Salaam kwa miezi mitatu kwenye Divisheni ya Mahakama ya Ardhi ili kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo imefikia 2,200. Idadi ya Majaji wote nchini imefikia 85 na kati yao, 69 ni wa Mahakama Kuu na 16 ni wa Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, jumla ya Mahakimu 300 wameajiriwa ili kupunguza tatizo la upungufu wa Mahakimu nchini. Mahakimu hawa wameshapangiwa vituo vya kazi. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliwapandisha vyeo watumishi 234. Kati ya hao, wapo Mawakili wa Serikali 212 na watumishi 22 wa kada nyingine zikiwemo za Makatibu Sheria, Maafisa Tawala, Wachumi, Maafisa Ugavi, Makatibu Mahsusi, Watunza Kumbukumbu, Madereva, Wapokea simu na Walinzi. Aidha, Mahakama kwa mwaka huu pamoja na bajeti ndogo imefanikiwa kuwajengea uwezo watumishi kwa kugharamia mafunzo ya muda mrefu watumishi watatu na watumishi 10 wamelipiwa mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, watumishi 144 katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali walithibitishwa kazini. Kati yao, 89 walithibitishwa kwenye cheo na 55 walithibitishwa kazini baada ya kuajiriwa kwa mara ya kwanza. Vile vile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliomba na kupatiwa kibali cha ajira mpya 152. Kati ya nafasi hizo, 115 zilikuwa ni za Mawakili wa Serikali na zilizobakia ni za watumishi wa kada za Wachumi, Katibu Sheria, Katibu Sheria Msaidizi, Mtunza Kumbukumbu Msaidizi, Katibu Mahsusi, Dereva, Wachambuzi wa Mifumo ya Kompyuta na Mtakwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara yangu ilikabiliwa na changamoto nyingi katika kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wizara na Taasisi zake ni kidogo na hakikidhi mahitaji, hasa ikizingatiwa kuwa kuna ongezeko la majukumu, na Sekta ya Sheria inategemewa na sekta nyingine katika kuimarisha uchumi wa nchi na maendeleo yake kwa ujumla;

(b) Wizara bado inakabiliwa na upungufu wa rasilimali watu, hali ambayo inaathiri ufanisi wa utoaji haki kwa wananchi;

(c) Kukosekana kwa majengo ya kudumu kwa baadhi ya Taasisi ambazo zinasimamiwa na Wizara na kusababisha Wizara kuingia gharama kubwa kwa ajili ya kulipia kodi ya pango;

(d) Vitendo vya rushwa vimeendelea kujitokeza katika baadhi ya vyombo vya utoaji wa haki, hali ambayo inasababisha wananchi kukosa imani na vyombo vya utoaji haki;

(e) Suala la mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo limekuwa kero kubwa kwa Wizara na kwa wanafunzi husika ambao ni wahitimu wa Shahada ya Kwanza ya Sheria. Hali hii inatokana na Sheria ya Utoaji wa Mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inayowaruhusu wanafunzi wanaosoma Shahada ya Kwanza *(undergraduate)* peke yake kupata mikopo hiyo;

(f) Uwezo mdogo wa wananchi walio wengi kutumia vyombo vya kutoa haki na huduma za Kisheria na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mfumo uliopo wa Sheria na Mahakama nchini; na

(g) Mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa watumishi walio wengi yanayotokana na maslahi duni na uhaba wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa changamoto zinazoikabili Wizara zinapatiwa ufumbuzi, ipo mikakati kadhaa itakayoendelea kutekelezwa kama ifuatavyo:-

(a) Wizara pamoja na Taasisi zake itaendelea kuainisha vipaumbele vyake kulingana na viwango vya bajeti kwa kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya ufinyu wa bajeti;

(b) Wizara itaendelea kuomba na kufuatilia vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kujaza nafasi zilizo wazi;

(c) Wizara itaendelea kutafuta majengo ya kudumu ya Ofisi na Mahakama kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo ili kuondokana na changamoto hii. Mfano, ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ambao ujenzi wake upo katika hatua za kukamilika, ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu - Dar es Salaam, Mahakama ya Hakimu Mkazi - Kisutu na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, huko Kinondoni;

(d) Kuendelea kusimamia sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi kwa lengo la kujenga maadili, uadilifu, uwajibikaji na utendaji wenye matokeo unaozingatia motisha na maslahi kwa watumishi wa umma ili kuwaepusha na vishawishi vya rushwa; na

(e) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itaendelea na mchakato wa kurejea Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya mwaka 2004 na Sheria iliyoanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ya mwaka 2007 kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, dhima yetu kubwa ni kupunguza mlundikano wa mahabusu na wafungwa Magerezani na mlundikano wa kesi Mahakamani. Kwa kuzingatia hilo, Wizara ikishirikiana na Mahakama, inakusudia kufanya mambo matatu mapya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, katika mwaka huu wa fedha, inakusudia kuajiri Majaji na Mahakimu wa muda watakaoshughulikia mlundikano wa kesi uliopo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huu umetokana na ukweli kwamba, kwa sasa zipo kesi 199,741 Mahakamani ambazo hazijasikilizwa katika Mahakama za ngazi zote. Tukiajiri Mahakimu na Majaji wa kutosha kwa kipindi cha Mkataba wa miezi 12, tutaweza kumaliza mlundikano huu na kuwaacha Mahakimu na Majaji wa kudumu kusikiliza mashauri mapya. Ni imani yetu kwamba hatua hii itaboresha utoaji wa haki hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, katika mwaka huu wa fedha Wizara yangu ikishirikiana na Mahakama, inatarajia kuanza maandalizi ya mpango kuanza kusikiliza kesi kwa kutumia mfumo wa *telejustice* ambao tunaamini utasaidia sana katika kuboresha utoaji haki hapa nchini na kupunguza gharama kubwa zinazoambatana na utaratibu wa sasa. Mpango huu unaunganisha Magereza na Mahakama kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na unawezesha kesi kusikilizwa bila watuhumiwa kutolewa Gerezani na kusafirishwa kwenda Mahakamani. Utaratibu huu utamwezesha Hakimu au Jaji kusikiliza kesi bila mtuhumiwa kupelekwa Mahakamani. Kwa sasa tunafanya uchambuzi ili kuona tuanze Gereza lipi na Mahakama zipi ili utekelezaji uanze rasmi katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu na la mwisho, Wizara yangu inashauriana na Uongozi wa Mahakama ili kuona uwezekano wa kuanzisha Mahakama ya Jinai *(Criminal Court)* kwa makusudio ya kupunguza mlundikano

wa kesi za jinai ambazo kwa sasa zinasikilizwa kwa utaratibu wa *sessions*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mahakama hii itaanzishwa, mashauri ya jinai yatakuwa na Mahakama yake ambayo itakuwa na Majaji ambao kila wanapoamka wanajua shughuli yao ni kusikiliza mashauri ya jinai peke yake. Ninaamini kuwa hili likifanyika, litachangia sana katika dhima yetu ya kuondoa mlundikano wa kesi Mahakamani na msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2012/2013 imeweka mipango yenye malengo ya muda wa kati ili kutekeleza dhima ya kutoa haki kwa watu wote na kwa wakati. Katika kufikia malengo hayo, maeneo ya kipaumbele yatakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Uratibu wa mchakato wa mabadiliko ya Katiba;

(b) Usimamizi wa usikilizaji na uendeshaji wa mashauri;

(c) Uimarishaji wa shughuli za usajili, ufilisi na udhamini;

(d) Uimarishaji na uboreshaji wa Vyuo vya Mafunzo;

(e) Uimarishaji wa utoaji wa ushauri wa kisheria nchini;

(f) Kufanya tafiti, mapitio, uandishi wa sheria na hati mbalimbali; na

(g) Usimamiaji wa haki za binadamu na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara itasimamia jambo kubwa na la kihistoria la uanzishwaji wa Katiba mpya. Mpaka sasa mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu ni Katiba gani Watanzania wanaitaka, umekwishaanza na unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma ya kupatikana kwa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo Mwaka 2014, Tume imejigawa katika makundi saba ambayo yatatembelea Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kuelimisha na kukusanya maoni kutoka kwa wananchi. Katika awamu ya Kwanza ambayo imeanza tarehe 2 Julai, 2012, Tume imeanza na Mikoa nane ambayo ni Dodoma, Kagera, Kusini Pemba, Kusini Unguja, Manyara, Pwani, Shinyanga na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya uratibu na ukusanyaji wa maoni ya wananchi utafanyika kupitia Mabaraza ya Katiba. Katika kipindi hicho, Tume itawaomba wananchi watoe maoni yao kuhusu rasimu ya Katiba. Kupitia kwenu Waheshimiwa Wabunge, naomba mwahamasishe wananchi wa Majimbo yenu ili waweze kujitokeza kwa wingi katika Mikutano ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Ukusanyaji wa Maoni katika awamu zote mbili. Aidha, ninawaomba wananchi kutoa mawazo yao kwa uwazi, uhuru na bila ya hofu yoyote. Tume itafanya kazi zake kwa uhuru, uwazi na tunawahakikishia kwamba maoni yote yatakayotolewa na wananchi, Taasisi, Asasi za Kiraia na makundi mengine yote yataheshimiwa na kufanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa zoezi hili, Wizara inawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wajitokeze kwa wingi na kutoa maoni yao kwa utulivu. Aidha, wananchi wanaombwa wawe tayari kusikiliza mawazo ya wengine hata kama hawakubaliani na mawazo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imejipanga kukusanya maoni ya Watanzania kutoka pande zote za ndani na nje ya nchi kupitia njia mbalimbali kama vile kufanya mikutano mbalimbali katika Mikoa yote, kupokea maoni kwa njia ya simu, barua pepe, tovuti ya Tume, Nukushi mitandao ya kijamii kama *facebook, twitter,* blog na pia kwa njia ya Posta. Kutokana na umuhimu wa zoezi hili, Wizara inawaomba wananchi wajitokeze kutoa maoni yao kwa utulivu ili yaweze kuzingatiwa. Aidha, wananchi wanaombwa kuwa tayari kusikiliza mawazo ya wengine hata kama hawakubaliani na mawazo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itakamilisha ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga na itajenga majengo ya Mahakama za Mwanzo za Mkomanzi, Kawe, Gairo, Mangaka, Bunda, Bariadi na Lukuledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, itaanzisha Mfumo wa Utoaji Haki kwa kusikiliza Mashauri na kupunguza Mashauri ya muda mrefu*(case backlog)* na yale ya sasa kwa kuimarisha Mfumo wa Mawasiliano ya Kompyuta katika kusikiliza Mashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, itaendelea kutoa haki katika

Mashauri ya Biashara ili kuboresha mazingira ya Uwekezaji kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuongeza kiwango cha kumaliza Mashauri *(Clearing rate)* kufikia asilimia 100 na kuimarisha matumizi ya suluhu muafaka *(Alternative Dispute Resolution (ADR);*

(b) Kuboresha kanuni ili kuondoa ucheleweshaji katika Mashauri ya Biashara;

(c) Kuimarisha na kujenga utaratibu wa kubadilishana uzoefu baina ya Mahakama Kuu-Divisheni ya Biashara na Mahakama nyingine duniani na kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi; na

(d) Kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kukamilisha ukarabati wa Masjala ya Mbeya na ujenzi wa Masjala ya Dodoma na Kuboresha Matumizi ya elekroniki katika shughuli za mahakama kwa kuimarisha mfumo wa kurekodi mashauri, kuweka maktaba ya kielektroniki na kuanzisha mfumo wa kupata taarifa za mahakama kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu za kiganjani (*sms*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itafungua Ofisi mpya katika Mikoa ya Kigoma, Njombe, Pwani, Manyara na Morogoro pamoja na katika Wilaya ya Temeke. Divisheni ya Mashtaka itaimarisha Mpango wa Kutenganisha Kazi za Upelelezi na Uendeshaji wa Mashtaka *(Civilianization of the Prosecution Service)* katika ngazi za Mikoa na Wilaya kwa lengo la kupunguza mlundikano wa kesi pamoja na masuala ya kiuchunguzi na

uendeshaji wa mashtaka katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Vile vile, uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi pamoja na kikatiba utaimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*) itaandaa hati ya makubaliano na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa juu ya utendaji wa shughuli za usajili wa vizazi na vifo katika Mamlaka zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, itafanya majaribio ya kutumia mfumo mpya wa *TEKNOHAMA* katika kutekeleza shughuli za usajili wa vizazi na vifo katika Wilaya tano za Temeke, Kinondoni, Ilala, Kibaha na Dodoma Mjini na itaendelea na mchakato wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakala (*RITA Tow*er) pamoja na kukamilisha rasimu ya Muswada ya Sheria ya Ufilisi kwa ajili ya kutayarisha Muswada wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo itaboresha mazingira na uendeshaji wa mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo kwa kununua na kuweka samani na vifaa vya kuendesha mashauri katika Mahakama ya Mazoezi ya Taasisi na kuajiri watumishi wapatao 84 hasa wa kada ya ukufunzi *(instructor).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama cha Lushoto kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kukijengea Chuo uwezo wa kuendesha mafunzo endelevu kwa watumishi wa Mahakama;

(b) Kuongeza Idadi ya Wanachuo wanaosoma ngazi ya Cheti na Diploma ya Sheria kutoka 1,380 ili kufikia wanachuo 1,600 kwa kuanzisha *campus* – Mwanza;

(c) Kutoa Elimu ya Sheria kwa Jamii kwa kuendesha kozi fupi na Semina pamoja na kutoa msaada wa huduma za kisheria bure *(legal aid);*

(d) Kujenga jengo la hosteli, jengo la kufundishia *(Lecture Theatre)* na kukarabati majengo ya Chuo; na

(e) Kuwaendeleza watumishi kwa kuwajengea uwezo kwa kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itawajengea uwezo watumishi katika kujadili na kuhakiki mikataba ya madai na ya mahusiano ya kimataifa *(Contracts and Treaties),* na kuimarisha uwezo wa kutayarisha taarifa za mikataba inayojadiliwa katika Mikutano ya kikanda na Kimataifa. Aidha, mfumo wa utoaji huduma za kisheria katika eneo la mikataba utaimarishwa ili kujenga mahusiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria itafanya mapitio ya mfumo wa sheria unaosimamia huduma za jamii kwa wazee, mapitio ya mfumo wa Sheria unaolinda haki za watumiaji, kutafsiri Sheria nne kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili. Wizara itaendelea kufanya uchambuzi

wa hukumu za Mashauri ya Mahakama ya Rufani ili kuainisha kanuni za kisheria na kuziweka kwenye Tovuti ya Tume kwa ajili ya kuwarahisisishia rejea watumiaji na wadau mbalimbali wa masuala ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria, itaandaa rasimu ya tafiti za marekebisho ya Sheria na Kanuni zinazohusu mfumo wa madai ili kuwawezesha Wananchi kupata haki zao za madai kwa muda muafaka na kwa gharama nafuu pamoja na kuandaa taarifa ya migogoro ya ardhi ambayo itapitiwa na wadau mbalimbali ili kupata maoni yao na kuwasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuandaa Miswada ya Sheria na Hati mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kujadiliwa na Bunge na hatimaye kupitishwa kuwa sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, itaendelea kushughulikia malalamiko yaliyobaki 7,165 na malalamiko mengine mapya yatakayopokelewa. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kutoa huduma ya ushauri wa kisheria katika masuala yanayohusu Katiba na haki za binadamu, kuandaa taarifa za utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu nchini kwenye mikataba ambayo nchi imeridhia na kuziwasilisha kwenye vyombo husika kwa ajili ya majadiliano. Vile vile, kutayarisha *program* mbalimbali za uhamasishaji wa jamii juu ya uelewa wa sheria mbalimbali zinazohusu masuala ya haki za binadamu pamoja na

kukamilisha Mpango Kazi wa Taifa wa Masuala ya Haki za Binadamu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kuzingatia umuhimu wake kitaifa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii, inao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba inakuza, inaimarisha na kustawisha amani, utawala bora na usalama wa raia nchini. Hivyo basi, pamoja na changamoto ya upungufu wa rasilimali unaolikabili Taifa letu, kuna haja ya kuipa Wizara hii kipaumbele kwa kuiongezea rasilimali zenye kukidhi mahitaji halisi ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Viongozi, Watendaji Wakuu na Watumishi wote katika Wizara yangu kwa ushirikiano na kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuandaa Mpango na Bajeti hii na hatimaye kuikamilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawashukuru kwa msaada wao wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu, hali ambayo inanifanya nitekeleze wajibu wangu kwa ufanisi mkubwa. Kipekee, napenda kuwashukuru Wakuu wote wa Taasisi za Wizara yangu nikianzia na Jaji Mkuu - Mheshimiwa Othman Mohamed Chande, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa - Jaji Frederick Mwita Werema, Jaji Kiongozi - Mheshimiwa Fakih A. R. Jundu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria - Ndugu Fanuel E. Mbonde, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Mheshimiwa George Masaju, Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba - Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na Makamashna wote 30 wa Tume hiyo, Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba - Mheshimiwa Asaa Rashid, Naibu Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba - Ndugu

Casmir Kyuki na aliyekuwa Msajili wa Mahakama ya Rufani Mheshimiwa Judge Francis Mutungi ambaye sasa ni miongoni mwa Majaji wapya walioteuliwa hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mkurugenzi wa Mashtaka - Dkt. Eliezer M. Feleshi, Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara - Mheshimiwa John Kahyoza, Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi - Mheshimiwa David E. Mrango, Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi - Mheshimiwa Mohamed Gwae, Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama - Bibi Enziel Mtei, Mkuu ya Taasisi ya Mafunzo ya Wanasheria kwa Vitendo - Mheshimiwa Jaji, Dkt. Gerald Ndika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria - Mheshimiwa Jaji, Prof. Ibrahim Juma, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - Ndugu Philip Saliboko, Kaimu Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria - Bibi Agnes Mgeyekwa na Bibi Mary Massay Katibu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na ambaye hivi karibuni ameteuliwa kuwa Kamishna wa Tume ya Upatanishi na Usuluhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla ya kumaliza hotuba yangu, niwapongeze watumishi walioteuliwa hivi karibuni kushika nyadhifa mpya za Ujaji wa Mahakama Kuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Judge Francis Mutungi, aliyekuwa Msajili wa Mahakama ya Rufani; Mheshimiwa Judge Mathiew Mwaimu, aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Haki za Binadamu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Mheshimiwa Judge Dkt. Gerald Ndika aliyekuwa Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo; Mheshimiwa *Judge* Joaquina De Mello aliyekuwa Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mheshimiwa Mugeta-aliyekuwa Naibu Msajili wa Mahakama ya Rufani; na Bibi Mary Massay, Katibu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kuteuliwa kuwa Kamishna katika Tume ya Upatanishi na Usuluhishi *(CMA).*

Aidha, ninawapongeza watumishi walioteuliwa kushika nyadhifa za Watendaji wa Mahakama nchini hivi karibuni ambao ni:-

(i) Bwana Hussein Kattanga aliyekuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) aliyeteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;

(ii) Bwana Ignus Pauli Kitusi aliyekuwa Msajili wa Mahakama Kuu, Kuwa Msajili Mkuu wa Mahakama;

(iii) Bwana Pauterine Mulisa Kente, aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Rufani la Kodi kuwa Msajili wa Mahakama ya Rufani; na

(iv)Bwana Benedict Bartholomeo Mwingwa aliyekuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, kuwa Msajili wa Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria na Serikali kwa ujumla, ninapenda kuwashukuru sana wadau wetu wa maendeleo kwa kuendelea kushirikiana nasi katika kuboresha Sekta yetu ya

Sheria. Wadau hao wa Maendeleo ni Denmark (*DANIDA*), Canada (*CIDA*), Benki ya Dunia (*WB*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watoto (*UNICEF*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (*UNDP*) na Serikali ya Uingereza (*DFID*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau wengine kutoka Sekta binafsi Vyombo vya Habari, na Vyuo vya Elimu vinavyoshughulika na masuala ya sheria kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Sheria. Kwa namna ya pekee, shukrani zangu za dhati ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao katika kuboresha utendaji wa Wizara yangu ili itoe mchango wake muhimu katika utoaji haki kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Katiba na Sheria ilitengewa jumla ya Sh. 138,723,656,600/=. Hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2012 jumla ya Sh. 94,753,937,434.96 zilikuwa zimetumika. Ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh. 186,323,718,000/= kwa ajili ya Taasisi, Idara na Vitengo vya Wizara. Kati ya fedha hizo, Sh. 123,932,043,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh. 37,553,608,000/= ni kwa mishahara. Fedha za Miradi ya Maendeleo ni Sh. 24,838,067,000/=. Kati ya hizi, fedha za ndani ni Sh. 11,403,000,000/=, na fedha za nje ni Sh. 13,435,067,000/= . Mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa mafungu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 8 - Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Matumizi ya Kawaida Sh.

33,944,588,000/=. Matumizi ya mishahara ni Sh. 0.00 na jumla ni Sh. 33,944,588,000/=; Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama, matumizi ya mishahara ni Sh. 460,437,000/= na matumizi mengineyo ni Sh. 1,471,716,000/=, Matumizi ya Maendeleo (ndani) ni Sh. 0.00 Matumizi ya Maendeleo (nje) Shilingi 0.00, jumla Sh. 1,932,153,000/=; Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; matumizi ya mishahara Sh. 2,205,296,000/= matumizi mengineyo Sh. 8,322,865,000/=, Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. 0.00 Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 700,000,000/= jumla ni Sh. 11,228,161,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 35 - Kurugenzi ya Mashtaka, matumizi ya mishahara Sh. 4,115,654,000/=, matumizi mengineyo Sh. 5,660,826,000/= Matumizi ya Maendeleo(ndani) Sh. 0.00; Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 2,989,224,000/= Jumla ni Sh. 12,765,704,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 40 – Mahakama, matumizi ya mishahara Sh. 27,583,442,000/=, matumizi mengineyo Sh. 57,832,463,000/= Matumizi ya Maendeleo (ndani) Sh. 11,403,000,000/=, Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 5,810,116,000/=, jumla ni Sh. 102,629,270,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria, matumizi ya mishahara Sh. 811,791,000/=, Matumizi Mengineyo Sh. 10,047,534,000/=, Matumizi ya Maendeleo (ndani) Sh. 0.00, Matumizi ya Maendeleo(nje) Sh. 3,441,727,000/=. Jumla ni Sh. 14,301,052,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, matumizi ya mishahara Sh. 1,823,740,000/=, matumizi mengineyo

Sh.3,795,802,000/=; Matumizi ya Maendeleo (ndani) Sh. 0.00 Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 0.00, na jumla ni Sh. 5,619,542,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria. Matumizi ya mishahara Sh. 553,248,000/=; Matumizi Mengineyo Sh. 2,856,000,000/=; Matumizi ya Maendeleo (ndani) Sh. 0.00; Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 616,350,000/= na Jumla ni Sh. 4,025,598,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa mwaka 2012/2013 inatarajia kukusanya kiasi cha Sh. 6,710,198,000/= kama maduhuli ya Serikali. Mchanganuo wa makusanyo kwa mafungu husika ni kama ifuatavyo:

Fungu 16 – Sh. 3,002,000/=; Fungu 18 – Sh. 300,000,000/= ; Fungu 19 – Sh. 983,000,000/=; Fungu 40 - Sh. 99,998,000/=; Fungu 41 – Sh. 4,282,150,000/=; Fungu 55 – Sh. 5,644,000/=; Fungu 59 –Sh. 200,000/=; Fungu 64 - Sh. 960,000,000/=; Fungu 90 - Sh. 76,403,000/= na jumla ni Sh. 6,710,198,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Waziri wa Katiba na Sheria kwa kusoma hotuba yako vizuri na kutumia muda wako vizuri sana. Tunashukuru sana.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.N.Y. MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA – MHE. PINDI H. CHANA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza, nachukua nafasi hii kipekee kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kunipa uhai hadi leo. Pia niruhusu niwashukuru wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa kuwa wanaendelea kunipa *support* ya hali ya juu sana. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru Ndugu Twaha Kifurebe ambaye ni Katibu wa Mbunge Jimbo la Karagwe kwa kazi nzuri anazozifanya. Pia naipongeza Radio Fadeko, Radio Karagwe ambazo ziko Jimboni kwangu kwa kufanya kazi nzuri ya kuwahabarisha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, Wizara hii ni nyeti sana, ningeomba ipewe muda wa kutosha katika kuchangia hotuba ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati ilikutana Dar es Salaam kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Kuchambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2012 /2013. Wizara hii ina Mafungu 13 kama ifuatavyo:-

(i) Tume ya Mabadiliko ya Katiba – Fungu 8;
(ii) Tume ya Utumishi wa Mahakama– Fungu 12;
(iii) Mwanasheria Mkuu wa Serikali – Fungu 16;
(iv) Mahakama Kuu – Fungu 18;
(v) Mahakama za Wilaya – Fungu 19;
(vi) Mkurugenzi wa Mashitaka – Fungu 35;
(vii) Mahakama – Fungu 40;
(viii) Wizara ya Katiba na Sheria – Fungu 41;
(ix) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora –Fungu 55;
(x) Tume ya Kurekebisha Sheria– Fungu 59;
(xi) Mahakama ya Kazi – Fungu 60;
(xii) Mahakama ya Biashara – Fungu 64; na
(xiii) Mahakama ya Ardhi – Fungu 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi nyingine zilizotajwa kuwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ni pamoja na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA),* Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(Law School of Tanzania)* na Chuo cha Uongozi wa Mahakama *(Institute of Judicial Administration).*

Mheshimiwa Naibu Spiika, Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Mwaka 2011/2012, wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge

lako Tukufu kwamba katika baadhi ya maeneo, ushauri wa Kamati ulizingatiwa, lakini maeneo mengine bado yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ili yaweze kuboreshwa. Ushauri wa Kamati ulifanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

(i) Mahakama na Taasisi zake kufanya bidii zaidi ili kupunguza malalamiko ya ucheleweshaji wa kesi Mahakamani unaosababisha msongamano wa Mahabusu Magerezani.

Kamati ilielezwa kwamba elimu imetolewa kwa Majaji na Mahakimu kuhusu utoaji wa adhabu mbadala *(Alternative Punishment),* Uandishi wa Hukumu, Menejimenti ya Mwenendo wa Mashauri *(case flow management)* na uwajibikaji unaolenga matokeo ili kuhakikisha kuwa kesi zinasikilizwa pasipo kuchelewa na hukumu kutolewa kwa wakati.

(ii) Kutokana na uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Serikali ianze mikakati ya kujenga Mahakama za Mwanzo kwa kila Kata sambamba na kuajiri Vijana waliomaliza shahada ya Sheria ili watoe huduma kwenye Mahakama za Mwanzo.

Kamati ilielezwa kwamba agizo la kujenga Mahakama za Mwanzo kwa kila Kata litatekelezwa endapo Bajeti ya Mahakama itaboreshwa. Aidha, agizo la ajira za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wenye Shahada ya Sheria, imetekelezwa kwa kuajiri Mahakimu wapya 300 ambao hivi sasa wameshapangiwa Vituo.

(iii) Serikali ifanye jitihada za kuongeza idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu lakini kwa angalizo kwamba wanaoteuliwa Wakidhi vigezo. *(Makofi)*

Kamati ilielezwa kwamba katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali iliongeza idadi ya Majaji kwa Mamlaka husika kuteua Majaji 10 wa Mahakama Kuu na Majaji watatu wa Mahakama ya Rufani.

(iv) Mvutano kati ya Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa na Kurugenzi ya Mashitaka ushughulikiwe.

Kamati ilielezwa kwamba Wizara imeanza kushughulikia mvutano huo unaohusu uendeshaji wa Mashtaka ya Rushwa.

(v) Utaratibu wa mikopo uangaliwe ili wanafunzi wa Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo wapate mikopo. Aidha, kuwepo na utaratibu unaofanana wa utoaji wa Shahada ya Sheria kwa Vyuo vyote. *(Makofi)*

Kamati ilielezwa kwamba mawasiliano yamefanyika kati ya Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Elimu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuanza mchakato wa kupitia upya Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (ya Mwaka 2004) na inayohusu kuanzishwa kwa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (Na. 5 ya mwaka 2005) ili Wanachuo hawa wapatiwe Mikopo. Aidha, Serikali itapitia upya mitaala ya kufundishia Sheria ili iwe sawa kwa Vyuo vyote vya Sheria. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara ya Fedha imetenga Shilingi bilioni 2.6 kama ruzuku kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya

Uanasheria kwa vitendo. Tayari fedha hizi zimeingizwa kwenye Bajeti ya Wizara Fungu 41.

(vi) Tathmini ya Kutembelea Magereza ya Watoto Zanzibar iliyofanywa na Tume ya Haki za Binadamu itolewe. Aidha, zijengwe Mahabusu za watoto ili wasichanganyike na watu wazima.

Kamati ilielezwa kwamba tathmini iliyofanyika Zanzibar mwaka 2008/2009 imeshakamilika, kusambazwa na kujadiliwa na Baraza la Mapinduzi. Aidha, tathmini iliyofanyika Tanzania Bara Mwaka 2010/2011 imekamilika na kutolewa. Tathmini ilibaini kuwa watoto katika Mahabusu hawapatiwi huduma nzuri kama vile chakula na matibabu. Vile vile hatua zinachukuliwa ili kuboresha Mahabusu na katika Mahabusu nyingine, Watoto wanahifadhiwa sehemu tofauti wakati wa usiku.

(vii) Kamati ilishauri Mabaraza ya Ardhi, yawe chini ya Wizara ya Katiba na Sheria badala ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kamati ilielezwa kwamba Baraza la Mawaziri lilikwishatoa maelekezo ya Mabaraza ya Ardhi kuhamishiwa Wizara ya Sheria. Aidha, Tume ya Kurekebisha Sheria ilipewa jukumu la kufanya utafiti na kuishauri Serikali namna Mabaraza haya yatakavyofanya kazi chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, lakini hata hivyo, bado suala hili halijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hoja na ufafanuzi wa hoja uliotolewa, Kamati yangu haikuridhishwa na utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka 2011/2012 kwa baadhi ya Taasisi na Mafungu husika.

Changamoto mbalimbali ziliainishwa kuikabili Wizara na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

(i) Kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wizara na Taasisi zake, ni kidogo na hivyo kutokidhi mahitaji hasa ikizingatiwa kwamba kuna ongezeko la majukumu na pia Sekta ya Sheria inategemewa na Sekta nyingine katika kuimarisha uchumi wa nchi na maendeleo yake.

(ii) Kukosekana kwa fedha za Mpango wa Kuwezesha Mazingira Mazuri ya Kibiashara (*Business Enviromental Strengthening Tanzania Program - BEST*) ambayo unaratibiwa na *Tanganyika Law Society,* ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi jengo la Mahakama Kuu Divisheni ya Mahakama Ardhi na Uhaba wa Majaji.

(iii) Vitendo vya rushwa kuendelea kujitokeza katika baadhi ya vyombo vya utoaji haki, hali ambayo inasababisha wananchi kukosa imani na vyombo vya utoaji haki.

(iv) Suala la mikopo kwa Wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo kuendelea kuwa kero kubwa kwa Wizara na kwa wanafunzi husika ambao ni Wahitimu wa Shahada ya Kwanza. Hali hii inatokana na Sheria ya Bodi ya Mikopo inayotoa mikopo kuruhusu wanafunzi wa Shahada ya Kwanza *(undergraduate)* peke yake kupata mikopo hiyo.

(v) Mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa Watumishi walio wengi yanayotokana na masilahi duni na uhaba wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri.

(vi) Uwezo mdogo wa wananchi walio wengi kutumia vyombo vya kutoa haki na huduma za kisheria na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mfumo uliopo wa Sheria na Mahakama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kutoa maoni, maagizo na ushauri kwa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mabadiliko ya Katiba - Fungu 08, Kamati inatambua juhudi za Serikali kwa kuwezesha kukamilisha mchakato wa kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba yenye Sura ya Muungano. Sambamba na hilo, Kamati inapenda kutoa rai kwa wananchi wote nchini kutoa ushirikiano kwa Tume hii ili iweze kukamilisha vyema jukumu lake la kukusanya maoni ya Mabadiliko ya Katiba na kisha kuwasilisha mapendekezo hayo kwa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati yangu ilipokutana na Wizara ya Katiba na Sheria ili kujadili Makadirio na Matumizi ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Wajumbe waliweza kushauri kwa baadhi ya maeneo ya Fungu 08 ili kufanya maboresho zaidi. Kamati inapenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwa msikivu na kukubali ushauri wa Kamati uliolenga kuboresha hali ya kifedha ya Taasisi zilizopo katika Wizara ya Katiba na Sheria.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza wakati Kamati ilipokutana na Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati haikukubaliana na mapendekezo ya jumla ya Sh. 39,950,000,000/= zilizokuwa zimekadiriwa na Serikali kwa

mwaka wa fedha 2012/2013 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Tume ambayo yaliainishwa kama ifuatavyo:-

(a) Kuimarisha mfumo wa Taifa wa Sheria kwa kuratibu, kukusanya na kuchambua maoni ya Wananchi;

(b) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali na uwajibikaji kwa kuandaa mpango wa Bajeti ya Tume;

(c) Kuimarisha mifumo ya taarifa na mawasiliano kwa kuweka mifumo ya kisasa ya teknolojia ya habari na mawasiliano itakayorahisisha kukusanya na kurekodi kwa usahihi maoni yatakayotolewa na wananchi; na

(d) Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kununua vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri na kuwapatia stahili Wajumbe na Sekretariati ya Tume.

Hivyo basi, Kamati iliiagiza Wizara kuchukua muda zaidi ili iweze kupunguza Makisio ya Bajeti iliyokuwa imeandaliwa awali na hivyo, kuufanya mchakato wa Marekebisho ya Katiba kuendana na hali halisi ya uchumi wetu.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 9 Mei, 2012 Kamati ilikutana tena na Wizara ili kuangalia maboresho yaliyofanyika kwenye Fungu 08 kwa lengo la kutoa unafuu kwa mafungu mengine ya Wizara hii ambayo au yalikuwa na fedha kidogo za maendeleo zisizokidhi au hayakuwa na fedha yoyote.

Kamati inafurahi kutoa taarifa kwamba, Wizara iliweza kufanya maboresho na hivyo kufanikiwa kuokoa fedha Sh. 6,005,411,160 zilizotolewa kwenye Fungu 08 pasipo kuathiri shughuli za Tume ya Mabadiliko ya Katiba na Kamati ikapendekeza fedha hizo zigawanywe kwenye Taasisi zilizopo katika Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama iliweza kupata mgao wa ziada wa Sh. 71,716,000/=;

(b) Fungu 35 – Kurugenzi ya Mashitaka iliweza kupata mgao wa ziada wa Sh. 1,119,495,536/=;

(c) Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria iliweza kupata magao wa ziada wa Sh.1,314,754,000/=;

(d) Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliweza kupata mgao wa ziada wa Sh.1,643,445,924/=; na

(e) Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliweza kupata mgao wa ziada wa Sh.1,856,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya maboresho kwenye Fungu hili la 08, Kamati ilielezwa pia kwamba hivi sasa Fungu hilo limebakiwa na Sh. 33,944,588,849/= ambazo zitaiwezesha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kufanya shughuli zake pasipo vikwazo vyovyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaisisitiza Serikali kufuatilia kwa makini utendaji kazi wa Tume hii ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo lake la kupatikana Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo Aprili, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Idara ya Mahakama na kujionea utekelezaji wa majukumu ya Idara hiyo. Aidha, Katika Kikao cha Kamati na Wizara ilielezwa kwamba katika mwaka 2011/2012, hadi kufikia mwezi Aprili, 2012, Tume ya Utumishi wa Mahakama iliandaa na kuratibu vikao vitatu vya kawaida, na kikao kimoja cha dharura. Pia, katika vikao hivyo vya kawaida, Tume iliajiri katika Masharti ya Kudumu na Malipo ya Pensheni Mahakimu 40, imethibitisha katika Cheo cha Mahakimu 68 na imepandisha cheo Mahakimu 71. Kamati inaiagiza Serikali kuongeza fedha zaidi na kuisaidia Tume hii ili iweze kukamilisha vyema majukumu yake, kwani kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu hasa wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati inazidi kurejea agizo lake lililotolewa mwaka 2011 kwamba sheria zote zinapoletwa Bungeni ziandikwe kwa lugha zote mbili za Kiswahili, na Kingereza. Kamati inashauri kitengo maalum kinachoshughulikia masuala ya kutafsiri Sheria katika Lugha ya Kiswahili au Kingereza kilichopo ndani ya Divisheni ya Uandishi wa Sheria, kiwezeshwe kwa utaalamu zaidi ili kumudu jukumu hili ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasikitishwa sana na hali mbaya ya uendeshaji wa Mashauri nchini. Taarifa zilizotolewa mbele ya Kamati na Waziri mwenye dhamana na Wizara hii zilionyesha kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2011/2012 hadi kufikia mwezi Mei, 2012 Mashauri 5,259 sawa na asilimia sita yalikuwa

yamehitimishwa na kubaki Mashauri 84,974 yatakayoendelea kuendeshwa katika ngazi mbalimbali za Mahakama pamoja na mapya yatakayopokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ni hatari sana kwa mustakabali wa utoaji haki nchini, kwani ikumbukwe kwamba haki inayocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa *(Justice Delayed is Justice Denied).*

Kamati inaiagiza Serikali kuongeza idadi ya watumishi hasa Mahakimu na Mawakili wa Serikali wa Kada mbalimbali ili kuongeza kasi ya uendeshaji wa Mashauri mbalimbali nchini kwa lengo la kulipatia ufumbuzi suala la mlundikano wa Mashauri Mahakamani linalosababisha pia msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado suala la Serikali kuingia Mikataba mibovu na Makampuni mbalimbali hasa ya Kigeni ni jambo linalosumbua jamii ya Watanzania. Hali hii inatafasiriwa kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Serikali ambayo imepewa dhamana ya kuishauri Serikali kabla ya kuingia Mkataba ama inajihusisha na rushwa au Watumishi wake hawana utaalam wa kutosha kuhusiana na Mikataba hii ya Kigeni. Kamati inaiagiza Serikali kuchukulia eneo hili kwa umuhimu wa kipekee, kwani lina athari hata kwenye uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Aidha, Serikali itoe mafunzo ya kutosha kwa Mawakili waliopo ili kupunguza gharama kubwa zinazotumika kulipia Makampuni binafsi hasa katika maeneo mapya ya makosa ya kutakatisha fedha *(Money Laundry, asset forfeiture and recovery na Trans National Crimes).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Fungu 18 – Makahama Kuu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati uliotolewa mwaka 2011 na hivyo kuongeza idadi ya Majaji 10 wa Mahakama kuu na mbili wa Mahakama ya Rufani ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli za Mahakama Ngazi ya Mahakama Kuu.

Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba hivi sasa kumeanza kujitokeza manung'uniko upande wa wananchi kwamba kuna kasoro za uandishi wa kesi na Mashauri Mahakamani pamoja na utoaji wa hukumu zenye utata. Tuhuma hizi japo hazina ushahidi wa moja kwa moja, bado haziwezi kubezwa na hivyo Kamati inapenda kutoa ushauri kwa Serikali hususan upande wa Mahakama kutoa mafunzo ya mara kwa mara hasa kwa Majaji/Mahakimu wapya kuhusu namna bora ya uendeshaji wa Mashauri katika ngazi ya Mahakama ili kudumisha imani kwa chombo hiki muhimu katika utoaji wa haki. Aidha, Kamati inazidi kusisitiza kwamba, Serikali izidishe kasi ya ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu ili kufikia lengo la kuwa na Mahakama Kuu kwa kila Mkoa kuliko ilivyo kwa hivi sasa ambapo Mahakama Kuu ya Tanzania ina Kanda 13 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imestushwa na taarifa kwamba takriban Majaji wapatao 30 nchini wanaishi kwenye nyumba za kupanga na kwamba wengi wao wameshatishiwa kutolewa kwenye nyumba hizo kwa sababu ni zaidi ya miaka mitatu kodi za nyumba hizo hazijalipwa. Kamati inaliona jambo hili kuwa linadhoofisha ari ya kufanya kazi kwa Majaji hawa na pengine ikawa siyo rahisi kutoa maamuzi ya haki kwenye mazingira hatarishi kiasi hiki. Kamati inaiagiza Serikali kutoa ufafanuzi wa Taarifa hizi ikiwa ni pamoja na mikakati inayochukuliwa ili

lisitokee tena. Aidha, Serikali itoe ufafanuzi pia wa Taarifa kwamba hivi sasa ni mwaka wa tano stahili za Majaji zimeidhinishwa, lakini Serikali haijazilipa hadi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Fungu 35 - Mkurugenzi wa Mashitaka, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka kwa kusimamia vyema uendeshaji wa Mashauri ya Jinai na Uratibu wa Kazi zinazofanywa na Vyombo vya Upelelezi. Kamati inapenda kupata ufafanuzi wa jinsi Ofisi zote mbili za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashitaka ambazo zinaundwa kwa mujibu wa Katiba zitaweza kufanya kazi bila ya migongano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inazidi kuipongeza Serikali kwa azma yake ya kutenganisha mashitaka na shughuli za upelelezi. Jambo hili limekuwa siku zote linazua wasiwasi wa kutotendeka haki kutokana na vyombo vilivyokasimiwa madaraka makubwa ya kukamata watuhumiwa, kufanya upelelezi na kufungua kesi kupewa pia jukumu la kuendesha mashitaka.

Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha zaidi Kibajeti Divisheni ya Mashitaka ili iweze kutekeleza mpango wake wa kutenganisha Mashitaka na Upelelezi *(Civilinazation of Prosecution Service)* kwa nchi nzima, kwani bado kuna maeneo mengine ya nchi yetu kwenye Mikoa na Wilaya ambapo mpango huo haujafika na hivyo kuendeleza wasiwasi katika mfumo wa utoaji haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Fungu 40 – Mahakama, Kamati inatambua juhudi za Serikali na kwa kukubali ushauri wa Kamati uliotolewa mwaka 2011 na

hivyo kubadilisha Muundo wa Utumishi wa Mahakama kwa kuajiri Mahakimu 300 waliohitimu Shahada ya Sheria kutoa huduma kwenye Mahakama za Mwanzo. Mageuzi hayo ya Mfumo wa Mahakama yana changamoto zake, kwani vijana hawa wasomi itabidi wakakae na kufanya kazi kwenye maeneo ya Vijiji ambako katika mazingira ya kawaida, imekuwa ni vigumu kwa vijana wengi kuyaafiki. Kamati inaiomba Serikali kuboresha miundombinu ya Mahakama za Mwanzo ikiwa ni pamoja na utoaji wa motisha kwa Mahakimu hawa wapya ili waweze kutekeleza majukumu yao kwenye mazingira rafiki.

Aidha, Kamati inaunga mkono dhamira ya Mahakama ya kufanya mabadiliko katika mfumo wake wa Utawala ili kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wake, kwani kwa kupitia Sheria yake mpya ya *Judiciary Administration Act No.* 4 ya Mwaka 2011, kumeanzishwa kada mpya ya Mtawala wa Mahakama *(Chief Court Administrator)*. Kada hii mpya itashughulikia masuala ambayo siyo ya Mahakama na kuwapatia fursa Wasajili kushughulikia masuala ya Kimahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inafuatilia kwa karibu utendaji kazi wa Mahakama kama Taasisi iliyopo chini ya Wizara tunazozisimamia. Kamati inadhani kuwa, hivi sasa umefika wakati kwa Mahakama zetu kufanya kazi kwa teknolojia ya juu zaidi kulikoni inavyofanyika hivi sasa. Baadhi ya mambo ambayo Kamati inaona ni vyema yakabadilishwa kimfumo. Ni uandishi wa mashauri Mahakamani ambapo Hakimu au Jaji hulazimika kuandika kwa mkono maneno ya shahidi au Mtuhumiwa wakati shauri likiendelea. Mfumo huu siyo wa uhakika sana kwa sababu Hakimu au Jaji ni binadamu na hivyo kuna

uwezekano mkubwa wa kuongeza au kupunguza maneno yanayotolewa na shahidi au mtuhumiwa. *(Makofi)*

Kamati inaamini hii imekuwa ni mojawapo ya sababu kubwa ya ongezeko la malalamiko dhidi ya maamuzi ya kesi nyingi na hivyo Kamati inashauri kwamba ni vyema mfumo wa *Hansard* ukaanza kutumika ili kudhihirisha kwamba siyo tu haki inatendeka, bali pia inaonekana kutendeka. *(Justice must not only be done, but must be seen done).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaiagiza Serikali kuimarisha mfuko wa Mahakama Kibajeti ili mfuko huo uweze kukidhi haja za mahitaji ya Mahakama. Moja ya Mahitaji ambayo bado ni changamoto kwa Mahakama pamoja na juhudi kubwa zinazoendelea kuchukuliwa ni kupunguza uchache wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo zipatazo 1105 kote nchini zinazohudumiwa na Mahakimu 750 tu wakati mahitaji halisi ni Mahakimu 2210.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inathamini mchango mkubwa unaotolewa na Wazee wa Mahakama, kwani jambo hilo linatoa fursa kwa jamii kushiriki katika masuala ya utoaji haki *(Community Participation in Justice).* Hata hivyo, Kamati inaona ni vyema Serikali ikaangalia upya ushirikishwaji huo, kwani kwa kiasi kikubwa inaweza kuwa sababu mojawapo ya mlundikano wa mashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara ya Katiba na Sheria – Fungu 41, bado Wizara hii imeendelea kuwa na ufinyu wa Bajeti pamoja na maombi ya Kamati kwa miaka yote miwili iliyopita ili Wizara iongezewe Bajeti na hivyo kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha. Kamati inazidi

kuisisitiza Serikali kwamba pamoja na uwezo mdogo uliopo, bado ipo haja ya kuiongezea Bajeti Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mmoja wetu hapa Bungeni ni shahidi wa matatizo yaliyopo katika maeneo yetu kutokana na mfumo wa utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya ardhi. Migogoro mingi ya ardhi inatokana na suala hilo kushughulikiwa na Wizara tatu, yaani Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria. Kamati inaamini kabisa kwamba mfumo huu una mapungufu ya kutatua migogoro ya ardhi nchini. Kamati inashauri kwamba, kwanza ufanyike utafiti wa Sheria na Migogoro ya Ardhi na kisha suala la utatuzi wa migogoro ya ardhi likasimamiwe kwa Wizara moja hususani ya Katiba na Sheria, kwani migogoro hiyo kwa kiasi kikubwa inahusisha taratibu na tafsiri za kisheria. Aidha, Kamati inasisitiza kwamba, Serikali iongeze kasi ya kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Mfumo wa Utoaji haki katika masuala ya Madai *(Civil Justice System)* ili kupata suluhisho la kudumu kuhusu usuluhishi wa migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inazidi kuhimiza Serikali kutekeleza ushauri uliotolewa na Kamati mwaka 2011/2012 kwamba ni vyema na mapema iwezekanavyo Serikali ilete mbele ya Bunge lako Sheria zenye matatizo, zinazokinzana na zilizopitwa na Wakati ili ziweze kurekebishwa, kwani Sheria hizo zimekuwa ni kikwazo na kuathiri dhana nzima ya utoaji wa haki nchini. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(Registration, Insolvency and Trusteeship Agency-RITA)* ndicho chombo chenye dhamana ya kusajili matukio

muhimu ya maisha *(key life events)* yakiwemo matukio ya vizazi na vifo.

Hata hivyo, hali ya usajili wa matukio haya muhimu nchini bado iko chini. Takwimu za mwaka 2010 zilizotolewa na Ofisi ya Takwimu ikishirikiana na Shirika la kuhudumia watoto Duniani *(UNICEF)* kupitia Ripoti ya Utafiti na Demografia ya Afya Tanzania *(TDHS)* zinaonyesha kuwa usajili wa vizazi kwa kundi la watoto walio na umri chini ya miaka mitano kwa Tanzania Bara uko kwenye 14.5%. Kati ya hao ni 6.2% tu wenye vyeti vya kuzaliwa. Ripoti hiyo pia inaonyesha kuwa watoto wanaozaliwa nchini kwa mwaka ni kati ya 1,500,000 hadi 1,800,000. Hiki ni kiwango kikubwa sana ambacho zaidi ya watoto 1,300,000 kwa mwaka hawasajiliwi wala kupewa vyeti vya kuzaliwa na hivyo hawajulikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaiagiza Serikali kuiwezesha kibajeti Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ili iweze kutekeleza mpango wake ilioubuni wa *U5BRI (Under five Birth Registration Initiatives)* ili kuongeza kiwango cha Usajili na kutoa Vyeti hasa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba moja ya vikwazo vinavyofanya Usajili kuwa chini ni ada ya Serikali inayolipwa pamoja na gharama nyingine anazoingia mzazi pale anapohitaji kupewa Cheti cha Kuzaliwa kwa ajili ya mtoto wake kule Wilayani ambako umbali ni kati ya km 5-100 kutoka Vijiji vingine.

Kamati inaiagiza Serikali kuchukua maamuzi ya haraka ili kuondoa ada hiyo hasa kwa kundi la watoto walio na

umri wa chini ya miaka mitano kwa cheti cha kwanza tu *(first issue).* Hii pia itaendana sanjari na mipango mingine ya Serikali ya kutoa huduma za afya bure kwa watoto wote walio na umri wa chini ya miaka mitano. Utaratibu huu unatumika na baadhi ya nchi nyingine za Afrika kama vile Burundi na Nigeria zimefanikiwa kuongeza viwango vya usajili kwa watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, Serikali itapata takwimu sahihi kwa ajili ya mipango yake ya maendeleo, lakini pia Serikali itakuwa imejiweka kwenye nafasi nzuri ya kupimwa hasa katika kutimiza malengo ya Milenia, MKUKUTA na kuliweka Taifa la Tanzania kwenye taswira nzuri Kimataifa kwamba inajali haki za binadamu za wananchi wake. Aidha, upungufu wa mapato utapunguzwa pale ambapo mtoto ataombewa au atataka kupata nakala ya pili kwa kupotea au kama atataka nakala ya Kompyuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo Sura 108 kama ilivyorejewa mwaka 2002 inatamka kuwa: "Tukio la Kizazi au Kifo lifanyike kwenye Wilaya lilipotokea na Katibu Tawala wa Wilaya ndiye Msajili wa Wilaya." Kwa mantinki hiyo, Mfumo wa Usajili umeishia Wilayani na hivyo kutengeneza pengo kati ya mahali matukio yanapotokea na wakati mwingine kusajiliwa (Mahospitalini 50% na Majumbani 50%) na mahali ambapo cheti halisi cha kizazi au kifo kinatolewa, yaani kwa Katibu Tawala Wilaya. Hii imekuwa ikisababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi, kwani inaongeza gharama kwa kukifuata cheti Wilayani ambako Vijijii vingine viko zaidi ya kilometa 100 na hivyo kusababisha wananchi hata kama wamesajiliwa wasifuate Vyeti hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, itambulike kwamba mahali ambapo matukio haya yanatokea yaani kwenye Vituo vya tiba (50%) ambavyo viko chini ya Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO) au Majumbani (50%) ambako kuna Watendaji wa Vijiji/Mitaa na Kata, Watendaji wote hawa wako chini ya Mfumo wa Serikali za Mitaa na hawawajibika kwa Katibu Tawala na hivyo kusababisha shughuli za Usajili kutotekelezeka ipasavyo. Kamati inashauri Serikali itafute mfumo ambao utaleta ufanisi mzuri wa upatikanaji wa vyeti hivyo pasipo usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, nawashukuru Mheshimiwa Mathias M. Chikawe - Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki - Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vile vile, nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya Kujadili na Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2012/2013. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Sheria. Uendeshaji, Haki za Binadamu na Utawala Bora umesaidia kufanikisha kazi hii

kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana - Mwenyekiti, Mheshimiwa John P. Lwanji -Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Abas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Azza H. Hamad, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa Jason S. Rweikiza, Mheshimiwa Rashid Ali Abdalllah, Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed, na Mheshimiwa Dkt. Hadji H. Mponda. *(Makofi)*

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, namshukuru Ndugu Peter Magati - Katibu wa Kamati hii, na Ndugu Catherine Kitutu - Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka huu wa fedha 2012/2012 na naomba nifanye hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imeanzishwa kwa mujibu wa kipengele cha 12 cha Nyongeza ya Waraka wa Rais uliochapishwa kama Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba 2010. Majukumu ya Ofisi hii yameainishwa katika Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2010 *(The Ministers [Assignment of Ministerial Functions] Notice, 2010*) lililochapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Desemba 2010. Kwa mujibu wa Nyongeza ya Pili ya Tangazo hilo, pamoja na mengine, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imekasimiwa majukumu ya masuala ya kikatiba, uendeshaji na utoaji wa haki, uendeshaji mashtaka na haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 wakati nawasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, 2011 nililiambia Bunge lako Tukufu kwamba: “ Tatizo kubwa linalozikabili mahakama zetu sio uhaba wa uwezo wa kusimamia fedha zinazotolewa kwa ajili yao, bali ni uhaba wa fedha zenyewe! Pili, tatizo la uhaba wa fedha linasababishwa na ukosefu wa uelewa wa mahitaji halisi ya

Mahakama. Tatu, tatizo la ukosefu wa uelewa wa mahitaji halisi ya Mahakama linasababishwa na ukosefu wa watu wanaoelewa mahitaji hayo Serikalini au ukosefu wa wafanya maamuzi ya migawanyo ya fedha wanaofahamu mahitaji halisi ya Mahakama." Tatizo la vipaumbele vya Mahakama kutozingatiwa katika migawanyo ya bajeti za Serikali za kila mwaka limeendelea katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Maelezo ya Makadirio ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013 kwa Fungu la 40 kwamba Mahakama, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mahakama ya Rufani iliidhinishiwa Shilingi bilioni 33.201. Kwa mujibu ya maelezo hayo, hadi mwezi Mei, 2012 Mahakama ya Rufani ilikuwa imepokea Shilingi bilioni 26.251 au asilimia 79 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Matokeo ya kuipatia Mahakama ya Rufani fedha pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa, Maelezo ya Wizara yanasema kwamba, Mahakama ya Rufani iliweza kufanya vikao 26 kati ya 30 vilivyokuwa vimetarajiwa kufanyika katika kipindi hicho.

Kwa upande wa Mahakama Kuu, Maelezo ya Wizara yanasema kwamba, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mahakama Kuu iliidhinishiwa Shilingi bilioni 19.569. Hadi mwezi Mei 2012, Hazina ilikuwa imetoa Shilingi bilioni 12.919 zikiwa ni Shilingi bilioni 6.159 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi bilioni 6.759 kwa ajili ya mishahara.

Hii ina maana kwamba Mahakama Kuu ilipatiwa asilimia 66 ya bajeti yake. Mfuko wa Mahakama *(Judiciary Fund)* ambao ulipigiwa upatu mkubwa wakati wa mjadala wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama kwamba ndiyo

mwarobaini wa matatizo ya fedha za Mahakama, uliidhinishiwa Shilingi bilioni 20 katika mwaka wa fedha 2011/2012. Hata hivyo, kiasi kilichotolewa ni Shilingi bilioni 14.548 au asilimia 72.74 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge hili Tukufu. Kwa rekodi hii, ni wazi kwamba hata kiasi cha Shilingi bilioni 28.38 ambazo, kwa mujibu wa randama ya Fungu 40 - zimetengwa kwa Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2012/2013 zitatolewa chini ya nusu ya makadirio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelezo ya Wizara yametoa takwimu zinazoonyesha mafanikio makubwa katika kusikiliza na kutoa maamuzi ya Mashauri katika Mahakama zetu za ngazi zote. Hivyo, kwa mfano, tunaambiwa kwamba katika vikao 26 kati ya 30 vya Mahakama ya Rufani, asilimia 143 ya Mashauri yaliyofunguliwa yalisikilizwa na kutolewa maamuzi. Aidha, tunaambiwa na Wizara, "Mahakama Kuu imefanikiwa kusikiliza na kuyatolea maamuzi asilimia 123 ya Mashauri yaliyofunguliwa. Kwa upande wao, Mahakama za Hakimu Mkazi na za Wilaya zilifanikiwa kusikiliza na kuyatolea maamuzi asilimia 125 na 109 za Mashauri yaliyofunguliwa, wakati ambapo Mahakama za Mwanzo zimefanikiwa kwa asilimia 99.7 katika kusikiliza na kutoa maamuzi ya Mashauri yaliyofunguliwa katika Mahakama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hali halisi ingekuwa ndiyo hii inayoelezewa na Wizara, basi ni wazi kwamba nchi yetu ya Tanzania isingekuwa na tatizo la mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu zote. Kwa hiyo, Wizara isingetaja kama mojawapo ya changamoto za Mahakama ya Tanzania, *"ongezeko la Mashauri, hivyo kusababisha mlundikano wa mashauri mahakamani."* Wala Wizara

isingekuwa na changamoto za bajeti finyu isiyokidhi majukumu ya Mahakama, au ya fedha kutokutolewa kadiri ya mpango wa kazi wa mwaka na kwa wakati, kama inavyodaiwa katika Maelezo ya Wizara, yanayotangaza mafanikio makubwa katika usikilizaji wa Mashauri na utoaji wa maamuzi ya Mashauri hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, kwa jinsi zilivyowasilishwa katika maelezo ya Wizara, takwimu za mafanikio ya Mahakama ya Tanzania katika kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri zinapotosha ukweli ambao upo katika maelezo hayo hayo. Hivyo, kwa mfano, licha ya maelezo ya Wizara kutaja mafanikio mazuri yaliyopatikana, maelezo hayo hayo yanaonyesha kwamba, kwa sababu ya bajeti finyu isiyokidhi majukumu ya Mahakama, Mahakama ya Rufani ilifanikiwa kupunguza mlundikano wa Mashauri kwa asilimia 10.7 tu. Aidha, kwa sababu hiyo hiyo ya bajeti finyu, Mahakama Kuu ilifanikiwa kupunguza mlundikano wa Mashauri kwa asilimia sita wakati Mahakama za Hakimu Mkazi na za Wilaya zilifanikiwa, kwa mlolongo huo huo, kupunguza mlundikano wa Mashauri kwa asilimia 9.4 na asilimia 11.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo kusema kwamba wastani wa mafanikio ya kupunguza mlundikano wa mashauri katika Mahakama zetu ni asilimia 9.4 tu, kwa ushahidi huu wa Serikali yenyewe, kwa sababu ya kutopatiwa fedha za kukidhi mahitaji halisi ya utoaji wa haki. Mahakama ya Tanzania imeshindwa kabisa kutatua tatizo la mlundikano mkubwa wa kesi katika ngazi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya maendeleo ya Mahakama ya Tanzania vile vile imekumbwa na tatizo la

mgawanyo mbovu wa fedha. Hili nalo linaelekea kuwa tatizo sugu. Kwa mfano, Maelezo ya Wizara yanasema kwamba katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mahakama ya Tanzania ilitengewa Shilingi bilioni 13.546 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Mei, 2012 Mahakama ilikuwa imepokea Shilingi bilioni 2.285 kutoka Hazina, ikiwa ni asilimia 16.86 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Ijapokuwa Serikali inaita kazi zilizofanyika kwa fedha hizi pungufu kuwa ni mafanikio mazuri, ni vigumu kukubaliana na tathmini hii. *(Makofi)*

Kwanza, hata kwa mapambo ya lugha ya kirasimu ya aina hii, ni vigumu kuamini kwamba kazi zilizofanywa na asilimia 16.86 ya gharama zilizotarajiwa zinaweza kuleta mafanikio mazuri. Vinginevyo, Serikali iwaeleze Watanzania kwa nini ililiomba Bunge hili Tukufu liidhinishe Shilingi bilioni 13.546 kama ilikuwa inajua kwamba mgawo wa Shilingi bilioni 2.285 utaleta mafanikio mazuri? *(Makofi)*

Pili, Serikali yenyewe imekiri kwamba Mahakama ya Tanzania ilikumbana na changamoto ya bajeti finyu isiyokidhi majukumu ya Mahakama. Aidha, Serikali inakiri kwamba kuna matatizo ya upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, kompyuta, uduni wa mazingira ya kazi na nyumba za kuishi watumishi hususan Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa umma. Vile vile, hali ya majengo ya Mahakama haijaridhisha kiasi cha kutosheleza mahitaji, kwani kiasi cha fedha za maendeleo kinachotolewa na Serikali ni kidogo sana ukilinganisha na idadi na hali halisi ya majengo ya Mahakama hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kama ni kweli, kama inavyodaiwa kwenye maelezo ya Wizara kwamba suala la

usafiri kwa ajili ya shughuli za Mahakama limepewa uzito unaostahili kwa Serikali kununua magari manne kwa ajili ya Waheshimiwa Majaji, inakuwaje basi katika maelezo hayo hayo Serikali inakiri kwamba upungufu wa vitendea kazi kama vile magari na kadhalika bado ni changamoto kubwa? Ukweli ni kwamba kauli za aina hii zinalenga kuficha ukweli wa hali halisi ambayo ni mbaya sana.

Kwa mfano, Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Singida inayohudumia Mkoa mzima wa Singida wenye Mahakama tatu za Wilaya na Mahakama zaidi ya 40 za Mwanzo, haina gari hata moja na inategemea gari moja la Mahakama ya Wilaya ambalo nalo halifanyi kazi kwa sababu ya ukosefu wa spea. Kwa hali ilivyo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Singida haiwezi kuwa ni mfano wa kipekee wa mapungufu haya, kwani Mahakama nyingine nyingi za Hakimu Mkazi na za Wilaya zinakabiliwa na matatizo ya aina hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya mwaka 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilielezea upungufu mkubwa wa watumishi wa ngazi mbali mbali wa Mahakama ya Tanzania ambao ni matokeo ya moja kwa moja ya kunyimwa fedha na Serikali. Tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi wowote, na kuna uwezekano kwamba linazidi kuwa kubwa zaidi. Kwa mujibu wa maelezo ya Wizara: “Uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa bado unaendelea kuwa tatizo. Maslahi yasiyokidhi hali ya utendaji katika Mahakama inapelekea baadhi ya watumishi kuacha kazi.”

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mahakama ya Tanzania imeendelea kufedheheka kwa kuwa mdeni mkubwa na sugu. Hadi wakati tunaandika maoni haya,

Mahakama ya Tanzania inadaiwa na Majaji na Watumishi wengine wa Mahakama, watoa huduma, wenye nyumba za kupangisha Majaji, wajenzi na Wazabuni mbalimbali jumla ya Shilingi bilioni 5.2. Yote haya ni madeni ya miaka ya nyuma hadi kufikia mwaka wa fedha 2010/2011!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Malipo na Mafao ya Majaji *(Judges (Remuneration and Terminal Benefits, Act*) ya mwaka 2007, Majaji wanastahili kulipiwa, nje ya malipo ya mshahara, nyumba yenye samani ya Daraja A; gharama za matibabu kwa ajili yao wenyewe na familia zao; gari ya Serikali pamoja na dereva. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kuwa kila Jaji Mteule, huandikiwa barua ya ajira kutoka Ofisi ya Rais inayofafanua stahili hizi.

Hata hivyo, kwa sababu ya kutokupatiwa fedha zinazokidhi mahitaji ya Mahakama, sasa Majaji wetu wanaishi katika nyumba za kupanga ambazo zinadaiwa kodi na wenye nyumba. Wanalazimika kujilipia gharama za matibabu yao na ya familia zao, na baadhi wanatembelea mikweche ya magari. Fedheha hizi kwa Majaji wetu na Watumishi wengine wa Mahakama ya Tanzania zinaonyesha siyo tu ukiukwaji makusudi wa sheria tajwa, bali zinathibitisha jinsi gani ambavyo mfumo wa utoaji haki na uhuru wa Mahakama haujawa kipaumbele cha Serikali hii ya *CCM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipendekeza, wakati wa mjadala wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama, kwamba badala ya Mahakama kutegemea ukomo wa bajeti unaowekwa na Hazina, sheria ielekeze kama ilivyo kwa

Bunge na Vyama vya Siasa, vyenye Uwakilishi Bungeni na nchi jirani ya Kenya, kwamba bajeti ya Mahakama ya kila mwaka isiwe pungufu ya asilimia tatu ya bajeti ya kila mwaka ya Serikali ili kuiwezesha Mahakama kuwa na uhakika wa fedha zake na kuiwezesha kupanga mipango yake kwa uhakika zaidi. Pendekezo langu lilikataliwa.

Matatizo ya bajeti ya Mahakama ambayo tumeyaeleza hapa yanathibitisha wazi kwamba utaratibu wa sasa wa kutegemea mgawo wa Hazina hauwezi kutatua matatizo ya fedha ya Mahakama ya Tanzania. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli Bungeni ni kwa nini inakataa kuihakikishia Mahakama fedha zake kwa kurekebisha Sheria ya Uendeshaji Mahakama ili kuweka *a minimum percentage* ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya Mahakama, kama ilivyofanya kwa Bunge na kwa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki iliyocheleweshwa ni haki iliyonyimwa. Ndiyo maana ibara ya 107A(2)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inatamka kwamba “Katika kutoa uamuzi wa Mashauri ya Madai na Jinai kwa kuzingatia sheria, Mahakama zitafuata kanuni zifuatazo, yaani, kutochelewesha haki bila sababu ya msingi.” Takwimu za Mahakama ya Tanzania juu ya mlundikano wa kesi katika ngazi mbalimbali za Mahakama zinaonyesha jinsi hali ilivyo mbaya. Kwa mfano, hadi tunaandika maoni haya, Mahakama ya Rufani ina mlundikano wa kesi 1,743; Mahakama Kuu kesi 8,911; Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara kesi 285; Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kesi 1,238; na Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi kesi 5,543.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mlundikano wa kesi katika ngazi za chini katika Mahakama ya Tanzania ni mbaya zaidi. Kwa mfano, Mahakama za Hakimu Mkazi zina *backlog* ya kesi 25,002; Mahakama za Wilaya kesi 31,025 na Mahakama za Mwanzo kesi 124,959.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushahidi huu, ni wazi kwamba Mahakama ya Tanzania imeshindwa kutekeleza wajibu wake huu wa kikatiba kwa sababu ya kunyimwa fedha na vitendea kazi vingine na Serikali hii inayodai kwamba dira yake ni "haki kwa wote na kwa wakati." Kwa maana nyingine, maelfu ya mahabusu na wafungwa ambao wamejaa katika Magereza yetu wakisubiri maamuzi ya kesi zao, na maelfu ya wadaawa ambao kesi zao zimelundikana katika Mahakama zetu zote wanateseka kwa sababu sera za utoaji haki za Serikali hii ya *CCM* hazitekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, na dawa ya Serikali na Chama ambacho sera zake hazitekelezeki na hivyo kusababisha mateso kwa wananchi ni ile aliyoigusia Baba wa Taifa katika kitabu chake cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania: "Hatulazimiki kuendelea na uongozi mbovu wa Chama na Serikali. Wala tukiendelea na hali hii, bila kubadili uongozi wa Chama na Serikali, sina hakika kama tutafika huko salama. Masuala muhimu ya nchi yetu hayatashughulikiwa, na masuala mengine muhimu yataachwa yajitatue yenyewe. Nasema katika hali kama hiyo sina hakika kama tutafika salama; na tukifika salama tukiwa na uongozi huu huu wa Chama na Serikali, mbele kutakuwa ni giza tupu. Majuto ni mjukuu, huja baadaye."

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, nakuomba dakika moja tu, ukae kidogo tu, kwa suala la kuweka sawasawa Meza hapa, halafu utaendelea. Kwa vile, hotuba yako itakwenda, itazidi kidogo saa 7.00, naomba nichukue nafasi hii, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, atuongoze ili tupate muda zaidi kidogo, ili tuweze kusikiliza hotuba hii na tupate mchangiaji mmoja, au wawili hivi asubuhi hii.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuchelewa kuanza kwa ratiba hii ya leo ya Hotuba hii, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuongeza nusu saa baada ya saa 7.00 kamili, ili angalau hotuba hii pamoja na kupata nafasi ya Wachangiaji angalau wawili katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuongeza nusu saa baada ya saa 7.00 kamili.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliridhia Hoja ya Kuongeza Muda)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa, nakuomba Mheshimiwa Tundu Lissu, uendelee. Makatibu, naomba muangalie muda wake.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI & WAZIRI KIVULI, SHERIA, KATIBA NA UTAWALA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sasa naomba kuzungumzia Uteuzi wa Majaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua ukweli kwamba Mheshimiwa Rais Kikwete ameteua Majaji wengi wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano kuliko Marais wengine wote waliomtangulia kwa ujumla wao. Rekodi hii peke yake inaonyesha kwamba Rais anatambua umuhimu wa Mahakama Kuu kuwa na Watendaji wa kutosha wa utoaji haki ili kutekeleza dira ya 'haki kwa wote na kwa wakati.'

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuteua Majaji wengi ni jambo moja. Kuteua Majaji wengi wenye uwezo, ujuzi na wanaofaa kukabidhiwa madaraka ya Jaji wa Mahakama Kuu ni jambo lingine kabisa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa na dalili zinazoanza kuonekana wazi kwamba baadhi ya Majaji walioteuliwa na Rais hawana uwezo, ujuzi na/au hawakufaa kukabidhiwa madaraka ya Jaji ya Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ibara ya 109(6) ya Katiba, mtu anaweza kuteuliwa Jaji wa Mahakama Kuu ikiwa ana sifa maalum, na amekuwa na mojawapo ya sifa maalum kwa muda usiopungua miaka kumi. Sifa hizo, kwa mujibu wa ibara ndogo ya (7), maana yake ni: "mtu aliye na shahada ya sheria kutoka Chuo Kikuu kinachotambuliwa na Mamlaka ya Ithibati Tanzania na amekuwa Hakimu; amefanya kazi katika Utumishi wa Umma akiwa na sifa za kufanya kazi ya Uwakili au ni Wakili wa

kujitegemea; ana sifa ya kusajiliwa Wakili, na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi." Sharti la kuwa na sifa hizo kwa miaka kumi mfululizo linaweza kutenguliwa endapo Rais, baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama, atatosheka kwamba mhusika ana uwezo, ujuzi na kwa kila hali, anafaa kukabidhiwa madaraka ya Jaji wa Mahakama Kuu na kuna sababu za kumfanya mtu huyo astahili kukabidhiwa madaraka hayo",(Ibara ya 109(8).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama inaundwa na Jaji Mkuu ambaye ni Mwenyekiti wake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufaa atakayeteuliwa na Rais kwa kushauriana na Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi na Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais. Jukumu la kwanza la Tume hii, kufuatana na ibara ya 113(1)(a): "ni kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu."

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba utaratibu huu wa uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu ulilenga kumwezesha Rais, ambaye sio lazima awe Mwanasheria na/au mwenye ufahamu wa masuala ya kisheria kuteua Majaji baada ya kupata ushauri kutoka kwa Viongozi waandamizi wa Mahakama ya Tanzania na pia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye anawajibika kikatiba: "Kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mambo yote ya kisheria." (ibara ya 59(3). Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Rais hana mamlaka ya kufanya uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu nje ya utaratibu huu uliowekwa na Katiba. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina taarifa kwamba utaratibu huu wa kuteua Majaji umeachwa kufuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa tulizonazo sasa, watu wanateuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ambao hawajawahi kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama, na kwa sababu hiyo, hawajafanyiwa *vetting* yoyote na mamlaka hiyo ya kikatiba juu ya uwezo na ujuzi wao, na kama wanafaa kwa kila hali kukabidhiwa madaraka ya Jaji wa Mahakama Kuu. Inaelekea watu hao wengi wao wakiwa wamekaribia muda wao wa kustaafu kwingineko katika utumishi wa umma, wanapewa zawadi ya Ujaji ili kuwawezesha kupata mafao ya Majaji wastaafu ambayo yameboreshwa sana katika miaka ya karibuni. Matokeo yake ni kuwa na Majaji ambao wamechoka, na hawawezi au hawajui namna ya kufanya kazi ya Jaji wa Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya kukiuka utaratibu huu wa kikatiba wa uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu ni makubwa na yameanza kujitokeza wazi. Kwanza, wapo Majaji ambao, kwa sababu ya kutokufanyiwa *vetting* na Tume ya Utumishi wa Mahakama, hawana uwezo wa kuandika mwenendo wa Mashauri na hukumu zinazosomeka kwa sababu ya, ama kutokuwa na uwezo na ujuzi wa sheria, au kutokuwa na weledi wa lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo lugha rasmi ya mwenendo wa Mashauri na hukumu.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba wapo Majaji ambao kwa sababu hizo hizo za kutokufanyiwa *vetting* juu ya uwezo na ujuzi wao na mamlaka husika ya kikatiba, wameshindwa kabisa kuandika hukumu za kesi walizozisikiliza na hivyo

kusababisha mlundikano wa kesi Mahakamani usiokuwa na sababu yoyote ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kazi ya Jaji wa Mahakama Kuu, kama ilivyo kazi ya Mawakili na Wanasheria kwa ujumla, ni kazi ya kisomi. Ni kazi inayohitaji watu wenye uwezo mkubwa kitaaluma na utafiti, weledi wa uchambuzi (*analytical skills*) na wa kuandika na kuzungumza kwa lugha ya kimombo fasaha. Watu hawa hawaitwi 'wanasheria wasomi' kama mapambo tu. Wanatakiwa kuwa wasomi kweli kweli. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuwa na Majaji wasiokuwa na sifa hizi, siyo tu kunafifisha utoaji wa haki kwa wadaawa katika Mashauri yaliyoko Mahakamani, bali pia kunaifedhehesha taaluma nzima ya Sheria, Mahakama ya Tanzania na Mamlaka yao ya Uteuzi, yaani Rais mwenyewe.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe ufafanuzi juu ya jambo hili na pia itoe kauli mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba utaratibu wa uteuzi wa Majaji uliowekwa na Katiba utaheshimiwa kwa Rais kuteua Majaji watakaotokana na ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama ili kuondokana na aibu na fedheha hii ya kuwa na Majaji wasiojua wanachotakiwa kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wetu wa Tawala za Mikoa na Wilaya umefafanuliwa katika ibara 2(2) na 61 za Katiba na katika *She*ria ya Tawala za Mikoa, Sura 189 ya Sheria za Tanzania. Mfumo huu ulirithiwa kutoka mfumo wa Dola la kikoloni uliokuwa umeangikwa kwenye Majimbo na Wilaya. Mabadiliko ya mwaka 1962 yaliyofuta Majimbo kuanzisha Mikoa hayakuwa mabadiliko ya mfumo, bali

yalikuwa ni kugawa Majimbo yaliyokuwa makubwa kijiografia kwenda Mikoa iliyokuwa midogo kieneo.

Mambo mengine yote ya kimfumo, kwa mfano, Mamlaka ya Kugawa Maeneo katika Majimbo na Wilaya na Kuteua Wakuu wa Maeneo hayo hayakubadilishwa kimsingi, bali yalihamishwa kutoka kwa Gavana wa Kikoloni kwenda kwa Rais. Katika mfumo huo wa kikoloni, wananchi hawakushirikishwa kwa namna yoyote katika maamuzi ya kugawa maeneo kuwa Majimbo na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dola la uhuru halijabadilisha mfumo huo kwa namna yoyote ya maana hata baada ya nusu karne ya uhuru. Kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni, wananchi ambao ibara ya 8(1)(a) ya Katiba inadai kwamba 'ndiyo msingi wa mamlaka yote', wameendelea kutegemea karama za watawala za kutengewa Mikoa au Wilaya Mpya.

Vile vile, malengo ya kuteua Wakuu wa Maeneo haya nayo hayajabadilika sana. Wakati ambapo wengi wa Wakuu wa Majimbo na Wilaya wa kikoloni walikuwa Maafisa wa kijeshi walioshiriki katika vita mbalimbali za kikoloni na kwa hiyo, lengo la uteuzi wao lilikuwa ni kudhibiti wananchi kwa manufaa ya kiuchumi ya kikoloni; wengi wa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wa Tanzania ya leo ni makada wa *CCM*. Mamlaka ya watu hawa hayatokani na wananchi, kwani hawachaguliwi na mtu yeyote; na, kwa sababu hizo hizo, hawawajibiki kwa wananchi kwa utekelezaji wa kazi na majukumu yao.

Aidha, kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni, wengi wao bado ni wanajeshi. Kwa vyovyote vile, lengo la uteuzi wa

Wakuu hawa wa Wilaya ni kudhibiti wananchi, na katika zama hizi za Vyama Vingi vya Siasa, Vyama vya Upinzani, kwa manufaa ya *CCM*. Hii inathibitishwa na matakwa ya Katiba ya *CCM* yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa kutumia mamlaka yake chini ya ibara ya 2(2) ya Katiba, amegawa Mikoa mipya ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu. Aidha, kwa kutumia mamlaka hayo hayo, Mheshimiwa Rais Kikwete amegawa Wilaya mpya za Chemba katika Mkoa wa Dodoma; Mbogwe katika Mkoa mpya wa Geita; Mlele katika Mkoa mpya wa Katavi; Buhigwe, Kakonko na Uvinza katika Mkoa wa Kigoma; Butiama katika Mkoa wa Mara; Momba katika Mkoa wa Mbeya; Wanging'ombe katika Mkoa mpya wa Njombe; Nyasa katika Mkoa wa Ruvuma; Busega na Itilima katika Mkoa mpya wa Simiyu; Ikungi na Mkalama katika Mkoa wa Singida na Kaliua katika Mkoa wa Tabora. Sambamba na ugawaji wa Mikoa, na Wilaya mpya, Mheshimiwa Rais Kikwete pia aliteua Wakuu wapya wa Mikoa na Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Mikoa na Wilaya wote ni, na wanatakiwa kuwa wanachama wa CCM. Hii ni kwa sababu, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1977, Wakuu wa Wilaya wamekuwa ni Wajumbe wa Vikao vyote Vikuu vya CCM katika ngazi ya Wilaya. Kwa mfano, kwa mujibu wa Katiba ya CCM Toleo la 1982, Mkuu wa Wilaya ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya (ibara ya 42(3); ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya (ibara ya 44(3); na ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya (ibara ya 46(3).

Hata baada ya miaka 30 tangu toleo hilo la Katiba ya CCM litolewe, na licha ya miaka 20 ya mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa nchini, hali bado iko vile vile kuhusiana na nafasi ya Wakuu wa Wilaya katika vikao rasmi vya CCM. Ndiyo maana, kwa mujibu wa ibara ya 76(1)(c) ya Katiba ya CCM Toleo la 2010, Mkuu wa Wilaya ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya; ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya (ibara ya 78(1)(c); na ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya (ibara ya 80(1)(c).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushahidi wa kutosha kwamba kugawa Mikoa na Wilaya ni namna tu ya kupata fursa ya kuwapatia makada wa CCM ambao kwa sababu mbalimbali wamekosa nyadhifa na marupurupu Serikalini kwa kuwateua kuwa Wakuu wa Mikoa na wa Wilaya. Uthibitisho wa kauli hii ni uteuzi wa Wakuu wapya wa Mikoa na Wilaya uliofanywa katika siku za karibuni na Mheshimiwa Rais Kikwete. Katika uteuzi huo, kati ya Wakuu wa Mikoa wapya, wawili ni Wabunge wa Viti Maalum katika Bunge hili hili.

Aidha, kati ya Wakuu wapya wa Wilaya, watano ni Wabunge wa Viti Maalum katika Bunge hili hili; 15 ni waliowahi kuwa Wabunge au Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki; na 22 waligombea Ubunge, lakini wakashindwa kwenye hatua za kura za maoni za ndani CCM au kwenye Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika hali inayoonyesha kukithiri kwa matumizi mabaya ya madaraka na rasilimali za umma, Wabunge wa Viti Maalum walioteuliwa kuwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya

wameendelea kushiriki katika vikao vinavyoendelea vya Bunge hili Tukufu.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu hawa Wakuu wa Mikoa na Wilaya Wabunge wanalipwa mshahara upi wanapokuwa Bungeni.

Aidha, Serikali itoe kauli ni kwa nini watu hawa wanaendelea kuja Bungeni kuhudhuria vikao vya Bunge wakati wameshakubali uteuzi wao kama Wakuu wa Mikoa au Wilaya?

Vile vile, Serikali ilieleze Bunge hili, watu hawa wanamwachia nani majukumu yao ya Ukuu wa Wilaya wao wanapokuja Bungeni na kwa nini iwe hivyo? Zaidi ya hayo, kwa vile ibara ya 67(2)(g) ya Katiba inamwondolea mtu sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge “ikiwa mtu huyo ameshika madaraka ya Afisa Mwandamizi katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano”,

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu kama Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wakuu wa Mikoa au Wilaya bado wana sifa za kuendelea kuwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Wilaya Wanajeshi, kuna utata mkubwa wa Kikatiba kuhusiana na baadhi ya wateuliwa wa Ukuu wa Mikoa na Wilaya. Kwanza, orodha ya Wakuu wapya wa Mikoa na Wilaya walioteuliwa na Rais Kikwete inaonyesha kuwapo pia Wanajeshi nane, ambao kati yao watatu wanatajwa kuwa Maafisa Wastaafu wa Jeshi. Watano waliobaki hawatajwi kama wastaafu na kwa

hiyo inaelekea bado wako katika utumishi wa Jeshi. Kama tulivyokwisha kusema katika maoni yetu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanatakiwa kuwa wanachama wa CCM na wajumbe wa vikao vyote vikuu vya chama hicho katika Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati jambo hili linaweza lisizue mshangao katika mazingira mengine, kuwateua Wanajeshi kuwa Wakuu wa Mikoa na/au Wilaya katika mazingira ya sasa ya kisiasa ambapo wanatakiwa wawe wanachama wa CCM na wahudhurie vikao vya maamuzi vya chama hicho, ni jambo lenye mgogoro mkubwa Kikatiba. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa Ibara ya 147(3) ya Katiba, ambayo inasema:-

*"Itakuwa ni marufuku kwa Mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa...."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 147(4) inatafsiri 'mwanajeshi' kuwa:-

*"... ni Askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu kama Wakuu wapya wa Mikoa ya Kagera, Wilaya za Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Misenyi na Mlele ni 'Wanajeshi' au walikwisha kustaafu ili Bunge hili Tukufu lifahamu kama Uanajeshi wao, Ukuu wao wa Wilaya, uCCM wao vinaendana na matakwa ya Katiba ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendekeza rushwa na ufisadi, uteuzi wa baadhi ya Wakuu wapya wa Wilaya unaashiria kukithiri kwa rushwa na ufisadi na kukosekana kwa maadili kwa mamlaka ya uteuzi. Hapa, Mheshimiwa Naibu Spika, tutatumia mifano ya Wakuu wa Wilaya ya Kishapu katika Mkoa wa Shinyanga na Mbarali Mkoani Mbeya. Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Wilson Elisha Nkhambaku, ambaye ndiye Mkuu mpya wa Wilaya ya Kishapu, aliteuliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuwa mgombea wake wa Ubunge katika Jimbo la Singida Magharibi. Licha ya kuwekewa pingamizi dhidi ya uteuzi na aliyekuwa mgombea wa CCM, Bwana Nkhambaku alifanikiwa kuteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Singida Magharibi kuwa mgombea Ubunge wa CHADEMA katika Jimbo hilo. Hata hivyo, muda mfupi baada ya kampeni za uchaguzi kuanza rasmi, Bwana Nkhambaku alionekana katika mkutano wa kampeni za uchaguzi wa CCM katika Jimbo la Kibaha Vijijini uliohutubiwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM Yusufu Makamba na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. Katika mkutano huo, Bwana Nkhambaku alitangaza kwamba amejitoa kwenye kugombea Ubunge wa Jimbo la Singida Magharibi kwa tiketi ya CHADEMA na kwamba alikwisharudi CCM!

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 48 cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 ya Sheria za Tanzania kinaruhusu mgombea Ubunge yeyote aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kujitoa katika kugombea uchaguzi husika. Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 91B cha Sheria hiyo kinatamka wazi kwamba ni kosa la jinai ya rushwa ya uchaguzi kumrubuni au kumshawishi mgombea kujitoa kugombea kwa malipo, au ahadi ya malipo. Kwa mujibu

wa kifungu hicho, adhabu ya kosa hilo ni kifungo kisichozidi miaka mitano jela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu cha 21(1)(b) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi, 2010 kinakataza mtu yeyote, moja kwa moja au kwa namna nyingine yoyote, yeye mwenyewe, wakala wake au kupitia chama chake cha siasa, kwa niaba yake kutoa au kusaidia kutoa au kumpatia wadhifa au sehemu ya ajira mpiga kura au mtu mwingine yeyote kwa nia ya kumshawishi mpiga kura huyo kuacha kupiga kura au kumrubuni kutenda kitendo hicho. Vilevile, kifungu cha 21(1)(f) cha Sheria hiyo kinatamka kwamba ni rushwa ya uchaguzi kwa kila mpiga kura ambaye amepokea au amekubali kupokea wadhifa, sehemu au ajira kwa ajili yake mwenyewe kwa ajili ya kuacha kupiga kura wakati wowote wa uchaguzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 94 cha Sheria ya Uchaguzi, makosa hayo mawili ya jinai yana adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo cha kati ya mwaka mmoja hadi mitatu jela au vyote viwili kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa, ni kwamba uteuzi wa Wilson Elisha Nkhambaku kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, ni ushahidi wa wazi wa rushwa ya uchaguzi. Ni wazi kwamba mtu huyo alirubuniwa au kushawishiwa kujitoa kugombea Ubunge kwa niaba ya CHADEMA. Hilo lilikuwa kosa la jinai kwa mujibu wa kifungu cha 91B cha Sheria ya Uchaguzi. Sasa mtu huyo amepewa wadhifa wa Mkuu wa Wilaya. Nalo ni kosa la jinai kwa mujibu wa kifungu cha 21(1)(b) na (f) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali itoe kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu kama ni sera ya Serikali hii ya CCM kuhonga wagombea wa vyama vingine kwa kuwapa

nyadhifa katika utumishi wa umma ili wajitoe kama wagombea wa vyama vyao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi Bungeni kama mtu aliyepokea rushwa ya wadhifa ili ajitoe kuwa mgombea Ubunge anastahili kupewa wadhifa wa Mkuu wa Wilaya au wadhifa mwingine wowote katika utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendekeza siasa za kibaguzi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na kusikitishwa sana na uteuzi wa Bwana Kifu Gulamhussein Kifu kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali. Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, Bwana Gulamhussein Kifu alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini. Hata hivyo, matokeo ya uchaguzi wake yalipingwa katika Mahakama Kuu na baadaye katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Mnamo tarehe 18 Juni 2002, Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika Shauri la Rufaa Na. 2 la 2002 katika Manju Salum Msambya dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Kifu Gulamhussein Kifu, ilifuta matokeo ya uchaguzi wa Bwana Gulamhussein Kifu kwa sababu Mahakama ya Rufani ilithibitisha kwamba mtu huyo alifanya kampeni kwa misingi ya ukabila.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Rufani ilinukuu kauli ifuatayo ya Bwana Gulamhussein Kifu wakati wa kampeni za uchaguzi huo:-

*"... Waha wenzangu tuelewe kwamba mwaka huu ni mwaka wetu kujikomboa. Tumetawaliwa na kabila la Wabembe kwa muda mrefu. Kabila la Wabembe tunajua ni watu wa Kongo siyo wa Tanzania. Ni ajabu Waha tulio wengi katika Jimbo hili tuendelee kutawaliwa na kabila*

*chache. Muha popote alipo ahakikishe anipigie mimi Muha mwenzie. Angalieni wanakuja watu huku. Yuko mtu aliyepandikizwa na Msambya. Huyu mtu anakuja na Kabourou.... Kabourou na Msambya wote ni damu ya Kongo, wote ni Wanyakumawe."*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano mwingine wa kampeni, Mahakama ya Rufani ilithibitisha kwamba Bwana Gulamhussein alitamka maneno yafuatayo:-

*"Tumetawaliwa na wageni kwa muda mrefu ... umefika wakati wa kujikomboa kutoka kwa wageni kutoka Kongo.... ni wakati mzuri kunichagua mimi kama Muha, Muha mwenzenu ... kwa kuwa sisi ndio tulio wengi katika jimbo hili."*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu huyu aliyepatikana na hatia ya kufanya siasa za kibaguzi za aina hii ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba uteuzi wa Bwana Gulamhussein Kifu uko sambamba na matakwa ya Katiba yetu inayopinga aina zote za kibaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusogeza maendeleo kwa wananchi. Kuna dhana imejengwa na kuaminishwa kwa wananchi kwa miaka kwamba lengo la kugawa Mikoa au Wilaya mpya ni "... kusogeza na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi", na kwa hiyo inaonekana kama jambo jema. Ndio maana suala la kutenga maeneo katika Wilaya au Mikoa mipya limejitokeza sana katika chaguzi za miaka ya karibuni kama sehemu ya ahadi za kampeni za wagombea Urais wa CCM. Dhana hii haina budi kuhojiwa na ukweli wake, kama upo, kuthibitishwa. Kwanza, nchi zote

jirani na Tanzania ambazo zina Mikoa au Majimbo machache zaidi yetu hazina tofauti kubwa ya kimaendeleo na nchi yetu. Nyingine kama Kenya, kwa mfano, yenye Majimbo 11 na ambayo sehemu yake kubwa ya Kaskazini na Kaskazini Mashariki ni nusu jangwa ina uchumi mkubwa kuliko wa Tanzania ambayo sasa ina Mikoa ishirini na saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hakuna ushahidi wa kuthibitisha kwamba kugawa Mikoa au Wilaya mpya kunaongeza bajeti ya maendeleo ya maeneo husika hasahasa katika miradi ambayo ina umuhimu kiuchumi au kijamii kwa wananchi. Badala yake, ushahidi uliopo unaonyesha kwamba gharama za uendeshaji wa Serikali – yaani bajeti ya matumizi ya kawaida - zinaongezeka pale ambapo Mikoa na Wilaya mpya zinapotengwa. Kwa mfano, kwa mujibu wa Juzuu ya III Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Mikoa kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013, bajeti ya matumizi ya kawaida ya Mikoa katika mwaka wa fedha 2010/2011 ilikuwa shilingi trilioni 1.887 na shilingi trilioni 2.321 katika mwaka wa fedha 2011/2012. Hii ilikuwa kabla ya kuongezwa kwa Mikoa minne mipya na Wilaya mpya kumi na tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baada ya kuongezwa kwa Mikoa mipya minne, bajeti ya matumizi ya kawaida ya Mikoa katika mwaka huu wa fedha imepanda hadi kufikia shilingi trilioni 2.882. Hii ndio kusema kwamba katika kipindi cha miaka miwili 2010/2011 – 2012/2013, bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa takriban asilimia 53. Kwa mujibu wa Makadirio haya, bajeti ya matumizi ya kawaida ya Mikoa mipya minne ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu ni shilingi bilioni 257.443 kwa mwaka huu peke yake. Kwa upande mwingine, bajeti ya matumizi ya

kawaida ya Wilaya kumi na tano zilizotajwa hapo juu ni shilingi bilioni 2.502 kwa mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Makadirio haya, gharama za kuendesha Serikali katika maeneo haya mapya kwa mwaka huu wa fedha peke yake ni takriban shilingi bilioni 260.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ulinganisho, kwa mujibu wa Juzuu ya IV Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Wizara na Mikoa kwa mwaka huu wa fedha inaonyesha kwamba bajeti ya maendeleo kwa ajili ya Mikoa mipya minne iliyogawanywa mwaka huu ni shilingi bilioni 60.021. Hii ni sawa na asilimia 23.3 ya bajeti ya matumizi ya kawaida kwa kipindi hichohicho. Makadirio haya hayaonyeshi fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Wilaya mpya 19 zilizoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushahidi huu, dhana kwamba kutenga Mikoa na Wilaya mpya ni kusogeza maendeleo kwa wananchi, ni kivuli cha kisiasa tu chenye lengo la kuhalalisha ongezeko la matumizi ya watawala. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba wakati umefika kwa nchi yetu kuweka utaratibu wa kikatiba na kisheria utakaodhibiti kama sio kupunguza ongezeko la maeneo ya kiutawala ambayo sio tu ni mzigo kwa walipa kodi bali ni mzigo kwa uchumi kwa ujumla kwani yanatumia rasilimali ambazo zingeelekezwa katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekaji nyara na haki za binadamu. Mnamo usiku wa kuamkia tarehe 3 Julai 2012, Dkt. Steven Ulimboka, kiongozi wa Madaktari waliokuwa wamegoma kwa kudai haki na stahili zao mbalimbali, alitekwa nyara na kisha kuteswa kwa namna ya ukatili

mkubwa na baadaye kutupwa vichakani katika Msitu wa Mabwepande nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam. Tukio hili la kinyama na la aina yake lilitokea sambamba na kauli ya Waziri Mkuu ndani ya Bunge hili Tukufu kwamba Serikali ilikuwa imeamua kuwa 'litakalokuwa na liwe' kuhusiana na mgogoro huo wa Madaktari. Mara baada ya tukio hilo na kwa haraka kubwa, Serikali, kwa kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Waziri Mkuu mwenyewe, ilitoa taarifa ya kukanusha kuhusika kwake na tukio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, vyombo vya habari vimechapisha taarifa zinazoihusisha Serikali na kutekwa nyara na kuteswa kwa Dkt. Ulimboka. Katika toleo lake la tarehe 11-17 Julai, 2012, gazeti la Mwanahalisi linataja maafisa watatu – Jack Zoka na Rama, wanaodaiwa kuwa maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa na Ujasusi na ASP Ahmed Msangi ambaye ni Mkuu wa Upelelezi wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kuwa wahusika wakuu wa tukio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuteka nyara kwa lengo la kuua au kuumiza, ni kosa kubwa la jinai kwa mujibu wa sheria zetu. Chini ya kifungu cha 248 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania kinasema:-

*"mtu yeyote anayemteka nyara mtu kwa lengo la mtu huyo kuuawa au kuwekwa kwa namna inayoweza kusababisha mtu huyo kuuawa anakuwa ametenda kosa na anaweza kufungwa jela kwa miaka kumi."*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 250 cha Sheria hiyo, kuteka nyara kwa lengo la kumuumiza mtekwa nyara, ni kosa la jinai vilevile na

adhabu yake ni kifungo jela kwa muda wa miaka kumi. Kwa vyovyote vile, Dkt. Ulimboka alitekwa nyara kwa lengo la ama kuuawa au kuumizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa vyovyote vile, wahusika wa tukio hili la kinyama ni wahalifu kwa mujibu wa vifungu tajwa vya Kanuni ya Adhabu. Watu hawa wanatakiwa kuchukuliwa hatua stahili za kisheria. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mkurugenzi wa Mashtaka atumie mamlaka yake chini ya Katiba na chini ya Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, Na. 27 ya 2008 *(National Prosecutions Service Act, 2008)* na kuamuru kukamatwa kwa Jack Zoka, Rama na ASP Msangi ili tuhuma za kuhusika kwao na utekaji nyara na utesaji wa Dkt. Ulimboka ziweze kupelelezwa kwa kina na ukweli wake kuthibitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya hivyo, kutaonyesha wananchi kwamba Serikali haiungi mkono kwa vitendo vya kihalifu vinavyofanywa kwa kinachoelekea kuwa malengo ya kisiasa kama ilivyotokea kwa Waheshimiwa Wabunge Highness Kiwia wa Ilemela na Salvatory Machemli wa Ukerewe kukatwa mapanga mbele ya Askari Polisi, Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kuwekewa kinachoaminika kuwa ni sumu na Mhariri Mtendaji wa Mwanahalisi Saed Kubenea na Mshauri wa Habari na Mawasiliano wa gazeti hilo Ndimara Tegambwage kuvamiwa kwa mapanga na kumwagiwa tindikali mwanzoni mwa Januari 2008. Kufanya hivyo, kutaonyesha vilevile kwamba Serikali ya CCM haiko tayari kuruhusu vitendo vya mauaji kama namna mpya ya mapambano ya kisiasa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa mashtaka ya jinai. Mamlaka ya uendeshaji wa mashtaka ya jinai imekasimiwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa Ibara ya 59B(2) ya Katiba. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 59B(4), katika kutekeleza mamlaka yake, inasema:-

*"Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru, hataingiliwa na mtu yeyote au na mamlaka yeyote na atazingatia ... nia ya kutenda haki, kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki na maslahi ya umma."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni hii kuu imetamkwa pia na kifungu cha 8 cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, Na. 27 ya 2008 *(National Prosecutions Service Act, 2008)* ambayo pia imefafanua na kutilia nguvu mamlaka haya ya Kikatiba. Kwa mujibu wa Sheria hii, Mkurugenzi wa Mashtaka ana mamlaka sio tu ya kudhibiti mashtaka yote ya jinai bali pia kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai [kifungu cha 16(1)]. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) na (3), Mkurugenzi ana uwezo wa kutoa maelekezo ya maandishi kwa ofisa yeyote wa umma ili apatiwe taarifa yoyote inayohusu upelelezi au uendeshaji wa mashtaka ya jinai na ofisa huyo anatakiwa kutii maelekezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba kwa uhuru kamili na bila woga au upendeleo, Mkurugenzi wa Mashtaka amewekewa kinga ya ajira yake. Kwa mujibu wa kifungu cha 19(1) na (2) cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, sifa, masharti na mafao ya ajira ya Mkurugenzi wa Mashtaka yatakuwa sawa na yale ya ajira ya Jaji wa Mahakama Kuu. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 19(3), Mkurugenzi wa Mashtaka hawezi kuondolewa

kwenye madaraka yake isipokuwa kwa kushindwa kutimiza wajibu wake kwa sababu ya ugonjwa au kwa kukiuka Kanuni za Maadili ya Kitaaluma ya Maafisa wa Sheria, Mawakili wa Serikali na Wanasheria walioko kwenye Utumishi wa Umma chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 ya Sheria za Tanzania. Hii ndio kusema kwamba, kwa mujibu wa Sheria, utaratibu wa kumwondoa Mkurugenzi wa Mashtaka kwenye ajira yake hauna tofauti na utaratibu wa kumwondoa Jaji wa Mahakama Kuu kwenye ajira yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba utaratibu huu wa Kikatiba na kisheria umempa Mkurugenzi wa Mashtaka nyenzo za kutosha kisheria za kupambana na uhalifu mkubwa hapa nchini na vilevile kuzuia matumizi mabaya ya mfumo wa uendeshaji na utoaji haki na hasahasa ya mfumo wa mashtaka ya jinai. Licha ya kuwa na mamlaka na kinga hizi za kisheria, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeshindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Hii inathibitishwa na kitendo cha Serikali kurudia takwimu zilizotolewa mwaka jana ndani ya Bunge hili juu ya kesi kubwa za rushwa zilizofunguliwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai zikiwamo kesi za wizi wa fedha za Benki Kuu ya Tanzania *(EPA),* uhujumu uchumi, kuisababishia Serikali hasara, kusafisha fedha haramu na wizi wa kutumia silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa na kusikitishwa na kushindwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua na/au kuendesha mashtaka yanayohusu matukio makubwa ya ufisadi ambayo yametikisa Taifa letu, Serikali ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani miaka saba iliyopita. Hii ni kwa

sababu tangu mwaka 2007, kumekuwapo kwa ushahidi wa kutosha unaoowaunganisha viongozi na Maafisa Waandamizi wa Serikali ya Awamu ya Tatu na wa Awamu ya Nne na maswahiba wao wa kibiashara katika kashfa kubwa za *Meremeta Ltd., Tangold Ltd., Deep Green Finance Ltd., Kagoda Agricultural Co. Ltd., Kiwira Coal Mine, Radar ya BAE Systems, Richmond, Dowans* na nyinginezo nyingi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu juu ya kushindwa kwake kuwachukulia hatua stahiki wahusika wa kashfa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubambikizaji raia kesi za uongo, kwenye maoni yetu ya mwaka jana, tulilalamikia kushindwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai kutimizima wajibu wake Kikatiba na kisheria kuzuia matumizi mabaya ya utaratibu wa utoaji haki. Kwa kutumia mfano wa yaliyomkuta Diwani wa Kata ya Bumera katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Mheshimiwa Tengera Marwa, tulionyesha jinsi ambavyo Jeshi la Polisi limekithiri vitendo vya kukamata na kufungulia wananchi kesi za uongo zinazohusu tuhuma za makosa makubwa ya jinai ambayo hayana dhamana kisheria. Aidha, tulionyesha jinsi ambavyo msongamano wa mahabusu katika Magereza yetu kulingana na idadi ya wafungwa ni ishara ya kushindwa kwa mfumo wa dhamana chini ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Sura ya 20 ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yake mbele ya Kamati, Waziri wa Katiba na Sheria amesema kwamba Wizara yake imeunda Jukwaa la Taifa la Haki Jinai (*The National Criminal Justice Forum)* ili:-

*"... kutoa fursa kwa wadau wa Haki-Jinai kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizopo katika mfumo wa utoaji haki-jinai..."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliiambia Kamati kwamba katika miezi Februari na Mei ya mwaka huu, Kamati Maalum ya Jukwaa hilo, naomba kunukuu:-

*"... iliunda timu ndogo iliyotembelea baadhi ya magereza nchini kutatua baadhi ya kero zinazowasibu wafungwa na mahabusu."*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dharau kwa Mahakama Kuu, ni kupoteza muda na fedha na rasilimali kidogo tulizo nazo. Ufumbuzi wa matatizo ya kufurika kwa Mahabusu katika Magereza ya nchi yetu utapatikana kwa kufumua na kubadilisha kabisa mfumo wetu wa dhamana chini ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai ambao unakataza dhamana kwa idadi kubwa ya watuhumiwa wa makosa yaliyotajwa katika kifungu cha 148(5)(a) na (e) ya Sheria hiyo. Vifungu hivi viwili ndio chanzo kikubwa cha Polisi kubambikiza wananchi wasio na hatia kesi za uongo kwa lengo la kuwakamua na ndio chanzo kikubwa cha msongamano katika Mahabusu na Magereza yetu. Kama ilivyosema Mahakama Kuu katika kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni @ ole Saibul @ Mdosi @ Mjomba na wenzake 19 dhidi ya Mwanasheria Mkuu, Shauri la Madai Na. 117 la 2004, bila kuwepo utaratibu uliowekwa na sheria kama inavyoelekezwa na Ibara ya 15(2)(a) ya Katiba, "utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 148(5)(a) umetumiwa vibaya." Kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu ilitamka kwamba kifungu hicho kinachokataza

dhamana kwa watuhumiwa wa makosa ya wizi wa kutumia silaha ni kinyume cha Ibara ya 15(2)(a) ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kifungu cha 148(5)(e) cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai kinachoweka masharti ya dhamana 'yasiyotekelezeka' kwa watuhumiwa wa makosa ya uhujumu uchumi, Mahakama Kuu katika kesi ya Profesa Dkt. Costa Ricky Mahalu & Mwenzake dhidi ya Mwanasheria Mkuu, Shauri la Maombi Na. 35 la 2007 – ilitamka kwamba kifungu hicho ni cha kibaguzi kwa watuhumiwa maskini na kinakiuka matakwa ya Ibara ya 13(2) ya Katiba inayokataza ubaguzi 'ama wa dhahiri au kwa taathira...' Kwa kutumia mamlaka yake chini ya Ibara ya 30(5) ya Katiba, badala ya kukifuta kifungu hicho, Mahakama Kuu katika kesi zote mbili iliielekeza Serikali ifanye marekebisho katika kifungu cha 148(5)(a) na (e) ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai ili kuweka utaratibu bora zaidi wa kushughulikia dhamana za watuhumiwa wa makosa ya wizi wa kutumia silaha na wa uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni, Mahakama Kuu ilitoa muda wa miezi kumi na nane – kuanzia tarehe 13 Julai, 2007 na katika Kesi ya Profesa Dkt. Costa Ricky Mahalu, Mahakama Kuu ilitoa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 4 Oktoba, 2010. Hii ina maana kwamba Serikali ilitakiwa iwe imetekeleza maelekezo ya Mahakama Kuu juu ya kifungu cha 148(5)(a) kufikia tarehe 12 Desemba, 2008. Aidha, Serikali ilitakiwa kutekeleza maelekezo ya Mahakama Kuu kuhusu kifungu cha 148(5)(e) kufikia tarehe 3 Oktoba, 2011. Huu ni mwaka wa nne na nusu tangu kwisha kwa muda uliowekwa katika Kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni lakini Serikali haijafanya marekebisho tajwa ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai.

Aidha, miezi sita imekwishapita tangu muda uliowekwa katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu lakini Serikali haijatekeleza maelekezo hayo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu ni kwa nini imepuuza maelekezo ya kikatiba ya Mahakama Kuu kuhusu marekebisho ya sheria ambazo Mahakama ya Tanzania imetamka kwamba zinakiuka Katiba? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi kama, na lini, inatarajia kutekeleza maelekezo hayo ya Mahakama Kuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilianza kazi Mei Mosi 2012 baada ya Rais Kikwete kufanya uteuzi wa wajumbe na Makatibu wa Tume. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 6. 575 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha Mei hadi Juni, 2012. Kati ya fedha zilizoidhinishwa, Wizara imekiri kupokea shilingi bilioni 3.625 au asilimia 55 ya fedha iliyoidhinishwa. Katika randama ya Fungu 08 la Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyowasilishwa kwa Kamati mwezi uliopita, Serikali ilipendekeza matumizi ya shilingi bilioni 39.95 kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Tume kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Hata hivyo, baada ya Kamati kuhoji busara ya makadirio haya makubwa, Wizara ilipunguza jumla ya shilingi bilioni 6.005 katika makadirio ya bajeti ya Tume na hivyo kubakiwa na makadirio ya shilingi bilioni 33.944.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inatambua umuhimu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kupatiwa rasilimali zote zinazohitajika ili kuiwezesha kutekeleza vyema majukumu yake mengi na makubwa. Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni inaamini kwamba umuhimu wa Tume sio leseni ya matumizi yasiyoelezeka na yasiyokubalika ya fedha za umma hasahasa katika mazingira ambayo wananchi wanahubiriwa na watawala kwamba miradi ya maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii haitekelezeki kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ya Serikali. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, ni fursa adimu na ya heshima kubwa ya kulitumikia Taifa inayokuja mara chache sana katika maisha ya Taifa. Ni fursa wanayopata watu wachache sana katika historia ya Taifa lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya makadirio ya bajeti ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba yanatishia kuigeuza heshima ya kutumikia waliyopewa wajumbe wa Tume kuwa hongo ya Serikali. Hii ni kwa sababu, katika bajeti ya shilingi bilioni 33.944, Serikali inapendekeza kuwalipa wajumbe na watendaji wa Tume posho mbalimbali za jumla ya shilingi bilioni 14.633 au asilimia 43 ya bajeti nzima ya Tume kwa mwaka huu wa fedha peke yake. Hivyo, kwa mfano, kila mjumbe wa Tume atalipwa posho ya kikao (*sitting allowance*) ya shilingi laki mbili kila siku kwa mwaka mzima, kikao kiwepo au kisiwepo! Posho hizi za vikao peke yake zitagharimu jumla ya shilingi bilioni 9.594 kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kila mjumbe wa Tume atalipwa jumla ya shilingi elfu hamsini kila siku kwa mwaka mzima kama posho ya majukumu (*responsibility allowance*), awepo kazini au asiwepo kazini! Posho hii nayo itawagharimu walipa kodi wa Tanzania shilingi milioni 630 kwa mwaka huu wa fedha peke yake. Vile vile kuna shilingi milioni kumi ya posho ya matibabu "... kwa wajumbe

ambao hawamo kwenye utaratibu wa Serikali wa kugharamia matibabu na madawa.” Zaidi ya hayo, wajumbe wa Tume na Sekretarieti yake watalipwa posho ya kujikimu wanaposafiri ndani ya nchi kikazi ya jumla ya shilingi bilioni 4.399 kwa mwaka huu wa fedha pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio malipo ya posho hizi tu ndio yenye mgogoro. Kwa mujibu wa randama ya Tume, shilingi bilioni 2.032 “... zitatumika kulipia gharama za nyumba za wajumbe na Sekretarieti ya Tume.” Kwa mujibu wa majukumu yake chini ya Sheria ya Mabadiliko ya Sheria, Sura ya 83 ya Sheria za Tanzania, Tume inatakiwa kukusanya maoni ya wananchi nchi nzima na kwa sababu hiyo, wajumbe wanatazamiwa kuwa safarini katika sehemu mbalimbali za nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli mbele ya Bunge hili Tukufu kwa nini wajumbe na Sekretarieti wanapangishiwa nyumba Dar es Salaam wakati wanatakiwa kutembelea maeneo mbalimbali nchini wakikusanya maoni ya wananchi? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze Bunge hili Tukufu gharama zote za kila Mjumbe wa Tume, Sekretarieti na watumishi wengine wote wa Tume ili Wabunge na wananchi wa Tanzania wafahamu kodi wanazolipa zinavyotumika katika mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya aina hii ndio yanayoifanya Serikali isiaminike kwa wananchi pale inapodai kwamba matatizo makubwa ya malipo ya mishahara na marupurupu yanayowakabili watumishi wa sekta ya afya, elimu na kadhalika yanatokana na upungufu au ukosefu wa fedha. Serikali hii haiwezi kuaminika inapowaambia Madaktari wetu kwamba haiwezi kuwalipa

stahili zao kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, au inapowahubiria wanafunzi wetu wa elimu ya juu, juu ya 'sungura mdogo.' Kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali iwalipe wajumbe wa Tume mshahara wa kila mwezi hata kama ni kwa viwango vya juu kabisa vya mishahara ya watumishi wa umma kwa muda wote watakapokuwa wanatekeleza majukumu ya Tume. Aidha, kwa vile Sekretarieti ya Tume inaundwa na watu ambao tayari wapo katika Utumishi wa Umma, watu hawa waendelee kulipwa mishahara waliyonayo kwa kazi zao za sasa ila wahesabike kwamba wako Tume kwa *secondment*. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki yoyote ya kutumia mabilioni ya fedha za wananchi kuwapangishia nyumba wajumbe wa Tume na Sekretarieti juu ya malipo mengine makubwa yanayopendekezwa. Lazima, kama Taifa, tushone koti letu kulingana na ukubwa wa kitambaa tulicho nacho!

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni chini ya uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya maoni haya. Aidha, niishukuru familia yangu, mke wangu mpenzi Alicia Bosensera na mapacha wetu Agostino Lissu na Edward Bulali, kwa kuendelea kuvumilia upweke unaotokana na '*Daddy*' kuwa mbali muda mwingi kwa sababu ya majukumu mazito ya Kibunge. Aidha, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Singida Mashariki kwa imani na nguvu wanayonipa kila siku kwa kuendeleza msimamo wetu thabiti wa kukataa kunyanyaswa, kunyonywa na kupuuzwa na 'Ndaa ya Njou'.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi, wanachama na wapenzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wote wa Tanzania ambao wameendelea kutuunga mkono na kututia nguvu katika kipindi hiki muhimu katika historia ya nchi yetu. Nawaomba waendelee kutuunga mkono na kututia nguvu katika siku ngumu na za majaribu makubwa zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru na wewe binafsi na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Blandes, nimekuona umesimama, Mheshimiwa Blandes!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Natumia Kanuni ya 68(7) ambayo inasema:-

*"Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo kwa papo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa".*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na heshima zote ninazompa Wakili Msomi mwenzangu Mheshimiwa Tundu Lissu, wakati akiwasilisha taarifa yake ya Kambi ya Upinzani hapa Bungeni kwenye ukurasa wake wa tisa, kuna maneno

ameyatoa hapa, nitaomba kwa ruhusa yako niyanukuu, anasema:-

*"Kwa mujibu wa taarifa tulizonazo, sasa watu wanateuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ambao hawajawahi kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na kwa sababu hiyo hawajafanyiwa veting yoyote na mamlaka hiyo ya Katiba juu ya uwezo na ujuzi wao na kama wanafaa kwa kila hali kukabidhiwa madaraka ya Jaji wa Mahakama Kuu. Inaelekea watu hao wengi wao wakiwa wamekaribia muda wao wa kustaafu kwingineko katika utumishi wa umma wanapewa zawadi ya Ujaji ili kuwawezesha kupata mafao ya Majaji Wastaafu ambayo yameboreshwa sana katika miaka ya karibuni. Matokeo yake ni kuwa na Majaji ambao wamechoka, hawawezi na hawajui namna ya kufanya kazi ya Jaji wa Mahakama Kuu". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuomba mwongozo wako kwa sababu huu ni mhimili ambao una mamlaka yake na pia tuko hapa kujadili masuala ya Kibunge, lakini pia Mheshimiwa Tundu Lissu katika kufanya hilo naona ameingia katika kujadili mhimili mwingine wa Mahakama ambao hauna nafasi ya kuja kujitetea humu ndani na katika mjadala huu maneneo haya yanalenga moja kwa moja kwanza kudhalilisha Waheshimiwa Majaji kwamba hawana uwezo, kwamba wamechoka na hawajui wanafanya nini. Sasa naomba mwongozo wako kama hizi ndiyo taratibu za Bunge kujadili na kuudhalilisha mhimili wa Mahakama, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Blandes, ni kweli haya maneno uliyoyasoma yameandikwa na alichokuwa anakisoma Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kweli siyo tu kwamba ni hotuba yake yeye peke yake ni makubaliano ya Kambi Rasmi ya Upinzani kufuatana na kanuni zetu, kwamba hili ndiyo andiko lao. *(Makofi)*

Sasa mwongozo wetu tutautoa jioni ya leo ili tutoe nafasi ya kama wanaweza wakaleta *addendum* katikati hapa waweze kurekebisha kwa sababu kwa hakika kama wanadhamiria kusema maneno haya wanawavunjia heshima Waheshimiwa Majaji walioaminiwa katika nafasi hiyo kubwa lakini kwa vile ni kambi ambayo tunaiheshimu sana hapa Bungeni, tunatoa nafasi mpaka jioni kama watatoa *addendum* itakuwa ni jambo jema kama hawatatoa basi jioni tutatoa maoni yetu. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, tuna nafasi ndogo sana na tuna wachangiaji wawili ambao hawajawahi kuzungumza tangu tuanze awamu hii, naomba niwape nafasi hiyo. Naomba nimwite Mheshimiwa Suleman Said Bungara na atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Magige. Mheshimiwa Suleman hayupo tena, Mheshimiwa Magige, Mheshimiwa Suleman hatakuwepo tena kwenye orodha, Mheshimiwa Magige!

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba na Naibu wake, kwa hotuba nzuri waliyoileta ambayo inaleta matumaini kwa Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda sana niwapongeze Majaji na Mahakimu wote wa Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutetea haki za wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja katika Magereza zetu, kuna mlundakano wa mahabusu wengi sana na hii inasababishwa na kesi nyingi kutosikilizwa kwa wakati. Kwa kweli hali hii inasikitisha sana. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeona wana mpango wa kuajiri Majaji wa muda ambao watasababisha changamoto hii iondoke. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa hilo. Najua kuna Mahakimu watakaoajiriwa, naomba vijana wapewe kipaumbele. Tuna vijana wengi wazuri, tuna vijana wengi Mawakili, tunaomba sana Serikali iwape vijana kipaumbele kwa sababu vijana watafanya vizuri na mlundikano utapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika hotuba ya Waziri tumeona wanaleta mfumo mpya wa *tele justices*. Mfumo huu ni mzuri na mimi navyoona utapunguza gharama kwa Serikali. Nikitolea mfano katika Mkoa wangu wa Arusha katika Wilaya ya Karatu, watuhumiwa ambao wako Karatu wanakaa katika Gereza la Kisongo, kwa hiyo, wanapotaka kwenda kusikiliza kesi zao wanatakiwa wachukuliwe Kisongo wapelekwe Karatu ambapo ni umbali mkubwa sana zaidi ya kilomita 144. Serikali ingeweza kuhamishia kesi zao katika Mahakama ya Monduli ambayo ni karibu tukapunguza gharama lakini mpango huu wa *tele justice* naona utasaidia sana kwa sababu Mahakimu wataweza kusikiliza kesi hata wakiwa mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunatoa lawama nyingi sana kwa Mahakimu wetu, Majaji wetu lakini tumekuwa hatuoni changamoto, hatuangalii matatizo yao yanayowakabili. Majaji wetu, Mahakimu wana matatizo mengi, tumekuwa tukijiangalia sisi tu wenyewe na kuwasahau wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Majaji na Mahakimu wanaishi katika mazingira hatarishi ambayo ni hatari kwa usalama wa familia zao na wao wenyewe. Nyumba za Majaji, hakuna, nyumba za Mahakimu hakuna na siyo hivyo inavyoonekana Mahakimu wanaishi katika nyumba za watuhumiwa. Hebu niambie leo mimi ni Hakimu naishi katika nyumba ya mtuhumiwa na ninataka nimhukumu, hiyo hukumu nitaitoa kweli? Nadhani haitakuwa ya haki. Kwa hiyo, naomba Serikali ijaribu kuangalia hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo nyumba tu, Mahakimu wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Majengo ya Mahakama ni chakavu. Mahakimu wetu wanatoa hukumu kwenye makontena, kwenye *godown*, hebu niambie sisi tunakaa Bungeni hapa, tunakaa vizuri, Mahakimu wetu kwa nini wakae katika hali ngumu kama hiyo? Naomba sana Serikali itenge mfuko wa kutosha kwa ajili ya Mahakama zetu. Tumeona bajeti iliyopita Serikali ilitenga shilingi bilioni 20 lakini wakapewa shilingi bilioni 14.5 kwa mafungu mafungu, hizo zilizobaki sijui zimeenda wapi, hawajapatiwa. Hata mwaka huu tunaona Mfuko wa Mahakama kwa kweli hautoshi kabisa. Tunaomba tena Serikali jamani ijaribu kuangalia hawa watu siyo tunawatupia lawama tu kila siku lakini hatuangalii maisha yao wanaishije, kazi wanafanya vipi, imefikia majengo ya

Mahakama yanavuja nyaraka zinaharibika, kweli naomba Serikali ilifanyie kazi suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende katika Mahakama Kuu, Mahakama Kuu ya Tanzania nyingi hazina nafasi za kutosha, Majaji wamekuwa hawapati nafasi za kukaa, naomba kweli Serikali iliangalie hili iweze kujenga Mahakama Kuu zenye nafasi za kutosha. Vilevile naomba Serikali ijitahidi, ijenge Mahakama Kuu kila Mkoa ili kupunguza gharama na kusaidia kesi ziweze kwenda haraka kwa sababu watuhumiwa ambao kesi zao zinatakiwa zisomwe Mahakama Kuu wamekuwa wanatolewa sehemu moja mpaka nyingine kwa ajili ya kusikilizwa kwa kesi zao. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ijitahidi kujenga Mahakama Kuu kila Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ijaribu kuwaangalia hawa watuhumiwa ambao unakuta ametuhumiwa yuko mahabusu labda miaka mitano, saba lakini baadaye anaonekana hana hatia, tujaribu kuangalia maisha yake anapotoka pale anaanzia wapi? Anapotoka pale anakuta maisha ya familia yake yameharibika, watoto hawakwenda shule, vijana wamejiingiza kwenye uhuni. Naomba Serikali iweke utaratibu wa wazi utakaowasaidia watu hawa baada ya kutoka kule wajue pa kuanzia na iwe haraka iwezekanavyo kuliko kuharibu maisha ya watu na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuko kwenye mchakato wa Katiba mpya, mimi kama Mbunge wa vijana, natoa rai kwa vijana wenzangu wote Tanzania wajitokeze kwa wingi, watoe ushirikiano, watoe maoni yao ya Katiba ili na sisi vijana kama tulikuwa tumesahaulika, Katiba hii mpya iweze

kututambua. Naomba vijana wote Tanzania mjitokeze kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa Mahakimu wote na Majaji wote, wafanye kazi kwa bidii, Serikali matatizo yao yote watayashughulikia, wasikatishwe tamaa na mtu yeyote, waendelee kufanya kazi kwa moyo huohuo. Vilevile natoa raia kwa wananchi wote pamoja na Wabunge wenzangu, tuheshimu Mahakama, tusiingilie uhuru wa Mahakama, tuache wafanye kazi zao kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sina mengi zaidi ila nachoomba jamani muweke bajeti ya Mahakama ya kutosha tusibaki kuwalalamikia tu kuwe na bajeti ya kutosha, tusibaki kuwalalamikia tu, kuwe na bajeti ya kutosha ili changamoto zao zote ziishe, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Catherine Magige kwa kutumia muda vizuri. Anafuatia Mheshimiwa Akunaay na atakuwa mchangiaji wa mwisho asubuhi ya leo.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha nisimame mbele ya Bunge hili leo nizungumze juu ya chombo cha haki yaani Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, napenda kumpongeza Waziri Mathias Chikawe kuteuliwa kuwa Waziri katika sekta yetu na Mheshimiwa Angellah ambaye alikuwa ni Makamu wangu katika Kamati ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na naomba nizungumzie kwa maneno mafupi ili niweze kueleweka. Naomba kwanza nianze na eneo la bajeti finyu. Kwa kweli kuipa Mahakama shilingi bilioni 24 kwa ajili ya Fungu la Maendeleo, ni hela ndogo sana. Katika nchi hii majengo mengi ya Mahakama ni ya tangu ukoloni na ni madogo ambapo zamani kesi kwa mwezi labda ni mbili au tatu, sasa hivi kama taarifa zilivyotoka, kuna kesi maelfu mpaka malaki. Nashauri Serikali ifanye bidii ya kutafuta fedha ili majengo ya Mahakama yaongezeke. Waheshimiwa Wabunge wangetembelea Mahakama wangeshangaa na kusikitika kwa sababu Mahakama zingine unakuta Hakimu au Jaji amewalundika watu kwenye chumba, wengine wana magonjwa ambayo hatuyajui, wanatoka rumande harufu ya chumba hicho inabadilika, inakuwa kitu kingine. Kwa hiyo, naomba jengo la Mahakama liwe mahali ambapo mtu anategemewa kwamba kupewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninampongeza Rais kwa kuhakikisha kwamba Tume ya kukusanya maoni kwa ajili ya Katiba imeanza kazi lakini mategemeo ya wananchi kidogo wameanza kuwa na wasiwasi. Kuna habari zinasikika kwamba katika kuwaalika wananchi kuhudhuria kwenye mikutano ile, kuna njama zinafanywa, watu wengi wasipate taarifa. Sasa ushauri wangu ni kwamba Tume ichukue nafasi ya kutoa taarifa kwa vyombo vya habari pamoja na ofisi za Mkuu wa Wilaya zitoe taarifa. Wasiwasi wa wananchi ni kwamba wanaweza wakaitwa watu wachache wakawa wamefundishwa wakasema vitu vile ambavyo Serikali inavitaka na vile vya wananchi vikaachwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linalofuata, nataka pia niipongeze Serikali kwa mapendekezo ya kubadilisha mfumo wa usikilizaji wa mashauri kwa kuruhusu *tele conference* katika Halmashauri zetu na kuajiri Majaji na Mahakimu wa muda, hiyo itasaidia kesi ziishe mapema. Katika hili pia, kwa sababu Mahakama nyingi hazina watumishi hasa masekretari wanaopiga chapa, ni vema wakaajiriwa ili wananchi waweze kupata *judgement* zao mapema. Pia nashauri waajiri ma-*typist* wa muda hasa nafasi za jioni kutoka kwenye ofisi zingine za Serikali ili hizo nyaraka ziweze kupatikana kwa haraka. Kwa mfano, katika Wilaya ya Mbulu kwa miaka minne iliyopita hakuna *typist*. Kwa hiyo, nashauri kuwe na *temporary employments* katika nafasi mbalimbali kwa kuchukua watu wanaoaminika, itakuwa ni jambo nzuri katika kuboresha sekta ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni juu ya ucheleweshaji wa mashauri, Mawakili pia wanahusika kwa kupanga tarehe za mbali halafu hawapo lakini kubwa zaidi ni kwamba Mahakimu na Majaji hawafuatilii zile kanuni zinazoendesha hayo mashauri. Wakizingatia kanuni, Mawakili hao pia watakuwa na adabu ya kufuata *diaries* zao ili kesi za wananchi ziishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia juu ya lugha inayotumika Mahakamani. Lugha inayotumika katika Mahakama ya Wilaya na ya Mkoa na Mahakama Kuu katika maandishi ni lugha ya Kiingereza. Sasa wananchi ambao hawana Mawakili wanalazimishwa na Makarani kwamba maandishi yao yawe kwenye Kiingereza na hawajui na hawana fedha za kuweka Wakili. Sasa kuwe na watu wanaoitwa *paralegals* ambao *at least* wana cheti

cha sheria, wawe wanasaidia watu hata kama hawana leseni. Sasa naiomba Serikali, sisi tunajua inaruhusiwa mtu aandike Kiswahili hata Mahakama Kuu lakini Makarani wanaKataa ili wapate pesa. Sasa tunataka Jaji Mkuu aitangazie Tanzania nzima kwamba mtu anaruhusiwa kuleta maandishi yake kwa Kiswahili ili aweze kupata haki yake, watu wengi wanajua kuandika kesi zao kwa Kiswahili kuliko hata Mawakili wale walioanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linguine ni kuhusu Mahakama ya Biashara, ushuru wake ni ghali sana. Sasa ukiwa na wafanyabiashara wa kawaida ambao wanadai pesa ambazo zinafikia kiwango kinachotakiwa iende kwenye Mahakama ya Biashara lakini ada yake ni ya juu sana. Sasa biashara zao siyo zile za *cooperate business*, ni biashara ya mtu mmoja mmoja, mtu ameuza labda vitunguu, mtu kauza ng'ombe, naomba Serikali iangalie maeneo hayo ushuru upungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni juu ya Mabaraza ya Ardhi tuliyoyazungumzia kwenye Wizara ya Ardhi, kwa sababu baadaye inakwenda Mahakama Kuu, mimi nafikiri Jaji Mkuu awasiliane na Waziri wa Ardhi kwa sababu Mahakama zake zimepokonywa haki ya kutoa hukumu juu ya mashauri hayo. Mashauri yale kwenye Mabaraza yanapoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naishukuru Serikali kwa kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, tunaomba tuongezewe Mahakimu zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na nawashukuruni Waheshimiwa Wabunge tutaendelea mchana. Nisahihishe mambo kama mawili, nitoe ushauri siyo kusahihisha *in such*, ni kutoa ushauri.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Tundu Lissu kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, ametaja majina ya maofisa fulanifulani wa Serikali kuhusiana na kosa la jinai na ushahidi wake aki-*base* kwenye gazeti, mimi nadhani Waheshimiwa Wabunge tutakuwa hatutendi haki na mara kwa mara nimesema sana na kurudia mara kwa mara kwamba tuwatendee watu haki. Tusirahishe mambo ambayo ni makubwa kwa kufanya hivyo kwa sababu kuanzia sasa watu wengine watanukuu hapa kwamba ilisemwa Bungeni na kwa hiyo, huo ndiyo ushahidi, kinaanza kuwa sasa known kitu ambacho si sawa sana, kama gazeti tuliachie gazeti na mambo yake, la sivyo kama tunahakikika, tuchukue mambo haya tupeleke katika vyombo vinavyohusika kuliko kutaja majina ya watu, watu wengine wametumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa, huwezi kuwa na hakika sana kama jambo hilo ni kweli au si kweli. *(Makofi)*

Ni jambo ambalo litalifanya Bunge hili lizidi kuonekana tu ni mkusanyiko wa vituko, tutakosa kuheshimika katika jamii tusipokuwa makini sana kuhakikisha kwamba yule ambaye tunamtaja kwa jina ndani ya ukumbi huu kweli tuna hakika kabisa mtu huyo anahusika kabisa kabisa na ushahdi tunao. Tusipozingatia hili na hii ni *stand* ya Mabunge yote Duniani, kujizuia sana kuwapakapaka watu kwa sababu tuna-*feel like doing so* kwa sababu tuna *privilege* hiyo, hili jambo tujizuie Waheshimiwa. Leo sisi Waheshimiwa kesho watakuwepo wenzetu wengine na sisi

tutakuwa nje, tusitajwetajwe hapa katika mazingira ambayo kumbe hatuna nafasi ya kuweza kujitetea hapa.

La pili, linahusu mgao wa fedha za maendeleo, isije ikatoka picha hapa kwamba Bunge linajiwekea fedha nyingi kuliko Mahakama au taasisi nyingine. Mahakama kwenye fedha za maendeleo ina shilingi bilioni 24 Bunge ina shilingi bilioni 10 na hizi shilingi bilioni 10 ni kwa ajili ya ofisi za Wabunge nchi nzima kumalizia ujenzi ule ulioazwa zamani.

Vilevile kwenye hotuba ya Mheshimiwa Tundu Lissu anasema Mahakama ipate asilimia fulani kama ambavyo Bunge inapata asilimia yake kwenye Mfuko wa Bunge. Ni kwamba Mfuko wa Bunge ndiyo tunatarajia uanze mwaka huu wa fedha, haujaanza bado. *(Makofi)*

Bunge bado halipati asilimia yoyote ambayo tayari iko *pegged* kwamba Bunge linapata asilimia fulani, hapana. Sisi Bunge na Mahakama sote kilio chetu ni kimoja. Tunaendelea kuzungumza na Serikali kwamba tufike mahali tupate kaasilimia fulani. Kwa hiyo, kilio chetu ni cha pamoja ndugu zangu siyo kwamba Bunge linajipendelea kwa namna moja au nyingine dhidi ya Mahakama. Nilipenda nisema maneno haya ili katika mijadala yenu tusije tukawa na fikra za aina hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni na hapa mezani atakuwepo Mheshimiwa Jenista Mhagama.

*(Saa 7.30 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mkutano wetu wa Nane, Kikao cha Ishirini na Tatu na hoja iliyopo mbele yetu ni kuendelea kupitia ili tukubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Murtaza Mangungu na atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu na niseme kwamba hoja hii ni muhimu sana katika mustakabali na mwongozo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Sheria na Katiba na Naibu wake hasa kwa uteuzi lakini pia kwa utendaji ambao tunaamini kabisa utakuwa ni wa makini kwa sababu umeonekana kwa kipindi kifupi tu hasa kipindi ambacho Mheshimiwa Chikawe alivyorudi tena katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utangulizi tu, sisi Wabunge na wananchi na binadamu wote duniani tukumbuke ni dhaifu kuliko kiumbe kingine chochote na mfano wa jambo hili unaweza ukauona pale ambapo mwanadamu anazaliwa mpaka kuja kufikia umri wa kupata

akili zake timamu lakini angalia viumbe vingine ambavyo vinazaliwa siku hiyohiyo vinaweza vikajitambua na vikaweza kuishi kuliko mwanadamu ambaye inabidi alelewe mpaka kufikia umri wa kuweza kujitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati nasoma, Mwalimu wangu aliwahi kunifundisha na kuniambia kwamba moja kati ya matatizo ambayo mwanadamu huwa nayo ni ile kujiamini kwamba yeye anajua zaidi kuliko watu wengine wote.

**MBUNGE FULANI:** *Message sent!*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Lakini wataalamu wa *psychology* wanasema moja kati ya matatizo ya *psychiatric* ni kujiona kwamba unajua zaidi kulikoni mtu mwingine yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika hotuba hizi, mimi naomba kwanza nianzie na hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani na hii ieleweke tunaposema Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge tunatafsiri kwamba ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Kambi hii haihusishi vyama vya *CUF, TLP, NCCR* wala chama kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ukiisoma, ukurasa wa tano, msemaji amesema kwamba, namnukuu; kwa mujibu wa Sheria ya Malipo na Mafao ya Majaji ya mwaka 2007 pamoja na mambo mengine ambayo yameainishwa, ukienda kwenye ukurasa wa sita amesema kwamba fedha zinazokidhi mahitaji ya Mahakama hazipatikani sasa Majaji wetu wanaishi katika nyumba za kupanga ambazo zinadaiwa kodi na wenye nyumba na wanalazimika kujilipia

matibabu yao wao na familia zao. Lakini mtu huyohuyo ambaye ameandika hotuba hiyohiyo ukurasa wa tisa anasema kwamba kwa mujibu wa taarifa alizonazo yeye au walizonazo wao kwamba Majaji wamekuwa wakipendelewa na wanateuliwa kwa upendeleo ili kuweza kukidhi mahitaji na wapate *benefits* za Ujaji na upendeleo huu umekuwa ukifaywa kwa makusudi. Sasa tunakwenda wapi na tunaelekea wapi? Uteuzi wa Majaji ni suala la Kikatiba. Tunapozungumzia Katiba tunazungumzia na Wabunge pia, mbona kuna mfano wa Vyama vya Siasa ambavyo katika suala la uteuzi wa Wabunge wamepeana kiukoo, kiushemeji, kidada na kadhalika? Sasa upendeleo huu ambao unazungumziwa ni upendeleo wa aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu sana kuweza kuamini kwamba haya yanafanyika na mtu ambaye anajielewa. *Appointments* zote zinazotokea, zinatokana na uteuzi wa Rais. Lakini hii tunaamini kabisa ni katika ile dhana ya kusema kwamba nchi hii haitatawalika maana wameanza kuwatukana Mapolisi, wametukana vyombo vingine vya ulinzi, wametukana Usalama wa Taifa, ametukanwa na Rais pia na leo hii wanatukanwa na kudhalilishwa Majaji kwa kusema kwamba hawajui kiingereza na hata hawawezi kuandika hukumu hali ya kuwa wao wenyewe wameshinda kesi zilizohukumiwa na Majaji haohao, mbona hatukuona wakiKataa? Nasema dhana hiyo wamechelewa kuisema na nchi hii itatawalika na wasipotaka waondoke waKatafute mahali pa kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa 14 wa hotuba ya Waziri wa Sheria, amezungumzia sana suala la uboreshaji wa Mahakama za Mwanzo. Nimwombe tu kwamba moja kati ya mahitaji tuliyonayo sisi pale Kipatimu, tunahitaji Mahakama ya Mwanzo kwa sababu wananchi wanatembea kilomita nyingi sana, zaidi ya 100 kwenye kufuata Mahakama ya Mwanzo. Hili linajionyesha katika maeneo tofauti hata Ndugu yangu Dkt. Kitandula amezungumzia tatizo hili lipo kwake Mkinga na hata Kilindi tatizo hili lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine yote ambayo yameainishwa, naishauri Serikali iangalie kwa makini Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya, wapate zile stahiki ambazo wanastahili ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na waongoze vizuri mhimili huu wa dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia pamoja na kuwa najua Wizara ya Nishati na Madini inaleta hutuba yake wiki inayofuata, lakini nataka nizungumzia suala la Sheria ya Gesi. Sheria ya Gesi izingatie kulinda maslahi ya wananchi wa Lindi na Mtwara na hili ni jambo kubwa. Maelezo yangu yatakuwepo katika mchango wangu wa maandishi kwa sababu mimi ni mmoja kati ya Wabunge ambao tulikwenda kufanya *study tour* Trinidad and Tobago na bahati nzuri Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitupa Wanasheria wawili kutoka kwenye ofisi yake na wameweza kujifunza mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie pia sheria kandamizi ambazo zipo. Imefika wakati sasa tuzifanyie marekebisho na mfano wa sheria hii ni sheria ya

*Wildlife Conservation Act* ya mwaka 2009 ambayo inampa zaidi haki mnyama kuliko mwanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niliseme na ninaamini kwa kuwa Jaji Mkuu yuko atalishughulikia. Mahakama imekuwa ni chombo ambacho kinatumika kwenye kuzuia au kutotoa haki na kudhulumiwa kwa mali za umma. Mheshimiwa Jaji Mkuu na Majaji wote, naomba wazingatie kwamba kuna kesi nyingi sana ambazo zimejirundika si kwa sababu za msingi lakini ni kutokana na watu kutumia kama kiegemeo cha kuweza kutekeleza mambo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba mpya inaandikwa na naamini haitawezekana wananchi wote kutoa mawazo yao lakini naamini kwamba wale ambao wanashiriki basi wanawakilisha mawazo yao. Lakini ambalo nilitaka nilisema pia ni kwamba kumekuwa na maeneo ambayo watu wanazungumzia suala la kuingiza ushoga katika Katiba. Hili halitakubalika na halitakuwepo kwa sababu viongozi wa dini wote wamezungumza na kukemea kwamba hili jambo haliwezekani kwani hakuna haki ya mwanadamu ambayo inakiuka amri ya Mungu. Kwa hiyo, hili walielewe na tunalisema hivi kwa upana na uwazi na wala wasije kufikiria kwamba litakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, la mwisho nataka nizungumzie mkanganyiko wa sheria ambazo tunazitunga. Sheria Namba 30 ya mwaka 1974 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2004 inampa Waziri wa Fedha mamlaka na uwezo wa kukopa, lakini pia tumepitisha Sheria ya *Public Private Partnership* ambayo inaruhusu mamlaka husika za Serikali na taasisi zake kuweza

kuingia ubia na makampuni, mashirika na taasisi binafsi. Sasa kama yeye peke yake ndiye mwenye mamlaka haya, kidogo hapa kuna mkanganyiko na naamini kabisa Waziri wa Sheria hili amelisikia na Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelisikia. Tunaomba hili lifanyiwe kazi na lipate msukumo ambao unaweza ukaleta na kuchochea maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kabisa katika mkutano huu Waziri Mkuu alitoa tamko la Serikali kuridhia kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi. Ombi langu ni kwamba zoezi hili liharakishwe kwa sababu limekuwa linaleta kero na imekuwa ni malalamiko ya Jumuiya nyingi za Kiislam kwa kipindi kirefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi pamoja na kuwa yalikuwepo mengi lakini naamini kabisa mchango huu utazingatiwa na utaingizwa kama unavyoweza kuingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Murtaza Mangungu na sasa nitamwita Mheshimiwa Ahmed J. Ngwali atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema anayetuwezesha kuwepo hapa salama tukiwa wazima wa afya lakini vilevile nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumnukuu Mwanazuoni na Kiongozi wa Siasa za Kimapinduzi za Zanzibar, *Comrade* Ahmed Bin Aboubakar Shibli Bin Omar Kunlatein aliposema katika uhai wake, naomba nimnukuu:-

*"Fursa ni sawasawa na mali, inategemea utakavyoitumia, ukitumia kwa wema basi utapata matokeo mema lakini ukiitumia vibaya itakuangamiza".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwaomba wananchi wa Kusini Pemba hasa wakiwemo wa Jimbo langu la Ziwani, wajitokeze kwa wingi kutumia fursa hii siku ya tarehe 17/7/2012 mpaka tarehe 29/7/2012 wakati Tume ya Kukusanya na Kuratibu Maoni kwa ajili ya Katiba mpya itakapokuwepo Kisiwani Pemba. Naomba sana wananchi wa Pemba hasahasa wa Jimbo la Ziwani lakini na Majimbo mengine, watumie wosia aliotuachia *Comrade* Badawi kwa kutumia fursa hii vizuri sana kwa kutoa maoni yao kama ilivyo katika Ibara ya 18 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo inasema, naomba kunukuu:-

*"Kila mtu ana uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kila mwananchi aeleze fikra zake kwa kadri ambavyo yeye mwenyewe anaona bila kufuata nguvu za aina yoyote za kisiasa ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo muhimu kwa Wazanzibar na wananchi wa Kusini Pemba katika Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kuangalia zaidi mambo yanayohusu Muungano na Muungano kwa sababu

ukiachia mambo yanayohusu Muungano na Muungano kwa Wazanzibar hakuna lingine jipya kwa upande wao kwa sababu Katiba ya Zanzibar tayari ime-*cover* kila kitu kinachoihusu Zanzibar. Kwa hiyo, mwangaza mbili moja humponyoka lakini sisi tumepata bahati ya kuangaza moja tu. Kwa hiyo, Muungano na mambo ya Muungano ni muhimu sana kwa Wazanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekeze hoja yangu kwenye Sheria ya Takwimu. Sheria ya Takwimu, Sura ya 351, *section 3,* naomba ninukuu:-

*"Statistics means information in connection with, or incidental to, any census or all or any of the matters specified in the Second Schedule".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *second schedule*, Ibara ya 32 kuna mambo yameainishwa ambayo yanatakiwa yawemo katika sense, ni *community, social welfare, religious and personal services.* Kwa bahati mbaya sana, kipengele cha dini katika dodoso la sensa kimeondoshwa, hakipo. Sasa sijui ni kitu gani hasa wanachoogopa mpaka kupelekea kuondoa kipengele cha dini katika dodoso la dini, mimi sielewi kitu gani cha msingi. Wakifaya hivyo wanakwenda kinyume kabisa na Ibara ya 18(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo naomba ninukuu inasema:-

"Kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimblai muhimu kwa maisha ya shughuli za mwananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuelewa haki yangu ya kimsingi ya Katiba, kwa nini wanakiondoka? Nataka kujua habari ya sensa, nataka kujua Waislamu wangapi na Wakristo wangapi, haina shida! Mimi najua Mchungaji Msigwa ni Mkristo na mimi ni Muislamu shida yake iko wapi, mbona hatupigani? Tatizo lipo wapi? Kitu kibaya zaidi wameweka majumba ya ibada katika dodoso la sensa wakaacha kuweka waumini wa majumba hayo, tatizo lipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waislamu hivi karibuni nimesikia katika vyombo vya habari na Jumuiya mbalimbali za Kiislamu zimetoa taarifa kwamba zitagomea sensa ya watu na makazi itakayofanyika kuanzia tarehe 26. Ikiwa kweli Waislamu watagomea hiyo itakuwa *survey* na siyo sensa, kwa nini kipengele cha dini katika dodoso la sensa kisirejeshwe? Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Umoja wa Mataifa unao mwongozo unaoelekeza nchi zinazofanya sensa ya watu na makazi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unapozungumza hilo ujikite sana katika kuoanisha habari ya sensa na mjadala uliopo humu ndani.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sheria yenyewe iliyokiukwa! Nazungumzia kukiukwa kwa Sheria ya Takwimu, ndicho ambacho nazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Mataifa umetoa mwongozo wa nchi zinazofanya sensa ya watu na makazi na imeelekeza kipengele cha dini na madhehebu kiwepo

katika mwongozo huo. Mimi nashangaa kitu kimoja, sensa kama haitaingiza mambo ya dini na madhehebu, silka, mila na utamaduni wa watu wenyewe basi hiyo sensa haitakuwa katika kiwango cha kimataifa. Kwa sababu kwa mfano, mtu anayekuja kuwekeza Zanzibar ni lazima ajue madhehebu, silka, mila na utamaduni wa watu wa pale na dini zao ili anapokuja kuwekeza ahakikishe kwamba anawekeza kutokana na mila na dini iliyopo, lakini atakayekwenda kuwekeza Njombe atajua awekeze vipi lakini unapoondoa mambo kama hayo yaani unapopinda sheria kwa mtu mmoja au wawili ambao wamekaa wamepinda sheria, hicho kitu hakiwezekani. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba sioni kosa la watu ambao wanataka kugomea sensa kwa sababu ya kuondoshwa kipengele hicho, sioni. Zimekuwa zikitolewa takwimu mbalimbali ambazo zinapingana kabisa na hakuna takwimu sahihi, huyu anasema hivi na yule anasema vile, kila mmoja anatoa takwimu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanahistoria Bobezi Mohamed Saidi anasema, vyanzo tofauti vya sensa vinatoa matokeo tofauti. Kwa hiyo, naomba warejeshe kipengele cha dini katika dodoso la sensa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Ahmed J. Ngwali. Naomba nimwite Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya makadirio ya Wizara ya Sheria na Katiba. Naomba niende moja kwa moja katika Tume ya Kukusanya maoni ya Katiba na ndio utakuwa mchango wangu katika pointi moja hiyo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sheria ile inapitia mchakato mbalimbali wa kisheria, yalisemwa mambo mengi, tulipitia hatua mbalimbali na hatimaye Rais akakubaliana na maoni ya watu na baadaye sheria ikaundwa na baadaye Rais akaweza kutuundia Tume ya Kukusanya Maoni ya Watanzania ili waweze kutengeneza Katiba yao. Tume hiyo ilipoundwa kulikuwa hakuna mashaka. Watu wote walifurahi, hakuna aliyeibeza na watu walifikiri kwamba tumepata Tume nzuri chini ya Mwenyekiti, Makamu wake na Wajumbe wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Tume hii sasa imeanza kukusanya maoni ya wananchi na imeanza Mikoa mbalimbali ukiwepo Mkoa wa Kagera. Mimi nitajikita katika Mkoa wa Kagera kwa sababu siwezi kujua kinachotendeka katika Mikoa mingine. Katika kukusanya maoni, Tume hii sasa badala ya kuheshimika imeanza kufanya mambo ambayo hayapendezi kwa wananchi ambao wanatoa maoni. Kitu cha kwanza, wameandaa ratiba ambayo haiwezi kufanikisha watu kutoa maoni yao. Ninayo ratiba hapa ya Mkoa wa Kagera, ukiangalia jinsi walivyoandaa ratiba yao unaweza kuuliza, je, nani aliwasaidia katika kupanga ratiba hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze na Biharamulo. Biharamulo ina Kata 14, wameenda katika Kata sita tu na

sio Kata sita wanakwenda kwenye Kata moja, Kata nyingine kunakuwa na umbali wa kilomita 50 au 60. Nashangaa ni jinsi gani watu wanavyoweza kwenda kukusanya au kutoa maoni yao. Wamekuja Ngara, kuna Kata 20 wameenda kwenye Kata sita tu. Cha kushangaza kuna Wilaya ya Muleba ambayo ina Majimbo mawili ina Kata zaidi ya 40 wamekwenda kwenye Kata nane.

Mheshiumiwa Mwenyekiti naomba nikupe jiografia ya Muleba. Wamekwenda kwenye Kata ya Nyakabango. Nyakabango ni mpaka kati ya Chato na Jimbo la Muleba Kusini. Kituo kinachofuata ni Muleba Mjini, *distance* ya kilomita 100, wameacha Kata ya Kapitembe, Kasarunga, Yanshamba, Kata zote hizo karibu nane. Kwa hiyo, tunaanza kujiuliza hawa watu wana maana gani? Kinachonishangaza zaidi ni kwamba hawatoi matangazo, kwa hiyo watu hawaendi. Walipofika Ngara kwa mfano walifika Ngara Mjini siku ya Jumapili siku ya watu kwenda Kanisani, watu hawakuweza kwenda kutoa maoni yao na wakifika pale wakikuta watu kumi wanatoa maoni watu watatu, wanne halafu wanakula *relay* mita 100 wanakimbia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili nakuwa na mashaka kwa kweli. Kama kweli watu hawa wanadhamiria watu watoe maoni yao, ratiba hii ya Mkoa wa Kagera, mimi kupitia Bunge hili namtaka Waziri na hata watu wote wanaohusika na jambo hili katika sheria wa-*review* ratiba hii ili watu waweze kutoa maoni yao. Siwezi kusoma ratiba yote hii, ninayo hapa ya Majimbo yote na Wilaya zote yaani ni jambo la kushangaza kabisa. Mahali ambapo wamejitahidi kufanya vizuri ni Bukoba Manispaa. Kuna Kata 14 wameweza kwenda Kata nane, lakini pia Kata ziko

karibu karibu watu wanaweza kuendesha pikipiki, baiskeli wakaenda kutoa maoni yao. Ukienda Muleba Kaskazini wamekwenda kwenye Kata inayoitwa Lutoro na Mushabako yaani kule ni karibu kabisa na mpaka wa Karagwe. Kwa hiyo, ina maana watu wa Kata ya Kamachumu, Tishanda, Muliyakishajo wote wale hawapewi nafasi ya kwenda kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hili ndilo limenisimamisha hapa kuuliza, je, hawa watu waliowapa ratiba hii ni kina nani? Kwa sababu malalamiko ni mengi na tunapigiwa simu tunaulizwa hawa watu wamekuja kufanya nini hapa. Tunaomba sasa jinsi tulivyoiamini Tume hii wakati inateuliwa ifanye kazi yake. Hawa watu wametengewa fedha nyingi, wanakimbia nini? Hizi ni fedha za walipa kodi, hizi ni fedha za Watanzania, wote wapewe nafasi ya kutoa maoni yao, wawe huru, waseme chochote na wale watu ni wataalam, wasikilize maoni ya watu taratibu, watu waseme wanayoyaona halafu wenyewe watachambua na wataweza kutengeneza rasimu ya Katiba iliyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi, nilichoomba kuchangia ni hicho. Kwa niaba ya watu wa Mkoa wa Kagera ninasema Tume hii ya kukusanya maoni haikuwatendea haki na kama itaendelea hivyo basi ina maana labda kuna kitu nyuma yake. Watu wapewe nafasi, kwa vile Tume imegawanyika katika makundi warudie ili watu wote wa Kagera waweze kutoa maoni yao. Wanakimbia nini au wakati mwingine wanakwenda kwenye maeneo ambayo watu hawana uwezo. Si Kata zote zina uwezo na uelewa, zile Kata ambazo zina waelewa hawagusi kabisa, sijui wanaogopa nini. Pale kwenye miji

midogo, pale ambapo kuna watu ambao wanaweza kutoa maoni, wanakimbia wanakwenda pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hii haiwezi kuwa sawa, Watanzania hatuwezi kuikubali na sisi katika Mkoa wa Kagera kwa ratiba hii hamjatutendea haki. Mheshimiwa Waziri hapo ulipo, wewe ndio unasimamia jambo hili, uiambie hiyo Tume isitumie fedha zetu za Kitanzania bure, posho hizo wanazolipwa, magari waliyopewa, nyumba walizopangishiwa ni fedha za Watanzania, wafanye kazi kwa utulivu, waende Kata hadi Kata kama walivyotuambia, wasifanye mambo haya ya kukurupuka na hatimaye wao kuja kutoa mawazo kutoka kwenye vichwa vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hata kama muda umebaki, lakini kupitia Bunge hili nimeamua kusema hili ili kusudi Watanzania wa Mkoa wa Kagera waelewe na wajue kwamba malalamiko yao nimeyafikisha mbele yako Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Sasa kama nilivyosema nitamwita Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, inabidi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Bunge hili. Mimi nilikuwa nataka kuzungumzia kwanza kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu ninavyojua Tanzania tuko katika Utawala Bora lakini hii Wizara inayoshughulika na Utawala Bora tumeiweka

nyuma. Kwanza tumeipa fedha finyu, bajeti yake ni ndogo ambapo yeye ndiye anayeangalia vitengo vya sheria na sisi tunaangalia sheria ndiyo inayoongoza nchi yetu hasa ikiwa tunakwenda kwenye sheria huyo mwenye kusimamia sheria tunamnyima fedha za kufanyia kazi tunategemea nini? Kulikoni? Kwa sababu nashangaa bajeti yake ni finyu, mwaka jana ilikuwa finyu na mwaka huu iko vilevile finyu sasa ningeomba Serikali kama kweli tunazungumzia Utawala Bora, Wizara hii lazima tuiboreshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano ajira kwa Mahakimu wa Mwanzo. Serikali imefanya juhudi, imeajiri Mahakimu 300 wa Mahakama ya Mwanzo, lakini kazi hii tuliyoifanya bado ni kitendawili kwetu kwa sababu tunawachukua Mahakimu, tunawapeleka kwenye sehemu zao za kazi hakuna vitendea kazi, hakuna majengo bora, hakuna vifaa bora sasa tumeajiri Mahakimu wengi bila ya kwenda kufanya kazi si tunaharibu fedha za umma? Kwa sababu unampeleka mtu akafanye kazi ukampe na vitendea kazi si uongeze wingi wa Majaji wakati tunawapeleka kwenye vituo wakakae watizamane, ina maana hizo kazi zitakuwa hazitendeki. Kwanza Majaji wetu ni watoto wa kileo, unampeleka kijijini hakuna kitu, hakuna chochote akafanye nini? Kila siku tutakuwa nao Dar es Salaam hapa. Safari hazishi ili muwape posho na fedha zenyewe hazipo. Sasa naomba muwatupie jicho la rehema kwa kuiangalia hii Wizara. Mnaiongezea kazi na mnaiongezea fedha za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wakati tunaongeza Majaji, tuongeze na Mawakili wa Serikali. Mawakili pia hatuna, hivi vitu vinatakiwa viende sambamba. Tunalifanya moja na tunaangalia na lingine. Nafikiri hili nikilisema kama

nitakuwa nakumbusha ili na hilo lingine liweze kutendeka ili Mawakili wa Serikali tuweze kuwaajiri ili waweze kusimamia uendeshaji wa kazi za mashauri mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tuje Mahakama Kuu. Mahakama Kuu kuna Majaji wana uwezo wa kufanya kazi lakini Majaji hawa wapatao 30 tumewakodia nyumba za watu binafsi mwaka wa tatu kodi ambayo tunasema pango haijalipwa, kweli Hakimu huyu ataweza kufanya kazi kwa ufanisi? Hivyo hatakuwa na ari na moyo wa kufanya kazi. Anapokuwepo kazini anawaza nyumbani mama na watoto saa ngapi watatimuliwa. Sasa naomba Mahakama au Serikali nikiiambia hata Wizara hana kitu lakini Serikali muitazame. Wizara ya Fedha muwatazame hawa Wizara ya Sheria na Katiba na Mahakama zake ili muweze kuwapatia fedha angalau hawa Majaji waweze kulipiwa pango ili waweze kufanya kazi za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile huu mwaka wa tano stahili zao zilikuwa tayari zishapitishwa na Serikali, kilichosababisha ni nini mpaka leo hawajapewa? Kwa sababu mtu akiwa anadai chake kusema mwenyewe hawezi asemewe. Sasa naomba jamani chondechonde huku wakiangalia kodi hawalipiwi, huku stahili yake hapewi watafanya kazi vipi Majaji wetu hawa? Naomba na hili Mheshimiwa Waziri akija akitoa ufafanuzi na hili ningeomba angalau tulipatie ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye Mabaraza ya Ardhi. Mabaraza ya Ardhi mimi toka jana ilivyokuwa ikizungumziwa Wizara ya Ardhi, nilikuwa naona msongamano uliokuwepo, kwa sababu Mabaraza haya kuwa katika Idara ya Ardhi huko TAMISEMI tunajidanganya

wakati Wizara ya Katiba na Sheria ipo na hiki chombo cha ardhi siyo kitu cha sheria, kwa nini tusiwapeleke kwenye Wizara hii inayohusika? Kwa sababu watakapokuweko huku watakuwa wanafanya kazi kisheria, watakuwa wana uwezo na wenziwao Majaji wapo. Kama kuna msongamano watasaidiana japo kuna sheria na kanuni inayowalinda lakini kusema tunaiweka Wizara ya Ardhi au kusema tunaiweka TAMISEMI tunajidanganya au tutasema kwamba ahaa maana yake vijijini Wizara hii haiko lakini tuajiri watu tuwapeleke kwenye Halmashauri watakuweko huko ambao wafanyakazi wa Wizara ya Katiba na Sheria na Utawala Bora ambao wataweza kufanya kazi kufuatana na taratibu na sheria. Imekuwa kesi haziendi, mlundukano wa kesi uko mwingi, malumbano yanakuwa mengi, watu wanalumbana kwa jambo dogo la msingi, kitu chochote kikienda kwenye sheria kitafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Hata ukija kwenye Mabaraza, hao wengine sio Wanasheria wanafanya kazi kwa mujibu wa mila au tamaduni za sehemu ile. Sasa utakuta bado kuna mvutano wa kisheria. Naomba hata suala hili lingeangaliwa tena na likapelekwa kwenye Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija na wazee wa Mahakama, nakubaliana na michango inayotolewa na Wazee wa Mahakama katika jamii katika suluhisho, lakini kinachoshangaza narejea palepale kusema kwamba jambo lolote linalohusu sheria likae Mahakamani na mnawapeleka mjue kwamba wamesomea sheria. Japo watakuwa wana maadili ya kijamii ya uzee lakini hapo hapo na sheria ajue. Mfano Majaji wetu wastaafu mnaweza mkawafanya kwa sababu sheria tayari anaijua. Lakini mkasema tunawachukua wazee wa vijiji, mambo ya mila na tamaduni bado usumbufu upo, mlundikano wa kesi

utakuwepo, jamii itakuwa na matatizo na kila kitu kitakuwa akiendi sawia kama kinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija hii Kurugenzi ya Mahakama. Kitengo hiki kinahitaji kusaidiwa. Kwanza kipate ofisi kwa sababu ofisi hakina, pili vitendea kazi hakina hata bajeti yake ukitazama ndiyo hivyohivyo. Kwa sababu bajeti ya maendeleo ndiyo ingekuwa suluhisho ya Idara hii ingeweza kujenga maofisi, zingeweza kujenga nyumba za Majaji wetu, zingeweza kufanya kila kitu ambacho kinachostahiki kufanywa ili kuifanya Mahakama yetu, kufanya Wizara yetu, kufanya taasisi zetu za sheria zifanye kazi ili ziweze kumuondolea shida Mtanzania katika jamii hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa haya machache, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Assumpter Mshama na Mheshimiwa Mohamed Chomboh ajiandae.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika jambo muhimu hili lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa upendo alionao juu yangu. Napenda nimtukuze yeye kwa sababu ananiwezesha. Napenda tena kushukuru kupata nafasi kwa namna ya pekee ili nichangie vizuri katika suala la Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe pongezi kubwa kwa Waziri na Naibu wake pamoja na timu nzima ya Wanasheria kwa namna ya pekee wanavyofanya kazi kwa kulisaidia Taifa letu la Tanzania. Nimpongeze Mheshimiwa Angellah kwa kupata nafasi hiyo, kwa kweli unaweza. Pia napenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia mchakato wa Katiba kuanza na kwa namna ya pekee kufanya haraka uanze na kwa namna ya pekee kutuchagulia viongozi waadilifu, watu wenye uwezo, watu wanaoaminika na ni ajabu tayari wako uwanjani wanatenda kazi, katika hilo, Mungu ambariki sana. Pia nataka nimpongeze kwa timu alivyoitengeneza nusu kwa nusu Watanzania Bara na nusu Watanzania Visiwani, ameijali jinsia, ameangalia hata makundi, kwa kweli timu ile inatosha na tunaamini kwamba itatutendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa rai kwa Watanzania kwa namna ya tofauti, kwa siku ya leo Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa namna ya tofauti na ya ajabu sana kwa maneno waliyotumia katika kuwakilisha hotuba yao. Sitaki kusema kwamba aliyewakilisha si Mwanasheria lakini napata wasiwasi alisomea wapi Uanasheria wake? Asiyeweza kuangalia kwamba kum-*offend* mtu, kumdhalilisha, kumnyanyasa, mtu ameteuliwa, hana kosa lolote, akamfikisha mahali ambapo hata familia yake inashangaa, kwa nini mtu adhalilishwe namna ile. Hilo ni kosa na hao watu wangekuwa na uwezo wangeweza kumshtaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijali ni namna gani mtu atapokea, najali namna gani mtu amejisikia anapokuwa amedhalilishwa bila sababu yoyote. Nataka niwatie moyo

Majaji, kwamba kazi yenu ni nzuri na aliyewachagua amewaamini na anajua kwamba kazi mtaifanya bila kujali maneno yaliyosemwa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nifungue ukurasa wa 14. Ukisoma ukurasa wa 14 unasema:-

*"Uteuzi wa baadhi ya Wakuu wa Wilaya unaashiria kukithiri kwa rushwa."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe kuuliza kwamba Rais wetu alipomchagua mtu ambaye alikuwa anapambana na Mbunge wa Kawe, akamchagua na kumpa Ubunge na kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, je, ilikuwa ni rushwa na yule mtu anasimama anaendelea na anapinga hata Serikali. Rais wetu anaangalia uwezo wa mtu, namna gani anaweza aka-*deliver* na ndiyo maana amempa nafasi hiyo hata kama ametoka upande wa upinzani. Kwa hiyo, suala la kwamba eti ni rushwa sio kweli. Rais ameridhika amempatia nafasi, anaweza kuendelea kama alivyompa mtu aliyekuwa anampinga Mbunge wa Kawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye suala la Mahakama zetu. Suala kubwa ambalo mimi linanitatiza ni kupotea kwa mafaili. Unaweza ukawa na kesi unaenda kwenye kesi yako shauri limefika, faili halionekani. Mimi naomba kushauri kwamba kama inawezekana waweze kuweka *system* ya *computer,* ku-*computerize* kila kesi wakati inaendelea hata Hakimu aweze kutumia *computer* ili kusudi tuweze kuamini kwamba kesi inaendelea kwa halali. Kwa tendo hili linaweza kusababisha watu waone kuna dalili za rushwa. Ipo tabia ukifika Mahakamani faili

halionekani. Napenda nishauri uongozi wa Mahakama uweze kuangalia suala hilo na watu waweze kupata mafaili. Hakuna sababu ya faili kupotea wakati kesi inaendelea Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za Mahakimu. Kumekuwepo na upungufu mkubwa wa Mahakimu Tanzania. Utashangaa, mimi siku moja nimeona Hakimu mmoja, nimekutana naye *Airport* Mwanza anaelekea Musoma, huyohuyo ataelekea Bukoba, anaacha ameahirisha kesi ya Bukoba, akitoka Bukoba anaahirisha Musoma akirudi Dar es Salaam anaanza upya, matokeo yake kesi zinachukua muda mrefu. Hivi kwa nini Serikali tusipate Mahakimu kila Mkoa angalau mmoja kuliko Hakimu kuzunguka na kuazimwa kwenda kwenye Mahakama nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahabusu bila miundombinu ya kujisaidia. Mtu anapokuwa amekamatwa, amewekwa ndani wakati mwingine hana kosa lolote lakini anafika kule anakuta ndoo. Hivi ndoo kweli? Huyu mtu kwenda mahabusu ni kuondoa utu wake? Ndoo wanayotumia kila mtu anakaa kwenye ndoo hiyohiyo matokeo yake mtu anatoka kule ameambukizwa magonjwa na magonjwa mengine hayatibiki. Kwa nini tusiweke miundombinu ya choo mtu hata kama yupo mahabusu aende chooni kwa amani, kitendo cha kutumia ndoo kwa kweli sio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze adhabu ya kifo. Jamani kuna watu wamehukumiwa zaidi ya miaka kumi sasa. Yupo pale akisikia mtu amefungua mlango anadhani anakuja kuchukuliwa kunyongwa. Hivi kwa nini? Kama hiyo Sheria hatuitumii, tuiache na kusiwepo na

hukumu ya kifo kuliko kumhukumu kifo lakini kumuua humuui, matokeo yake kuna wanaodai kuuawa. Mwingine siku moja alisema si mniue tu maana auwaye kwa upanga atakufa kwa upanga, niko tayari kuliko kunitesa kukaa kila siku nangoja kufa kesho, kesho hauwawi. Naomba kama hatuwezi kuwaua basi tusiwahukumu kifo na tusiwaue, Mungu mwenyewe anasamehe, tunaweza kuiondoa bila kutesa watu kwa kusubiri kuuawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni uchakavu wa majengo. Zamani miaka ya 1960 kila Kata kulikuwa na Mahakama kama sio zote. Kwetu kila Kata ilikuwa na Mahakama lakini leo Tarafa nzima ina Mahakama moja na hiyo Mahakama haina Hakimu. Unakuta mtu anatoka Bukoba Vijijini kuja kwetu kule Gera wakati Kata zote zinayo majengo mazuri, ni kuyakarabati tu, tunachohitaji ni Mahakimu. Naomba tuweze kutengeneza Mahakama. Miaka ya 1960 yalikuwepo majengo, leo ni mwaka 2012 hakuna majengo na mimi nadhani katika suala hili Wizara hii badala ya kwenda mbele inarudi nyuma. Kwa hiyo, naomba wawekewe majengo watu waweze kuhukumiwa vizuri. Watu wanatembea *distance* kubwa sana jamani. Mtu kaibiwa kuku kesi inachukua miaka mitatu lakini yule aliyeibiwa kuku anataka kesi iendelee. Kwa hiyo, naomba hizi kesi tuziwekee mahali pa kuziamulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Mahakimu ambao hawafuati maadili. Tuseme ule ukweli wapo lakini jamani naomba hii Tume ya Utumishi wa Mahakama ifanye kazi. Hivi kweli Mahakimu huwa hawashtakiwi? Mimi sijawahi kusikia Hakimu ameshtakiwa. Hivi hawakosei na wao ni wanadamu! Kwa hiyo, tunaomba kama zipo Tume zifanye

kazi, Sheria ichukue mkondo wake hata wao wakikosea waweze kuhukumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia nyingine inayonishangaza sana ya kila siku mnasema hapa kesi ipo Mahakamani na watu wengine wamekuwa wajanja, wanaanzisha kesi, wanakimbilia Mahakamani ili mshindwe kuongelea, matokeo yake kesi inakaa miaka kumi, wananchi hawatendewi haki. Bora tuongelee kesi au tutunge sheria, sisi ndiyo watunga sheria kama tunaiona kesi imechelewa na inatakiwa kuongelewa tufungue kile kipengele watu wapate haki zao. Kwa kweli hii hali ni ya kutowatendea Watanzania haki na matokeo Watanzania wanaichukia Serikali yao kwa vitu kama hivi. Ana kesi miaka kumi, kumi na tano, mtoto mpaka anaenda shule, anaenda Chuo Kikuu baba yake bado anaenda Mahakamani, hiyo sio haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa mchango wangu kidogo jioni hii ya leo. Naanza kwa kuunga mkono hoja lakini pia kwa kujaribu kutafakari na maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Nilikuwepo alipokuwa akisoma na pia nimesoma Hotuba yake, kwa kweli kuna mambo nataka kidogo kuyazungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Katiba na Sheria katika shughuli zake ni pamoja na kusimamia mambo ya sheria za nchi. Mimi kuna sheria moja ningependekeza kwa kipindi kinachokuja kufanyiwa marekebisho hasa Sheria hii

ya Tume ya Uchaguzi ya kuchagua viongozi kama Wabunge. Sheria ya sasa ni kwamba mtu ambaye anaweza kusoma na kuandika, akiwa na akili timamu na akiwa na umri ambao umefika miaka kumi na nane, anaweza kugombea Ubunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuandika mtu anaweza kuwa anajua kuandika na tukamwona na umri atakuwa ana cheti cha kuzaliwa lakini hili suala la akili timamu lina kuna ya kupimwa ili tuweze kupata viongozi waliokuwa na akili madhubuti ya kuisaidia nchi hii na Bunge hili. Kwa sababu haiwezekani mtu mwenye akili zake timamu akawa anajenga fitna kila siku ya Mungu ya kugombanisha Watanzania kwa sababu tu eti Upinzani. Wapinzani wangapi tumeshawaona sisi? Hili ni jambo linasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waislamu kuna aya moja katika *Quran* inasema:-

*"Mtu fitna ni mtu mbaya kuliko hata muuaji."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtu fitina ndiye anasababisha watu wengine waweze kupata jazba ya *commit suicide* na kuua watu wengine. Huyu ndiye mtu fitna na mtu huyu anatafuta kila njia, akipata upenyo kidogo tu inafika hadi mambo mengine kujisingizia mwenyewe ili mradi ile fitna yake itendeke. Tumeona na tumesikia ni namna gani watu walivyojaribu kuwashawishi na kuwafitinisha Madaktari wetu na raia, matokeo yake sasa hivi lile limeonekana halifai wanajisingizia sasa. Fitna hawa! Wanataka kukamatwa, wanataka kuuliwa, huyu ni fitna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria hizi tunapotaka kuzisimamia ndugu zangu na viongozi wetu hawa lazima tupimwe. Tuwe tunakuja hapa, tunahakikisha kwamba tunakuja na akili zetu timamu, tupate viongozi madhubuti na viongozi wazuri wanaoweza kutuongoza na kuleta matokeo ambayo tunayategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ni Wizara muhimu sana na inasimamia haki za watu na Mheshimiwa Rais kadri ya uwezo aliopewa na kwa mujibu wa Katiba anahakikisha kwamba anachagua watu madhubuti wenye akili zao timamu, wenye elimu inayokubalika, leo akitokea mtu akaona watu wote hawafai anafaa yeye, *Subhana!* Huo ni mtihani mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ina watu madhubuti, ndugu zangu Majaji na Mahakimu fanyeni kazi kwa mujibu wa kazi zenu isipokuwa Wizara inahitajika kupewa nyenzo na kupewa nguvu zaidi ya bajeti yake ili ndugu zetu hawa pamoja na kwamba wanadhalilishwa hivyo basi angalau hizo pesa wazipate. Kwa sababu madhila wanayopewa na watu kwa maneno na kukashifiwa na kudharauliwa namna hii halafu hatuwapi tena haki yao, sio jambo zuri. Tuhakikishe Wizara inapewa uwezo wa kuweza kuwafanya ndugu zetu wafanye kazi vizuri kwa maana ya maslahi yao, nyumba zao, vipande vyao ili mradi kila stahili zao wanazostahili kupewa wapewe kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka pia kuzungumzia suala la Tume ya Katiba inayozunguka katika Mikoa yetu na Wilaya yetu. Ndugu zangu Zanzibar, nashukuru wameanza kwetu kule Kusini na wamejitokeza

watu kwa wingi na nawaambia waendelee kujitokeza na watoe maoni yao juu ya mabadiliko ya Katiba mpya tunayoitegemea kwa maslahi ya nchi yetu ili tuweze kupata Katiba ile ambayo itatupeleka zaidi ya miaka 50 mbele. Vizazi vyetu viweze kufaidika na lile jambo ambalo sisi sasa hivi tunalitayarisha kwa ajili yao. Tume itafanya kazi yake vizuri, wakusanye kila ambacho kinatolewa na wananchi kwa sababu hayo ndiyo maoni yao. Ni vizuri zaidi wakazingatia kwamba kile ambacho wanakitegemea, wanachokizungumza kije katika hatua za mwisho kwa maana ya Bunge la Katiba na kutoa yale maoni ambayo wanategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sina zaidi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana. Kwanza, naanza kumpongeza Waziri na nampongeza pia Naibu Waziri na napenda kumpongeza sana Katibu wetu wa Chama cha Wabunge Wanawake Mheshimiwa Angellah na tunakuamini kazi hii unaweza. Pia nawapongeza Mwanasheria Mkuu na viongozi wote pamoja na Majaji na Mahakimu ambao wengine wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia Tume hii ya kukusanya maoni kwa ajili ya Katiba na nampongeza Mheshimiwa Jaji Warioba kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa kuongoza Tume hii na tunaimani naye na timu nzima ambayo imeteuliwa kwa

kuangalia pia usawa wa kijinsia, Bara na Visiwani, wote tumechanganywa humo na makundi mbalimbali. Kwa kweli timu ile imesheheni watu wenye vipaji mbalimbali na tuna uhakika kwamba watatupatia maoni mazuri na tunapenda kutoa mwito tu kwamba waende sehemu nyingi ili kuwafikia na wananchi walioko vijijini na wanawake ili waweze kutoa maoni kwa ajili ya kupata Katiba ambayo itakuwa imemhusisha kila mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Mahakama zetu na hasa Mahakama za Mwanzo. Kwa kweli Mahakama nyingi za Mwanzo ni chakavu kama Wabunge wenzangu walivyosema. Zimejengwa muda mrefu sana, majengo yapo lakini hayafanyiwi ukarabati. Sasa mimi natoa wito kwa Serikali kama tulivyoamua kufanya ukarabati wa shule za msingi tukarabati pia Mahakama. Tunawapeleka Mahakimu ambao wamemaliza Vyuo Vikuu lakini mazingira wanayofanyia kazi kwa kweli ni magumu. Pia tuangalie pale ni mahali ambapo panapotolewa haki, hata mtu unapofika Mahakamani jengo limechoka, kila kitu kimechoka, vifaa vilivyomo mle ndani, watu wanakosa hata moyo wa kufanya kazi. Sasa naomba kuwe na mkakati maalum wa kuweza kujenga au kukarabati majengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mdogo tu wa Mahakama za Mwanzo zilizoko katika Mkoa wangu. Mahakama ya Pawaga imechoka, Mahakama ya Idodi, Mahakama ya Mlolo na Mahakama nyingine nyingi zikiwemo Mahakama za Njombe, Makete na Mahakama ya Kifanya, nyingi sana zimechoka. Sasa mimi naomba nitoe mwito, nimkaribishe Waziri au Naibu Waziri aje ajionee Mahakama zetu za Mwanzo tulizonazo zilivyokuwa na hali

mbaya na kama tunapeleka watumishi, watakosa moyo wa kufanya kazi, matokeo yake watakimbia, tutajikuta pia tuna Mahakama lakini watendaji hawapo na haki kwa wananchi zinaendelea kukosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ninaloliona ni usajili wa vizazi na hasa kundi la watoto. Nchi hii ina usajili mdogo sana. Watoto wengi hawasajiliwi na matokeo yake sasa tunawakosesha hawa watoto haki yao ya msingi ya kusajiliwa na kutambulika, hata kwenye idadi hawamo. Kwa hiyo, utambuzi wa watoto ni haki yao kwa kusajiliwa lakini kupata cheti cha kuzaliwa. Watoto wengi wanatimiza zaidi ya miaka mitano hawana vyeti vya kuzaliwa lakini pia watoto wengi wanaozaliwa vijijini hawazaliwi hospitali, kwa hiyo, hawapati vile vyeti vya mwanzo kumtambua ili akifikisha miaka mitano awe amepata usajili. Amezaliwa kijijini kwa Mkunga wa Jadi, hana hata cheti, matokeo yake kinachotokea baada ya miaka mitano wanalipa shilingi 10,000/- kupata cheti kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ndugu zanguni shilingi 10,000/- kwa kila mtoto kwa kijijini au mwananchi ambaye hana cheti, hivi kweli inawezekana? Watoto wengi wanatoka kwenye mazingira magumu, ni yatima, wale walezi wanahangaika hata wazazi wa kawaida ana watoto watatu, hatuna uzazi wa mpango, watu wanazaa watoto wengi, ana watoto watano akatafute vyeti vyao kwa shilingi 10,000/- kwa kila mtoto hivi kweli inawezekana? Hebu naomba hili la kupata vyeti tuliangalie. Vyeti vitolewe kwenye ngazi ya kijiji. Tuna wataalam mpaka Maafisa Watendaji wa Vijiji, watendaji wa Kata, kuna Makatibu Tarafa mpaka tunafika kwenye ngazi ya Wilaya, tuna mfumo mzuri, kwa nini huo mfumo hautumiki kuhakikisha

kwamba vile vyeti vinamfikia kila mtu pale alipozaliwa? Mimi naomba tuutumie huo mfumo kwa sababu tunaelewa kwamba Idara ya Vizazi na Vifo ilikuwa kwenye Ofisi ya Wilaya, mifumo iliyopo itumike ili wananchi wetu wasiteseke. Watu wanahangaika na nauli kwenda na kurudi kufuatilia vyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizopitwa na wakati na hasa zinazowakandamiza wanawake mfano Sheria za Mirathi, Sheria za Ndoa na sheria nyingine ambazo zinaruhusu watoto waolewe chini ya miaka 18. Tunaambiwa zinafanyiwa marekebisho na kwamba zitaletwa, marekebisho gani akina mama na watoto wanateseka. Mama anaachika, anaachiwa watoto halafu matunzo shilingi 10,000/-, hivi ni kweli? Halafu tunasema tunaendelea kuzifanyiwa marekebisho! Mheshimiwa Angellah umewekwa huko makusudi, ndiyo maana umeongezewa, Wizara ilikuwa na Waziri mmoja, umewekwa wewe mwanamke, naomba uwasaidie wanawake wenzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lete hizo sheria hapa tupitie, ndiyo maana watoto wanatupwa barabarani kwa sababu akina mama wanateseka. Akienda Mahakamani anaambiwa matunzo ni shilingi 10,000/-. Kwa hiyo, kama ana watoto wanne anapewa shilingi 40,000/- kwa mwezi. Hivi ni sahihi kweli jamani? Tunaomba kabisa hili lifanyiwe kazi na Tume ya Kurekebisha Sheria, tunaomba izilete hizo sheria mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mrundikano wa wafungwa pamoja na watu walioko rumande, ni wengi sana hebu tutafute adhabu mbadala ambazo zitatuletea maendeleo.

Watu wamerundikana, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imeenda huko Keko na Magereza nyingine wamerundikana wengine kesi zao ndogo sana na nyingine zinacheleweshwa. Kwa nini tusitafute adhabu mbadala badala ya kuwarundika na Magereza yanajaa, mwisho ndiyo huko tunakoona maambukizi ya virusi ya UKIMWI yanatokea. Kunatokea tabia ambazo zinaendelea katika Magereza na Mahabusu, tunaomba zitafutwe adhabu mbadala kwa ajili ya hawa watu. Inaweza kuwa ni kesi ya kuku tu ikampeleka akakaa kule mpaka hata hiyo thamani ya kuku imeisha yeye yuko rumande, gharama ya kumhudumia ni kubwa kuliko kesi inayo mkabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la kuangalia ni upungufu wa Mahakimu. Pamoja na kwamba majengo ni machakavu lakini pia bado kuna upungufu wa Mahakimu, tunahitaji kuendelea kuajiri na Serikali inafanya vizuri sana kuajiri. Pia tuangalie watoa huduma za sheria vijijini *paralegals* hawa wanaweza kusaidia sana katika vijiji vyetu na katika maeneo yetu ambako hakuna Mawakili, wenyewe wakafanya kazi nzuri na wapo wanaofanya kazi lakini hatuna sheria inayowaruhusu wafanye kazi hiyo, tunaomba tuwe na sheria inayowaruhusu wafanye kazi. Mimi nafikiri wakati umefika ili tuweze kutunga sheria ambayo itawatambua rasmi kwamba ni watoa huduma za msingi kwa sababu wao ndiyo wako jirani na jamii na wanaweza kuwa ni kiungo kizuri sana na Mahakama zetu za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kutafsiri sheria au hukumu zinazotolewa ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili. Unamwandikia mtu hukumu kwa lugha ya Kiingereza, mama wa kijijini au baba wa kijijini hajui hata kilichoandikwa

pale halafu unamwambia ndiyo hukumu yako, haelewi chochote. Hebu tumpe mtu hukumu kwa lugha anayoielewa na lugha ni Kiswahili na hiyo ndiyo lugha ambayo wote tunaifahamu na kila mwananchi na wanakijiji wanaifahamu. Sasa mnaandika Kiingereza halafu mnasema mmepitisha kesi, huyu baba au mama atakataje rufaa wakati haelewi chochote kilichoandikwa pale? Nafikiri ni wakati muhimu sasa wa kuangalia hukumu zinazotolewa huko kwenye Mahakama zetu za Mwanzo zote ziandikwe Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi zikiwemo komputa ni muhimu katika Mahakama zetu hata kama ni umeme, zikishakarabatiwa wapewe umeme hata wa *solar* ili Mahakimu wetu waweze kutumia komputa kuandika hukumu na kuandika taarifa mbalimbali ili tuweze kuwa na kumbukumbu sahihi na ziweze kutolewa kwa wakati kuliko muda mrefu wanaochukua kuandika kwa mkono, imeshapitwa na wakati. Hawa vijana wanaoajiriwa sasa hivi ni vijana waliosoma, wanafahamu matumizi ya komputa, hawawezi kuandika kwa mikono, hebu tuwape vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuongelea kuhusu *the amendment of the Evidence Act.* Matumizi ya TEHAMA yamekuwa ni sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Biashara na mikataba mingi ya biashara imekuwa ikifanyiwa kwenye mitambo ya kieletroniki. Wanasheria, wafanyakazi wa

Mabenki, *CEO's* na kadhalika wamekuwa wakipokea au kutoa maelezo kutoka kwa wateja wao au Makampuni yao kupitia mtandao wa kielekroniki. Pia biashara nyingi za kimataifa zimekuwa zikifanywa kupitia mitandao hii *(internet).* Kwa hivyo, naishauri Wizara kufanya marekebisho ya Sheria yetu ya Ushahidi (*Evidence Act*) kuweza kutumia saini ya digitali (*digital signature not electronic signature*), kwa mtazamo huu sasa ni wakati wa kutayarisha *Digital Signature Legislation.* Sisi Wizara ya Sayansi na Teknolojia, tuko tayari kushirikiana na Serikali kuifanya kazi hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Katiba, ni muhimu kutoa fursa kwa Watanzania waliopo nje ya nchi ili na wao waweze kutoa maoni yao. Wanaweza kutoa maoni yao kupitia mitandao ya kieletroniki kama *e-mail, facebook, twitter* na kadhalika.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba yenye matumaini kwa jamii na yenye maelezo ya kina na yanayojitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuridhia mchakato wa Katiba kuanza na hatimaye Tume imeshaundwa. Tume hii ni sawia kabisa, kwani imeweka wajumbe nusu kutoka Tanzania Bara na nusu kutoka Tanzania Zanzibar; lakini pia tumeona kwamba kuna uwiano wa kijinsia na makundi mbalimbali ya jamii yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Tume kwa uzalendo wao kwani pamoja na kwamba vitendea kazi vingine bado havijapatikana lakini wamekuwa imara na kazi ya kukusanya maoni wameanza rasmi tarehe 2 Julai, 2012. Nashauri elimu kwa umma kuhusiana na Katiba itolewe kwani ni jambo muhimu ili waweze kuwa na uelewa utakaowasaidia katika kutoa maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu rai kwa Tume ya Katiba, wajitahidi kwenda katika maeneo mengi kadri inavyowezekana ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi ili wapate fursa ya kutoa maoni yao kuhusu Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya msaada wa kisheria ni muhimu sana kwa wananchi wetu, hususan wasiokuwa na uwezo. Tumeona nchini mwetu zipo taasisi nyingi zinazotoa msaada wa kisheria na tunahitaji kuja na sheria mahsusi ya uratibu wa huduma hii ya msaada wa kisheria. Ni vema, taasisi zinazotoa huduma zikafahamika na ikiwezekana ijulikane nani anaenda katika eneo gani ili kila eneo la nchi yetu liweze kufikiwa na huduma hii ya msaada wa kisheria. Mfano, Mkoa wa Rukwa una Mawakili wachache, hivyo ni vema, taasisi hizi zikajitahidi kwenda katika maeneo ambayo hayapati huduma hii kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, tumejionea *Paralegals* ambao wamekuwa wakisaidia sana wananchi katika sehemu ambazo hakuna Mawakili wa Kujitegemea. Wamesaidia wananchi kuandaa nyaraka za kisheria, utetezi na wanawapa Uwakili wa kisheria kwa wananchi wenye mashauri Mahakamani. Hivyo, ni vyema sasa Serikali ikatueleza ni lini italeta Muswada Bungeni kuhusu Mawakili wa Jamii (*Paralegas*) ili waweze

kutambuliwa kisheria na waweze kusaidia wananchi katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda niliongelee, ni uchakavu wa majengo ya Mahakama na ukosefu wa majengo ya Mahakama. Tunayo majengo mengi, mengi yamechoka na sehemu zingine hakuna majengo kabisa. Ni kwa nini tusifanye tathmini ni shilingi ngapi zinahitajika kujenga Mahakama ambazo zimechakaa na ni kiasi gani kinahitaji kujenga majengo ambayo hayapo ili ikiwezekana Serikali iangalie mpango hata wa kukopa nje ya nchi au katika Taasisi zingine nchini ili ukosefu na uchakavu wa majengo ya Mahakama iwe ni historia; hii ni huduma muhimu kama ilivyo kwa hospitali na shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama zetu zimekuwa zikipungukiwa kiasi kwamba zingine zimekuwa zikihudumiwa na Mahakama zingine. Muhimu tuongeze ajira kwani tusipofanya hivyo wananchi wetu wanakosa haki yao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu ya Taarifa ya Utafiti wa Demografia ya Afya ya Tanzania *(TDHS)* zinaonyesha kwamba usajili wa vizazi kwa kundi la watoto walio katika umri chini ya miaka mitano (5), kwa Tanzania Bara uko kwenye 14% na wenye vyeti vya kuzaliwa ni 6% tu wakati kwa mwaka wanazaliwa watoto zaidi ya milioni moja na nusu. Kiwango hiki ni kikubwa sana kwa watoto ambao hawajasajiliwa wala kupewa vyeti vya kuzaliwa, hivyo hawajulikani. Hata katika kupima maendeleo ya MKUKUTA, kiwango cha usajili wa watoto ni kiashiria kimojawapo ambacho Tanzania inapimwa. Natoa wito

kwa Serikali ijitahidi katika bajeti zijazo kutenga fedha za kutosha za ndani ili kila mtoto nchi hii aweze kupata usajili lakini pia kupata cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi hawafahamu haki zao za kisheria, nashauri Wizara itoe elimu kwa wananchi kuhusu haki mbalimbali za kisheria na masuala mengine kama vile kuandika wosia, ili kuondoa adha wanayoipata wanawake wajane pamoja na yatima, lakini vilevile, Sheria za Ardhi na nafasi ya wanawake katika kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Mahakimu na Majaji wetu wakajikita katika kutoa adhabu mbadala kwani tumekuwa tukishudia wako washtakiwa ambao wamehukumiwa vifungo kwa makosa ambayo yanaweza kutolewa adhabu mbadala kama vile, kutumikia katika jamii kwa kufanya kazi kwa masaa kadhaa chini ya uangalizi wa Afisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mlundikano wa kesi uliopo, ni muhimu kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza idadi ya Majaji wanaoteuliwa ili kuendana na kasi ya mlundikano wa kesi uliopo pamoja na kesi nyingine nyingi zinazoendelea kufunguliwa. Walau kuwe na utaratibu wa kila mwaka kuteua Majaji wapya ili hata wengine wanapostaafu au kufariki pengo lisiwe kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Mahakimu ambao hawafuati maadili ya kazi zao, ni vema sasa, Tume ya Utumishi wa Mahakama ikawachukulia hatua Mahakimu ambao hawafuati maadaili ya masharti ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya Makarani ambao mara nyingi wamekuwa wakidai majalada hayaonekani; ni vema sasa, Mahakama iandae mpango maalum kuhusiana na utunzaji wa kumbukumbu pamoja na mkakati wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili ikiwezekana mafaili yatunzwe pia katika mfumo wa kieletroniki pamoja na ku-*digitilize* mafaili yote yaliyoko Mahakamani na nyaraka nyingine zinazohusiana na kesi. Kutokana na kesi kuchelewa kusikilizwa na matokeo yake kukaa muda mrefu, ni muhimu kwa Mahakama kuandaa kanuni kuhusu msukumo wa kesi na usimamizi au ufuatiliaji wake ili kuwa na kanuni zitakazoainisha kesi zipi zinasikilizwa na za aina gani zitasikilizwa katika kipindi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati. Wizara izifanyie marekebisho sheria zote zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uendeshaji wa mashauri Mahakamani uweze kuwa wenye ufanisi, kuna haja ya Mahakama zetu zote kutumia mfumo wa kurekodi mwenendo wa kesi kwa kutumia teknolojia katika Mahakama za ngazi zote nchi nzima; kwani kwa kufanya hivi, itawarahisishia kazi Mahakimu na Majaji, pamoja na hukumu za kesi kuandikwa mapema kwani kumbukumbu zote muhimu zitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono hoja hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu mkubwa ni juu ya hali za Mahakama. Mahakama za Mwanzo zina hali mbaya ya vitendea kazi na mazingira mabaya hasa majengo ya Mahakama hizo yanatisha na wala hayawashawishi watumishi kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bajeti, ni ndogo sana kiasi kwamba Serikali inashindwa kuwaandalia Mahakimu mishahara mizuri na Makarani na kuandaa makazi ya watumishi hao. Kama bajeti ingeboreshwa kwa kuwa na bajeti nzuri tungepata kuona Mahakama zinafanya kazi na kuondoa suala la rushwa ambayo imeshamiri kwenye Mahakama kutokana na hali bora ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Mahakama ya Mwanzo ya Karema. Mahakama hii ina watumishi wawili tu na jengo ambalo limezeeka sana na halina milango. Naiomba Serikali iangalie jinsi ya kuboresha Mahakama hii ambayo ni pekee kwenye Jimbo langu. Naiomba Wizara ipeleke mabati na vitendea kazi vinavyohusiana.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nishukuru kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii. Pia nikishukuru Chama changu cha *CUF* kwa kuweka misingi imara ya kusimamia haki za binadamu. Pia kuendeleza itikadi yake yenye kutoa neema kwa watu wote, itikadi ya utajirisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kilwa Kusini kwa kunipa ushirikiano katika kuendeleza Jimbo na pia kwa viongozi na

wanachama wenzangu kwa kuchangia mawazo na kupeana mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwa kunukuu Ibara ya 3(1) na Ibara ya 9 ya Katiba, imesema Tanzania inafuata siasa ya ujamaa na kujitegemea yenye kufuata misingi ya udugu na amani lakini tulishoshuhudia sisi *CUF,* ni siasa za CCM za kuvizushia vyama vyenye nguvu maneno yanayoashiria kuvunja udugu na amani. Mwanzoni *CUF* ilitajwa kuwa ni Chama cha Wapemba na pia ni cha Kiislam na sasa CHADEMA inatajwa kuwa ni Chama cha Wachaga na Wakristo. Tunapata muda mgumu kuona CCM inafanya makusudi kupandikiza chuki miongoni mwa wananchi na kuwagawa na hivyo kuhatarisha amani na kuvunja udugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 15 wa hotuba ya Kambi ya CHADEMA, umezungumziwa ubaguzi lakini wakati ule Kambi Rasmi ipo chini ya *CUF,* vyama vyote vya Upinzani vilipata nafasi ya uwakilishi kwenye kambi hiyo, tofauti na CHADEMA. Hii inatuonyesha pia kuwa huu ni ubaguzi unaoendeshwa na Chama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za CHADEMA ni kuwa *CUF* imejenga umoja na CCM hivyo ni CCM B lakini kuna *TLP*, *NCCR Mageuzi, UDP*, mbona havikuingizwa kwenye kambi hiyo? Hiyo ni dhahiri kuwa hata CHADEMA ni wabaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia sura za Wabunge wao wa Viti Maalum wapatao 25 wangeweza kugawanywa kwa misingi ya Mikoa au Kanda lakini sura kwa asilimia kubwa zimetoka upande mmoja. Hilo pia linatutisha kuona kuwa kuna aina fulani ya ubaguzi. Tunaitaka CHADEMA itoe kauli kwa nini ivitenge vyama vingine vya upinzani kwa kuvizushia vyama hivyo ni CCM B?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko ya Waislam kuhusiana na Mahakama ya Kadhi wakati Waislam wanasubiri kuundwa kwa Mahakama hizo kwa majaribio. Je, Serikali inasemaje kuhusu nafasi ya Waislam kuabudu hasa kwa saa za kazi, masomo au vikao hususan Ijumaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kesi za madai ambazo hufunguliwa katika Mahakama za Wilaya na kuendelea, inaonekana kuwa lugha inayokubalika katika kufungua kesi hizo ni Kiingereza. Je, Serikali haioni kuwa huo ni ubaguzi na pia kuidhalilisha lugha ya Kiswahili? Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya Kiswahili kiwe lugha rasmi ya kutumika katika kuandika kesi za madai?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kijiji cha Mtandi, Wilayani Kilwa, walijitolea mawe na mchanga ili kujenga Mahakama ya Mwanzo tokea mwaka 2003 na Jaji Samata aliahidi kusaidia ujenzi huo. Mwaka 2011, wananchi hao waliahidiwa tena kukamilishiwa ujenzi huo. Sasa tunamtaka Waziri atueleze ni lini Mahakama hiyo itajengwa ili kupunguza adha ya kwenda umbali mrefu kufuata Mahakama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Kilwa ambayo imeanza ujenzi wake, haikuonyeshwa katika Kitabu cha Bajeti ya Mheshimniwa Waziri ya mwaka 2012/2013 kuwa imetengewa fungu la fedha la kuimalizia. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa bado adha ya kutumia jengo lililokuwa la soko kama Mahakama haitaisha? Ni lini ujenzi wa Mahakama hiyo utakamilika?

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuanza kuwashukuru na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *AG, DPP, PCCB*, Mahakama na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, kitendo cha Mheshimiwa Chikawe (Waziri) kuteuliwa mara mbili kuitumikia Wizara hii, inamfanya Meshimiwa Waziri Chikawe afananishwe na "*general*" wa mapambano, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nilizozitoa kwa Wizara, naiomba Wizara ituletee Mahakimu wa ziada walau wawili kwenye Mahakama ya Wilaya ya Sengerema na walau Hakimu mmojammoja kwa kila Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo makubwa ambayo yanadhalilisha Mahakama zetu Tanzania, ni ucheleweshaji wa kesi katika Mahakama zetu. Jambo hili limekuwa likipigiwa kelele kwa muda mrefu na Mahakama zetu zinatambua changamoto hizo. Katika hili, narejea kwenye Hotuba ya Jaji Mkuu Mohamed Chande Othmani ya tarehe

3/2/2011 aliyoitoa katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamishwe kwa kuwa changamoto hii inafahamika, je, Serikali itachukua hatua gani au itatumia mbinu gani kuhakikisha kuwa changamoto hizi zimepungua? Ni wajibu wa Serikali kuelewa kwamba kuzifahamu tu changamoto bila ya kupatikana na utatuzi hatusaidii, bali kujua mbinu za kukabiliana na changamoto hizo ndio werevu. Kwa hili, naomba Serikali ione aibu. Suala la Mahabusu kugoma kula au kugoma kuchukuliwa katika magari yanayowapeleka Mahakamani kwa sababu ya kucheleweshewa kesi zao, ni aibu kwa Serikali na tukumbuke kuwa "*innocent until proven guilty*". Sasa inawezekana kabisa Serikali ikawa inawatia watu adhabuni ambapo mwisho wa hatma ya kesi zao wakaonekana hawana hatia. Je, inapoonekana kama hawana hatia wanapewa fidia gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la ucheleweshaji wa kesi haliwagusi watu wa chini tu, hata kesi kubwa ambazo zinagusa maslahi makubwa ya nchi nazo zinacheleweshwa. Hivyo tujiulize zinagusa maslahi ya nani ambaye anaonekana kwamba ataingia hatiani na hivyo alindwe ili asiingie hatiani? Ni kwa nini kesi hizi kubwa za ufisadi hazimaliziki? Kwa nini hatuelezwi zitaisha lini? Katika hilo, naomba nielimishwe, hivi kiongozi mwenye kinga Kikatiba dhidi ya Mahakama anawezaje kuwa shahidi wa utetezi wa kesi ya uhujumu uchumi katika nchi hii? Ni kwa nini na kwa misingi ipi? Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu sasa kuiondoa kinga hii kwa kuzingatia kwamba Watanzania wote ni sawa mbele ya sheria, binadamu wote ni sawa na binadamu wote hukosea, hakuna mwenye sifa ya Uungu. Ni

maoni yangu kwamba Watanzania watalizungumzia katika mjadala wa Katiba. Vilevile nawaomba Watanzania wajifunze historia za viongozi wengine wa Afrika na kwa ridhaa yao waiondoe kinga hii maana historia ni Mwalimu tosha wa maisha ya mwanadamu.

Mheshimiwa Naibu Mwenyekiti, wako ambao waliweza kutoa kauli za kwamba Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar yamepelekea Wanzanzibar kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano, napenda niwaeleze yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama si kwa sababu ya kuungana kwa Tanganyika na Zanzibar kusingekuwepo kwa Tanzania. Sura ya kwanza ya Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 2, nanukuu:-

*"Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kosa liko kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ukurasa 18, sehemu ya kwanza, Ibara ya 1 inasema, nanukuu:-

*"Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kujiuliza patakuwaje na nchi moja katika Jamhuri ya Muungano? Kama hakuna Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hakuna neno Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 4, sura ya pili, Ibara ya 9(1) ya Katiba ya Zanzibar inasema, nanukuu:-

*“Zanzibar itakuwa ni nchi ya Kidemokrasia na haki za kijamii”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara hii ni dhahiri kwamba kutakuwa na mambo ambayo yanathibitisha uwepo wa nchi ya Zanzibar na kuonyesha kwamba kuna mambo ambayo siyo ya Muungano yanapaswa kusimamiwa na Wazanzibar wenyewe na wala haiashirii Wazanzibar kuvunja Katiba, kwa nini Tundu Lissu hajasema kwamba kuwepo kwa Wizara 26, Wizara sita tu (6) ikawa ndizo za Muungano, 20 si za Muungano, hasemi kuwa kuna kasoro katika Muungano! Kwa kweli Tundu Lissu ni Mwanasheria aende tena kuisoma sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na madhumuni muhimu ya Sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yanasema katika Ibara ya 9(2)(a) na nanukuu:-

**“***mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali kufuatana na Katiba unatoka kwa wananchi wenyewe”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya nne, sehemu ya kwanza, ukurasa 16, Ibara ya 26 (1) ya Katiba ya Zanzibar inasema na nanukuu:-

*“kutakuwa na Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Mkuu wa nchi ya Zanzibar. Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ina Rais wake, ina Baraza la Mawaziri, kuna Watendaji Wakuu wa shughuli za

Serikali kama chombo cha kutunga Sheria, kuna Mahakama, leo iweje iambiwe kwamba imevunja Katiba ya Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya kumi, Idara Maalum, ukurasa 85, Ibara ya 121 (1) ya Katiba ya Zanzibar inasema, nanukuu:-

*"Kutakuwa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo kazi zake na shughuli zake zitakuwa kama zilivyoainishwa katika sheria zinazohusika.*

*(2) Idara maalum zilizoanishwa katika kijifungu cha (1) hapo juu ni:-*

*(a) Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU);*
*(b) Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM); na*
*(c) Chuo cha Mafunzo (cha wahalifu).*

*(3) Rais wa Zanzibar anaweza ikiwa ataona inafaa kuanzisha Idara nyingine yoyote kuwa Idara Maalumu".*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisema kuwa Wizara hii ni nyeti sana hivyo naomba iongezewe fedha za kutosha, kama ilivyo kwenye Wizara ya Elimu na Afya kwa sababu fedha zinazopelekwa kwenye Wizara hii hazitoshi kabisa, wakati kazi zinazofanywa na Wizara ni hi nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa Madaktari, naomba Majaji, Mahakimu na wafanyakazi wa Mahakama waongezewe mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba tena kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Aidha, pamoja na mambo mengine, nashauri Serikali iongoze juhudi katika kushughulikia kero mbalimbali zinazokabili sekta ya Mahakama nchini. Changamoto kubwa zilizopo ni pamoja na uchakavu wa majengo ya Mahakama mbalimbali nchini. Maeneo mengine Mahakama kama za Mahakimu Wakazi hazina Ofisi, wanachangia majengo na Ofisi za Wakuu wa Wilaya. Kuna uhaba wa vitendea kazi, Mahakama Tanzania zikiboreshwa, nina uhakika ustawi wa nchi hii katika sekta za kijamii, kiuchumi na kisiasa zitakuwa bora kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu ni kubwa kwamba kama haya yatafanyika hata msongamano wa Mahabusu katika Magereza utakwisha au kupungua kwa kiasi kikubwa. Aidha, kesi zitakamilika kwa wakati. Nashauri kabisa Serikali iwezeshe kiutendaji Mahakama za Tanzania. Kipimo cha ustaarabu ni pamoja na kuwa na Mahakama zinazotoa haki kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Mabadiliko ya Katiba, kwa kuwa Tume ipo katika mzunguko wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusiana na Katiba mpya, inatia shaka kama wananchi wanafikiwa ukizingatia mazingira na ukubwa wa nchi na kwa kuwa jambo hili ni la kihistoria, tuna imani wananchi wengi watapenda kushiriki zoezi hili. Hata hivyo, ratiba ya Tume haijawa shirikishi kwa wananchi kulingana na maeneo mbalimbali ya nchi yetu yalivyo. Mfano Tume inaweza kupanga ratiba maeneo ya wafugaji na wakati wafugaji watakuwa wanachunga mifugo yao. Je, uwakilishi wa wananchi katika utoaji wa maoni yao utakuwaje? Mfano mwingine Wilaya X, kuna msiba mkubwa na jamii husika yote ipo pale na wakati huohuo Tume ina ratiba ya kupokea maoni katika Wilaya X, je, Tume itafanyaje kuweza kupata maoni ya Wilaya X?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ushiriki wa wananchi katika utoaji wa maoni yao ni muhimu sana, je, kukiwa na idadi ndogo sana ya ushiriki wa wananchi katika eneo husika, je, Tume inafanyaje kupata maoni ya idadi kubwa ya wananchi katika eneo husika? Mfano Wilaya X inakadiriwa kuwa na idadi ya watu walio juu ya umri wa miaka 18 takriban 100,000 na walioshiriki kutoa maoni inakisiwa kuwa ni watu 5,000 tu, je, hatuoni kama idadi kubwa ya wananchi watakosa fursa ya kutoa maoni yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwezeshe Tume kutekeleza majukumu yake na ihakikishe imejianda kukabiliana na changamoto zilizo mbele yake. Tume ipange ratiba kulingana na eneo husika na shughuli za

kijamii katika eneo hilo. Hata hivyo, ni vema ratiba ya Tume iwe shirikishi, ili lengo la uanzishwaji wake liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Mahakama nchini, mazingira yanayomzunguka mtu ni njia mojawapo ya kumwezesha afanye yale yaliyotarajiwa kwa ufanisi mkubwa. Mahakama zetu na Mahakimu wake, wanafanya kazi katika mazingira magumu na ya ajabu sana kiasi cha kupelekea mhimili huu kunuka rushwa. Ikumbukwe pia si rahisi kutoa maamuzi ya haki kwenye mazingira magumu na hatarishi. Hali hii pia hupelekea Mahakama kuwa na mlundikano wa kesi nyingi na kesi kucheleweshwa hivyo haki kucheleweshwa. Miundoimbinu ya Mahakama zetu ni mibovu mfano baadhi ya Mahakama za Wilaya zinatumia majengo ya toka enzi za mkoloni hivyo kutokuwa na vyumba vingi vya usikilizwaji wa kesi na huwafanya Mahakimu kupeana zamu ya usikilizwaji wa kesi husika jambo ambalo husababisha mlundikano wa kesi. Maslahi ya Mahakimu ni vema yaboreshwe ikiwa ni pamoja na utoaji wa motisha na posho mbalimbali ikiwemo posho ya usafiri wa Hakimu anapotembelea vituo vingine kwa ajili ya usikilizwaji wa kesi. Umefika wakati wa kutenganisha kazi za Hakimu na masuala ya utawala. Hii itasaidia na kuwapa fursa Mahakimu kuzingatia kazi zao tu bila kujiingiza katika masuala mengine ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri miundombinu ya Mahakama zetu nchini iboreshwe na Serikali ni vema itafute fedha zaidi kwa kushirikiana na wadau ili kuboresha majengo na miundombinu ya Mahakama kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Mahakimu yaboreshwe na ni vema kuondoa *gap* kubwa la mshahara lililopo kati ya Mahakimu na Majaji na hasa ukizingatia Mahakimu ndio wanaokabiliana na kesi nyingi na ugumu mkubwa wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kujumuisha utawala na suala la kazi ya Hakimu ni bora/vema ubadilishwe ili kila mmoja atekeleze wajibu wake na hasa Mahakimu ili watende kazi yao kwa wakati na usahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria, Tume hii itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kupitia sheria zenye matatizo au upungufu na zile zinazokinzana na zilizopitwa na wakati kwa kuleta Bungeni ili zifanyiwe marekebisho lakini pia kutoa taarifa za utekelezaji wa majukumu yake kila nusu mwaka wa fedha wa Serikali katika Bunge.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuchangia bajeti hii kwa njia ya maandishi. Taarifa za Serikali zinaonyesha wingi wa mashauri yanayosubiri kusikilizwa kutokana na kutokuwepo watendaji. Nashauri maamuzi yafanyike kwa kuajiri Mahakimu kadri ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni vitendea kazi hasa majengo hii ikiwa ni pamoja na nyumba za kuishi na Mahakama zenyewe. Kwa upande wa Jimbo langu la Muleba Kaskazini, nashauri majengo ya Mahakama kule Machutwe yafanyiwe ukarabati ili yatumike. Pamoja na ukarabati, nashauri Kata ya Musabango ijengwe Mahakama ili kuweka huduma karibu na wananchi. Katika

kutekeleza uamuzi wa kuanzisha Mahakama hizi, suala la ukaribu wa wananchi lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri/nizungumzie utendaji wa Vyombo vya Dola na Mahakama. Imekuwepo hali ya Vyombo vya Dola kukiuka haki za binadamu katika kusimamia sheria. Wananchi wanatendewa kinyume na kunyanyaswa hali inayochafua taswira ya Serikali mbele ya umma. Mahakama iangalie namna ya kuzuia tabia hii kwa kusaidia vyombo vingine vinavyoshiriki katika kusimamia haki.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iongoze bajeti ya Mfuko wa Mahakama ili waweze kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwa ni majengo ya Mahakama pamoja na nyumba za Majaji wetu na Mahakimu ili waongeze ufanisi kwenye kazi zao. Tutakapowatengenezea mazingira mazuri, itawazidishia kufanya kazi zao kwa uadilifu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iangalie ni jinsi gani itawasaidia watuhumiwa wanaokutwa hawana hatia walipwe mara moja, mara wamalizapo kesi zao na kuwa huru. Hii itawasaidia watu hawa waweze kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba teknolojia ya *telejustice* ianze mapema ili kuipunguzia Serikali gharama na kusaidia kumalizika kwa kesi kwa wakati.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri hasa ukizingatia kazi kubwa

iliyoko mbele yao ya kuratibu na kusimamia Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Ni matumaini ya Watanzania itakapofika mwaka 2015 watapa Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niongelee fungu la fedha la Wizara hii halitoshi ndio maana maagizo mengi ya Kamati ya Katiba na Sheria na utawala yaliyotolewa bajeti iliyopita 2011/2012 hayakutekelezeka na hata mapendekezo kadhaa yaliyotolewa na Wabunge hayakuweza kufanyiwa kazi. Naiomba Serikali iiangalie Wizara hii kwani ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi. Iongozewe fungu kwa mwaka huu ili iweze kutekeleza majukumu yake muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ucheleweshaji wa kesi katika Mahakama bado ni sugu na unaleta msongamano mkubwa wa Mahabusu Magerezani. Naomba elimu zaidi itolewe kwa Majaji na Mahakimu ili kuhakikisha kuwa kesi zinasikilizwa pasipo kuchelewa na hukumu zitolewe kwa wakati badala ya kuwarundika watu Magerezani na kuitia Serikali hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye Mahabusu na Magereza za Watoto. Naungana na Kamati, ni kweli kabisa kuwa watoto katika Mahabusu na Magereza za Watoto hawapatiwi huduma nzuri kama vile chakula, matibabu na hata majengo yao yanatisha sana. Kwa mfano, Tanga tuna Gereza la Watoto liko barabara ya 14, hali yake hairidhishi kabisa. Mtoto ukimpeleka pale badala ya kumrekebisha ndio unamuangamiza kabisa, kiafya na kimaadili. Naomba Serikali ifanyie kazi hili kwani kizazi kipya

kitateketea kwani badala ya kufunda watoto waliopotoka kidogo tutawaangamiza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa watumishi walio wengi hasa Mahakimu yanatokana na maslahi duni na uhaba wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri. Mahakimu wako kwenye mtihani mkubwa kwani mafao yao ni duni na hawana vyombo vya usafiri hali inayopelekea kuhatarisha maisha yao na hivyo kushawishika kuchukua rushwa na kupelekea kutotenda haki Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa kuteuwa Tume ya Katiba na sasa imeshaanza kazi rasmi, ni matumaini ya Watanzania wote kuwa ifikapo mwaka 2015 tutakuwa na Katiba mpya Tanzania.

**MHE. SUBIRA K. MGALU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai unaoniwezesha kutimiza majukumu yangu kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Mahakama ya Mwanzo. Naipongeza sana Wizara kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa kukamilisha ajira 300 za Mahakimu Wakazi na kuwasambaza katika vituo vya Mahakama za Mwanzo katika Wilaya 102. Katika tangazo la kazi za Mahakimu Wakazi hao sifa ilikuwa ni Shahada ya Kwanza ya Sheria na amehudhuria Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(Law School)* kwamba ndio watapewa kipaumbele. Kipengele cha kuhudhuria Mafunzo ya Wanasheria kwa Vitendo kimewanyima fursa watoto wa Kitanzania waliotoka familia za kimaskini ambao wanahitimu Shahada ya Kwanza ya Sheria na kushindwa kuhudhuria Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo. Naomba Wizara itoe fursa sawa kwa wahitimu wa Shahada ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu kupunguza msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Magerezani, mwezi April 2012, nikiwa mjumbe wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Masuala ya Ukimwi, tulipata fursa ya kutembelea Gereza la Keko kuangalia hali ya mambukizi ya Ukimwi. Hali ya msongamano wa Mahabusu na Wafungwa wa Gereza hili ni mbaya sana. Cha kusikitisha, idadi ya mahabusu ni kubwa zaidi kuliko hata wafungwa. Kwa siku hiyo, Mahabusu walikuwa zaidi ya elfu moja na Wafungwa walikuwa chini ya thelathini na uwezo wa Gereza si zaidi ya watu mia tatu. Msongamano huu unatokana na ucheleweshaji wa kusikilizwa kesi Mahakamani na pia mwenendo wa uendeshaji kesi Mahakamani na hasa ucheleweshaji kutoa nakala za hukumu kuwezesha wahusika kukata rufaa. Naomba mikakati iliyoanishwa katika ukurasa wa 15 na 16 katika hotuba ya Wizara itekelezwe haraka ili kuondoa msongamano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uratibu wa upelelezi wa makosa makubwa ya jinai na uendeshaji wa mashauri makubwa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 20 – 22, yametajwa mashauri makubwa yakiwemo ya uhujumu uchumi. Hata hivyo, Wilayani Bagamoyo kuna kesi ya uhujumu uchumi inayohusu waliokuwa wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo akiwemo Mkurugenzi Mtendaji kwa kuisababishia hasara Halmashauri hiyo kwa kiasi cha zaidi ya shilingi milioni mia nane. Tangu watu hao wafikishwe Mahakamani kwa mara ya kwanza April 2010, kesi hiyo haijaanza kusikilizwa hata mara moja kwa miaka miwili sasa kesi hiyo kila mara inatajwa tu. Watumishi hawa wanaendelea kulipwa mishahara na Halmashauri inaendelea kupata hasara na wananchi wa Bagamoyo hawajui hatma ya pesa hizo zinazosemekana kupotea. Naiomba Wizara hasa Kurugenzi ya Mashtaka kutenda haki kwa wananchi wa Bagamoyo kwa kuwezesha kesi hii kuanza kusikilizwa ili pande zote mbili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iipe kipaumbele Wizara hii kwa kutenga bajeti ya kutosha ili iweze kukamilisha majukumu yake ipasavyo katika kufikia malengo yake ya dira na dhima. Aidha, dira ya Wizara hii ya kutoa haki sawa kwa wote na kwa wakati ni changamoto zama hizi za Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kufikia dira na dhima yake, Wizara hii inahitaji

mafungu ya kutosha kwa Idara na Taasisi zake ili ifanikiwe kuondoa mlundikano wa kesi, msongamano wa mahabusu, rushwa na ubambikizaji kesi, uhaba wa majengo na vitendea kazi, upungufu mkubwa wa rasilimali watu na ufinyu wa rasilimali fedha. Miundombinu za Mahakama za Mwanzo kukosekana na hata pale penye majengo marekebisho yake yanashindikana kwa ufinyu wa bajeti na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni sura ya Mahakama zetu na Wizara kwa ujumla. Wananchi hukata tamaa na mara nyingine huamua kujichukulia sheria mkononi. Nasisitiza Serikali itenge bajeti ya kutosha ya mwaka 2013/2014 ikiwezekana mara tatu ya bajeti ya mwaka huu na Wizara hii iwekwe katika orodha ya Wizara za kipaumbele kwa mwaka 2013/2014 - 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bajeti nne mfululizo, Wizara iliahidi kutenga mafungu kwa ajili ya marekebisho ya Mahakama za Mwamagembe na Ukimbu (Kayui) na pia Mahakama ya Wilaya ya Manyoni lakini kwa mara zote hakuna kilichotekelezwa. Napenda kujua kama Mahakama hizi za Mwanzo za Mwamagembe na Ukimbu safari hii 2012/2013 zitajengwa au kufanyiwa marekebisho. Aidha, napenda kujua nini kitafanywa kwa Mahakama ya Wilaya ya Manyoni kama nayo itarekebishwa. Mahakama za Mwamagembe na Ukimbu, ziko Tarafa ya Itigi, Wilaya ya Manyoni. Aidha, napenda kujua ni lini Mahakama mpya kwa ajili ya Kata za Idodyandole, Aghondi, Ipande, Rungwe na Sayaranda zitajengwa ili kuwapa nafuu wananchi wasiendelee kwenda mbali kutafuta haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanahangaika kupata vyeti vya uzazi, vifo kutokana na umbali wa Makao ya Wilaya ambako *DAS* hutoa vyeti hivyo na vile vya ndoa. RITA ifanye utaratibu kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kuona uwezekano wa kuifanya huduma hii muhimu kwenye Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakala za hukumu za kesi zinazotolewa na Mahakama bado ni kitendawili na mara nyingi zimetumika kama chambo cha rushwa na mahangaiko kwa wananchi wanaotaka kuendelea kutafuta haki pale wanapopenda kukata rufaa. Naishauri Wizara ilimalize tatizo hili sugu kwa kuzitaka Mahakama ziwe wazi kwenye hili vinginevyo litazidi kuipaka matope kwamba Serikali inakumbatia rushwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha ila nipatiwe majibu ya kuridhisha ili niache usumbufu wa kusimama kwenye Kamati ya Matumizi.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria, ni Wizara nyeti hasa wakati huu tunapoelekea kutengeneza Katiba Mpya. Katiba ndio sheria mama ya nchi na mara nyingi machafuko katika nchi yametokana na ukiukwaji wa Katiba. Ninaamini Tume ya Katiba itafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara hii kuwa na maeneo mengi lakini imepewa siku moja jambo linalofanya uchangiaji mdogo sana, hasa ikizingatiwa inahusu mhimili wa *Judiciary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais kwa uteuzi wa Majaji wengi ili kupunguza tatizo la ucheleweshaji wa mashauri ambapo ilikuwa ni kero kwani *'justice delayed is justice denied'* hivyo tunaomba ongezeko hili la Majaji liwe chachu ya kumaliza *cases* kwa haraka. Pamoja na jitihada za Rais, kumekuwa na taarifa kuwa baadhi ya Majaji wanashindwa kuandika hukumu na kwamba utaratibu wa Kikatiba wa mchakato wa sifa za Jaji hazifuatwi. Jambo linalotia dosari mhimili huu nyeti wa haki za Watanzania. Ni vema Serikal ifuate utaratibu wa kikanuni uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msongamano wa mahabusu, ni tatizo kubwa na halikubaliki kwa nchi inayodai ni ya kidemokrasia. Demokrasia ni pamoja na kutoa haki na kinachosikitisha, wengi wa mahabusu kimsingi mashauri yao ni ya kubambikizwa na mengine yalipaswa yapatiwe adhabu za nje tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kuona kuwa pamoja na kuwa na wahitimu wengi wa sheria, bado tuna upungufu wa watumishi, yawezekana tatizo hili linachangiwa na wanafunzi wa *Law School* kukosa udhamini *(loan)* wa masomo hayo. Huko nyuma tulielezwa kuwa *Law School* ni *option* na kwamba wanaopenda kuwa *Goverment Attornery* ndio wanaowajibika kusoma. Kimsingi *Law School* yapaswa kuwa *compulsory* ili kila mwanafunzi wa sheria apate uzoefu wa kazi za kisheria zaidi. Ni mategemeo yangu kuwa Wizara itatenga fedha kwa ajili ya kuwadhamini wanafunzi ili kuondoa tatizo la Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuwa Tanzania bado tuna hukumu ya kifo yaani *'death sentence'* kwa miaka

mingi. Lakini tunaitambua kwa miaka mingi toka Awamu ya Pili hakuna 'mkosaji-muuaji '*murder*'aliyeuawa. Hali hii imepelekea wafungwa hawa kuishi kwa wasiwasi mkubwa '*psychological tention'* na hata ukiwaona wanasikitisha na hata kuomba ama wauawe kama sheria inavyosema au wasamehewe na kupewa adhabu nyingine.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji elimu ya sheria kwa wananchi wetu ni muhimu ili wapate kuzielewa. Imebainika kwamba wananchi wengi hawana uelewa wa sheria za nchi yetu na hasa zile zinazowagusa moja kwa moja hivyo kusababisha kukosa haki zao za kimsingi. Hivyo naishauri Wizara kuandaa mpango mkakati wa kutoa elimu ya sheria kupitia kata, vijiji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya Kiswahili katika sheria zetu. Ni kipindi kirefu Serikali imekuwa ikichapisha vitabu vyake vya sheria kwa lugha ya Kiingereza, lakini wananchi wengi na hasa wa vijijini wamekuwa wakipata tabu katika kutafsiri lugha hiyo. Hivyo, naishauri Wizara kujitahidi kuchapisha sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa maoni katika Tume ya Mabadiliko ya Katiba, nimesikia kwamba katika mikutano ya utoaji wa maoni inayoendelea hapa nchini, kunakuwa na uvamizi wa wananchi wasio wakaazi katika maeneo hayo hivyo kunapelekea kuwasemea wananchi wa hapa pasipo ridhaa. Hivyo naishauri Wizara kuiarifu Tume ya Kukusanya Maoni ya Katiba, ni vyema wakati Tume ikifika katika eneo wakaulizwa wananchi wenyewe

kuwa mkusanyiko huo ni wananchi halali na ndipo kazi ainze.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ucheleweshaji wa kesi hata ambazo tayari mshindi amefanikiwa mpaka Mahakama ya Rufaa. Kuna kesi zinaendeshwa mpaka zaidi ya miaka kumi na tano na mara nyingi wanaokuwa wanafanyiwa urasimu ni wazee ambao umri wao umesogea sana hivyo Mahakama zinaona zicheleweshe ili wazee hao wakose haki zao. Mfano mzuri ni Mahakama ya Kanda Kuu Tabora, kuna kesi toka mwaka 1996 - 1998 mpaka leo hazijakwisha ilihali maamuzi yametoka na Mawakili wanafanya *delaying tactics,* wazee hawa wanazilaani Mahakama kila siku ya Mungu na inawezekana laana hizi ndio Mahakama nyingi zinasuasua. Je, Waziri atakuwa tayari kuunda Tume itakayohakikisha kesi zote ambazo zinatakiwa ziwe zimekwisha kwa muda mrefu ila zinacheleweshwa makusudi zinashughulikiwa kwani kwa kufanya hivyo Mheshimiwa Waziri utabarikiwa duniani na kesho akhera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki ya Binadamu na Utawala Bora, ni muda mrefu sana tumekuwa tukilalamikia Tume ya Haki za Binadamu, kunyimwa meno na hivyo kubaki inatoa *recommendations* tu. Je, ni lini Tume hii itapewa meno na kutokuwa *ruber stamps*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi za mauaji ya Albino, Je, Serikali inaweza kutuambia mpaka sasa imeshahukumu kesi za mauaji ngapi ya albino na ni watu wangapi wamekutwa na hatia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watanzania wengi wanadhulumiwa haki zao hususani walioko vijijini na hii ni kwa kutojua sheria. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu ili iweze kufika maeneo mengi ya vijijini lakini pia kuziwezesha hizi *small units paralegal* waweze kusaidia eneo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara midogo ya Wanasheria wa Halmashauri zote nchini, hii inavunja moyo sana na wakati mwingine kusababisha Wanasheria wengi kuhamia maeneo yenye maslahi na hivyo Halmashauri kukosa Wanasheria mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni kuiomba Serikali ianzishe haraka Mahakama ya Kadhi kwa kuwa sheria zetu baadhi zinapingana na maadili ya Kiislam na hii inawanyima haki Waislam walio wengi, hususani kwa wale wanaoamini juu ya *Islamic Law.* Mfano, Sheria ya Mirathi, Sheria ya Ndoa na masuala ya talaka. Moja ya sheria zenye upungufu mkubwa ni ile ya *Presumption of marriage* kwamba ukikaa na mwanamke au mwanamme kwa zaidi ya miezi sita, hiyo inahesabika kama ndio mke na mume, lakini katika mfumo wa dini, kitendo hiko ni zinaa. Sasa katika mwingiliano kama huu, *Islamic Societies* zinataka *Islamic law of marriage,* I- *prevail* hivyo ni vyema kuanzisha Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika masuala ya talaka, katika *Uislam* mwanaume akitamka tu inakuwa ni sheria lakini katika mfumo wa Mahakama ni lazima kuwe na *document,* yote hii inanyima fursa kwa jamii hii kuweza kuishi *according to their believe*.

**MHE. LUCY P. OWENYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshwaji wa kupata nakala ya hukumu. Napenda kujua ni kwa nini inachukuwa muda mrefu kupata nakala ya hukumu baada ya kukata rufaa? Hii husababisha matatizo makubwa kwa wahusika kupata haki zao hata wengine kushindwa kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tujuavyo 80% ya wananchi Tanzania wanaishi vijijini na kule vijijini usafiri wa uhakika haupo, inabidi watu watoke mbali mpaka Wilayani kufuata Mahakama ya Mwanzo. Kwa mfano, kule Old - Moshi, mdai inabidi aende mpaka Moshi Mjini kwa masuala ya Mahakama ya Mwanzo. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama za Mwanzo kulekule vijijini? Kwa kuanzia hata kikanda ili kuwapunguzia wananchi matatizo wanayopata kwenda mpaka Wilayani kupata huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kikatiba ni haki ya kila mwananchi kuzielewa sheria za nchi na wakizielewa itakuwa ni rahisi kwao kuzifuata lakini sheria zetu zimeandikwa kwa lugha ya Kingereza ukizingatia wananchi wengi wanajua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kuandaa sheria zote kwa lugha zote mbili Kiswahili na Kingereza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi, pamekuwepo na malalamiko mengi kuwa wanaoendesha Mabaraza haya huko vijijini, wengi hawana uwezo kabisa na wanapokea hongo na kunyanyasa sana wananchi. Kwa kuwa Wizara ya Katiba na Sheria ndio yenye jukumu la kusimamia sheria na ndio Wizara yenye wataalam, ni jambo la busara kwa Mabaraza ya Ardhi kuhamishwa au yawe chini ya Wizara ya Katiba na Sheria badala ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wao kwa hotuba yao. Naunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani kwani yana lengo la kuibua mjadala juu ya namna bora ya utoaji haki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika maeneo machache, nitaanza na suala la lugha katika Mahakama. Suala hili lina sura mbili, ya kwanza inahusiana na Taarifa zilizotolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu kushuka kwa kiwango cha ubora wa uandishi wa kumbukumbu za Mahakama na hata ripoti za hukumu zinazoandikwa kwa Kiingereza. Tatizo linaonekana kuwa, Majaji au Mahakimu ama hawana stadi za kutosha za uandishi au kiwango chao cha Kiingereza hakitoshi au yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni muhimu kumbukumbu zote na ripoti zote ziandikwe kwa lugha safi, sahihi na nyofu kwa ajili ya rekodi za mashauri na hukumu ili ziwe na marejeleo tegemevu kwa watu mbalimbali, nashauri Mahakama zichukue hatua za haraka za kuwa na

wataalam wa lugha ya Kiingereza ili wafanye kazi ya kuhariri baadhi ya kumbukumbu na ripoti zote. Lazima hili lifanyike ili tuondoe aibu ya kuwa na Mahakama ambazo hukumu zake nyingi hazieleweki sawasawa kwa kuwa hazikuandikwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kiingereza kinaendelea kutumika katika Mahakama kwa kuweka kumbukumbu na ripoti za hukumu, jambo hili lazima liangaliwe kwa makini na kupata ufumbuzi. Vinginevyo kwa kuzingatia sera ya matumizi ya Kiingereza katika Mahakama zetu, labda Majaji au Mahakimu wathibitishwe kuwa wanaweza kuandika kwa Kiingereza kabla ya kuteuliwa katika nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la lugha lina sura nyingine. Tunaweza kujiuliza kwa nini mpaka sasa, miaka 50 baada ya uhuru bado tunatumia Kiingereza katika Mahakama zetu? Tunayo lugha yetu ya Taifa ambayo wataalam wote na watendaji wote huitumia vizuri, uamuzi wa kutumia Kiswahili katika kuandaa Miswada ya Sheria, kuandika kumbukumbu na ripoti za shughuli za Mahakama kutarahisisha mchakato wa utoaji haki kwani kumbukumbu na ripoti zitakuwa sahihi na Majaji au Mahakimu hawatapata tabu katika uandishi wa ripoti. Baadhi ya nyaraka ambazo zitahitajika kutafsiriwa kwa Kiingereza, wapewe wataalam wa tafsiri kwa manufaa ya watu wasiojua Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee suala la adhabu mbadala. Adhabu mbadala kwa mhalifu aliyehukumiwa Mahakamani inamhusu mtu aliyepata adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitatu pamoja na faini

au bila faini. Adhabu mbadala yenyewe, kwa mujibu wa Sheria ya Huduma kwa Jamii ya mwaka 2002, Ibara ya 3(2) (a) na (b), ni “huduma kwa jamii” inayojumuisha kazi za ujenzi, upandaji miti, uhifadhi wa mazingira, usafi na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa ya adhabu mbadala ni kuwa itasaidia kupunguza msongamano katika magereza yetu. Tangu sheria ipitishwe na kusainiwa na Rais miaka kumi iliyopita. Mheshimiwa Raisi Kikwete alishahimiza Mahakama kuanza kufanya mipango ya kutekeleza sheria hii, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, je, Wizara imeandaa utaratibu gani wa utekelezaji wa sheria hii? Naomba atakapokuja kufanya majumuisho atufahamishe hatua iliyofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea kidogo kuhusu hali tete ya uadilifu katika utoaji haki katika Jimbo la Bukombe. Bukombe iko pembezoni na watu wengi wakaao vijijini hawajui kusoma na kuandika, au hata kama wanajua wana hofu kubwa kuhusiana na chombo cha utoaji haki cha Mahakama. Watumishi (Mahakimu) wasio waadilifu mara nyingi hutumia ujinga na wananchi ili kujinufaisha wenyewe. Malalamiko ambayo sisi tunapata yanahusu ucheleweshwaji wa mashauri ambayo hupigwa tarehe ya mbele mara nyingi kabla ya kuamuliwa. Pia wenye mashauri huishi na hisia ya hofu kwamba haki haikutendeka. Je Serikali imejiandaaje ili kuboresha hali ya utoaji haki kwenye ngazi ya vijiji kwa kuwa huko watu hawajui haki zao? Naomba jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongeza za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Idara na kadhalika wa Wizara husika kwa kazi nzuri na jitihada zao za kuboresha Sekta ya Sheria nchini, kimuundo, kimiundombinu na kitaaluma kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi napenda kuchangia maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni faraja kubwa kuona Wizara imejipanga kuhakikisha kuwa ifikapo Aprili, 2014 Katiba mpya itakuwa tayari imekamilika. La msingi ni kwa Serikali kuwapatia Wizara fedha za kutosha ndani ya Bajeti ili kweli dhamira njema ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Katiba mpya itimizwe. Kwa upande wa wananchi hao wanawajibika kutoa ushirikiano wakati wa kutoa maoni kwa Tume husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba imetoa fursa ya makundi mbalimbali ya wananchi kuweza kutoa maoni yao kwa uwazi na uhuru kwa Tume. Hata hivyo, nataka kupata ufafanuzi ni jinsi gani Tume imejipanga kuwezesha watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali kumudu kuweza kutoa maoni hayo mbele ya Tume kwa mfano, kwa upande wa Viziwi, ambao hutumia lugha ya alama kwa ajili ya mawasiliano, je, Tume imeandaa wakalimani wa Lugha ya Alama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wenye ulemavu wa uoni hafifu, hasa *Albino* na wale wasioona, je, katika maandalizi ya programu za kuelimisha umma Tume ya Mabadiliko ya

Katiba imejiandaaje kwa suala la matumizi ya maandishi ya nukta nundu kwa wenye ulemavu hawa ambao nao ni haki yao kutoa maoni yao kama ilivyokuwa kwa Watanzania wengine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana ufafanuzi na endapo masuala hayo hayakuwa yamezingatiwa na Tume bado hatujachelewa sasa, yazingatiwe kikamilifu kwani Katiba ndiyo inayoongoza mustakabali wa Taifa. Hivyo ni muhimu kupata maoni toka kila kundi la wananchi kama Sheria husika ilivyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kuwezesha wenye ulemavu kutoa maoni kutokana na aina ya ulemavu wao lisiishe tu kwenye uundwaji wa Katiba mpya bali hata kwenye uendeshaji wa mashauri katika Mahakama ya ngazi mbalimbali kwa mfano, Kiziwi/bubu akishtakiwa au kushitaki Mahakamani inamwia vigumu kujieleza kwa kusema mpaka apate msaada wa Mkalimani wa lugha ya alama. Vinginevyo mhusika kama huyo anaweza akakosa haki kwa kushindwa kujieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni umuhimu wa Wizara kuongeza kasi ya kuendesha mashauri mbalimbali Mahakamani ili kutoa hukumu, hivyo kupunguza mlundikano wa mahabusu katika Magereza nchini. Magereza yetu yana mahabusu wengi kuliko uwezo wa magereza yenyewe, jambo ambalo linaigharimu Serikali fedha nyingi kwa ajili ya chakula, matibabu na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuunda Idara itakayoshughulika na masuala ya mikataba. Kwa vile kwa muda mrefu mikataba tunayoingia na

wawekezaji imezua migogoro mingi nchini, sasa nina uhakika migigoro hiyo itakwisha kwa sababu Wizara sasa itasomesha wataalam wa masuala ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchanganuo huu, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kwapongeza Mheshimwa Waziri Chikawe na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kushika nafasi zao katika Wizara hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na yenye maelezo ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kutamka kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, naunga mkono maoni ya Kamati kama ilivyosomwa leo asubuhi, ufuatao ni mchango wangu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Katiba; nampongeza Mheshimiwa Rais kuunda Tume na hatimaye Tume imeshaanza mashauri kama ilivyopangwa na ihakikishe kwamba maoni ya wananchi yanapokelewa bila hila au ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa majengo Mahakama na watumishi katika Wilaya nyingi hakuna majengo ya Mahakama za Mwanzo na hata kama yapo majengo yamechakaa sana mfano Wilaya ya Mbulu. Aidha, Mahakama nyingi hazina Mahakimu, Makarani na wapiga chapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa Mawakili, wananchi wengi haki zao zinapotea kwa sababu hakuna Mawakili. Nashauri Leseni za Mawakili, zitolewe kwa kusambaza huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usajili wa watoto na vifo; vyeti vya kuzaliwa vinapatikana kwa shida, elimu kuhusu shughuli za *RITA* inahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu idadi ya Majaji na Mahakimu kuondoa mlundikano wa Mashauri, nashauri Majaji na Mahakimu waongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Para Legals;* ili kuwasaidia wananchi wapate msaada wa kisheria kwa urahisi, nashauri Sheria ya Mawakili irekebishwe ili watu ambao wana diploma au vyeti vya Sheria waruhusiwe kuwakilisha washtakiwa wadaiwa Mahakamani au Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashauri mchakato wa kuwaingiza watumishi wasio Mahakimu au Majaji ukamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri mafunzo kwa watumishi wote wa Mahakama wakiwemo Majaji na Mahakimu yatolewe mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ucheleweshwaji wa Mashauri, justice *delayed is justice denied*, mara kwa mara mashauri yanachelewa hadi miaka 10, mashauri yanachelewa sana jamii inaingizwa kwenye chuki za kudumu.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuwapongeza Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe; Naibu Waziri Mheshimiwa Angela Kairuki; Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha hotuba hii ya bajeti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa masikitiko kwa ucheleweshaji wa Sheria zilizopitwa na wakati zinazowahusu wanawake na watoto. Ningeomba kwa kweli Serikali inapojibu hoja hizi itueleze ni sababu gani hasa za msingi zinazofanya sheria hizi zisirekebishwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi sana wananyanyasika kwa sababu pia ni kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha wa kujua sheria zao. Naomba Serikali itamke wazi ni chombo gani kinachopaswa kumuelimisha mwanaume. Bado kuna mila na desturi potofu ambazo zinawakandamiza wanawake, je, Serikali hailitambui jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali itambue kuwa Mahakama zetu rushwa imetawala, bila pesa hakuna haki, sheria zinapindishwa, hivi kweli Serikali haijui jambo hili. Je, hakuna mkakati wowote wa kuunda chombo cha kudhibiti hizi rushwa katika vyombo vya Mahakama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wazi wiki hii katika vyombo vya habari vikimnyanyapaa yule mwanamke aliyezaa na Mhindi kupokonywa haki ya kulea mtoto wake wa miezi minne tu wakati sheria ipo wazi kwa ajili ya hilo. Hivi kweli Serikali inaacha vyombo hivi vipotoshe sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tu tumesoma katika vyombo vya habari yule mwanamke aliyeteswa na mumewe na kuburuzwa katika gari na kung'olewa sikio, amepoteza maisha na huku yule aliyesababisha maafa hayo akiachwa bila kukamatwa, inauma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuteua Majaji wengi wanawake ametujengea heshima kubwa sisi wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo ambalo nilichangia katika bajeti iliyopita ni kuhusu mashauri ambayo yalipelekwa Mahakamani hasa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kusikilizwa na Jaji mmoja au Majaji watatu katika mashauri yanayohitaji kusikilizwa na kuamuliwa na Jaji mmoja hakuna tatizo lakini, shauri linalohitaji kusikilizwa na Majaji watatu hapo lipo tatizo kubwa kweli kwa sababu inapotokea huwa si rahisi kuwapata Majaji wote watatu kwa wakati mmoja, shauri husika haliwezi kusikilizwa kila linapotajwa ili kuweza kupatikana kwa Majaji wote watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wangu mdogo unaonesha kuwa mashauri ya Tume hiyo hayafiki mwisho wala kwa wakati unaotarajiwa na Wanasheria wenyewe wanasema *justice delayed is justice dinied*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nashauri Mheshimiwa Waziri anayeleta Muswada wa kurekebisha Sheria hiyo ya Majaji watatu ili awe Jaji mmoja kama suala ni Sheria ndogo (*subsidiary legislation*) zinazotungwa na Mheshimiwa Waziri au kama suala husika lipo chini ya Jaji

Mkuu, basi Mheshimiwa Jaji alifanye ili mashauri husika yasikae muda mrefu yawe yanafika kwa muda uliopangwa.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji kwa maandalizi ya hotuba na kwa namna ilivyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Majaji na Mahakimu kuanzia Mahakama za Mwanzo ni nyeti na kwa namna ya kazi zao (*nature*) hawa watu wanastahili kupewa stahili kama vile nyumba, usafiri na kadhalika. Hivi kama Hakimu anaishi ndani ya nyumba ya kupanga na watu wengine katika nyumba ya mtu binafsi, anasafiri kwa usafiri wa daladala au bodaboda na huyo huyo anasikiliza na kuhukumu kesi unatarajia yeye atende haki gani. Je, usalama wake uko wapi au basi afanye kazi kwa woga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo utaratibu wa kada hii ya watumishi iangaliwe na kupewa umuhimu ili watende kazi ya kutoa haki lakini pia walindwe kwa usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mahabusu linatia huzuni sana, wamerundikana sana katika Magereza yetu kuliko uwezo wa majengo yenyewe, ni kwa nini basi hukumu hazitolewi mapema ili kifungo kianze kutumika mara moja? Kuwaweka muda mrefu mahabusu mbali ya

kupata mafunzo wengi wao wanapata magonjwa ya kuambukizwa mwisho wa siku ni Serikali ile ile inapata hasara ya kugharamia magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Law School* limekuwa ni tatizo kubwa tena lenye kulalamikiwa sana. Kutokana na hali ilivyo hivi sasa wahitimu wengi wa Vyuo Vikuu wa Kitivo cha Sheria wamekuwa wakishindwa kujiunga na *Law School* ili kutimiza ndoto zao za kuwa wanasheria kutokana na sheria ya mikopo yao. Je, ni kwa nini basi isirudishwe kama zamani kwamba watu wakihitimu Shahada ya Sheria wafanye kazi hiyo ama ya Uhakimu au Uwakili bila kupitia Law School? Ningeshauri yaongezwe hayo masomo ya *Law School* kwenye mitaala ya Vyuo Vikuu ili kuondoa utata huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii katika maeneo ya Mahakama, msongamano wa mahabusu Magerezani, Tume ya Ukusanyaji wa maoni ya Katiba, uvunjwaji wa Sheria na Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu wa Mahakama katika nchi yetu pamoja na rasilimali watu kitu ambacho kinapelekea kesi nyingi kuchukua muda mrefu sana na hii inavunja haki za binadamu na sheria ya nchi hii. Kwanza upelelezi kwa ngazi ya Polisi inachukua muda kinyume na muda halisi uliowekwa kisheria na hii yote inatoa mwanya kwa Polisi kuomba rushwa kwa visingizio wanafanya *overtime* ili kuwa-*frustrate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si sawa na ukosefu wa utawala bora. Vile vile kumekuwepo na uhaba wa Wanasheria katika kanda ambao wanakuwa *overwhelmed* na mafaili ambapo inachukua muda hata zaidi ya miezi sita. Vile vile hata Mahakama zetu hazina rasilimali watu wa kutosha na majengo ni mabovu. Naomba tuangalie huu mhimili kwa umuhimu wa uhakika wa kutoa haki kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na wimbi kubwa la ubambikizaji kesi wananchi kwa sababu tofauti, mfano, sababu za kisiasa, fitina na katika kutafuta hela (yaani kuhongwa). Kazi kubwa ya ubambikizaji kesi imekithiri katika Mkoa wa Kipolisi wa Tarime/Rorya. Unakuta vijana au wazee ambao ni nguvu kazi ya Taifa hili wanakamatwa kwa mfano, kwa kosa la uzururaji, kisha huambiwa watoe fedha kuanzia Sh. 200,000/= hadi 3,000,000/=, wananchi hawa wakikosa fedha hubadilishiwa kesi na kuwa *murder* au *armed robbery*. Kesi ambazo huchukua muda mrefu sana na mwisho wa siku wengi wao huachiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si haki kabisa na pengine unakuta wananchi wanabambikizwa kesi kisa, visa vya kisiasa na baadaye hubambikwa *murder* au *armed robbery*. Wakati mwingine wanabambikiwa kesi kisa chuki au fitina za kimapenzi. Naomba sana hili la ubambikaji kesi za jinai ambazo hazina dhamana liondolewe kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo lingine ambalo linasababisha msongamano wa mahabusu gerezani kwa sababu kuna kesi ambazo zina dhamana za wazi, lakini unakuta wananyimwa dhamana kitu ambacho si haki na kinyume na sheria. Hii pia inapelekea mwanya wa kuomba

rushwa, sababu mtu anakosa, mfano kosa la kutukana mtu; huyu anakosa dhamana. Hivyo, tunaomba sana hili liangaliwe vizuri ili tuwatendee haki wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna unyanyasaji mkubwa kwa watuhumiwa ambao unakuta wametii sheria ya kukamatwa bila shuruti, lakini wanapigwa sana hadi wengine wanakufa, wengine wanakuwa walemavu au wanahasiwa hii sio haki kabisa. Napenda kupata utatuzi kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kutoa mapendekezo yangu kwenye Tume ya kukusanya maoni ya Katiba, muda wa ratiba zao hazikidhi matakwa ya kuwafikia Watanzania wote. Kwa jinsi ilivyo sidhani kama tutakuwa na *representation* ya kutosha. Vile vile napinga dhana nzima ya kupokea maoni kwa njia ya barua. Hii haitatoa uhalisia kwani kundi la watu laweza kuketi na kuandika maoni hata zaidi ya mmoja. Hivyo nashauri sana hili tendo la kupokea maoni kwa njia ya barua, si njia muafaka kabisa kwa mustakabali wa mabadiliko ya Katiba.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Katiba na Sheria ni muhimu sana katika kuongoza na kulinda haki za binadamu. Pia kwa kuwa sasa hivi Tume ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba tayari imeanza kazi yake na wananchi wanatakiwa kutoa maoni yao juu ya mabadiliko ya Katiba ili kupata Katiba mpya yenye kulenga mahitaji ya wananchi wa Tanzania. Ili wananchi waweze kuchangia hoja zao, napenda kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Katiba iliyopo kuchapishwa na kugawia wananchi ili waweze kusoma na kujua ni mambo gani yabadilishwe na mambo gani yaongezwe au kupunguzwa;

(ii) Wananchi wafanye mikutano ya hadhara kufundishwa maana ya Katiba na mambo mengine yanayotakiwa kuwemo katika Katiba; na

(iii) Wananchi wajue kuwa Katiba ni yao wenyewe, kwa hiyo, wana wajibu wa kushiriki mijadala yote ya Sheria ya mabadiliko ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kusema Katiba mpya ni muhimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kushika wadhifa huu kwa mara ya pili na pia kumpongeza Naibu Waziri kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo. Halikadhalika nampongeza Katibu Mkuu na Viongozi au Watendaji wote katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iongeze bidii kwa kufikisha Katiba ya nchi yetu kwa wananchi haraka iwezekanavyo ili waweze kuisoma na kujua nini wafanyie marekebisho kwani wananchi kupata Katiba ni haki yao ya msingi. Je, ni lini Katiba hiyo itafika kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vipi Serikali inaweza kuweka au kutunga sheria ambayo itamlinda mgonjwa na pia kulinda haki za mama mjamzito na watoto. Tumeona ni vipi wanadhalilika toka anapopata ujauzito hadi kujifungua kwani kuna wanaonyanyaswa au kuteseka katika kipindi hicho. Naomba nipatiwe maelekezo ni vipi Sheria au Katiba inaweza kuwalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la ucheleweshwaji wa kesi, naomba iongezwe bidii. Vinginevyo, naipongeza Wizara kwa kujenga Mahakama kwenye baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na timu yake yote kwa bajeti ya Wizara yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Aidha, ningependa kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambulisho wa umri wa mtoto katika Sheria za Tanzania unakinzana kwa kiasi kikubwa na hivyo kusababisha watoto wengi kukosa haki za msingi ambazo wanastahili kupata wakiwa kama watoto. Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inatoa fursa kwa mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri kuanzia miaka kumi na tano na Mahakama inaweza kuruhusu mtoto wa kike mwenye umri usiopungua miaka 14 kuolewa. Sheria hii kimsingi inamnyima haki za msingi mtoto wa kike na kuwafanya watoto wengi wa kike hususan waliopo vijijini, wasio na uwezo na watoto yatima kuishia katika ndoa za utotoni na hivyo kushindwa kuendelea na shule ili kujenga maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, Wizara ya Katiba na Sheria ifanye uchambuzi wa Sheria zote zinazosimamia haki za watoto ili umri wa mtoto wa kike uwe ni miaka chini ya kumi na nane kama inavyotambulika chini ya Sheria ya Makosa ya Kujamiana ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki za mtoto, mirathi na matunzo, sheria zinazosimamia mirathi zimeweka masharti mbalimbali ambayo yanamzuia mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa kutoweza kupata urithi, mpaka awe amehalalishwa kwa kufuata desturi au taratibu zinazojulikana na kutambulika katika jamii hiyo. Utaratibu huu unawanyima haki watoto wa namna hii pindi upande wa baba unapoamua kutowahalalisha ndani ya ukoo. Kwa kuwa vipimo vya kisayansi vinaweza kuthibitisha baba wa mtoto ni nani, naishauri Wizara ya Katiba na Sheria ifanye mapitio katika Sheria za mirathi ili kuondoa vipingamizi vya aina hii vinavyowanyima haki watoto wa nje ya ndoa ambao nao wanahitaji huduma zote muhimu kama watoto ili kuwawezesha kukua katika maisha na elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha pamoja na kwamba watoto wote wanastahili haki sawa kwa kuwa wote kama binadamu wana mahitaji sawa, utaratibu wa kupata fedha za matunzo baina ya watoto waliozaliwa ndani ya ndoa na watoto wa nje ya ndoa ni tofauti.  Kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa, wazazi watatumia sheria iliyojumuishwa, wakati watoto halali watatumia Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ili kudai haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto kama raia mwingine yeyote anastahili haki kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri wa Tanzania ambapo Ibara ya 12 inatambua kwamba watu wote ni huru na sawa na Ibara ya 13 inatambua aina yoyote ya ubaguzi wa rangi, jinsi, kabila, imani au hali ya kiuchumi, muungano wa kisiasa na kadhalika ni kinyume cha sheria. Kutokana na misingi hii ya Katiba, naishauri Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba Sheria zinazosimamia haki kwa mtoto anayezaliwa nje ya ndoa na mtoto aliyezaliwa ndani ya ndoa zinakuwa na usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Sheria zinazosimamia mirathi na haki za matunzo kwa watoto zifanyiwe marekebisho ili kuondoa upungufu ufuatao:-

(a) Kiasi cha Sh. 100 kwa mwezi au malipo ya mkupuo ya Sh. 15,000/= kwa ajili ya matunzo ya mtoto ni kidogo sana na hivyo kiongezwe. Ni jambo la busara kama kiasi cha fedha za matunzo ya mtoto kingetolewa kama asilimia fulani ya mapato ya baba.

(b) Utaratibu wa kusitisha fedha za matunzo ya mtoto wakati mama anapoolewa kunamuathiri mtoto hususan mama anapoolewa na mwanaume mwingine ambaye anakataa kukaa na mtoto.

(c) Kusimamisha fedha za matunzo ya mtoto anapofikia umri wa miaka 16 au 14 ni kinyume na ufafanuzi wa mtoto. Mara nyingi ni katika umri huu ambao mtoto anahitaji matunzo zaidi katika elimu, afya, chakula na kadhalika.

(d) Ingawa Sheria inawataka Mahakimu kufuatilia ili kuona kama fedha zinazotolewa zinatumika ipasavyo au mtoto anatunzwa vizuri. Kiutendaji jambo hili halifanyiki na hivyo ni vyema sheria zikaweka wazi sharti hili la kiutendaji ili kuhakikisha fedha za matunzo zinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya Dola visimamie haki za watoto na wanawake. Umefika wakati kwa Serikali kuweka sheria zitakazovitaka vyombo vya dola visimamie sheria kuwasaidia wanawake na watoto wanaonyanyaswa kijinsi au kubakwa ili waweze kuwa mstari wa mbele katika kutoa taarifa kwa matukio ya aina hii pindi yanapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto na wanawake wengi wanashindwa kutoa taarifa ya matukio ya aina hii Polisi au kwenda Mahakamani kutokana na lugha za kejeli zinazotolewa kwao pindi wanapowasilisha malalamiko au kesi zao kwenye vyombo hivi. Aidha, naishauri Wizara ya Katiba na Sheria kuweka masharti katika sheria yatakayotoa adhabu kali kwa wazazi ambao watafanya majadiliano na watuhumiwa wa makosa ya jinai kwa watoto wao kwa lengo la kumaliza kesi husika nje ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile watumishi wa vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria hususan Mahakama na Polisi wachukuliwe hatua kali pindi itakapothibitika kwamba, wanawanyanyasa wanawake au watoto wanapokwenda kutoa taarifa za kufanyiwa makosa ya jinai hususan kubakwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zinazolinda haki za watoto na wanawake zifanyiwe marekebisho ili zitoe adhabu kali zaidi kwa watu wanaofanya matendo ya unyanyasaji kwa watoto na wanawake. Aidha, sheria zilizopo hivi sasa zisimamiwe kwa ukamilifu kuhakikisha kwamba haki inatendeka pindi mtoto au mwanamke anapofanyiwa vitendo viovu, hivi sasa pamoja na sheria hizi kuwepo, bado wananchi wengi wanaona kwamba haki za watoto na wanawake zipo kwenye karatasi tu na hazitekelezwi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama zetu nyingi zimegubikwa na rushwa katika mfumo wa uendeshaji wake wa mashtaka, hivyo basi kupelekea wananchi kutokuwa na imani na maamuzi katika Mahakama zao. Kwani Mahakama zetu si safi na kuonekana kuwa wenye pesa na uwezo wa kutoa rushwa ndio ambao watapata haki zao katika Mahakama kwani wananchi wa hali ya chini kutokuwa na imani na Mahakama zao na kukosa haki zao kwani kutokuwa na pesa kwao ndio kunawafanya wasiwe na imani na Mahakama zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana kuwa haki inatolewa tu kwa wale ambao wana pesa na wapo katika hali nzuri ya kiuchumi na si kwa Mtanzania maskini. Hivyo basi, tunaitaka Serikali itoe tamko kama kuna watu wa usalama katika Mahakama zetu au la /hapana. Kama watu wa usalama hawapo katika Mahakama zetu kuna mpango gani wawepo na kubainisha uchafu wa

Mahakama na kupelekea wananchi kuwa na imani na Mahakama zao kuwa zinaweza kuwaletea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Mheshimiwa Waziri katika majibu yake atuambie ni utaratibu gani ambao Serikali itatumia kuzisafisha Mahakama zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na urasimu wa watu katika kada ya chini kwenye masuala ya kupata *document* zao au ripoti zao kutoka Mahakamani. Vile vile kumekuwa na usumbufu sana, hususan Makarani wetu katika Mahakama wamekuwa ni wasumbufu na wababaishaji. Mfano, hukumu kucheleweshwa, inaweza kufikia miezi sita mpaka 12 bado hukumu haijatoka. Hivyo basi, jambo hili ni kero kubwa kwa wananchi wetu. Pia nataka kujua Serikali inasemaje kuhusiana na suala hili la kucheleweshwa kwa hukumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limekuwa kama utaratibu katika Mahakama zetu kwani kama *Court* ime-*order injuction* ina maana muda mrefu utapotea kusubiri hukumu kwa usumbufu wa Makarani katika kutoa *documents* kwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ada ya kufaili ushauri katika Mahakama. *Fee* ya kufaili *advice* katika *courts* imekuwa kama vile biashara kwani ada yake ni kubwa ambayo si kila mtu anaweza kuimudu. Vile vile kupelekea gharama katika Mahakama kuwa ni kikwazo au *barrier* katika kupata haki za watu. Mfano, pamoja na mtu kuwa na *attachment* ya *document* zote husika bado kunakuwa na gharama kubwa kama vile kiwango cha milioni 40. Pamoja na kuwa na vielelezo vyote stahiki bado mtu

anachajiwa milioni tatu. Hivyo basi suala la gharama katika kufaili au kufungua shauri katika Mahakama limekuwa ni *barrier* kwa watu kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara iwe na kiwango maalum cha kuchaji pesa katika kufaili kesi na mashauri mbalimbali katika Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama ya Kadhi; katika Mahakama Kuu kuna kitengo cha Mahakama ya Kadhi na pia Rufaa na maombi ya marejeo kutoka Tume ya Usuluhishi kama vile *arbitration* na mengineyo. Kwa kuwa kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa taarifa au *documents* kutoka katika Tume ya Usuluhishi ambayo inapelekea kupoteza sana muda na kufikia mpaka miezi sita, hali ya kuwa bado hakuna taarifa yoyote katika Mahakama Kuu na kuweza kulitolea maamuzi. Hivyo basi, inafika mpaka miezi sita hali ya kuwa faili halijatoka *CMA* na kufika Mahakama Kuu, hivyo, kupelekea mlundikano na ucheleweshaji wa hukumu. Hivyo basi, ku-*delay* kwa *CMA* katika kupeleka *documents* katika Mahakama Kuu imekuwa ni kero kubwa na kupelekea kesi kuchukua muda mrefu katika kupata maamuzi kutoka Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali ichukue hatua kuhakikisha mafaili yanafika kwa wakati na endapo kutakuwa na ucheleweshaji pia tunataka kujua ni hatua gani Serikali itachukua ili kuondoa kero hii na kupelekea *documents* kufika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Suit by a poor person;* katika suala hili la mtu asiyekuwa na uwezo katika kufungua kesi tunaitaka Serikali au Wizara ianzishe utaratibu mzuri wa mtu

maskini kuitumia fursa hii kwani bado wananchi wengi ambao wanapaswa kutumia fursa hii wanashindwa kwa kutokuwa na uelewa kuwa wanaweza kushtaki hali ya kuwa hawana pesa na hali duni ya maisha. Hivyo basi, kumejengeka dhana ya kuwa, watu wanaoshtaki ni wale wenye pesa tu. Hivyo basi, naishauri Serikali kupitia Wizara husika kutoa uelewa kwa watu wasiojiweza, nao waone kuwa wana haki ya kushtaki endapo watadhulumiwa haki zao na kuondoa dhana ya kuwa asiye na uwezo hawezi kupata haki wala kushtaki.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Baada ya kuunga mkono hoja naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa Mahakama za Mwanzo na Mahakama ya Wilaya mpya ya Kalambo. Kama ilivyokuwa katika mchango wangu katika bajeti ya mwaka jana ambapo nilichangia kwa kueleza jinsi ambayo wananchi wa Jimbo langu la Kalambo na Wilaya mpya ya Kalambo yenye jumla ya Kata kumi na saba (17) inavyokosa haki kwa kukosa vyombo vya kupatia haki kwa kutokuwa na Mahakama hata moja. Hivyo kuwalazimu wananchi kutembea zaidi ya kilomita mia moja na kwa maeneo mengine hadi kilomita mia moja na hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hapo juu Serikali ione ni jinsi gani ambavyo wananchi wanavyokosa haki zao na kubaki wanalalamika chini chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutoa kilio changu katika bajeti ya mwaka jana nililichangia pamoja na kuuliza swali, nilitegemea kwamba uvumbuzi ungeweza kupatikana ili wananchi wangu waweze kupatiwa na kutendewa haki kwa wakati. Kwa bahati mbaya sana pamoja na kilio hiki cha muda mrefu hakuna lolote lililotokea ili kuleta nafuu kwa wananchi wa Wilaya ya Kalambo katika kupata haki badala ya kuwalazimisha kuchukua sheria mkononi. Katika jitihada za kuhakikisha wananchi wa Kalambo wanapata haki zao, nimejitahidi kwa kuiandikia Wizara kutaka kujua *status* baada ya ajira ya Mahakimu 300 na Wizara ijue Kalambo tunategemea wangapi kupitia kwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, bado sijapata majibu.

**MHE. ZAHRA ALI HAMADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama ya Kadhi; pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa tamko kuhusu Mahakama ya Kadhi, kuna haja ya Serikali sasa kuliona suala hili kwamba, umefika wakati wa kulishughulikia kwa vitendo ili kuondoa manung'uniko kwa Waislamu na Taasisi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usikilizaji wa kesi, Serikali iongeze idadi ya watumishi hasa Mahakimu na Mawakili wa Serikali wa kada mbalimbali ili kuongeza kazi ya uendeshaji wa Mashauri mbalimbali nchini kwa lengo la kulipatia ufumbuzi suala la mlundikano wa mashauri Mahakamani. *Speed* ya uendeshaji kesi bado ni mbaya na ya kusikitisha kwenye mwaka 2011/2012. Hadi kufikia mwezi Mei, 2012, mashauri 5,259 sawa na asilimia sita yalikuwa yamehitimishwa na kubaki mashauri 84,974 yatakayoendelea kuendeshwa katika ngazi mbalimbali za Mahakama pamoja na mapya, hali hii ni mbaya kwa

mustakabali wa utoaji haki nchini. Uchelewaji wa kesi hazihusu wanyonge tu, pia zinahusu kesi za maslahi ya Taifa, ni vizuri tukafanya kila mbinu kuhakikisha kesi zetu zinasikilizwa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini kuniwezesha kuchangia hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Baada ya kupitia katika randama za Wizara, nashauri Serikali iangalie namna yoyote iongeze bajeti ya Wizara hii nyeti na muhimu ambayo ina changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuleta mabadiliko ya Sheria kupata Katiba mpya. Ni wakati muafaka kwa Watanzania kupata fursa kujadili Katiba wanayoitaka. Pia napenda kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kuteuliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuongoza Wizara hii nyeti na muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali iangalie namna ya kuboresha Mahakama zetu kwa kuwapatia vitendea kazi na vya kisasa. Ni vema Serikali iangalie namna ya kuboresha wapiga chapa na wahudumu wengine ili tuweze kwenda na wakati. Pia Serikali iangalie namna ya kuboresha majengo ya Mahakama zetu pamoja

na samani katika majengo hayo. Tunaomba Wizara iendelee kutoa elimu juu ya sheria mbalimbali hasa vijijini ambako hakuna Wanasheria na wananchi wengi wanapata shida sababu ya kutojua sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Manyara, tunaishukuru Serikali kujenga Mahakama ya Mwanzo na ya Mkoa (*high court*) Babati. Tunaomba mjitahidi kumalizia sehemu ndogo ya ukarabati wa majengo na kuweka samani. Tunashauri Mahakama hizi ziwe za kisasa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wananchi kuhusu muda wa kesi na sababu ya kuchelewa kutoa hukumu au muda wa kuendesha kesi. Wahusika wote hawako chini ya Wizara hii, wako Wizara ya Mambo ya Ndani, upande wa upelelezi na wakichelewa kutoa ushahidi na kuomba kuimarisha kila mara pamoja na Mawakili, kesi zinachelewa, lakini pia Hakimu au *Judge* lazima wapitie sheria mbalimbali na kuzisoma ili waweze kutoa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara iendelee kuangalia sheria mbalimbali zilizopitwa na wakati ili zirekebishwe pamoja na sheria kandamizi. Tunaomba Mkoa wa Manyara ambako inaweza kujengwa Mahakama ya Mwanzo na Mahakama Kuu (*high court*) ni vyema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pia waweze kufungua ofisi zao Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba iendelee kutolewa elimu juu ya wananchi ambao wanavunja sheria kwa kuchochea wananchi, kwa kutoa lugha za kichochezi, ubaguzi na mara nyingi walio wengi kufanya vurugu bila

kujua wanavunja sheria. Tungeomba sheria za haki za binadamu na baadhi za sheria zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili na nyepesi ili wananchi wengi wapate uelewa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara iandae *CD* au *DVD* ya Sheria Mbalimbali zilizokuwa *updated* ili wananchi wengi waweze kupata na kupitia. Itakuwa na gharama ndogo kuliko vitabu. Pia tunaomba Sheria ya Ardhi Na. (4) na (5) ziweze kupatikana kwa urahisi. Tunapongeza Mheshimiwa Rais kuteua Mheshimiwa Jaji Mkuu na Majaji wengine na tunaomba aendelee kuteua wengine hadi nafasi zote zilizokuwa wazi au mahitaji yatosheleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na Mungu awabariki.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa hotuba nzuri. Pia nimpongeze Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ni Wizara muhimu sana kwa utoaji haki kwa wananchi wetu. Pamoja na umuhimu huu mkubwa bado Wizara hii inapewa bajeti kidogo sana. Nikiangalia katika Jimbo la Busanda kuna upungufu mkubwa sana katika Ofisi za Mahakama ya Mwanzo. Hata ambazo zipo zina upungufu mkubwa wa miundombinu kama vile ofisi na nyumba za kuishi watumishi. Kwa mfano, pale Katoro kuna Mahakama ya Mwanzo, ofisi zake ziko katika hali mbaya sana. Hata hivyo, wameanzisha

ujenzi wa ofisi ambayo imechukua muda mrefu bila kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara katika bajeti ya mwaka huu ofisi ya Katoro ipate kipaumbele katika kuikamilisha. Vile vile Mahakama zilizochakaa kama vile Mahakama ya Chigunga pia ifanyiwe ukarabati ili kuboresha mazingira ya Mahakama kwa ujumla. Pia Wizara iangalie uwezekano wa kusogeza huduma hii kwa wananchi hata kwa kuona uwezekano wa kuanzisha Mahakama za Mwanzo kila Kata hali ambayo itarahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni lile la usajili wa watoto chini ya miaka mitano. Ndani ya hotuba nilishukuru kwamba Mkoa mpya wa Geita ni miongoni mwa mikoa itakayofanyiwa utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huu. Niombe kwamba usajili huu ufanyike katika ngazi ya Vijiji na vyeti vitolewe katika ngazi ya Kijiji. Hii itarahisisha usajili wa watu wengi na watajitokeza kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliokuwepo wa mwanzo umelalamikiwa sana na wananchi walio wengi maana vyeti vilitakiwa kuchukuliwa Makao Makuu ya Wilaya. Sasa wananchi ambao hawakuwa na uwezo wa nauli, wengi hawakufikia malengo haya ya usajili. Utaratibu ninaopendekeza ni kama ule wa mpiga kura, ambapo waandikishaji wanafanya hatua zote na mwisho wanampatia kitambulisho mpiga kura. Niombe hata katika usajili na watoto ufanyike vijijini na waliosajiliwa wapewe vyeti vyao papo kwa papo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kupata maoni kwa ajili ya Katiba mpya, napenda kukumbusha kuwa wananchi wapatiwe nakala za Katiba ya zamani. Wengi wa wananchi vijijini ikiwemo Vijiji vya Busanda ombi lao kubwa ni kupata nakala za Katiba iliyopo ili iwarahisishie kujua kilichopo ndani ya Katiba ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuongeze suala la elimu kwa umma kuhusu yaliyomo ndani ya Katiba ya sasa, lakini pia kuhusu mchakato mzima wa namna ya kupata Katiba mpya. Kampeni zifanyike kwa kiwango kikubwa sana hasa vijijini ambako wananchi wengi wanahitaji kueleweshwa. Serikali ikiwekeza katika kuelimisha wananchi upo uhakika wa kupata maoni dhahiri kutoka kwa wananchi wa kada zote Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishie hapa, lakini niombe Wizara iangalie changamoto zangu za Busanda na iangalie namna ya kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED SAID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye maelezo ya kina na yanayojitosheleza. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuridhia mchakato wa Katiba kuanza hatimaye Tume imeshaundwa. Tume hii ni sawa kabisa, kwani imeweka wajumbe nusu kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, lakini pia tumeona kuna uwiano wa kijinsia na makundi mbalimbali ya jamii umezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Tume kwa uzalendo wao kwani pamoja na kwamba vitendea kazi vingine bado havijakamilika, lakini wamekuwa imara na kazi ya kukusanya maoni wameanza rasmi 2/7/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa umma kuhusiana na Katiba ni jambo muhimu sana. Hivyo, Wizara ijitahidi sana elimu kwa umma iwafikie wananchi ili waweze kuwa na uelewa utakaowasaidia katika kutoa maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Tume ya Katiba, wajitahidi kwenda katika maeneo mengi kadri wawezavyo ili kuwafikia wananchi wengi na maeneo mengi zaidi kupata fursa kwa wote ya kutoa maoni yao kwa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningeliongelea ni uchakavu wa majengo ya Mahakama na ukosefu wa majengo ya Mahakama. Tunayo majengo mengi yamechoka na sehemu nyingine hakuna majengo kabisa. Ni kwa nini tusifanye tathmini ni kiasi gani kinaweza kujenga majengo hayo ambayo yamechakaa sana ili ikiwezekana Serikali ikakopa kwa wahisani na kuwa historia kwa majengo ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Utafiti wa Demokrasia ya Afya ya Tanzania zinaonesha kwamba usajili wa vizazi kwa kundi la watoto walio katika umri wa chini ya miaka mitano kwa Tanzania uko kwenye 14% na wenye vyeti vya kuzaliwa ni 6% tu. Wakati kwa mwaka wanazaliwa watoto 1,500,000 kiwango ambacho ni kikubwa zaidi kwa watoto ambao hawajasajiliwa wala kupewa vyeti vya kuzaliwa, hivyo hawajulikani. Hata katika kupima maendeleo ya MKUKUTA, kiwango cha usajili wa watoto ni kiashiria kimojawapo ambacho Tanzania

inapimwa. Natoa rai kwa Serikali ijitahidi katika bajeti zijazo kutenga fedha za kutosha za ndani ili kila mtoto nchi hii aweze kupata usajili lakini pia kupata cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu hawafahamu haki zao za sheria, nashauri Wizara itoe elimu kwa wananchi kuhusu haki mbalimbali za kisheria na masuala mengine kama vile kuandika wosia, ili kuondoa adha wanayoipata wanawake wajane pamoja na yatima, lakini vile vile Sheria za Ardhi na nafasi ya mwanamke katika kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni wakati sasa Mahakimu na Majaji wetu wakajikita katika kutoa adhabu mbadala kwani tumekuwa tukishuhudia wako washtakiwa ambao wamehukumiwa vifungo kwa makosa ambayo yanaweza kutolewa adhabu mbadala kama vile, kutumikia katika jamii kwa kufanya kazi kwa masaa kadhaa chini ya uangalizi wa Afisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Mahakimu ambao hawafuati maadili ya kazi zao, ni vema sasa Tume ya Utumishi wa Mahakama ikawachukulia hatua Mahakimu ambao hawafuati maadili ya masharti ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati. Wizara izifanyie marekebisho sheria zote zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uendeshaji wa Mashauri Mahakamani uweze kuwa wenye ufanisi kuna haja ya Mahakama zetu zote kutumia mfumo wa kurekodi

mwenendo wa kesi kwa kutumia teknolojia katika Mahakama za ngazi zote nchi nzima. Kwani kwa kufanya hivyo itawarahisishia kazi Mahakimu na Majaji, pamoja na hukumu za kesi kuandikwa mapema kwani kumbukumbu zote muhimu zitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kuendelea vyema na mchakato wa Katiba Mpya. Naomba kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ihakikishe kuwa fungu la bajeti ya Mahakama lililotengwa katika bajeti linaifikia Idara ya Mahakama kama ilivyotengwa katika bajeti ili kuwezesha Idara ya Mahakama kufanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ihakikishe kwamba inajenga nyumba za Majaji na Mahakimu ili usalama wa Majaji na Mahakimu uzingatiwe, kwani kitendo cha Mahakimu kukaa sehemu za kupanga ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifanye ukarabati wa Mahakama zetu. Kwa mfano, Mahakama za Mwanzo, Mzenga, Chole na Maneromango ndani ya Wilaya ya Kisarawe ni chakavu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali iwawezeshe Wazee wa Baraza kulipwa posho zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba Tume ya Kukusanya Maoni ijitahidi kuweka utaratibu mzuri ili kila mtu aweze kupata nafasi ya kutoa maoni, kwani kuna taarifa kwamba maeneo mengine watu wamekosa nafasi ya kutoa maoni kutokana na hamasa kubwa ya wananchi waliojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali ihakikishe kuwa Tanzania inaanzisha Mahakama ya Kadhi ili masuala ya ndoa na mirathi kwa Waislam yaweze kusikilizwa katika Mahakama hizo. Kwa wale Waislam wanaohitaji masuala yao ya mirathi na ndoa yahukumiwe kwa mujibu wa imani yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, na Watendaji wote Wakuu wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuwasilisha bajeti nzuri na yenye matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa ushauri juu ya kero zinazojitokeza kutokana na utendaji wa Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu suala la kuendelea kulundikana kwa kesi Mahakamani na mahabusu Magerezani kwa muda mrefu. Naishauri Wizara

itafute mkakati wa kupunguza msongamano huu ili haki iweze kupatikana kwa wahusika wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na upungufu mkubwa wa Watumishi wa Mahakama katika ngazi zote licha ya wahitimu wengi katika fani hii kutoka vyuo mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi. Je, ni nini chanzo cha upungufu huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ifanye utafiti wa kutosha ili kubaini na hatimaye kurekebisha upungufu huu.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima kwa kuandaa bajeti nzuri, lakini zaidi kwa kuendesha Wizara na shughuli, vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza jinsi mchakato wa Katiba mpya unavyokwenda na unavyosimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa mchakato wa Katiba mpya, unakwenda vizuri, ninahimiza tuendelee hivyo na kuzidi kuwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza na kuomba kuwa maeneo mapya ya Utawala, (Wilaya Mpya na Mikoa) yakumbukwe katika usambazaji wa Watendaji hasa Mahakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia na kushauri mambo mbalimbali kwenye Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata majibu kuhusiana na masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Katiba imeanza kazi kabla ya bajeti yake kupitishwa Bungeni. Je, fedha hizo zimetoka fungu gani? Kwani fungu 08 la Tume limeanza mwaka huu na bado halijapitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Muhambwe, kwenye Wilaya ya Kibondo, kuna Hakimu mmoja tu wa Mahakama ya Wilaya, kuna kesi nyingi na kadhalika. Je, ni lini Serikali itaongeza Hakimu wa Wilaya Kibondo na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kwamba kutokana na ongezeko la kesi za ardhi, na Mabaraza ya Ardhi yako machache: Kwa nini Wizara ya Katiba na Sheria isilete mabadiliko ya sheria ili kesi hizi zisikilizwe kwenye Mahakama za Wilaya? Kwani, hatuwezi kujenga majengo ya Mabaraza haya kila Wilaya, ikiwa ni pamoja na kuajiri Mahakimu 133 kwenye kila Mahakama ya Wilaya watakaoshughulikia kesi za ardhi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili itimize majukumu yake vizuri. Lakini Ofisi hii imekuwa inaachia watuhumiwa kwa '*nole proseque*' bila kutoa sababu. Kwa nini Serikalini isifanye mabadiliko ili '*state*

*attorneys*' wanapowaachia watuhumiwa watoe sababu za kufanya hivyo kama ilivyo Kenya na nchi nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata majibu ya Serikali, kwa nini *report* ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora, *current* ni ya mwaka 2008, wakati *NGO'S* kama *LHRS* wana *report* za haki za binadamu hadi mwaka 2011? Pia nashauri Serikali iongeze bajeti ya Tume hii ili iweze kufanya kazi zake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Elimu ya Mafunzo ya Sheria kwa vitendo (*Law School of Tanzania*), napenda kushauri kama nilivyowahi kuuliza swali Bungeni kwamba: Kwa nini wanafunzi hawa wa Shule ya Sheria hawapatiwi mikopo? Waziri alinijibu kwamba, Sheria ya Bodi ya Mikopo *(HESELB Act, 2004)* itabadilishwa, lakini kwenye mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye Kamati, jambo hili halipo. Nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inaonekana kuna fedha zimetengwa na Wizara kwa sababu ya kuwasaidia wanafunzi. Napenda kupata majibu, ni utaratribu gani utatumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la watu, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kwamba, ni wakati muafaka sasa kila Mkoa kuwa na Mahakama Kuu kwenye kila Mkoa. Mfano, kutoka Kigoma kwenda kanda ya Tabora, umbali ni mkubwa na kadhalika na pia inaongeza gharama na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Tume ya kurekebisha Sheria kwamba, wakati inafanya marekebisho, ifanye marekebisho makubwa na ishauri maeneo mapana

ili kuepuka kurekebisha sheria moja kila baada ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Mahakama (Muhambwe) Wilayani Kibondo, katika Jimbo la Muhambwe, bado kuna upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Lakini hata Mahakama ya Wilaya ina majengo yaliyojengwa na 'Wakoloni', lini Serikali itatenga fedha kujenga Mahakama ya kisasa Kibondo Mjini pamoja na kujenga Mahakama za Mwanzo? Naomba kuwasilisha.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wengine wa Wizara hii kwa kuratibu na kusimamia masuala ya sheria hapa nchini. Binafsi, pamoja na kuunga mkono hoja hii, namwomba Waziri anijibu hoja zifuatazo:-

Je, wananchi wetu wa Tanzania wana uelewa upi kuhusu Katiba? Ni juhudi zipi zimefanyika ili kuelimisha umma wa Watanzania juu ya Katiba ya nchi yetu? Kuelekea Tanzania ya Katiba Mpya: Je, Wizara imefanya juhudi zipi za makusudi ili kusambaza nakala za Katiba iliyopo angalau kwa kila Mtaa au kwa kila Balozi ili wananchi wetu wapate kuisoma na kuichambaua?

Je, Wizara imefanya juhudi zipi za makusudi ili kuwezesha Watanzania wote wa jinsia zote ili waweze kushirikiana katika zoezi la kutoa maoni juu ya mchakato wa kuanzishwa kwa Katiba mpya?

Je, Waziri na Watendaji wengine wa Wizara mnafahamu wazi kuwa Sekta ya Sheria imetawaliwa na rushwa ya kila aina; fedha au ngono au motisha mbalimbali. Ni hatua zipi za makusudi zinachukuliwa na Wizara ili kukabiliana na tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uhaba wa Mahakama za Mwanzo katika nchi yetu ni kubwa, inajenga Mahakama ya Mwanzo kwa kila Kata. Serikali imejiandaaje kukabiliana na tatizo la Mahakimu wa Mahakama hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Sheria katika nchi yetu ni ngeni na kutokana na mazingira halisi ya utamaduni wa Mtanzania zinaonekana dhahiri kuwa uelewa kwa Watanzania ni mdogo sana, mathalan Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi, pia Sheria ya Ushindani Huria, na nyingine nyingi. Je, Serikali kupitia Wizara hii imejipanga vipi kutoa elimu juu ya sheria ambazo ni ngeni katika mazingira ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Watanzania kubambikiwa kesi na kwa kuwa hawana uwezo wa kuwaweka Mawakili wa kuwatetea: Je, Wizara haioni kuwa kuna ulazima wa Mawakili wa Serikali kuwatetea wanyonge wasio na uwezo kwa kuwatetea kwa gharama ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini suala la rushwa katika Mahakama zetu litazikwa kabisa na kutokomea?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Sheria ya Ndoa za Kimila hadi sasa katika kipindi hiki cha Maendeleo ya Sanyansi na Teknologia zina manufaa yoyote ile?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria nyingi za nchi yetu zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza ambayo ni lugha ngumu kwa Watanzania wengi. Je, Wizara ina mpango gani wa kutafsiri sheria hizo kwa Kiswahili chepesi ili Watanzania wengi wazisome na kuzielewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu, Naibu Mwanasheria Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Angela Jasmini Kairuki aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria. Tunamtakia kila la kheri katika kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanafunzi wa *Law School,* ninaishauri Serikali iingie mkataba na Mawakili wa kujitegemea, watoe elimu ya vitendo kwa wanafunzi hawa kuliko kuendelea kufundishwa na Wahadhiri wa Chuo Kikuu kwa nadharia tu. Pia Serikali itoe mikopo kwa wanafunzi wa *Law School,* kwani ili mwanafunzi huyu awe Wakili na kufuzu mafunzo haya kama ilivyo kwa Madaktari Wanafunzi wa Vitendo *(interns).* Sheria husika ziletwe, zibadilishwe ili zisaidie vijana wetu kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tumeomba Serikali ilete haraka utaratibu wa ku-*record* mwenendo wa shauri Mahakamani na kutoa *Hansard* ili kuondoa *human*

*errors* na *deliberate errors.* Serikali kupitia Bunge hili imekuwa ikiahidi mara nyingi kuanzisha utaratibu huu. Naamini safari hii katika bajeti ya mwaka 2012/2013 fedha imetengwa ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge hili kutunga Sheria ya *Prosecutions Act 2008*, tulitegemea Askari Polisi wetu waachane na kazi ya kuendesha mashtaka, badala yake washughulike na upelelezi tu, yaani *investigation* na kazi ya *prosecution* iachiwe *state attorney* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nyingi zimekuwa zikiishutumu Idara ya Mahakama kwa kuongoza kuomba na kupokea rushwa. Inawezekana ni kweli na pengine ni tabia ya watumishi, lakini mojawapo ya sababu ya kuomba rushwa ni mishahara midogo sana ya watumishi wa Idara ya Mahakama. Nashauri kwamba, ili kupunguza tatizo hili, ni kutoa mshahara unaoendana na hali halisi ya kiuchumi. Ni vizuri Serikali ikatafuta njia ya kuboresha kipato cha watumishi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Watumishi, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Watumishi wa kada nyinginezo ni muhimu sana ili kuwapa uwezo wa kufanya kazi zao kwa uhuru zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote na Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri yenye kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kondoa, kuna upungufu wa Mahakimu, kuna Hakimu mmoja tu ambaye amefanya kazi nzuri ambayo ni nzito kwa kuwa yuko peke yake. Kwa msingi huo, tunaomba tuongezewe Mahakimu ili kupunguza kuelemewa kwa Hakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Wilaya ya Kondoa ni miongoni mwa Wilaya zilizoanza zamani sana, mpaka sasa Wilaya haina Mahakama. Majengo yanayotumiwa ni mali ya Halmashauri wakati ambapo Halmashauri ina upungufu wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii niliwasilisha mwaka 2011 wakati wa bajeti ya Sheria ambapo hoja hii haikujibiwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majengo ya Mahakama Kondoa ili kuondoa usumbufu kwa Watendaji? Kwani majengo waliyoazimwa hayatoshi na pia kupunguza usumbufu wa Watendaji wa Halmashauri ambao majengo yao yanatumiwa kama Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ziara zangu katika Kata mbalimbali, Vijiji, Vitongoji, Mitaa, Taasisi na Idara mbalimbali zilizomo Jimboni kwangu, nimepokea maoni, hoja na maswali kadhaa ambayo yanahitaji ufafanuzi, majibu na/au maelekezo ikizingatiwa kuwa Wizara hii ni nyeti na kwamba Watanzania walio wengi hawana ufahamu juu ya sheria za nchi, Katiba na kadhalika. Hivyo wamenituma nije niwasilishe hoja zao katika Wizara hii kwa ajili ya kupata ufafanuzi, majibu na kadhalika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii tunachangia ikiwa tayari mjadala wa kupata maoni ya wananchi kuhusu Katiba yakiwa yanaendelea. Hilo ni jambo la kupongezwa kwa hatua ambayo Serikali kupitia Tume ya Kuratibu Maoni imekuwa ikitekeleza. Ukiwa mjadala unaendelea, kumekuwepo minong'ono kuwa baadhi ya mambo hayatakiwi kuhojiwa katika Tume hiyo kama kuhoji kuhusu Tume ya Uchaguzi, kutangaza matokeo ya uchaguzi, kuhoji Mahakama kutokuwa na uwezo wa kutengua matokeo ya Rais, na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitaka Serikali itupe ukweli juu ya minong'ono hiyo. Nini ukweli na uhalisia wake? Pia wananchi wanalalamika kuwa muda uliotolewa ni mdogo ikizingatiwa maoni ni mengi. Serikali inasemaje? Serikali inasema nini kuhusiana na sheria zilizopitwa na wakati *(ordinance)* sheria za kikoloni hasa ambazo zinatumika katika majeshi yetu? Mfano, Askari Magereza anapotenda kosa, hata kama la kibinadamu kama kupitiwa na usingizi, huadhibiwa kwa kukatwa mshahara wake, kutopandishwa cheo na kukosa nafasi ya kujiendeleza kimasomo, na pengine kuhamishwa na kupelekwa eneo lenye mazingira magumu. Hivi Serikali haioni kuwa huo ni uonevu, kukiuka haki za binadamu na pia kuwaweka askari rehani? Kwani askari hawalindi fedha wala magari wala majumba, hulinda watu, tena wenye hulika tofauti, majambazi, wezi, magaidi, wahujumu, watumia madawa ya kulevya na kadhalika. Ni lini basi sheria hizi zitabadilishwa au kuondolewa kabisa, ili kuwafanya askari wetu wafurahie utendaji wa kazi zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara za Sheria kama Mahakama zimekuwa zikilaumika kuwa hazitoi haki au zinatoa kwa upendeleo au zikijihusisha na vitendo vya rushwa mara nyingi. Serikali haioni kuwa kwa sasa kuna haja ya kuboresha mishahara, motisha na vitendea kazi vya kutosha ikiwa ni pamoja na kuwapatia mikopo ya masharti nafuu ili waweze angalau kuweza kumudu kujenga nyumba zao au hata kuwa na usafiri wao kwa nia ya kuharakisha utendaji kazi wao ikizingatiwa kuwa mahitaji ni makubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasemaje kuhusiana na sheria, tangazo namba 130/2002 wakati Waziri akiwa Mheshimiwa Brigadia Hassan Ngwilizi juu ya kuondoa na kupiga marufuku vizuizi vyote nchi nzima? Lakini bado bugudha ya vizuizi ipo na inaendelea hasa katika Manispaa ya Lindi. Kinachojionyesha ni kuwa wanapokuja viongozi wa Serikali (Rais, Mawaziri) mageti huondolewa (siyo halali) na wakishakuondoka, mageti na vizuizi hivyo hurejeshwa. Tunaitaka Serikali itoe ufafanuzi juu ya kero hiyo ambapo maeneo mengine kazi ya Afisa Maliasili Misitu Uvuvi na kadhalika au Afisa Biashara au *TRA* zote hufanywa na askari wanaokuwepo getini hapo, hali inayopeleka kukosekana mapato maeneo husika na kujenga misingi ya mwendelezo wa rushwa.

Tunaomba Serikali iwaelekeze wananchi wa Jimbo langu juu ya Sheria iliyoanzisha Vyama vya Msingi wa Vyama Vikuu vya Ushirika vya Mikoa na Sheria inavyovilazimisha Vyama vya Msingi kujiunga na Vyama Vikuu vya Mikoa. Hata kama hakuna maslahi na pia sheria inayowalazimisha wakulima kuuza mazao yao kwenye Vyama hivyo vya Msingi na Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba ufafanuzi juu ya wanaoitwa Wahamiaji haramu kuhukumiwa katika Mahakama zetu wakati ambapo pengine Sheria zetu zinapingana na Sheria za nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna baadhi huwa ni wapita njia tu kuelekea maeneo mengine, lakini hulazimika kujificha ficha na hatimaye kupelekea vifo. Je, Serikali haioni kuwa huku ni kukiuka haki za binadamu? Je, Serikali inafurahia kuona Raia wake yanawakuta hayo wakiwa nchi nyingine? Naomba maoni ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasema nini kuhusu Sheria ya upigaji kura kwa mahabusu katika Selo na Magereza zetu? Pia kugombea nafasi na uongozi kwa wenye vifungo visivyozidi au kukiuka vifungo vilivyotajwa na Sheria ya Uchaguzi; lini watu hawa watashiriki chaguzi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasema nini kuhusiana na kuwa na Sheria ya Kulinda Watumiaji na Wasafiri wa Vyombo vya Baharini ikizingatiwa kuwa watu wengi hupoteza maisha kila siku kutokana na kuzama au matukio ya aina hiyo pasi na kulipwa bima au fidia inayostahili?

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ya utawala bora ni pamoja na kumpa haki mtuhumiwa kusikilizwa pale inapotokea ametuhumiwa kutenda kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Askari Polisi, kanuni na taratibu za Jeshi zinaelekeza kwamba askari akituhumiwa kutenda kosa, hatua ya kwanza ni kumfukuza

kazi. Baada ya hapo anatiwa nguvuni na kushtakiwa Mahakamani. Matokeo ya hukumu yanaweza kumtia hatiani askari huyo au kumkuta hana hatia, lakini kwa matokeo yoyote yale askari kashafukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini mantiki ya Sheria hii ambayo kwa makusudi inavunja haki za binadamu? Je, Serikali itakuwa tayari kuleta marekebisho ya Sheria hii kandamizi?

**MHE. SLIYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kuwa Wizara inao mpango kwa kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama ya Mwanzo. Katika Jimbo langu la Kibaha, Mahakama ya Mwanzo ipo katika hifadhi ya barabara *(road reserve).* Ni jengo chakavu kabisa, tena la miti na matope. Hapa ni kilometa 35 tu toka jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe maelezo, ni lini Mahakama hii iliyopo maili moja itabomolewa na kujengwa Mahakama mpya na mwanzo?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tatizo la kesi kuchukua muda mrefu na kufanya wenye haki yao kuchukua muda mrefu sana. Kuna tatizo la jinsi amri mbalimbali zinavyotolewa na Mahakama mara nyingi amri hutolewa hata bila kusikiliza upande wa pili. Jambo hili husababisha hasara, taabu na maumivu kwa wananchi ambao hawastahili. Jambo hili linafanya dhana ya haki na heshima ya Mahakama kupata doa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umefika sasa Mahakama zipatiwe vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi. Inachukua muda mrefu baada ya hukumu hata kupata nakala ya hukumu ambayo inakupa haki na nafasi ya kutetea jambo lako mahali popote. Vifaa kama Computer, *Photocopiers, Printers* ziwepo kuanzia Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri na kazi nzuri wanayoendelea kufanya, napenda kuunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja katika eneo moja la ucheleweshwaji wa kesi kwa watuhumiwa wa kesi mbalimbali, ninapata shida sana ninapoona watuhumiwa wengi wa makosa mbalimbali wanapowekwa Rumande kwa zaidi ya mwaka mmoja kusubiri hukumu zao. Wakati mwingine kesi haziendeshwi, nina maana zimeahirishwa kutokana na Mahakimu kutokuwepo Mahakamani kwa dharura kwamba wamepangiwa kazi nyingine au ushahidi haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, upelelezi unachukua muda mrefu, hata kwamba kesi husika ipo bayana wala haihitaji upelelezi wa miaka mingi. Tendo hili linakera wananchi wengi hasa wale wanaopenda kufuatilia na kutetea haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuachana na mwendo huo na badala yake itende haki kwa kutoa hukumu kwa watuhumiwa kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka Mahakama mbalimbali kuanzia za Mwanzo, Wilaya, Mkoa na Mahakama Kuu, juu ya ucheleweshaji wa kesi mbalimbali na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa washtakiwa na washitaki. Hii inasababishwa na kiasi kidogo sana cha fedha zinazotengwa kuhudumia Mahakama zetu. Hii inasababisha ucheleweshaji mkubwa katika kusikiliza kesi na kuzitolea maamuzi katika. Katika kipindi hiki, Serikali itenge fedha za kutosha ili kuziwezesha Mahakama zetu ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na kutenda haki kwa kila anayehitaji.

Sambamba na hilo, kumekuwa na tatizo kubwa sana la uhaba wa nafasi katika Mahakama zetu, kwani nyingi zilijengwa wakati wa Mkoloni na hivyo uwezo wa kuhudumia watu wengi kwa wakati mmoja kwa sasa haupo, maana idadi ya watu imekuwa kubwa kulingana na miaka ya nyuma. Vitendea kazi pia katika Mahakama zetu ni vichache na vimepitwa na wakati. Hata karatasi wakati mwingine zinakosekana na hii inatia aibu Mhimili huu mkubwa wa Serikali. Sababu kubwa ni bajeti ndogo ya Mahakama, hivyo Serikali ilione hilo kama ni changamoto kubwa inayohitaji kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Wabunge kikatiba, ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka wazi majukumu ya Wabunge kwamba Bunge ni chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano Tanzania ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi, kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Ibara ya 36(2) inayotamka madaraka ya Rais ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka za viongozi wanaowajibika kuweka Sera za Idara, Taasisi za Serikali na Watendaji Wakuu wanaowajibika kusimamia utekelezji wa Sera za Idara na Taasisi hizo katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na nukuu hizo hapo juu, majukumu ya Wabunge kwa Serikali na madaraka ya Rais ya Uteuzi, imeonekana kwamba kumekuwa na *double standards* katika utendaji kazi wa Wabunge.

Kutokana na ukweli kwamba Rais amekuwa akitumia madaraka yake Kikatiba kuteua Wabunge kuwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao kiutendaji wanawajibika kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika ibara ya 36(2), Wabunge hawa kwa mujibu wa ibara ya 63(2) wamekuwa wanakiuka wajibu wao wa kuisimamia na kuishauri Serikali, maana wao wanakuwa ni sehemu ya Serikali na hivyo hawawezi kujisimamia na kujishauri wenyewe. Sasa kwa namna hii ni kwa vipi Wabunge hawa wanaweza kuwawakilisha wananchi wao waliowachagua kama wao hawawezi kuuliza maswali yanayohusu maeneo yao na ambayo wametumiwa na wananchi wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, imetokea hapa Bungeni Wakuu wa Wilaya walipouliza maswali waliambiwa

kwamba wao ni sehemu ya Serikali na hivyo hawawezi kuiuliza Serikali maswali. Sasa ni kwanini utaratibu huu bado unaendelezwa na kuteua Wabunge kuwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya ilhali wao ni sehemu ya Serikali? Kwanini busara isitumike kuteua watu wengine ambao hawawajibiki moja kwa moja kwa Serikali? Hii *double standards* inabidi iondolewe ili kuwapatia wananchi haki yao ya kikatiba ya kuwahusisha kikamilifu na Wabunge wao waliochagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili hawa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanapokea mshahara na marupurupu yapi kati ya Bunge na Serikali? Ni wakati gani wanawajibika Bungeni na kwenye maeneo yao ya kiutawala, yaani Mkoa na Wilaya? Jambo hili liangaliwe kwa jicho la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko nchi nzima hasa kutoka maeneo ambayo Tume ya kukusanya maoni ya Katiba Mpya imepita kwamba Wakuu wa Wilaya wamekuwa wakiingilia zoezi hili kwa kuwapanga watu na kuwapa maneno ya kuongoza ili kulinda maslahi ya Chama Tawala na Serikali yake. Natahadhirisha kwamba mtindo huu ni wa kuwanyima wananchi haki yao ya msingi ya kutoa maoni na hivyo Katiba itakayoandaliwa itakuwa ni ya maslahi ya wachache na siyo ya Watanzania wote na hivyo kupelekea manung'uniko muda mfupi baada ya kuundwa kwa Katiba hiyo, jambo ambalo linaweza kuleta pia machafuko nchini. Ni busara kuwakemea Wakuu hawa wa Wilaya kufanya kazi ambayo siyo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa kwa baadhi ya washitakiwa watoto, yaani ambao hawajafikisha umri wa miaka 18 kuendelea kuchanganywa kwenye mahabusu za watu wazima na kufanyiwa vitendo viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna msongamano mkubwa wa kesi hivyo na kuleta malalamiko mengi kuwa kesi zinachelewesha ili haki zipindishwe. Lakini ukiuliza sababu kubwa ni Mahakama kutengewa fedha kidogo katika kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Bunda wamekuwa wanalalamika kwa miaka mingi kwamba hawana jengo la Mahakama. Je, Serikali katika mwaka huu wa fedha imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya za Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna malalamiko kuwa Ofisi ya *DPP* imekuwa ikichelewesha majadala ya mashtaka, hivyo kukwamisha baadhi ya kesi kuchelewa kufika Mahakamani au kutofikishwa Mahakamani kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato wa Katiba Mpya, na zoezi linaloendelea la kuchukua maoni, wananchi wamelalamikia kwamba muda unaotumika kukusanya maoni katika eneo husika ni mdogo, kwani ni saa tatu kwa kila eneo, hivyo kufanya watu wengi wasitoe maoni yao katika fursa hii muhimu.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja na kusema mimi ni mwana Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala.

Wizara hii ni nyeti sana kwa sababu inasimamia vyombo vya kutoa haki kama Mahakama mbalimbali pamoja na Ofisi ya *DPP*. Kwa sababu hiyo, inabidi Wizara hii iwe *proactive* na ihakikishe inaziwezesha Taasisi hizi bila '*unnecessary bureaucracy au redtape'*. Serikali izipatie taasisi hizi fedha za kupunguza changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na Mahakama ambazo ziko katika hali mbaya sana au mlundikanao wa kesi katika Mahakama. Kuna ucheleweshaji mkubwa wa kesi kutokana na upungufu wa Mahakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa kuwapelekea *young graduates* wa Sheria kwenye Mahakama za Mwanzo ni mzuri, lakini ni muhimu kuwawekea hawa vijana mazingira mazuri ya kazi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanapewa nyumba nzuri, pamoja na posho ya mazingira magumu. Bado maisha ya vijijini ni magumu, hakuna *social amenisties.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoishauri Serikali wakati wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, uteuzi wowote ufuate sifa na uwezo na siyo urafiki, udini na ukabila. Umpandishe mtu cheo na umpe kazi ambayo hana uwezo nayo, ukilazimisha kumpa kazi ambayo hana uwezo nayo atakuwa kituko. Zingatia *principle* ya *management* inayojulikana kama *Peter principle: "Never promote somebody to his/her highest level of incompetency."* Naogopa kuona jinsi Majaji wanavyozalishwa kila siku bila kuzingatia uzoefu wao. Ni kweli tuna upungufu wa Majaji, lakini uteuzi ukifanywa kiholela, tutapata *half-cooked judges.* Tume ya mabadiliko ya Katiba imeanza kazi ya kukusanya maoni wakati wananchi walikuwa hawajapewa elimu ya Katiba ya sasa. Sina hakika kama watapata

mawazo mazuri ya kupata Katiba nzuri. Pia *sample* yao ni ndogo sana. Lakini pia ni muhimu kwa Wizara kuona umuhimu wa kuishirikisha Kamati ya Katiba Sheria na Utawala katika mchakato huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majaji na Mahakimu wanashughulikia kesi mbalimbali na zenye uzito tofauti, kesi nyingine ni za hatari, hivyo ni muhimu Mahakimu kama Majaji wakapewa nyumba zenye uhakika na kwenye sehemu nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye mchakato wa Katiba, Serikali iliahidi kusambaza nakala za Katiba ya sasa ili wananchi wazisome kuwawezesha kutoa maoni mazuri kwa Tume. Serikali haijafanya hivyo, naiomba Wizara ishughulikie jambo hilo. Hakimu wa Wilaya ya Ngara anashirikiana na matapeli kuwadhulumu walimu pensheni zao wanapostaafu. Matapeli wanawakopesha walimu ambao wanakaribia kustaafu fedha kidogo, kisha wanashirikiana na Hakimu, huyo Hakimu anamwandikia Meneja wa Benki ya *NMB* Ngara kwamba Mwalimu fulani atakapokuja Benki kuchukua pensheni yake akatwe fedha anazodaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo huo mdogo wanaufanya uwe mkubwa sana. Kuna Mwalimu aliyekuwa anadaiwa Shilingi milioni tatu wakazifanya Shilingi milioni thelathini na wakazichukua kweli!

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii adimu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wao kwa umakini na umahiri wao katika utendaji na uendeshaji wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba suala la haki ni suala muhimu sana na ni suala ambalo linamgusa kila mtu na busara kila mtu kuhakikisha kwamba haki yake anaipata. Suala la msingi ambalo linanipelekea kuipongeza Wizara hii ni kuweza kuongeza idadi ya Mahakimu ambayo kwa kiasi kikubwa unaweza kusaidia msongamano wa wafungwa na mahabusu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Waziri aliweke wazi tatizo la kufumbia macho suala zima la uendeshaji kesi unaopelekea kubaki kwa mahabusu wengi Magerezni na pia kupelekea mahabusu watu wazima kuchanganyika na watoto na pale linapotokea hilo kama mambo ambayo yanajitokeza Magerezani, ambayo ni hatari sana, kuwaweka mahabusu watu wazima na watoto, kuna suala ambalo linahofiwa kutokea la kuingiliana bila hiari au kushawishi ama kwa mazingira ambayo hayaepukiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri aeleze katika majumuisho yake, namna gani anaweza kuliondoa suala hili ama kama haiwezekani Serikali inatamka nini juu ya suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi, japo nikipata nafasi ya kuongea pia basi nitawezwa kuchangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo kwenye kipindi cha mpito cha maandalizi ya kutunga Katiba Mpya. Kwa umuhimu wa pekee nilipendekeza, basi Tume hii ingechukuwa muda wake mchache na muhimu kupita Magerezani na kupata maoni ya wafungwa na mahabusu ili kupata maoni yaom maana nao ni Watanzania wenye maoni juu ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mlundikano wa wafungwa Magerezani ni kubwa mno na kwa kweli mahabusu ni wengi kuliko wafungwa na wengi wanakaa muda mrefu sana na sababu ni kuwa kazi zao bado, upelelezi unakuwa haujakamilika na wengi wao ni masikini na watu wenye kipato cha chini na wakati mwingine wanakuwa na makosa ya adhabu ndogo au kwa kesi za kubambikiwa na Askari wa Jeshi la Polisi wasio waaminifu na kusababisha watu hao kukaa Gerezani kwa muda mrefu. Wakati mwingine hawa wanakuwa ndio wanaotegemewa sana kimaisha na familia zao ambazo ni duni mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imepelekea chuki kati ya wananchi na vyombo vinavyosimamia sheria za nchi na chuki kwa Serikali kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kuangalia upya ni namna gani ya kuweka ukomo wa mahabusu kukaa Gerezani wakati akisubiri kesi yake, kukamilishwa kwa upelelezi, wakati akisubiri kesi yake kukamilishwa kwa upelelezi. Ikumbukwe kuwa, wengi wanafungwa kwa kuwa hawana uwezo wa kujitetea Mahakamani na hawana fedha ya kuweka Wakili.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya pia ni mapendekezo yangu katika kupunguza mlundikano Magerezani, muda ambao mahabusu wamekaa kusubiri kesi yao ikamilike kwa upelelezi, basi muda huo aliokaa Gerezani uhesabiwe baada ya kupewa hukumu yake ya kifungo. Kama mtu alikaa Gerezani kwa kusubiri upelelezi kwa muda wa mwaka mmoja na akahukumiwa miaka mitatu, basi akae kutumikia kifungo kwa muda wa miaka miwili kwa kuwa tayari muda wa mwaka mmoja umekwishakaa Gerezani na hapo tutakuwa tumekwenda sambamba na haki za binadamu na kurudisha imani kwa wafungwa na mahabusu, wanyonge wanaopoteza matumaini yao dhidi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano hai, ni katika taarifa ya miaka 50 ya Uhuru. Magereza walitoa changamoto zinazowakabili, ni pamoja na mlundikano wa wafungwa na mahabusu ambao uwezo ni 29,552 na waliopo Gerezani ni 38,000 na zaidi. Ongezeko hili ni kubwa mno, ni lazima mkakati mahsusi ufanyike ili kupunguza hatari ya mlipuko wa magonjwa ya ngozi na magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya hewa. Pia ikumbukwe kwamba kati ya Magereza 127 yaliyopo nchini bado Magereza 25 yanatumia mitondoo, wakati bado Magereza hayana Waganga wa kutosha, Wataalam wa Maabara na Vituo vya Tiba kwa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara irejee hukumu ya Jaji Mstaafu Mheshimiwa Barnabas Samatha katika Shauri Na. 48 la Tabu Fikwa dhidi ya Jamhuri (1988 TLR 48). Katika shauri hilo, alishauri vyombo vya Dola na Mahakama kwa ujumla kuwachukulia wafungwa kama zao

la hali ya kiuchumi na kijamii na kuangalia njia mbadala ya kutoa hukumu na siyo kuzingatia hukumu ya kifungo pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara itazingatia haya, basi tutapunguza sana tatizo la msongomano Magerezani na kuhakikisha kila mtuhumiwa na mfungwa anatendewa haki kwa mujibu wa sheria zilizopo na hivyo kupunguza tatizo hili kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Sheria na Katiba kwa kazi ngumu na pia kwa kuteuliwa kwao kwa kushika nafasi hii muhimu hasa ukizingatia nchi yetu inaendeshwa kwa utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu awabariki sana.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake Wizarani pamoja na Taasisi wanazozishughulikia hasa ukizingatia ufinyu wa bajeti wanayopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, naomba kutoa mapendekezo kwamba, Wizara lazima (Mhimili) ipewe fedha za kutosha; na nasisitiza ule mpango wa kuwekewa mfuko wao uharakishwe na utekelezwe. Kama sote tujuavyo, hivi ndivyo mhimili wa usimamizi na kweli ni msingi wa mihimili yote iliyobakia. Hakuna Serikali wala Bunge litakalofanya kazi sawa sawa bila ya kuwa mhimili huu ni dhaifu. Kama sote tujuavyo, Bunge kazi zake ni kutunga sheria na siyo utekelezaji wa sheria hizo. Serikali nayo ni maguvu na haiwezi kwenda au kuendesha mambo yake bila Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara jinsi wanavyojipanga. Ni wazo lao la kuajiri Mahakimu wa muda ili kumaliza msongamano wa kesi nyingi zilizoko Mahakamani. Hivi sasa hili ni wazo zuri, kwani litapunguza dhiki na usumbufu wa washtakiwa na usumbufu kwa familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko kuwa kesi au mahabusu ni wengi Magerezani, kiasi ambacho familia zao zinasumbuka na watoto kuparaganyika na hata wakati mwingine watoto kuwa wa mitaani. Lakini akina mama nao kuwa malaya kwa ugumu wa maisha. Hii ni sababu kubwa Mahakama, Majaji na Wizara inachukiwa. Lazima kesi ziharakishwe na maamuzi yatolewe. Lakini zaidi, matumizi yalikuwa siyo ya lazima kwa Serikali kwa kuwalisha na kuwatibu mahabusu walioko Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ni kero, na madawa ya kulevya pia. Nashauri pawepo na Mahakama maalum kwa kushughulikia kesi hizi. Rushwa (wala rushwa) kwa wanaokamatwa na madawa ya kulevya na mihadarati, wauaji wa albino na vikongwe (wazee) wabakaji watoto chini ya umri wa miaka 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi kesi hizi huchukua muda ambao siyo wa lazima, lakini zaidi, kadiri muda unapokuwa mrefu ndipo uzito wa kosa lenyewe linavyopoteza ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, mafunzo na taaluma zitolewe kwa Mahakimu, wamwogope Mungu,

kwani kazi ya Hakimu ni nguvu na uwezo alokuwa nao Muumba peke yake.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango kuhusu mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, fungu la 08 - Tume ya Mabadiliko ya Katiba, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume haikutekeleza kwa upana *program* kabambe ya kuendesha *programm* ya elimu kwa umma. Matokeo yake ni kwenye Mikoa mbalimbali nchini niliotembelea katika kipindi cha toka Tume iundwe, wananchi kwenye mikutano ya hadhara wamekuwa na malalamiko ya kutopata elimu ya kujiandaa kutoa maoni. Malalamiko kama hayo yamejitokeza katika awamu ya kwanza ya ukusanyaji maoni kwenye Mikoa iliyoanza hivi sasa. Hivyo katika mwaka 2012/2013 hususan katika Mikoa ya awamu ya pili, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ichukue uzoefu wa nchi nyingine mbazo kabla ya kipindi cha kukusanya maoni, kuna kipindi na *programm* kabambe ya kutoa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara ya Katiba na Sheria ieleze katika majumuisho, ni lini italeta Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 kuhusu ufungaji na Katiba ikiwemo muundo wa Bunge la Katiba, na uhalalishaji wa Katiba hususan suala la kura ya maoni kusimamaia na Tume ya

Uchaguzi ambapo muundo wake wa sasa umelalamikiwa na wadau wote kuwa hauko huru na haki?

Suala la marekebisho ya sheria hii kwa awamu nyingine ni muhimu katika kujenga muafaka wa Kitaifa, kuelekea kuwa na Katiba mpya na bora, kama ilivyoahidiwa pia na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Aidha, Wizara ifuatilie taratibu za manunuzi yaliyofanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba iwapo yamezingatia sheria na kanuni za ununuzi na fedha za umma, kwa kuwa yamefanyika kwa wingi na kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, fungu la 35 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika mwaka wa fedha 2011/2012 michango ya Wabunge mbalimbali tulihoji hatua zinazochukuliwa na Ofisi ya *DPP* kuhakikisha, kutokana na majalada yaliyowasilishwa na TAKUKURU, yanayohusu tuhuma za rushwa kubwa, katika majumuihso Wizara ieleze ni majalada mangapi ya ufisadi mkubwa *(grand corruption)* na ya kesi zipi yaliwasilishwa na TAKUKURU kwa *DPP,* mangapi yameshapelekwa Mahakamani, na nini hatma kwa majalada ya tuhuma za miaka mingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, fungu la 40 - Mfuko wa Mahakama ni muhimu, matakwa yote ya sheria ya uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011 yakatekelezwa kwa ukamilifu ikiwemo Mahakama kutengewa kiwango cha kutosha cha fedha. Hivyo, Serikali itoe maelezo Bungeni, ni kwanini Mfuko wa Mahakama haukupewa kiwango kilichopangwa na Bunge cha Shilingi bilioni 20, badala yake imepokea Shilingi bilioni 14.7, sawa na chini ya asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze kiasi cha fedha kilichopangwa mwaka 2011/2012 kwenye kiwango cha mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, Wizara ieleze imefika wapi katika kuweka mfumo maalum wa kuharakisha mashauri yaliyopo Mahakamani, yanayochelewesha miradi ya maendeleo kama ya fidia ya wananchi wa Kwembe kwa ajili ya mradi wa Chuo Kikuu Muhimbili *(MUHAS)* na ya kuhusu maeneo ya mradi wa mabasi yaendayo kasi *(DARTS)?*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Mathias Chikawe na Naibu Waziri, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Katibu Mkuu na wale wote walioshiriki kuandaa Hotuba ya Bajeti, yenye maelezo yaliyojitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Rais kwa kuridhia mchakato wa Katiba. Nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuridhia mchakato wa Katiba kuanza na hatimaye kuunda Tume yenye uwakilishi wa Wajumbe nusu kutoka Tanzania Bara na nusu kutoka Tanzania Zanzibar. Vile vile katika uteuzi wake, amezingatia umuhimu wa wanawake na kuwateua wengi wa kutosha kuwa katika Tume ile. Tunamshukuru sana Rais, kwa kutambua kuwa wanawake wanaweza na kuwateua katika Tume na katika nafasi mbalimbali wakiwemo na Majaji Wanawake. Pia natoa pongezi kwa Tume, nawapongeza Wajumbe wote wa Tume, kwa kuteuliwa kwa uzalendo wao waliouonesha, kwani pamoja na kwamba vitendea kazi bado havijapatikana, lakini wamesimama imara na kuanza kazi

ya kukusanya maoni katika Mikoa minane toka tarehe 2 Julai, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, Viongozi na Watendaji wa Serikali, Vyama vya Siasa na Wananchi wote, watoe ushirikiano wa hali na mali kwa Tume hii ili iweze kutekeleza wajibu wao kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kuwahamasisha wanawake na wananchi wajitokeze kwa wingi kwenda kutoa maoni yao mbele ya Tume katika maeneo waliyopangiwa na kutuma maoni yao kwa anuani iliyotolewa na Tume ili Katiba Mpya itokane na maoni ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, Nchi yetu ipo katika mchakato wa kutoa maoni juu ya Katiba ili kupata Katiba Mpya, bado zipo Sheria zinazowakandamiza wanawake na watoto, ambazo zimetungwa na Bunge, zinahitaji kurekebishwa. Sheria hizo ni Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inayoruhusu mtoto wa kike kuolewa chini ya umri wa miaka 18, Sheria ya Mirathi na Sheria ya Matunzo ya Mtoto, Sheria za Kimila na Sheria nyingine zinazomkandamiza mwanamke na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ya kukarabati na kujenga Mahakama zetu, naomba niseme hali ya Mahakama zetu ni mbaya, majengo yamechakaa na maeneo mengine hakuna Mahakama kabisa; hivyo, wananchi wanatembea masafa marefu kwenda kutafuta Mahakama. Naishauri Serikali ijitahidi kuongeza fedha katika kasma hii ili Mahakama zetu ziweze kuboreshwa, ikiwezekana Serikali

iweke mpango wa kukopa katika Taasisi za Fedha hapa nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ya Serikali ya kuajiri na kupeleka Mahakimu katika Mahaka nchini. Naishauri Serikali iongeze ajira katika eneo hili kwani isipofanyika hivyo wananchi wetu wanakosa haki yao kwa wakati na kuichukia Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya utafiti iliyofanywa na Demografia ya Afya Tanzania, inaonesha kwamba, usajili kwa kundi la watoto walio chini ya umri wa miaka mitano kwa Tanzania Bara upo kwenye asilimia 14 na wenye vyeti vya kuzaliwa ni asilimia sita tu. Wakati watoto wanaozaliwa ni zaidi ya milioni moja kwa mwaka, kiwango hiki cha watoto ambao hawajasajiliwa ni kikubwa sana, naiomba Serikali katika Mwaka wa Fedha ujao (2012/2013), itenge fedha za kutosha za ndani ili kila mtoto hapa nchini apate usajili na apate cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa ya kuhakikisha wananchi wanazijua sheria, bado lipo tatizo la baadhi ya wananchi kutojua sheria. Naishauri Wizara itoe elimu kwa wananchi kuhusu haki mbalimbali za kisheria na masuala mengine kama vile kuandika Wosia, ili kuondoa adha wanayoipata wanawake wajane na yatima, lakini vilevile Sheria za Ardhi na nafasi ya wanawake katika kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mrundikano wa wafungwa katika magereza yetu hapa nchini, kuna haja sasa ya kuangalia upya makosa ambayo yanaweza

kutolewa adhabu mbadala kama vile kutumikia katika jamii kwa kufanya kazi kwa saa kadhaa chini ya uangalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya Mahakimu wetu, bado baadhi yao wanalalamikiwa kutotenda haki. Nashauri tujitahidi kuwakumbusha Mahakimu wetu watekeleze wajibu wao ipasavyo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuandaa Hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na msongamano mkubwa sana wa wafungwa na mahabusu kwenye magereza yote hapa nchini. Hili linawanyima haki Watanzania waliofungwa au kutuhumiwa na hivyo kurundikwa kama wanyama maeneo ambayo ni ya kurekebisha tabia na siyo sehemu ya mateso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutenganisha adhabu za watuhumiwa kwa kutoa adhabu mbadala kwa makosa madogo utatekelezwa lini? Siyo kila kosa ni lazima watuhumiwa wapelekwe magerezani au mahabusu. Wapo watuhumiwa wa kuiba shilingi elfu kumi, wengine godoro, wengine nguo, baiskeli na vinginevyo. Serikali inatumia gharama kubwa za vyakula, mavazi na malazi, kwa makosa ambayo yangeweza kupatiwa adhabu mbadala, lakini pia familia zinazoachwa nyumbani zinateseka kwa kukosa huduma ya wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu uliowekwa kwenye magereza na mahabusu ya wanawake kuwavua nguo zote kila siku kwa kisingizio cha upekuzi wakati wafungwa wapo ndani ya *fence* na Afisa Gereza yupo muda wote. Naiomba Serikali ilieleze Bunge udhalilishwaji huu kwa wanawake utaondolewa lini? Haki siyo kwenye Katiba ya Nchi, kitendo cha kuwa mahabusu au gerezani hakimwondolei ubinadamu wala haki zake za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahabusu wanakaa muda mrefu sana magerezani bila kesi zao kusikilizwa. Sheria gani inayosema mtuhumiwa atengwe na familia yake miaka sita huku hajasikilizwa na kuonekana na hatia? Je, kwa mtu kama huyu kesi yake ikisikilizwa na asipoonekana na kosa analipwa nini kufidia mateso aliyoyapata; na familia yake inalipwa nini kwa kukosa huduma za baba au mama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Nzenda Wilaya ya Urambo, kuna watuhumiwa wamekaa miaka sita hadi tisa bila kusikilizwa hata siku moja. Wamekuwa wakihamishwa gereza moja baada ya lingine, wengine wamechanganyikiwa (*mental problem*) na hata hawaelewi kwa nini wapo pale na familia zao zilishawasahau miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Watanzania walioko kwenye hali kama hii, kwenye gereza hili na magereza mengine, Mahakama ina mikakati gani ya dhati ya kuwaondoa kwenye mateso na gharama za kuendelea kuwaweka pale; jambo ambalo hata ukimpeleka Mahakamani hawezi tena kujitetea kwani hajitambui?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Watanzania kuwa Tume ya Kuratibu Mapendekezo ya Katiba Mpya, itawashirikisha vilivyo waweze kutoa mawazo yao kwa uhuru na haki na pia itapatikana kabla ya Uchaguzi wa Mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Viongozi wa Siasa akiwepo Katibu wa Siasa na Uenezi kuitisha Vyombo vya Habari na kuainisha masuala ambayo Chama kingependa yawepo kwenye Katiba na yale ambayo kingependa yasiwepo siyo kuingilia haki na madaraka ya Tume?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Serikali ieleze kwa nini haikutoa tamko wala karipio kwa kauli za Viongozi wanaotoa maelekezo kwa wananchi juu ya utoaji wa maoni yao kwa mapendekezo ya Katiba Mpya?

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la udhaifu mkubwa linalozidi kujitokeza kuhusu uadilifu wa Mahakimu hasa ngazi ya Mahakama za Mwanzo; naomba kutoa mfano wa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Nguruka, Wilaya ya Kigoma. Hakimu huyu hana uadilifu kabisa, mlevi na anatumia nafasi yake kusumbua raia. Nimewahi kutoa taarifa mpaka kwa Hakimu Mkazi Kigoma, akakiri Hakimu huyu anapaswa kuwa Kata za karibu na Makao Makuu ya Wilaya ili awe chini ya uangalizi. Mwaka jana nililizungumza hili Bungeni na leo narudia kwa kuwa inaelekea Wizara haijatoa uzito wa malalamiko ya Vikao vya Serikali ngazi ya Kata *(WDC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya *RITA* inafanya kazi nzuri na muhimu, natambua utendaji bora wao, hivyo

naomba waongezewe fungu ili waongeze ufanisi. Naomba kutoa ombi kwa *RITA* kuhakikisha wanafika Wilaya ya Mpya ya Uvinza, kwani kuna tatizo sugu la vijana na watoto wengi kukosa vyeti vya kuzaliwa na hivyo kupata usumbufu wa kupata huduma kama elimu na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ombi kwa Mkoa wa Kigoma kupata Mahakama Kuu. Mkoa wa Kigoma una kesi nyingi zinazohitaji huduma ya Mahakama Kuu, lakini bado inategemea huduma hiyo kutoka Mkoa wa Tabora. Umbali kutoka Kigoma mpaka Tabora ni kilometa 700. Ombi langu hili linatokana na ukweli huo wa umbali, lakini zaidi ukweli kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa ina eneo kubwa na jengo kubwa ambalo kwa maoni ya wataalamu, linatosha kutumika na *Resident Judge* wakati utaratibu wa miundombinu unaendelea. Naomba tupate *residenti judge* wakati taratibu zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Mahakimu; nashauri Mahakimu hasa ngazi ya Mkoa na Wilaya wapatiwe nyumba na kwa kipindi cha mpito Mahakimu hawa walipwe kodi za nyumba ili kuboresha maisha ya watu hawa muhimu kwa ustawi wa haki nchini.

Naomba Wizara katika mwaka huu wa fedha itenge fedha kukarabati Jengo la Mahakama ya Mkoa wa Kigoma. Jengo hili ni la zamani na lina nyufa nyingi, likifanyiwa ukarabati lina uwezo wa kutumika hata na *Resident Judge* kama nilivyopendekeza hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Wilaya ya Kigoma, inatoa huduma eneo kubwa, lenye jiografia ngumu, hasa Ukanda wa Ziwa, nashauri ipatiwe *boats*

kurahisisha usafiri katika Ukanda wa Ziwa, ambalo ni eneo lenye ukubwa sawa na nusu ya eneo lote. Pia wapatiwe pikipiki kwa usafiri Ukanda wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Wilaya Mpya ya Uvinza kuna Mahakama tatu ambazo ni Uvinza, Kalya na Simbo, ambazo zote hazina Hakimu wa Mahakama. Naomba sana tupate huduma hii katika Mahakama hizi kwani ni hasara kuwa na miundombinu iliyojengwa.

**MHE. UMMY ALLY MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Katiba na Sheria, juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Pia ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mathias Chikawe, kwa kuteuliwa kwa mara ya pili kuiongoza Wizara hii. Ninampongeza Mheshimiwa Angellah Kairuki, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri. Nina imani kubwa sana kuwa, wataiongoza vyema Wizara hii na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafarijika na jitihada kubwa sana zinazofanywa na Wizara katika kusimamia masuala ya utoaji haki kwa wote na kwa wakati na pia katika kuandaa na kusimamia Sera za Utawala wa Kisheria na kusimamia masuala ya haki za binadamu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie kuhusu Sheria Kandamizi Dhidi ya Wanawake na Wasichana. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inatambua na kuzingatia usawa wa binadamu na imekwenda mbali kukataza vitendo vyovyote vya kibaguzi ikiwemo ubaguzi wa Jinsia. Hata hivyo, kinyume na Ibara

ya 13 ya Katiba, bado kuna Sheria ambazo ni kandamizi na zinazowadhalilisha wanawake na watoto. Natambua kuwa kuna kazi kubwa sana inafanywa na Wizara ila kuna kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa kwa Wizara kuharakisha mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria hizi ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kulinda, kukuza na kuthamini haki za wanawake na wasichana katika nyanja mbalimbali. Sheria zinazotakiwa sasa kufanyiwa marekebisho haraka ni pamoja na:-

1. Sheria ya Ndoa ya 1971 ambayo pamoja na mengineyo, inachochea ndoa za watoto wa nchini ya umri wa miaka 18. Hiki ni kikwazo kwa nchi kufikia malengo ya Usawa wa Jinsia na uwezeshwaji wa wanawake hasa katika elimu, afya ya mama/uzazi na mtoto.

2. Sheria za Mirathi za Kimila mfano *Local Customary Law* (*Declaration*) ni wakati mwafaka sasa kufanyiwa marekebisho kwa sababu inaruhusu Sheria za Kimila za Mirathi ambazo hazizingatii Usawa, Jinsia na Haki za Wanawake. Je ni lini tutaletewa Muswada wa Marekebisho ya Sheria hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, kwa uwasilishaji wake mzuri. Pia nawapongeza Majaji na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuiwezesha Tume ya Mabadiliko ya Katiba na kuanza kazi kwa umakini. Pamoja na hilo, nawashukuru wananchi wote hasa pale ambapo wameanza kutumia demokrasia yao kutoa maoni katika vituo vilivyojengwa. Hata hivy, kwa Vituo vya Zanzibar hasa Kusini, wananchi wameitikia wito na wanakwenda kwa wingi, kiasi ambapo wengine hawapati nafasi ya kutoa maoni kwani muda unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ianzishe Ofisi ya Mahakama ya Rufaa Tanzania kwa upande wa Zanzibar ili napo kuwe na Ofisi Maalum ambayo itarahisisha kazi kwa upande wa pili wa Muungano. Pia uwepo utaratibu mzuri wa *Register* wa Zanzibar kuwalipa posho inayoridhisha ingawa wao ni waajiriwa wa Zanzibar, lakini wanafanya kazi nyingi za Mahakama hii ya Rufaa kama kutafuta Vitabu vya Sheria, majalada na kadhalika. Hivyo, naomba waongezewe posho badala ya shilingi elfu ishirini au elfu thelathini wanazolipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ianzishe Mahakama Kuu kwa kila Mkoa ili ipunguze usumbufu kwa wananchi wanaotafuta huduma za Mahakama ambapo pia Mahakama hizi zikianzishwa zitapunguza mrundikano wa kesi za Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itilie mkazo kwa kuiwezesha Mahakama kifedha, iipe za kutosha kwa ajili ya kuendesha shughuli zake. Tumeona jinsi fedha za bajeti za mwaka 2011/2012, zilivyokuwa kidogo na kushindwa kuendesha kesi vizuri. Naishauri Serikali iiwezeshe Mahakama kwa kuipa fedha za kutosha, ijengewe nyumba

za wafanyakazi na kuboresha miundombinu ambayo imechakaa kama Majengo ya Mahakama na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mahakimu waongezewe mishahara ili:-

(a) Wakopesheke, waweze kujenga nyumba zao wenyewe, kwani kwa watumishi hawa kupanga nyumba ni *risky* kwao, wanaishi na washtakiwa ni hatari kwao, lakini pia hawana fedha za kutosha kulipia kodi kwenye nyumba ambazo *at least* zina hadhi, hivyo hulazimika kupanga nyumba ambazo ni duni.

(b) Wakopesheke ili wanunue magari ambayo watatumia kwenda na kurudi nyumbani kutoka kazini, hii itakuwa salama kwao, kuliko hivi sasa ambavyo watumishi hawa husafiri pamoja na washtakiwa au ndugu wa washtakiwa ambao wanaweza kuwaumiza watumishi hawa. Hivyo, natoa rai kuwa Serikali iwaongeze mishahara watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziongezwe Shule au Vyuo vya Sheria Wanasheria wengi walio na Diploma wazalishwe waweze kupangiwa kazi kwenye Kata zote waweze:-

(a) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya Sheria mbalimbali hasa zile ambazo zinawazunguka kama vile Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sheria ya Ardhi na *Gender Based Violence* na Haki za Binadamu.

(b) Kuwasaidia wananchi kwenye Kata, Vijiji na Vitongoji hata ngazi ya Kaya, juu ya Sheria mbalimbali

watakaosimamia utekelezaji wa Sheria na Haki za Binadamu. Wanasheria hawa wakiwaelimisha wananchi, ni wazi makosa mengi yatapungua na hivyo kupunguza msongamano wa kesi Mahakamani na kupunguza msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misongamano ya kesi, mahabusu na wafungwa, itaifanya Wizara ya Katiba na Sheria kuboresha matumizi ya Sheria zitakazotumika. Pia hakutakuwa na haja ya kupanua magereza, kwa sababu hapatakuwa na msongamano wa mahabusu na wafungwa na hivyo hizo fedha zitanunua chakula bora na dawa za kutosha kwa mahabusu na wafungwa wachache wanaokuwepo magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri, Watumishi wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Jaji Mkuu na Majaji, Mahakimu wa Mahakama zote, Mwanasheria Mkuu, *DPP* na Watumishi wote wa Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushe kwa miaka mingi mfululizo nimepewa ahadi ya kujenga Mahakama ya Wilaya ya Hanang kwani toka Wilaya imeanza imekuwa inatumia Mahakama ya Tarafa. Nilipowasilisha maombi, Wizara haikusita kuona umuhimu wa kuwa na Jengo la Mahakama ya Wilaya; hivyo, naomba utekelezaji uanze kwani ahadi iliwapa matumaini Wananchi wa Wilaya yangu, kama hautaanza ni rahisi Serikali kuonekana haitekelezi ahadi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Katiba iliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais iwe makini kuona kuwa kuna watu wanafuatilia mikutano yake nchi nzima bila shaka kushinikiza maoni ya kikundi na ku-*influence* watu bila kutambua. Kwa maoni yangu huku ni kuzingatia uhuru wa wananchi katika kutoa maoni yao. Siyo sahihi jambo linalotakiwa na kikundi likaonekana katika Mikoa yote kwa ujanja unaotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ikae na Wizara ya Ardhi kuona nini kifanyike ili haki ya watu inayopotea kupitia Mabaraza ya Ardhi isiendelee kupotea. Kwa maoni yangu, *Customary Laws are outdated* kwani makabila yamechanganyika; hivyo, inakuwa ngumu kuona ni *customs* gani ifuatwe. Ingefaa Mabaraza ya Ardhi yangerudishwa katika mfumo wa Mahakama ya Ardhi ili washughulikie mambo ya Sera na taaluma yanayohusu ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia mawasilisho ya mafanikio.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia suala la matumizi ya *Internet* nchini. Kwa kuzingatia faida za matumizi ya mtandao, bahati mbaya watu wengi nchini wamekuwa wakitumia vibaya mitandao. Kumekuwa na matukio mengi kupitia mitandao ambayo yamekuwa yanalenga kudhalilisha wananchi hasa Viongozi wa ngazi za juu, jambo ambalo linalidhalilisha Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali izingatie mambo yafuatayo:-

1. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina Sheria inayodhibiti au kuhalalisha matumizi ya *Internet*, hili ni jambo la kushangaza sana ikizingatiwa kuwa wananchi wengi nchini wanatumia *Internet* bila kuwa na Sheria inayoidhinisha matumizi hayo.

2. Kwa kuwa kumekuwa na matukio mengi ya uhalifu utokanao na matumizi ya *Internet* na mitandao kwa ujumla, ni lazima sasa Serikali itunge Sheria, yaani *Cyberlaws* ili kulinusuru Taifa letu na madhara makubwa yatokanayo na uhalifu kupitia mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itilie maanani uwepo wa *cyberlaws* nchini ili tuepukane na madhara ambayo ni pamoja na kudhalilishwa Viongozi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kwa Wizara hii ya Katiba na Sheria katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, matumizi ya Lugha ya Kiingereza katika kutoa hukumu hizi inawahusu Watanzania; ni vyema maelezo au hukumu hizi zikatolewa kwa Lugha ya Kiswahili ambao hutumiwa na Watanzania wengi. Je, kuna sababu gani ya kutumia Lugha ya Kiingereza kwa miaka 50 sasa na Watanzania kuendelea kupata shida nayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, lugha hii pia ni tatizo kwa Mahakimu au Majaji katika kutoa hukumu, ifike wakati sasa Mahakama zitumie Lugha ya Kiswahili kutoa hukumu.

Jambo la pili ni kuchakaa kwa Mahakama zetu hasa Mahakama za Mwanzo. Serikali inapaswa kuangalia hali ya Mahakama zetu hasa za Mwanzo, hali inatisha hakuna vifaa, samani, *stationery* na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni uhaba wa nyumba za Mahakimu. Mahakimu kupanga nyumba za wenyeji ni kuwanyima uhuru wa kutenda haki kwa maeneo fulani, hakuna *privacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kucheleweshwa kwa kesi na mrundikano wa mahabusu magerezani bila ya kutolewa kwa hukumu zao; hili ni tatizo kubwa kwa nchi yetu, Serikali ichukue hatua za makusudi ili kuondoa usumbufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mchakato wa Katiba Mpya. Katika mchakato wa Katiba Mpya unaoendelea sasa, nashauri Serikali itoe nakala za Katiba za kutosha kwa Lugha ya Kiswahili ili wananchi wapate kutoa maoni yao kwa dhati na kwa uelewa wa Katiba iliyopo. Naiomba Tume iwe huru na itoe nafasi ya kutosha kukusanya maoni kwa makundi mbalimbali na pale itakapoonesha ulazima kurudia makundi au eneo fulani, hilo lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Usajili wa Vifo na Vizazi inapaswa kuwezeshwa ili kutenda kazi yake vizuri. Suala la vyeti vya kuzaliwa ni muhimu sana, maana sasa

watu wengi sana huhangaika mara wanapochaguliwa kwenda sekondari au chuo na kadhalika. Elimu inapaswa kutolewa kwa wananchi ili kuepukana na adha zisizo za lazima.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu Masista wa *Holy Spirit Sister* wa Rauya Marangu Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masista waliotajwa hapo juu wanamiliki shamba huko Sanya Juu Hai, wana Kituo cha Afya, Shule ya Sekondari na sasa wanataka kujenga kituo cha kulelea wazee, wanafuga mifugo na wanalima mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lalamiko langu ni jinsi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wanavyopindisha Sheria. Masista hao wanamiliki shamba hilo kihalali, wanayo hati ya kumiliki ardhi hiyo, wavamizi walianza kuvamia shamba hilo na walipeleka kesi Mahakama Kuu Kanda ya Kilimanjaro iliyopo katika Kesi Namba 3/2005 na Mahakama iliamua kwamba:-

(a) Wavamizi waliovamia eneo hilo kabla ya 2004 waendelee kubaki katika shamba hilo hadi kesi ya msingi itakapoamuliwa. Wavamizi hao ni 11.

(b) Wavamizi wengine walioingia katika shamba hilo la Masista wapatao 600 wasiruhusiwe kuuza ardhi hiyo na wasiruhusiwe kujenga na wala wasizike katika eneo hilo.

Amri hiyo ya Mahakama ilitolewa tangu mwaka 2008. Jitihada za Masista hao kutumia Mahakama au Polisi kuwaondosha wavamizi hao zimeshindikana hadi leo, tumemwandikia Waziri wa Mambo ya Ndani atumie Polisi kuwaondoa wavamizi imeshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alipokuwa anahitimisha Hotuba yake alizungumzia juu ya Masista kukutana na wavamizi ili kutafuta suluhu. Ikumbukwe kesi ya msingi haijamalizika Mahakamani, wavamizi wanaendelea kujenga majengo mapya, wanaendelea kuzika wafu wao na Mwenyekiti wa Kijiji anaendelea kuuza shamba la Masista.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua msimamo wa Wizara katika suala hili. Mahali ambapo Mahakama imekwishaonesha njia, watu wanaendelea kuvunja amri ya Mahakama tunafanya nini? Sasa huo Utawala wa Sheria, Utawala wa Kidemokrasia, unaoheshimu haki za binadamu uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja iwapo Waziri atajibu hoja hii.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia na Mahakama. Mara nyingi katika Mahakama yetu ucheleweshwaji wa kesi ndiyo tatizo kubwa sana katika nchi yetu, kwani kesi nyingi sana zinapotea bila ya kujulikana maamuzi yake na mwisho wake. Kwa mfano, kuna kesi nyingi za biashara, walemavu wa ngozi *(albino),* washtakiwa wa kesi hizi huwa mwisho unakuwa haujulikani, kwani hukumu zao huwa zinachelewa sana mpaka waathirika wanakata tamaa. Kwa nini

wanaojihusisha na viuongo vya binadamu, wenye ulemavu wa ngozi *(albino)*, kesi zao zisihukumiwe mara tu wanapofikishwa Mahakamani na hukumu hiyo iwe ni kifungo cha maisha ili iwe fundisho kwa wengine na siyo kuwaweka mahabusu?

Je, watu wangapi wamehukumiwa toka biashara hii haramu ilipojitokeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya magereza yetu nchini na wingi wa mahabusu; ni kwa nini kuna tatizo la ucheleweshaji wa kesi hata kama ya kuiba kuku ambapo siyo vizuri kwani ni mzigo kwa Serikali badala ya kupunguza hasara inayoongeza hasara kwa Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano; Zanzibar wafungwa wote huwa kuna mashamba yao wanalima mazao mbalimbali, wanachonga, kwa nini magereza yetu yote yasiwe na muundo wa kuzalisha kwani Tanzania tuna meneo mengi sana ya wazi kuliko kuwalimbikiza tu kuiongezea mzigo Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba watoto watengewe magereza yao kwani kama kuna Mahakama yao kwa nini kusiwepo magereza yao?

Kumweka mtoto gereza moja na mtu mzima ni uharibifu, mtoto badala ya kujifunza kulingana na umri wake basi anapotoka au akitoka gerezani huwa ameathirika kisaikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kwa hali tuliyonayo sasa kuboresha maslahi ya Majaji ili kuwafanya wasishawishike kuomba na kupokea rushwa. Pia kumwandalia mazingira mazuri pale tu anapohukumu kesi ya hatari kwa mtuhumiwa, kwani jamaa wa mtuhumiwa huwa wapo pale hukumu inapotokea sasa unakuta Jaji anatoka kama mtu tu wa kawaida. Je, unajua jamaa wa aliyehukumiwa kama hawataweza kumjeruhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaji waandaliwe mazingira ya kiusalama pale tu wanapomaliza kutoa huduma. Naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kusema sisi Wabunge ni sehemu ya kusimamia Utawala Bora na siyo kuwa kichocheo cha kuvunja amani katika nchi yetu. Suala la amani ni kitu muhimu sana na tuwe tayari kuilinda amani ya nchi kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kirefu hiki tumeona uvunjifu wa amani unachochewa na baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Siasa, kama vile mgogoro wa wanafunzi na mgogoro wa madaktari. Kwa hiyo, naishauri sasa Serikali ibadilike, isiwe inavilea Vyama hivi au Viongozi hao wa Sheria, naomba sheria ichukue mkondo wake bila ya kujali Chama gani au Kiongozi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mabadiliko ya Katiba; Kwanza, natoa pongezi, Wajumbe wa Tume ni watu wenye uwezo na wenye sifa za kuwa Wajumbe wa Tume. Mwenyekiti wa Tume, Mheshimiwa Warioba ni mtu makini na naamini ataiongoza Tume hii kwa ufanisi mzuri. Kitu

ninachokiona ni muda mdogo huu wa kukusanya maoni na sifikirii kuwa kwa muda huu uliowekwa, Tume itamaliza kufanya kazi yake. Naishauri Serikali iongeze watu wanaopita kuchukua maoni na wafanye kazi mpaka Jumamosi na Jumapili, kuanzia asubuhi hadi angalau saa mbili za usiku, kwani suala la kuongeza muda zaidi ya tarehe 26 Aprili, 2014 halitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo ya wananchi wote kuwa mabadiliko haya yafanyike pamoja na maoni ya kubadilisha Tume ya Uchaguzi na mchakato mzima wa Uchaguzi wa Mwaka 2015.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza kwa kumpongeza Waziri na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa kuiandaa bajeti hii na hatimaye leo hii kuletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwa leo ni kuiomba Serikali iiongezee fedha Wizara hii na pia kuzipata zote tena kwa wakati ili kufanikisha yale yote yaliyopangwa kufanyika katika kipindi hiki cha mwaka wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu makubwa ya Wizara hii na Taasisi zake, Serikali inalazimika kabisa kuhakikisha Wizara hii inaipa Mahakama bajeti yake ili itekeleze majukumu yake hasa kutatua masuala ya kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia malalamiko au madai ya Waislamu wa Tanzania juu ya Mahakama ya Kadhi ni jambo ambalo Serikali ni lazima walichukulie kuwa ni muhimu na la lazima katika kutekeleza masharti muhimu kwa imani yao hasa kwenye mambo ya mirathi, ndoa na talaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHADHI JUMA MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Napenda kuipongeza Wizara na Taasisi zake, kwa kuendelea na mageuzi na maboresho yenye lengo la kuimarisha utendaji kazi na utolewaji wa haki. Pongezi za pekee kwa Waziri na Serikali, kwa kupitisha Sheria na kwa kuanza utekelezaji wa Sheria hiyo yenye kuunda Kada Maalum ya Watawala wa Mahakama.

Kwa muda mrefu uendeshaji wa Mahakama Kiutawala ulikuwa chini ya Majaji na Wasajili (*Registrars*), walilazimika kufuata maelekezo ya Majaji. Mfumo huo ulidumaza utendaji kazi wa Mahakama, kwa kiasi kikubwa ni mfumo huo ndiyo uliokwamisha maboresho ya Mahakama. Kwa mfano, licha ya fedha kutolewa na wafadhili chini ya *Legal Sector Roform,* bado ujenzi wa Mahakama ya Rufaa umeshindikana; hali hii haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kutambua kazi nzuri inayoendelea kufanywa na Wakala wa Usajli, Ufilisi na Udhamini katika kuandikisha na kutoa vyeti kwa Watanzania hasa watoto wadogo. Suala la watoto kusajiliwa ni miongoni mwa haki za msingi za mtoto na ni suala lenye uhusiano wa karibu na uraia wa watoto hao.

Kwa bahati mbaya, kiwango chetu bado hakiridhishi na watoto wengi wanaendelea kukosa kusajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa. Hali hii husababisha usumbufu mkubwa kwa watoto hao na wazee wao baadaye katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Wizara ikalisimamia suala hili kwa umakini zaidi na ikibidi jukumu hili maalum likatolewa *RITA* na kuwa na Taasisi Maalum ya kushughulikia uandikishaji wa vizazi na vifo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuandaa Hotuba nzuri. Naiomba Wizara iandae mkakati wa kumaliza mrundikano wa kesi Mahakamani katika ngazi zote kuanzia Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama za Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, naiomba Wizara isimamie upatikanaji wa nakala za hukumu ili kuwapa raia haki yao kukata rufaa na kupata haki kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi yahamishiwe yawe chini ya Wizara ya Katiba na Sheria badala ya utaratibu wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kuratibu Ukusanyaji wa Maoni ya Mabadiliko ya Katiba ihakikishe kuwa ina rasilimali za kutosha na ifike kwenye kila Kijiji Tanzania kuwa na muda wa kutosha kuwasikiliza Watanzania.

Baraza la Ardhi Wilaya ya Simanjiro lisikilize kesi za ardhi kutoka Kiteto kwani zaidi ya asilimia 80 ya kesi zinazosikilizwa Wilayani Simanjiro zinatoka Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shughuli ya kutenga mashtaka na upelelezi isimamiwe na itekelezwe katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wazee wa Mahakama watazamwe kwa karibu zaidi na wao pia wafanyiwe *training* ili wajue nafasi zao na kuongeza ufanisi.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iiboreshe Mahakama ya Wilaya ya Meatu, pia iongeze au kufungua Mahakama zaidi kwenye Kata ambazo hazina Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mahakama za Mwanzo sita tu kati ya Kata 26 za Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuipongeza Wizara hii ya Sheria na Katiba, kwa kazi nzuri wanayoifanya ikiwemo kazi kubwa ya Mabadiliko ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kwa kuwa mchakato huu umeshaanza na unaendelea katika Mkoa wa Dodoma,

kwa sasa ni imani yangu kuwa kila mwananchi mwenye nia ya kutoa au kuwasilisha moni yake kupitia Tume hiyo, atapata nafasi kadiri eneo alipo litakavyofikiwa na Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kuhusu makazi ya Mahakimu. Suala hili limekuwa tatizo la muda mrefu sasa na imekuwa kero kwa Mahakimu wenyewe na kwa raia pia. Nasema hivi kwa sababu zifuatazo:-

Mfano, Hakimu anatakiwa kutoa hukumu kwa raia na hukumu hiyo ni ya kifungo au faini au vyote viwili na raia huyo ni *landlord* wa hakimu. Je, baada ya hukumu hiyo Hakimu atakuwa na amani ya kuishi kweli au mwenye nyumba atamwacha Hakimu aendelee kuishi kwenye nyumba yake? Hata kama hatafukuzwa kwenye nyumba hiyo; je, atakuwa na amani ya kutosha ya kuishi hapo?

Ombi langu kwa Serikali ni Mahakimu wapatiwe nyumba za kuishi ili kuondokana na kero hii na kufanya kazi yao iwe nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Polisi na usafiri wa kuwapeleka mahabusu Mahakamani. Hii imekuwa kero ya muda mrefu kwani limekuwa likitumika gari moja tu kwa ajili ya kuwachukua mahabusu kutoka mahakamani na kuwarudisha na hivyo kusababisha ucheleweshwaji wa kesi kwa muda mrefu sana. Mfano wa hili ni Mkoa wa Kilimanjaro, ambao umekuwa na gari moja tu la kubebea mahabusu kuwapeleka Mahakamani. Hili ni tatizo kubwa na mfano ikitokea Mahakamani hata kama kesi ya mtuhumiwa ilipaswa kusomwa siku hiyo, rai yangu ni kuwa,

jambo la ziada lifanyike ili hali hii iweze kudhibitiwa kwani inawatesa sana mahabusu, Mahakimu na hata ndugu wa watuhumiwa hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana pia na ufinyu mdogo wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara hii ya Katiba na Sheria. Kwa mfano, bajeti iliyopita ya mwaka 2011/2012, ilitengwa kidogo na haikufika yote katika Wizara na hivyo kuendelea kuitesa Wizara hii katika kufanikisha majukumu yake ikiwemo kukarabati majengo, Ofisi za Mahakama mbalimbali za mwanzo na Mahakama Kuu. Mfano wa Mahakama ya Mwanzo ya Herolosi ya Wilaya ya Arusha Mjini imekuwa mbaya sana na kwa kuwa Mkoa wa Arusha una hali ya mvua na baridi, hii imesababisha hata kuharibika kwa mafaili kutokana na mvua na vumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie sana suala la kupeleka hela kwa wakati katika Wizara hii, tofauti na ilivyokuwa mwaka wa fedha uliopita. Fedha hazifiki zote na hata hizo zilizofika zilifika kwa awamu tofauti au kwa lugha nyingine kwa mafungu mafungu na kusababisha Wizara kutotimiza matakwa yake vizuri kama ilivyojipangia.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambayo inafanya kufikisha, kuharakisha na kurahisisha upatikanaji wa haki nchini. Uamuzi wa kuteua *Administrator* wa Mahakama ni wa busara. Kiongozi huyu na Ofisi yake wawezeshwe kutimiza majukumu yao hasa ikizingatiwa kwamba ni utaratibu mpya ambao unaweza kuwa *resisted* na Majaji, Mahakimu na Watumishi wengine wa Mahakama waliozoea utaratibu wa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hatua ya Wizara kuamua kutumia *ICT* kwenye masuala ya Utawala wa Mahakama na utoaji haki. Napendekeza Wizara hii iwasiliane na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa ajili ya ushauri wa kitaalamu ili kupunguza gharama za mifumo hii. Tayari Mkongo wa Taifa umefika kila Wilaya. Kama Wizara na Mahakama wasipokuwa waangalifu, wanaweza kuingizwa kwenye manunuzi ya ghali ya kutumia *(V-SAT)* kwa *connectivity* pasipo lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia (Serikali) imenunua *bandwith* kubwa ambayo tunaweza kutazama namna ya kusaidia sehemu kidogo ya *bandwith* hii kwa ajili ya matumizi ya Mpango huu wa *ICT* wa Wizara na Mahakama. Pia itazame umuhimu wa *Synergies* na *Complementaries* kati ya *NIDA* na *RITA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa *Criminal Bench* ni muhimu sana *resources* zitengwe kwa ajili hiyo. Rushwa kwenye Mahakama bado ni jambo linalolalamikiwa sana. Mlolongo mrefu wa udhibiti wa nidhamu ya Majaji na Mahakimu utazamwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mradi wa *Digitalization* ya kesi na majalada uharakishwe. Kadhalika na *Commercial Justice* ni muhimu iwe imara ili kujenga *confidence* ya nchi kama *investment desination*, lakini pia kupunguza *risk* ya kufanya biashara nchini.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama zinafanya kazi katika mazingira duni sana hasa zile za Mwanzo. Vitendea kazi bado duni sana na vilevile bado Mahakama zetu zinarekodi mashauri kwa kuandika;

ni vyema ili kuepuka kukosea, utaratibu wa matumizi ya *Hansard* katika mahakama zote, yaani ya ngazi zote kuanzia Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama Kuu utumike. Serikali itafute fedha kwa ajili ya *Hansard* ili kazi za Mahakama ziwe rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama zetu zina mrundikano wa kesi uliokithiri. Wananchi wanalalamikia ucheleweshwaji wa kesi zao; kesi nyingi huchukua zaidi ya miaka mitano matokeo yake mahabusu hurundikana ndani ya magereza zetu wakati hazina uwezo wa kuwahifadhi kwani magereza nyingi nchini hazina uwezo hata wa kuwalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kufahamu kama mtuhumiwa atakaa gerezani (Mahabusu) kwa zaidi ya mwaka hadi miaka mitano na kuendelea na mwisho wa siku aonekane hana hatia; je, Serikali itampa fidia kwa kumpotezea muda wake kwani siyo kosa la mtuhumiwa kuchelewesha kesi? Serikali itoe ufafanuzi juu ya jambo hili ambalo ni kero kwa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho ya mazingira ya kazi ya mahakama zetu, nashauri maboresho ya maisha ya Mahakimu pia yatazamwe; maeneo mengi nchini hakuna nyumba za Mahakimu, matokeo yake hulazimika kupanga. Haipendezi na hali hii inasababisha kumpa wakati mgumu Hakimu pale anapotakiwa kukata shauri la mwenye nyumba wake au mpangaji mwenzie.

Vilevile ni vyema Serikali ianglie umuhimu wa kuwakopesha vyombo vya usafiri. Mazingira ya kazi, makazi na usafiri yakiboreshwa, rushwa isiyo ya lazima itapungua,

ingawa wapo watendaji wenye vipato vizuri na mazingira mazuri wasio na maadili bado wanapokea rushwa. Hili ni suala la kimaadili zaidi, ingawa wapo watumishi wenye maadili wakiwemo Mahakimu, lakini kutokana na uduni wa maisha, wanashawishika kupokea rushwa, tuwaboreshee maisha ili wasitetereke kimaadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usimamizi wa Haki za Binadamu na Utawala Bora bado halisimamiwi vizuri. Haki za Binadamu zinavunjwa mno, wananchi wanabambikizwa kesi hovyo, Vyombo vya Dola ikiwemo Polisi wamehusika kuvunja haki za binadamu kwa kiwango kikubwa ikiwemo hiyo kero ya kubambikiza wananchi kesi pindi inapotokea kutokuwepo maelewano baina ya Polisi na baadhi ya wananchi na mambo mengine mengi yanaainishwa katika Ripoti (Vitabu) mbalimbali vya Haki za Binadamu zilizotolewa na Tume ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri elimu iendelee kutolewa ili wananchi watambue haki zao. Vilevile ni haki ya wananchi kuelewa Sheria zetu; hivyo, Sheria zetu zitafsiriwe ili zieleweke.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napeda kumshukuru Mwenyezi Mungu, muweza wa yote ulimwenguni. Naanza mchango wangu kwa Wizara hii kutokana na umuhimu wa masuala ya kisheria katika nchi yetu na kwa kuwa wananchi walio wengi hawajui chochote kuhusu Sheria kiasi kwamba hawajui hata haki zao za msingi kwa kutojua sheria, naishauri Serikali kuanzisha Somo la Sheria katika Shule zote za Sekondari nchini na liwe na Mkakati Maalum ili wanafunzi

wanapomaliza angalu wawe na ufahamu wa mambo ya kisheria. Hii itapunguza hata vitendo vya uvunjaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali irudishe mashuleni Somo la Ufundishaji wa Katiba ya nchi (Katiba ya Jamhuri ya Muungano); hii itasaidia watu walio wengi kuifahamu Katiba ya nchi yao kinyume na hali halisi iliyopo sasa kwamba, watu wanadai Katiba Mpya wakati hii kongwe iliyopo haijulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa Majaji katika nchi yetu umekuwa ni tatizo sugu, kwa sababu tu bajeti ni finyu ya kusomesha Majaji. Naiomba Serikali iiongezee bajeti ya kutosha Wizara hii iweze kuwasomesha Majaji wa kutosha. Hii itapunguza uhaba wa Mahakimu wa kila ngazi na kutoa fursa ya kesi kuendeshwa kwa haraka ili kupunguza msongamano wa mahabusu gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya vitendo vya rushwa juu ya Mahakama zetu na Majaji wetu ni jambo linalolalamikiwa sana na wananchi wengi nchini mwetu. Naiomba Serikali iwaangalie Majaji wetu katika stahili zao zote na kuwainua kimaslahi ili waepukane na vishawishi vya kupokea rushwa. Hii itaipa heshima Taasisi yetu hii muhimu na wananchi watajenga imani na Chombo chao hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafungwa, nashauri Serikali kwa wale wafungwa waliohukumiwa adhabu za muda mfupi na Serikali ikaridhika na mwenendo na tabia zao nzuri na wafungwa hao wakaonesha uaminifu katika kutumikia vifungo vyao, Serikali iwaruhusu wafungwa hao kutumikia vifungo vyao nje ya magereza; hii itaipunguzia

Serikali mzigo wa kuwatunza wafungwa hao lakini pia itapunguza wingi au msongamano katika magereza.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni fursa adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa neema yake kubwa ya uhai na uzima.

Nianze na Mahakama ya Kadhi, Waislamu wamekuwa na kilio cha siku nyingi kuomba Mahakama ya Kadhi kwa zile kesi ambazo zinawahusu wao wenyewe; mfano, ndoa, talaka na mirathi. Mimi naipongeza Serikali kwa kuonesha nia ya dhati kukubali kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi. Kwa kuwa Serikali imekubali kuanzishwa Mahakama hii, lakini gharama zote za uendeshaji zitakuwa ni kwa Waislamu wenyewe, kwa maana hiyo, Serikali haitahusika na gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nahisi Waislamu hawajatendewa haki kwa sababu na wao ni watozwa kodi wa nchi hii. Naomba Serikali iangalie nchi nyingi Duniani ambazo zina mfumo kama huu; mfano, Zanzibar, Kenya, India, Uingereza na nyingine; Serikali zao zinawajibika kuendesha gharama za Mahakama za Kadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali hii sikivu ya Chama cha Mapinduzi, iige Serikali ambazo zinagharamia Mahakama hizi za Kadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magereza yetu yanakiuka haki za binadamu. Wafungwa wengi, yaani idadi kubwa wanarundikwa vyumba vidogo sana, wanalala chini katika magodoro machafu na wengine hata magodoro

hawapati, wanaenda haja katika ndoo moja katika chumba hicho hicho wanacholala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku si kukiuka haki za binadamu tu, bali pia ni hatari kwa afya zao. Kama hii ni sahihi, nashauri Serikali ikubali kugharamika kujenga Magereza makubwa ya Kisasa, ambayo yatakidhi haja kwa wafungwa na kuondoa usumbufu wanaoupata. Wafungwa ni binadamu isipokuwa wameingia hatiani kwa makosa ambapo binadamu yeyote yanaweza kumtokea.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikiliza michango katika hoja kama Mheshimiwa Naibu Spika alivyotoa mwongozo hapo asubuhi, kwa kweli tunakimbizana na muda na ni lazima hoja hii leo tuihitimishe. Kwa hiyo, bila kupoteza muda, naomba nimwite mtoa hoja lakini kwa kuanzia na watu wanaoambatana naye. Tutaanza kumpa nafasi Mheshimiwa *AG,* atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri na baadaye atamalizia Waziri mwenyewe. Kwa hiyo, naomba *AG* nikupe dakika kumi na baada ya hapo Mheshimiwa Naibu Waziri na baadaye tutampa nafasi Mheshimiwa Waziri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini kama ilivyo ada nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia na wazazi wangu, Walimu wangu walionifundisha kuanzia darasa la kwanza na watu wote ambao walishawahi kukaa na mimi zaidi ya dakika moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao wajibu kama Mwanasheria kwenye taaluma yangu, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali nina wajibu kwa Mawakili na taaluma ya sheria lakini pia ninapaswa kuwaelekeza Mawakili popote walipo na hasa Mawakili walioko humu Bungeni kufuata misingi yetu ya taaluma bila kuathiri haki yao kama Wabunge. Kwa ajili hiyo, nimefedheheka sana na mambo mawili ambayo yametokea Bungeni hivi leo na ninaomba kusema maneno machache kutokana na mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ni hotuba ya ndugu yangu, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Wizara hii ya Katiba na Sheria na baada ya kuwa amezungumza, nilizungumza naye nikimwomba aondoe maneno aliyoweka kwenye hotuba yake kuhusiana na mambo ya Mahakama hasa kuhusiana na Majaji kwamba hawana uwezo. Katika ukurasa wa 9 wa hotuba ya Mheshimiwa huyu, Ibara ya pili, kuna maneno pale *paragraph* ya pili kwamba:-

*"Kwa mujibu wa taarifa tulizonazo sasa watu wanateuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ambao hawajawahi kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na kwa sababu hiyo hawajafanyiwa veting yoyote na Mamlaka hiyo ya Kikatiba".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Tundu Lissu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani aondoe maneno hayo. Vinginevyo nikuombe wewe kama Mwenyekiti unayesimamia Kanuni zetu, uamuru taarifa zilizotajwa katika *paragraph* hiyo ziambatanishwe na hotuba yake. Nafahamu Mheshimiwa Tundu ni mtaalam wa sheria au

*Esquire* na kama ni hivyo ni Ofisa wa Mahakama anayepaswa kutofedhehesha Mahakama na Majaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwa Kanuni zetu za Bunge, haturuhusiwi ku-*deal* na *"strangers", "strangers"* ni watu ambao siyo Wabunge, watu ambao hawapo humu ndani. Sasa ndugu yangu, ninasema kwa sauti ya upole kwa sababu ndiyo madhara ya kuwa Mwanasheria Mkuu. Amezungumza, amewataja watu wengine ukurasa wa 18 ambao siyo Wabunge na kwa kuwataja watu hawa anasema kwamba kuna habari zimechapishwa kwenye gazeti la Mwanahalisi na analitaja na anataja watu. Taarifa hizo ni kinyume na Kanuni yetu ya 64(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli lakini pia hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala, lakini pia hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahsusi kuhusu jambo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba baadaye Mheshimiwa Tundu Lissu aondoe maneno hayo, la sivyo nitakuomba uamuru kwamba yaondoke na baada ya kuondoka twende kwenye Kamati ya Maadili na Haki za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tundu Lissu pia amezungumzia kuhusu Mahakama kudharauliwa kwa msingi kwamba marekebisho katika kifungu cha 108 (5) hayafuatwi.

*(Hapa Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu alisimama ili Kiti kimsikilize)*

**MWENYEKITI:** Jicho langu bado halijakuona, naomba Mwanasheria Mkuu amalize kwanza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nafikiri hayo ni mambo ya uzushi kwa sababu jambo hilo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekata rufaa na jambo hilo bado liko Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kutekwa, suala la kupigwa Kiwia, suala la Said Kubenea, suala la Harrison Mwakyembe, suala la uendeshaji masuala ya jinai na ubambikizaji, mengi ya mambo aliyoyasema ni uzushi na siyo kweli kwamba Serikali inahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni kuhusu takwimu, ndugu yangu Mheshimiwa Juma Ngwali unachosema Mheshimiwa siyo sharia. Mimi nashauri kwamba Waheshimiwa Wabunge wengine muwe mnatafuta ushauri, nina maafisa wangu ambao wanasaidia kila Mbunge bila kujali chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kinachohusika kuhusu takwimu ni kifungu cha 15, shabaha ya kufanya takwimu hii siyo kutoa huduma za kiroho. Huduma za kiroho toeni huko Misikitini na Makanisani, shabaha ya takwimu hii ni kuwapatia watu huduma zinazostahili. Ukisoma kifungu cha 15, kinasema nitasoma kwa Kiingereza, nadhani mnafahamu na naomba mwende mkasome vizuri badala ya kukimbilia huku Bungeni. Kifungu cha 15 kinasema:-

*“The Bureau may, collect statistics relating to all or any of the matters specified in the Second Schedule”.* Hii uliyokuwa unazungumzia sasa ndivyo inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 17 kinasema na nitasoma kwa Kiingereza, takwimu ni *sampling,* kinasema:-

*“Statistics relating to all or any of the matter set out in the Second Schedule may be collected by sampling, in place of a full enumeration, where the use of that method is considered appropriate”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi hatutoi huduma za kiroho wewe. Wewe kama unataka kufanya huduma za kiroho fanya sensa yako. Haya mambo ya kusimama hapa na kudanganya watu nafikiri ni utovu wa uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwie radhi kwa maneno ninayotumia wakati mwingine, nimalizie na hili la Mheshimiwa Harrison Mwakyembe. Mheshimiwa Mwakyembe alishasema tuache na tuheshimu maneno yake. Yeye alisema muache yametosha, sasa mnataka kitu gani tena?

*(Hapa Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa akiongea kuonyesha kutokubaliana na maelezo ya Mwanasheria Mkuu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Tundu Lissu nafikiri hufahamu kuwa kuna Kamati ya Maadili, nafikiri tutakwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Yako mambo mengi ya kuzungumza lakini niishie hapo, niwaachie Waheshimiwa Mawaziri.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Haya sijui Mwongozo au Taarifa, Mheshimiwa Said.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Ibara ya 68(7), naomba nisome kwa ridhaa yako.

*"Halikadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambako hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukumbi huu umejengwa na mali za Watanzania, gharama yake ni kubwa sana. Sidhani kwa namna tulivyo humu ndani na tunavyoheshimika kama tunaweza kwa muda mfupi kuharibu mali za Watanzania. Pale anapokaa Mheshimiwa Tundu Lissu amebomoa kwa kupiga makofi kana kwamba anatumia miguu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ameamua sasa baada ya kuharibu pale, amehamia eneo linguine. Nataka nipate mwongozo wako kama mambo haya yanaruhusiwa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Mwenyekiti wa Bunge, mwongozo umeombwa wewe.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo huna hoja, basi tuendelee, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema hadi nimefika siku ya leo ambapo Wizara yetu imewasilisha katika Bunge lako Tukufu Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na napenda pia mbele ya hadhara hii na wananchi wote kwa ujumla kumuahidi kwamba nitatekeleza majukumu yangu yote kwa bidii, uadilifu, umakini na uweledi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria kwa ushirikiano mkubwa na mwongozo anaonipatia kila siku katika kutekeleza majukumu yangu kama Naibu Waziri. Namuahidi kuendelea kumpa ushirikiano wa dhati kabisa katika kutekeleza majukumu ya Wizara kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii pia, kuwashukuru wafanyakazi wote na watendaji wote wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Taifa (TUCTA) na ninapenda kuwahakikishia kwamba niko pamoja nao na

nitaendelea kuwawakilisha vyema Bungeni na katika sehemu mbalimbali. Napenda pia kuwashukuru UWT Dar es salaam pamoja na Baraza Kuu la UWT Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru mume wangu mpenzi, Balozi Mbelwa Kairuki na familia yangu yote, kwa kunipa ushirikiano mkubwa na kwa uvumilivu wao mkubwa pindi ninapokuwa mbali nikitekeleza majukumu yangu ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna ambavyo wanaliongoza Bunge hili hususani kwa leo Mheshimiwa Jenista Mhagama wakati huu ambapo unaliongoza Bunge hili. Kwa umuhimu wa pekee, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa michango yao mbalimbali yenye kujenga ambayo imetolewa kuhusiana na hotuba yetu, tumeipokea michango hiyo na tunaahidi kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu niweze kuchangia kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na zilizojitokeza katika hotuba ya Wizara yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda nijikite katika Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi yaani *RITA*. Hoja mojawapo imetolewa na Mheshimiwa David Kafulila ambapo aliitaka Wakala ihakikishe kuwa Wilaya mpya ya Uvinza inapata usajili kwani kuna tatizo sugu la

vijana na watoto wengi ambao hawana vyeti vya kuzaliwa na wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa katika kupata huduma hiyo pamoja na elimu. Kwa niaba ya Serikali, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Kafulila kwamba Wakala wa *RITA* utahakikisha kwamba vifaa pamoja na mafunzo kwa watendaji wote wa Wilaya zote mpya yatafanyika ikiwemo pia Wilaya mpya ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine imetolewa na Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim, Mbunge wa Muyuni ambaye alizungumzia kiwango kidogo cha usajili kwa watoto walio chini ya miaka mitano kwamba ni kubwa mno na alitoa rai kuwa ni jukumu la *RITA* kuhakikisha kwamba inasajili vizazi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mahadhi kwamba, *RITA* inayo mikakati ya usajili wa watoto walio chini ya miaka mitano. Tunao pia Mpango ambao unajulikana kama *Under Five Birth Registration Initiative,* ambao kama ambavyo Waziri asubuhi hii wakati anasoma Hotuba yake alieleza kwamba, Mpango huo ulikuwa katika majaribio na majaribio haya yalianza katika Wilaya ya Temeke katika Kata 14 na umeisha leo hii. Tunatarajia kuanza awamu tatu za Mpango utakaodumu kwa miaka mitatu. Mpango ambao tutaanza na Mikoa mitano; Mkoa wa Simiyu, Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Geita, Mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Wabunge watajiuliza ni kwa nini tunaanza na Mikoa hii mitano, lakini kwa takwimu ambazo zimepatikana kutokana na *Tanzania Demographic and Health Survey* iliyofanyika nchini kwetu, hivi karibuni ilionesha kwamba ni mikoa hii mitano ndiyo ina takwimu za

chini kabisa katika usajili wa vizazi vya watoto wetu wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni ushauri kutoka kwa Mheshimiwa January Makamba, Mbunge wa Bumbuli, ambaye alishauri Wakala wa *NIDA* na *RITA* wafanye kazi kwa ushirikiano. Napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ushauri huu umepokelewa na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine kuhusiana na *RITA* ambayo imejitokeza na imechangiwa na Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Amina Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa John Lwanji na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ni kwamba, tujitahidi kusogeza huduma za usajili mpaka katika ngazi ya Kata pamoja na hospitali mbalimbali. Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o pia ameelezea kwamba, Wazazi mbalimbali wamekuwa wakitozwa hadi shilingi elfu kumi kupata cheti cha kuzaliwa kwa watoto walio chini ya miaka mitano. Napenda kuwahakikishia wananchi wote na kuwatamkia leo hii kwamba, gharama za kupata cheti cha kuzaliwa ni shilingi 3,500. Endapo unakuwa na tangazo la kizazi, ambalo unapatiwa ukijifungulia hospitalini, ndani ya siku tisini ukienda kusajili inakuwa ni bure. Unapokuwa umepoteza tangazo hili ndiyo gharama zinajitokeza. Kwa hiyo, endapo kuna mwananchi yeyote anatozwa shilingi elfu kumi au zaidi, hiyo ni batili na tungependa tupatiwe taarifa ili tuweze kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kuliambia Bunge lako kwamba, Serikali kupitia Wakala wa *RITA,* katika mwaka huu tunatarajia kupitia Mpango wa *Under Five Birth Registration Initiative* kushusha huduma hadi katika ngazi za chini kabisa; katika ngazi za Mtaa, katika ngazi za Kata na vile vile, baadaye ikiwezekana hata mtu anapozaliwa Hospitalini aweze kupata usajili wa kizazi chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia kuja na fomu za kujiandikisha kwa mkono halafu baadaye zikishawasilishwa ndiyo mtu atakuja kupatiwa cheti, lakini anaweza akatumia fomu ile ambayo ameandikiwa na muuguzi au aliyoipata katika ngazi ya Mtaa, Kata au Wilaya ili aweze kuitumia endapo kuna mahitaji maalum. Serikali kupitia Wakala wa *RITA,* tunao Mpango wa kwenda katika shule zetu ili kuweza kubaini watoto wote ambao waPo katika umri wa miaka 6 – 18, ambao bado hawajapata vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wameongelea pia elimu kwa umma itolewe kuhusiana na shughuli za Wakala wa *RITA*. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumepokea ushauri na tutaufanyia kazi. Hoja nyingine iliyojitokeza ambayo imetolewa na Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o, Mheshimiwa Amina Makilagi na Mheshimiwa Catherine Magige ni kuhusiana na sheria zilizopitwa na wakati kama vile Sheria ya Ndoa na Mirathi. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali haijakaa kimya, mwaka jana wakati Wizara hii inafanya majumuisho ya Bajeti yake kupitia Mheshimiwa Celina Kombani, tuliahidi kwamba, tutaanza mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi, yaani *White Paper.* Napenda kuwaambia kwamba, ushauri huu bado unafanyiwa kazi na bado upo katika hatua ya Serikali na

endapo hatua hizi zikikamilika basi Waraka utawasilishwa katika Baraza la Mawaziri na baadaye mchakato utaenda kwa wananchi ili watoe maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Mheshimiwa Lediana Mng'ongo amelizungumzia ni kuhusiana na ni lini tutaleta Sheria ya kuwatambua Mawakili Jamii au *Paralegals.* Kwanza kabisa, napenda kuwatambua *Paralegals* wote nchini, wanafanya kazi kubwa sana na wiki moja tu mara niliporipoti katika wadhifa wangu huu mpya, nilikaa na mtandao wa *Paralegals* wote nchini. Zipo *NGOs* zaidi ya 80 na tulikaa nao tukawaonesha andiko ambalo tumeliwasilisha katika Kamati ya Makatibu Wakuu na wao wameleta maoni yao na kwa kiasi kikubwa tutayazingatia ili tuweze kuboresha Waraka huo na baadaye kuandaa Muswada tutakaouwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niingie kwenye michango ya maandishi kama muda utaniruhusu. Kuhusiana na tatizo la upungufu wa Watumishi wenye sifa zinazotakiwa na maslahi duni katika Mahakama bado halijapatiwa ufumbuzi. Napenda kuwahakikishia kwamba, Serikali imetambua tatizo hili na ndiyo maana kupitia Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka jana na wote leo mmeelezwa kwamba, tumeshampata Mtendaji Mkuu wa Mahakama, kwa hiyo, kupitia Mfuko wa Mahakama tunaomba tu mtupitishie fedha za kutosha ili shughuli zote ziweze kufanyika kama ambavyo tumepanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wengine ambao waliongelea vitendo vya rushwa Mahakamani. Kwa kiasi kikubwa ipo Tume ya Utumishi wa Mahakama ambayo

ndiyo ina mamlaka ya kuangalia taratibu zote za nidhamu kwa ajili ya Majaji, Mahakimu na Watendaji wote waliopo katika Mahakama ambao siyo Mahakimu na wamekuwa wakikemea kwa kiasi kikubwa na kuchukua hatua mbalimbali kwa wale wote ambao wamekuwa wakikiuka maadili. Siku moja, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, aliwahi kusema katika kazi ambazo zinahitaji maadili makubwa kabisa ni kazi ya Uhakimu na Ujaji na endapo unaona huwezi kuwa na maadili hayo yanayohitajika, basi nadhani nyadhifa hizo hazikufai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Raya amelalamikia kwamba, ada za kufungua mashauri Mahakamani ni kubwa mno. Napenda kumweleza kwamba, tumelichukua na tutalifanyia kazi ili kuangalia ni kwa namna gani tunaweza tukaboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa, Wabunge wengi wameongelea ukosefu wa majengo ya Mahakama. Mheshimiwa Waziri leo hii ameeleza kwamba, mwaka huu tutajenga takriban Mahakama saba za Mwanzo. Tumeeleza tutajenga Mahakama ya Kawe, Mahakama ya Bunda, Mahakama ya Mangaka, Mahakama ya Gairo, Mahakama ya Bariadi, Mahakama ya Lukuledi na Mahakama ya Mkomazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukifanya hivi kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini kila mara bajeti ikiruhusu tutakuwa tunajitahidi kuongeza idadi kubwa ya ujenzi wa Mahakama. Pia tunaangalia uwezekano, ikiwezekana tushirikiane na Wizara ya Fedha, tuone ni kwa namna gani tunaweza kupata hata mkopo wa Serikali ili tuweze kujenga Mahakama zote ambazo zipo katika hali chakavu. Vilevile

tuweze kuwapatia huduma ya Mahakama wananchi wote ambao wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma ya Mahakama, kwani tunaamini kwamba, huduma ya Mahakama ni muhimu kama ilivyo huduma ya maji, huduma ya shule na huduma ya afya.

Mheshimiwa Josephat Kandege, ameelezea ukosefu wa Mahakama ya Mwanzo Kalambo na Mahakama ya Wilaya ya Kalambo. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya, kupitia Mkoa wake wamejitolea kujenga Mahakama mbili za Wilaya; Mahakama ya Wilaya ya Nkasi na Mahakama ya Wilaya la Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana. Kuna Wabunge wawili hapa wameniandikia kuniuliza kwa nini sijampa nafasi Mheshimiwa Tundu Lissu kuzungumza, aliomba mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu Na. 60, Kanuni ndogo ya (b) inasema; Mbunge akitaka kusema anaweza kusimama kimya mahali pake au kutumia *alternatives* mbili ambazo sisi humu ndani hatuna, akishasimama mahali pake Spika akishamwona ndiyo atampa ruhusa ya kuzungumza.

Waheshimiwa Wabunge, walisimama Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Tundu Lissu na jicho la Spika liliwaona hawa watu wawili, kwa hiyo, nikampa ruhusa Mheshimiwa Said Nkumba akasema mwongozo alioutaka

Kiti kitoe ufafanuzi, alipomaliza nikampa nafasi Mheshimiwa Tundu Lissu naye aseme kile alichotaka kusema wakati amesimama kwa mujibu wa Kanuni, lakini nasikitika sana, badala ya kusema kile alichotaka kuniambia, akaanza tena kukishutumu Kiti kwamba, mimi ndiyo natakiwa kumjibu Mheshimiwa Said Nkumba. Kwa hiyo, kabla hata sijamwelekeza nini anachotakiwa kufanya yeye akaanza kukishutumu Kiti kwa nini kinataka yeye ajibu, kitu ambacho sicho. Mimi nilikuwa naendelea na utaratibu wa Kikanuni wa kuwapa nafasi wale jicho la Spika lililowaona ili waweze kusema yale wanayotaka kuyasema ya kimwongozo ndani ya Bunge.

Kwa hiyo, naomba tu wale Wabunge ambao wameanza kuandika hapa na kuniuliza, hiki ndicho nilichokifanya. Niliwapa nafasi wale wote ambao nilikuwa nimewaona, lakini bahati mbaya sana tulishindwa kuelewana na Mheshimiwa Tundu Lissu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Waziri aweze kuhitimisha hoja yake. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nihitimishe hoja ambayo niliiwasilisha leo asubuhi ndani ya Bunge lako Tukufu. Kabla sijahitimisha hoja hiyo, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuendesha vizuri mjadala huu mpaka hapa tulipofikia. Naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja yangu kwa michango yao mizuri. Nataka niwahakikishie na kuwaahidi kwamba, michango hiyo nimeichukua yote, mimi na timu yangu tutakwenda kuifanyia kazi na kulingana na uwezo wetu tutayatekeleza yale ambayo tutaweza

kuyatekeleza. Nitashukuru kama mtaanza kuyapitisha haya niliyoyaomba ili tukayatekeleze haya na yale ya kwenu basi tutayazingatia kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru pia Mheshimiwa Jaji Fredrick Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Angellah Kairuki, kwa ushirikiano wao mkubwa sana wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Hawa wamekuwa wapo karibu nami sana na wamekuwa wakinisaidia na kunipa ushauri mara kwa mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizopo chini yake, kwa kuandaa vyema bajeti hii na ninaomba waendelee na umoja huu na ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao na majukumu yote tuliyopewa na Rais kwa weledi na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kuwa, Waheshimiwa Wabunge ni Wawakilishi wa Wananchi; ni wazi kuwa yote waliyoyasema ni kwa niaba ya wananchi wanaowawakilisha. Nia ya Wabunge wote na wananchi ni kuona kuwa nchi yetu inaendeshwa kwa misingi ya sheria zilizowekwa. Haki za Binadamu zinaheshimiwa na kulindwa na haki inapatikana bila upendeleo na kwa wakati. Hiyo ndiyo misingi ambayo na sisi tunaiamini katika Wizara yetu. Ndiyo hasa dhima ya Wizara hii kutoa haki sawa na kwa wakati kwa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea michango yote ya Wabunge na tumefarijika kupata maoni na ushauri wa jinsi ya kuboresha Sekta yetu ya Sheria na kwa niaba ya Wizara, naomba kuahidi kuwa tutashughulikia michango yote kwa umakini na kuwapa majibu sahihi na ambayo pia ni stahiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo kuhusu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge, ni vyema niwatambue waliochangia ambao wapo katika makundi makubwa mawili: Kwanza, wapo waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni na kundi la pili ni wale waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe, Mheshimiwa Deogratius A. Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mbunge wa Musoma, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Rita E. Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mbunge wa Amani, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Eustuce O. Katagira, Mbunge wa Kyerwa, Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla,

Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Suleiman S. Jafo, Mbunge wa Kisarawe na Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Lucy P. Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Nagu, Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim, Mbunge wa Muyuni, Mheshimiwa Benedict N. Ole Nangoro, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Meshack J. Opolukwa, Mbunge wa Meatu, Mheshimiwa Joyce J. Mukya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa January Y. Makamba, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Viti Maalum…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hao ni Wabunge wa Viti Maalum, ukisema maalum, kidogo itatupa utatanishi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inafanana na maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani Kusini Pemba, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mbunge wa Mbulu, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, Mheshimiwa Cecilia D. Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Charles J. P. Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Lolesia J. Bukwimba, Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mbunge wa

Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mbunge wa Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Selemani S. Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Subira K. Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Janet Z. Mbene, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mbunge wa Mfenesini, Mheshimiwa Kapt. Mstaafu John Z. Chilligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki na Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimewataja wote ambao wamechangia kwa maandishi, kama kuna niliyemsahau basi nitafurahi kupata jina lake ili naye nimtambue vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge ni pamoja na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mbunge wa Mbulu, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar,

Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mbunge wa Mkenge, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Jaji Fredrick M. Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Angellah J. Kairuki, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia. Kimsingi, mmetoa michango mizuri sana, yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa majukumu katika Wizara yangu. Hii inaonesha ni kwa namna gani Waheshimiwa Wabunge mko tayari kutoa michango yenu ya kimawazo kwa minajiri ya kuiendeleza Sekta hii muhimu ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa ni mingi na ni wazi kuwa kwa muda huu tulionao si rahisi kutoa maelezo ya kujibu kila hoja iliyotolewa. Nieleze tu kuwa, michango yote iliyotolewa tunaithamini sana na tunaifanyia kazi kikamilifu. Kama ilivyo kawaida, tutawaandalia majibu ya hoja zote kwa kina na tutawasambazia kabrasha lenye majibu ya hoja zenu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni vyema nikaanza kujibu hoja za jumla ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa la kwanza ambalo limezungumzwa na wengi ni suala la Tume ya Katiba na limezungumzwa kwa hisia tofauti na kwa *angle* tofauti.

Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, amelizungumza kwa mtazamo wake na Kambi yake, amedhani Tume ina gharama sana. Kuna waliochangia pia wakaona Tume inahitaji ipewe fedha nyingi zaidi kwa sababu ya umuhimu na uzito wa kazi ambayo inaifanya. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema limetazamwa kwa mtazamo tofauti na wachangiaji mbalimbali. *(Makofi)*

Sasa niseme maneno yafuatayo kuhusu Tume ya Katiba, Tume ya Kuandika Katiba Mpya ni sisi ndiyo tulitungia sheria. Tume ile inafanya kazi kwa utaratibu wa Sheria. Haifanyi kazi kwa kujipangia wenyewe kitu gani wafanye, ni sheria ambayo tulitunga sisi Bunge hili kwa kuona umuhimu wa kufanya jambo hili, kuleta Katiba Mpya. Tukatunga sheria tukasema Tume iwe hivi, tukaipa majukumu katika ibara kadhaa ya Sheria ile ifanye vitu gani. Tume hizi hazifanyi kazi ndogo, Tume hii inafanya kazi baada ya miaka 50, sijui kama itafanya tena kazi itateuliwa Tume nyingine katika miaka 50 ijayo au miaka 20 au miaka 30 ijayo. Niseme kwa zile takwimu ambazo Mheshimiwa wa Kambi Rasmi ya Upinzani amezisema eti Tume inapata shilingi 200,000 kila Mjumbe kwa siku na kadhalika. Niseme zimekuwepo Tume nyingi sana katika nchi hii, imekuwepo Tume ya Mheshimiwa Jaji Warioba, ilikuwa inaangalia masuala ya rushwa, mwaka 2006/2007, ilikuwepo Tume nyingine ya Jaji Bomani, hizi zilikuwa zinapata shilingi 220,000.

Enzi hizo na *inflation* ya sasa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi Rasmi mnaijua; shilingi 200,000 ni nini kwa kazi nzito kama hii ambayo nchi yetu ina-*undertake* katika muda ambapo pengine hatutafanya tena kama tukiandika

Katiba nzuri na nina hakika tutaandika Katiba nzuri hatutafanya tena kazi hii! Shilingi 200,000 ni nini? *(Makofi)*

Kwa mtu aliyeacha shughuli zake zote pamoja na kwamba Tume hii watu waliopata wanapata heshima kubwa, lakini pia na watu wenyewe wanazo heshima kubwa ndiyo maana wameingia mle. Kama wasingekuwa na heshima kubwa wasingeingia mle.  Wameanza kuwa na heshima kubwa ndiyo maana wakaingia mle. Sasa huwezi ukawapeleka pale ukawaambia ninyi hatuwalipi kwa sababu kwa kuingia tu ndani ya Tume hii tunawapa heshima kubwa. Watakwambia heshima tunayo kubwa toka mwanzo kabla hatujaingia ndani ya Tume. Kwa hiyo, hawa ni watu ambao wameacha shughuli nyingi; wapo wafanyabiashara, wapo viongozi wakubwa wamekwenda katika Tume ile. Najaribu kufikiria tu, kwa mfano, ukimchukua Mheshimiwa Salim Ahmed Salim ukampeleka akatazame mgogoro mahali kule; 200,000 ni nini kwake? Kwa heshima hiyo na kwa kuipenda nchi yake na uzalendo mkubwa yeye na wengine, Wajumbe wale wamekubali kuingia katika Tume hii. Sasa hivi wapo vijijini, vijiji vya ndani kabisa alikuwa ananiambia dada yangu pale Mheshimiwa Rwamlaza, zile Kata amezitaja mimi kuzitamka nitashindwa ni huko ndani kabisa wapo viongozi hawa wanafanya kazi ya kukusanya maoni ya wananchi. Kazi hii ni kubwa si ndogo. (*Makofi*)

Niseme katika kazi kama hii tuweke kwanza matokeo ya hiyo kazi siyo fedha. Shughuli ya demokrasia ina gharama kubwa sana, ninyi mnajua. Tukifanya tu uchaguzi katika nchi hii ni mabilioni na uchaguzi ni lazima tufanye na tusipofanya shughuli haieleweki, tunaambiwa hatuna utawala bora na kadhalika.

Kwa hiyo, naomba mkubali kwamba, pamoja na kwamba sikusudii maana hivi viposho posho hivi ni sawa na mishahara yenu Waheshimiwa Wabunge, mnapenda itangazwe kila siku kwenye radio? Wala siyo haki, hata mshahara wangu mimi sipendi utangazwe, siyo sawa, ni kati yangu mimi na mwajiri. Mwajiri ameniajiri tumekubaliana atanilipa nini. Sasa leo mnataka nisimame hapa niseme fulani shilingi fulani, si sahihi. Kwa hiyo, nasema tukubali Tume hii itatufanyia kazi nzuri na sisi sote tumeshiriki na tutaendelea kushiriki. Niwashauri vile vile kwamba, Tume hii sasa hivi ipo Dodoma, Waheshimiwa Wabunge ambao pengine hamtaiwahi kwenye Majimbo yenu, maana mtakaa hapa mpaka mwezi wa nane, pengine hamtaiwahi Tume hii katika Wilaya zenu, basi wakati mwafaka wa kutoa maoni yenu ni huu. Tume ipo Dodoma nendeni mkatoe maoni na niwashauri wengine wote na wananchi kwa ujumla, toeni maoni yenu kwa njia zote ambazo tumezisema kwa kwenda kwenye Tume, kwa kuiandikia kwa posta, kwa kuipelekea *email,* kwa *fax*, kwa *box*, kwa *twitter,* kwa *face book* na kadhalika na kila kitu mnaweza mkapeleka maoni yenu kwa Tume hii. Nawapeni changamoto hii Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu mko hapa na ninyi najua mnapenda kwenda kuzungumza, nendeni mkazungumze pia mkajionee hali halisi ya utoaji wa maoni ambao unafanywa na Tume hii. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa lililozungumzwa hapa ambalo ndiyo dhima ya Wizara yangu kwa mwaka huu, kuondoa mrundikano wa kesi katika Mahakama zetu. Kesi ni nyingi sana na matatizo yanayofanya mrundikano huu ni makubwa. Kwa mfano, hapa sitaki kusema kitu chochote kibaya. Nasema katika kesi za ardhi, nyingi zilizopo Dar es Salaam kwa mfano ni *appeals* ambazo

zimetoka kwenye Mabaraza. Sasa hivi wanazo kesi za *appeals* 2,200 kwenye *High Court Dar es Salaam*.

Ndiyo maana basi walipoteuliwa wale Majaji kumi na Mheshimiwa Rais, tukawaomba kwanza wakae pale miezi mitatu wazishughulikie hizi kesi 2,200 wajaribu kuzimaliza kabla hawajakwenda kwenye vituo vingine kufanya kazi. Hilo litafanyika. Kwa hiyo, mrundikano wa kesi mahakamani ni mkubwa na sisi tunajaribu kutafuta kila njia za kupambana na jambo hili. Ndiyo maana katika Hotuba yangu nikasema tuna njia nyingi; moja, tunafikiria tutaajiri Mahakimu na Majaji wa muda ili waweze kushughulika katika Mahakama Kuu kwa kipindi cha angalau miezi 12, wajaribu kupunguza mrundikano wa kesi zilizopo zaidi ya 100,000 na zaidi ili tuweze kupunguza mrundikano huu na kuacha Majaji na Mahakimu ambao wako pale kwa muda wa kudumu waendelee na kesi zao za kawaida. Sasa hivi hata katika Majaji hawa kumi ambao wameteuliwa juzi, wameingia nimemwuliza mmoja jana una kesi ngapi akasema tayari ninazo 300, ameingia juzi tayari anazo 300.

Kwa hiyo, unaweza ukaona *extent* ya mrundikano ulivyo katika Mahakama zetu. Ndiyo maana tunasema tujaribu tuwaingize Majaji na Mahakimu wa mkataba waende wakajaribu kufuta mrundikano huu ili baadaye turudie kwenye *zero* halafu twende kwa utaratibu wa kawaida. Tukitumia njia zingine ambazo tunazitumia sasa, kwa mfano, hii tuliyoizungumza ya *teleconference*, *telejustice,* hili ni suala ambalo tunaweza tukapunguza sana kwa sababu ni suala watu wanakaa, huna hata haja ya kutumia *diesel* kumpeleka mtu mahakamani, mnakaa mnawasha *screen* mnazungumza mnalimaliza. Hili tunakusudia kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi

na Teknolojia katika kuhakikisha kwamba, tunalitekeleza kwa gharama nafuu zaidi ili tusije tukaingia katika hali ambayo kwa sababu teknolojia ni mpya tukaingizwa na wajanja tukagharamia zaidi kuliko tunavyopaswa kugharamia. *(Makofi)*

Tunazo *agency* nyingine pia za kupunguza msongamano wa kesi, ukishapunguza kesi unapunguza pia msongamano wa mahabusu na wafungwa. Sasa hivi tunatumia *platform* ya *DPP* na timu yake, wanapita katika magereza kadhaa na humo wanakwenda kuna kesi zile za upesi upesi za rahisi wanazimaliza huko huko watu wanatolewa. Mpaka sasa hivi nataka niwaambie wametolewa watu zaidi ya 1,030 ambao wametolewa kwa mtindo huo. Tunadhani hii nayo itapunguza mrundikano wa kesi. Maana ukishawapunguza kule mahabusu na kesi nazo zinapungua. Kwa hiyo, hili nalo tumesema mwaka huu tutaweka *efforts* zetu, tutaweka nguvu zetu zote katika kupunguza mrundikano wa kesi hasa katika mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la jumla ni suala la Mabaraza ya Ardhi, limeandikwa na wengi sana na baadaye nitawataja. Nilitaka kulizungumzia kwa ujumla tu kama *concept;* jana alikuwa anazungumza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na akasema wazi kabisa kwamba, Mabaraza haya bado yanafanya kazi vizuri na mimi nakubali yapo yanayofanya vizuri lakini hayajasambaa kila mahali. Pia Katiba ya Nchi hii inasema masuala yote ya utoaji wa haki yatafanywa na Mahakama.

Kwa hiyo, tunadhani bado tutaongea na wenzetu wa ardhi, bado katika Serikali tutaongea ndani tuone kama unawezekano na hasa tukishashauriwa na Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo sasa hivi wanafanya utafiti kuhusu jambo hili, wakishatushauri vizuri tutaona kuna uwezekano gani wa kuweza kurudisha maamuzi haya yote yaanzie kwenye Mahakama zetu za mwanzo halafu yaende mpaka juu. Kuliko hivi sasa Mahakama haina usemi na Mwenyekiti wa Mabaraza yale hata wanapomwambia lete *proceedings* zako ana hiari tu, Mwenyekiti yule akitoa maamuzi leo asubuhi yanaweza yakatekelezwa jioni. Hayampi mtu mwingine nafasi ya kukata rufaa tofauti na maamuzi ya Mahakama ambayo unapewa muda wa kutosha kukata rufaa.

Pale linaweza likatolewa asubuhi jioni limetekelezwa. Tunataka kutenda haki, kwa hiyo, lazima tuwape nafasi. Tunazungumza ndani ya Serikali ili tuone ni utaratibu gani mzuri tutautumia katika kutatua migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uteuzi wa Majaji limezungumzwa sana na Kambi Rasmi ya Upinzani na mimi nimesikitishwa na jinsi lilivyosemwa. Pengine kulikuwa na hoja lakini jinsi hoja ile ilivyosemwa, nimesikitika sana. Niseme Ibara ya 112 ya Katiba yetu ipo wazi kabisa, inaunda Tume ya Mahakama ambayo ndiyo imekuwa inamshauri Rais wakati wote. Nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, haijatokea hata siku moja katika nchi hii, Rais akamteua Jaji wa Mahakama Kuu bila kuzingatia mapendekezo yaliyopelekwa kwake na hii Tume ya Uajiri wa Mahakama. Tume hii ni nzito ndani yake yuko Jaji Mkuu, ndani yake yuko Jaji Kiongozi, ndani yake yuko Jaji wa Mahakama ya Rufaa, ndani yake yuko

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndani yake wako watu wengine wawili walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuingia humo. Kwa sasa kwa mfano walioteuliwa ni Profesa Juma, ambaye ni Jaji, mwingine pia Jaji Rutakangwa, ambaye ni Jaji wa Mahakama ya Rufaa hawa ndiyo wamekaa wanamshauri akipata ushauri wao na Wakili Mheshimiwa Mkate, ambaye ni Jaji pia, Wakili mzito kabisa. Hawa ndiyo wanakaa wanatazama yale majina wanayapendekeza kwa Mheshimiwa Rais.

Sasa kumtuhumu Rais kwamba anateua watu wasiofaa; tuanze kuituhumu Tume, lakini Tume iliyokaa na watu kama hawa unaanzaje kuituhumu? Katika Sekta yetu ya Sheria hakuna watu wanaowazidi hawa; nani anamzidi Jaji Mkuu; na nani anamzidi *Attorney General?* Kwa kweli ukisema hawa nao wanampotosha Rais, ndiyo maana nikasema pengine ipo hoja lakini jinsi ilivyosemwa na Kambi Rasmi ya Upinzani haikupendeza na kwa kiasi fulani sikuongea nao Majaji, niliwa-*avoid* mchana huu. Nilikuwa mimi mwenyewe nasikitika nasema nakwenda kuonana na Mheshimiwa Chande pale namwambia nini! Kwa hiyo, nimewa-*avoid* sijawaona, *I hope* nitawaona jioni nitawaomba radhi huyu Mheshimiwa Tundu Lissu ni Wakili mwenzangu nitawaomba radhi kwa niaba yake Waheshimiwa Majaji hawa kwamba ninayo hakika kabisa hakukusudia kusema hayo aliyoyasema. Vinginevyo, labda Mheshimiwa Lissu anamjua Jaji angalau mmoja na anaweza akamtaja, aseme Jaji huyu ametolewa tu mitaani na Mheshimiwa Rais. Yupi? Hakuna, hawa Majaji wote walioteuliwa wamepitia mchakato huu wa Kikao kizito sana cha watu ambao ndiyo wenye sheria ya nchi hii. Nimesikitishwa na jinsi ilivyofanywa.

Niseme tu hakuna katika uteuzi wowote ambao Rais ameufanya wa Majaji ambao haukuzingatia taratibu za Kikatiba na taratibu za Kisheria. Kwa ujumla, katika Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani, lilizungumzwa pia suala la uteuzi wa *DCs* kwamba ni Wanajeshi. Nataka nimhakikishie Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, hata kama aliyeteuliwa alikuwa Mwanajeshi, akishateuliwa ana-*cease* kuwa Mwanajeshi. Ndiyo yaliyomkuta hata Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipoingia tu kwenye siasa anatoka kwenye masuala haya, hawezi kubaki kwenye Jeshi akaendelea sijui kuwa *DC* haiwezekani. Sasa *DCs* na *RCs* ni Wawakilishi rasmi wa Rais. Sasa kumtegemea Rais apeleke Wawakilishi rasmi wa kwake ambao ni *CUF* pale Nachingwea ni kitu cha ajabu sana. Haiwezekani.

Lazima atapeleka watu wake, hawa ni Wawakilisha wake yeye. *These people* ni *quasi political appointments* zao, watafanya kazi za Rais, wanamwakilisha Rais. Kule mnawaita Magavana, wale ndiyo wenyewe, wanamwakilisha yule bwana kule, sasa yeye ana nchi kubwa ya kutawala Tanzania anavigawa vipande vipande anakumegea Mheshimiwa Chikawe wewe utakuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa; sasa amteue mtu ambaye hamjui? Itakuwaje haiwezekani! Kwa hiyo, kumtegemea Rais kwamba atawateua wengine, anawateua watu wa CCM tu; sasa ulitegemea amteue nani? Amteue mtu wa chama gani kingine? Hata wewe Mheshimiwa Tundu Lissu mathalani ungepewa nafasi hiyo ungeniteua mimi? Aah thubutu! (*Makofi*)

Kwa hiyo, *DCs* na *RCs* ni Wateule wa Rais na Rais huyu anatoka kwenye chama kinachotawala na ni lazima anawagawia kipande cha kutawala watu wale, hawezi

kuwateua watu ambao siyo Wanachama wa Chama ambacho kinatawala. (*Makofi*)

La ujumla lingine lilizungumzwa kuhusu adhabu ya kifo. Nafikiri lilizungumzwa na dada yangu, Mbunge wa Nkenge kwamba, watu wanaomba afadhali wanyongwe kuliko kukaa bila kunyongwa. Kwa kweli Tanzania tume-*exercise moratorium* kwenye *death penalty* zaidi ya miaka 16, sasa hajanyongwa mtu kwa kipindi chote hiki. *Argument* hii ya kwamba, wale walioko kule jela eti wanaombwa wanyongwe, mimi nilisikia nikafanya ziara nikaenda Gereza la Tanga Maweni pale wenyewe wanasema ndiyo wapo wale *condemn,* nakumbuka siku ile nilikwenda, Jaji Musa Kipenka ambaye sasa ni Jaji wa Mahakama ya Rufaa, alikuwa ndiyo Jaji *in charge* Tanga, tulikwenda kuwaona wale mabwana maana wote walikuwa mabwana wanavaa *uniform* za *blue* tofauti na wenzao, nikazungumza nao nikawauliza huko ninakopita watu wengi sana wa *NGOs* wananiambia eti ninyi mnachukia sana hapa mnateseka sana ni afadhali mnyongwe. *Wallahi Billahi!* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Kipenka ni shaidi yangu; alipiga magoti yule Mzee tena alikuwa na miwani ninamkumbuka, akasema Mheshimiwa hawa watu wabaya hawatupendi, hawatutakii mema, sisi tunaomba mambo mawili; nenda kamwambie Mheshimiwa Rais atusamehe turudi nyumbani kwa wake zetu  na watoto. *These people want to live, they don't want to die.* Anayekwambia kwamba, wapo tayari kunyongwa ni mwongo.  Mimi nimewaona kwa macho yangu, wanataka waachiwe warudi, wanaomba radhi, wanakubali kosa, hii nimeiona Maweni, shahidi yangu

Mheshimiwa Kipenka pale, Jaji wa Mahakama wa Rufaa, tulikuwa wote.

Kwa hiyo, sisi ku-*exercise moratorium* na kutokuifuta *death penalty*, ni makusudi, *death penalty* hii Watanzania wameulizwa mara mbili na Tume ya Kurekebisha Sheria imezunguka nchi hii mara mbili katika nyakati tofauti ikiwauliza Watanzania mnasemaje; tufute adhabu hii au tuiache? Majibu *unanimous* msifute, iacheni. Sasa sisi tunaongozwa pamoja na mambo mengi, lakini tunaongozwa na matakwa ya wengi. Sisi ni Serikali sikivu, tunasikiliza maoni ya wananchi wetu. Wakisema tusifute, hatufuti, lakini sasa kutekeleza adhabu hii, Rais anatakiwa ndiyo aweke mkono wa mwisho pale baada ya kushauriwa na Kamati ile ambayo inamshauri ambayo bahati mbaya na mimi nimo na Mwanasheria Mkuu nae yumo. Tunamshauri bwana huyu, sasa hii sijui itakuwa siri, lakini ipo siku moja nilishauri nikasema Mheshimiwa huyu kwa jambo alilolifanya afadhali anyongwe, akasema uta-*sign* wewe. *(Kicheko)*

Nikajua inaweza ikawa siyo rahisi kwa sababu ni binadamu. Ukisha-*sign* ile unajua unai-*condemn* roho ya mtu yule anaondoka, anakufa, sasa wewe unaenda kulala usingizi sijui unategemea mtu na mtu lakini kwa watu waliopita kuanzia Mheshimiwa Mkapa mpaka sasa Mheshimiwa Kikwete, wamekuwa kidogo na roho ile *reluctant* ku-*sign*. Kwa hiyo, adhabu hii ipo na sisi tunadhani bado ina-*serve purpose* ya kuwafanya watu waogope kufanya matendo maovu ya kuuwa watu kwa makusudi kwa kukusudia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba mkubali kwamba adhabu hii iendelee kuwepo, lakini kunyonga itategemea sana na nafsi ya yule mwenye kuandika ile karatasi kwa wino mwekundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la Mahakama ya Kadhi. Suala hili limekuwepo katika Bunge hili kwa muda mrefu, hivi sasa linashughulikiwa vizuri sana na Ofisi ya Waziri Mkuu. Nataka niwaarifu tu kwamba, mpaka sasa kuna Kamati ambayo kuna upande wa Serikali na kuna upande wa Viongozi wa Dini ya Kiislamu, wanazungumza na makubaliano yanaelekea kwamba, tukubali kutumia Sheria ya Mwaka 1963 ambayo inamruhusu Waziri wa Katiba na Sheria kuandika Kanuni ambazo zitatambua *ruling* ya Sheikh na kuipa nguvu ya utekelezaji wa Kimahakama.

Kwa hiyo, Sheikh akitoa maamuzi yake huyo Kadhi, akitoa maamuzi yake, akipelekwa *Primary Court* kwa kutumia Kanuni zile *Primary Court, Magistrate,* atazitambua na atasema basi hukumu hii itekelezwe. Kwa sababu vinginevyo yule Kadhi kama angekuwa yupo anatoa amri, Mwislamu anaweza akaslimu siku hiyo hiyo akawa Mkristo akasema hapana hainihusu hii, akabadilisha na dini basi. Ukiipa uzito wa Kisheria na hapo ndipo tunapojaribu kwenda, kwa hiyo, ushiriki wa Serikali utakwenda mpaka ngazi hiyo na kuhakikisha angalau basi Waislamu wenyewe wanaiendesha na kuihudumia. Kwa sababu hili pia wanasema ni suala la imani na vilevile ni suala la ibada; kwa hiyo, hauwezi ukaliingilia na Serikali haiwezi kuingilia huko, ndiyo maana tukasema waifanye wenyewe, Serikali kama inavyohudumia wananchi wengine na kuyasaidia makundi mengine ya jamii, inaweza ikasaidia katika

uanzishwaji, *training* na kadhalika. Ndiyo maana nikasema nilisemee hili kwa ujumla.

Niangalie sasa mchango mmoja mmoja, nione ni zipi naweza kuzijibu. Kama nilivyosema awali, muda wangu ni mfupi sana, kujibu zote hizi sitaweza, lakini niseme tu kwamba, wote *of course* tutawaletea majibu yetu. Nianze na hili la kuendelea kuwepo kwa mrundikano wa mashauri Mahakamani. Hili limezungumziwa na wengi, nataka niwataje waliolizungumzia, nimelitolea maelezo lakini sikuwataja waliolizungumzia. Amelizungumzia Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Mhonga Ruhanywa, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Profesa Mheshimiwa Peter Msola, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, nae amelizungumzia, Mheshimiwa Amina Mwidau na Mheshimiwa Subira Mgalu, wote wamelizungumzia.

Nimelitolea maelezo, nimewaelezeni hatua ambazo tunakusudia kuchukua katika kupambana na mrundikano wa kesi katika Mahakama zetu, sitaki kurudia lakini nasema matumizi ya TEHAMA yatakuwa ni makubwa sana. Tunataka kwenda na wakati kwa sababu tunadhani matumizi ya TEHAMA katika kupunguza mrundikano huu hasa Mahakamani, itatupunguzia gharama, itaongeza ufanisi. Sasa hivi, Majaji wetu na Mahakimu wetu wote wanaandika *proceedings* kwa mkono, hatutaki waendelee kufanya hivyo, tunataka waondoke huko. Tunataka Majaji wetu watumie utaratibu kama huu wa *Hansard* ambao

sasa hivi vifaa tumevifunga pale *High Court* bado tuna *train* watu tuanze kutumia. Huu utaratibu unatu-*guarantee* vitu vingi, kwanza, zile kumbukumbu ni sahihi maana pale unapocheka panaandikwa amecheka, kupiga makofi kapiga makofi, sasa ile ni muhimu. Ukimwachia tu Hakimu anaandika anavyotaka hujui anaandika nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi ni binadamu, kesi zimetokea za Hakimu, wakati mwingine hata Jaji kuandika kitu kingine na kusema kitu kingine. Sasa hatutaki tubaki kule, tunataka tuondoke huko, tutumie TEHAMA zaidi, teknolojia ya sasa hivi ili tuweze ku-*improve service delivery* kwa wananchi maana Wizara hii shughuli yake kubwa ni *service delivery*. Tunataka kutoa huduma kwa wananchi *in the best possible way* na kwa gharama nafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la uteuzi wa Majaji nimelizungumzia lakini lilizungumziwa na Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina nae alilizungumzia na Mheshimiwa Susan Lyimo nae alizungumzia, na mimi nasema maelezo ni hayo, hakuna hata Jaji mmoja aliyeteuliwa bila kuzingatia utaratibu uliowekwa na Sheria. Kama yupo mimi nataka mtu asimame aniambie fulani, nitashukuru sana, lakini najua hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wao unafanywa kwa makini sana kwa sababu nafasi hiyo ni nzito sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ucheleweshaji wa kusikiliza na kuamua kesi unaosababishwa na kiasi kidogo cha fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mahakama. Mimi nakubali, Mahakama yetu kama Bunge letu bado

linahitaji kutengewa fedha nyingi, Mahakama hii mahitaji yake ni makubwa, majengo, bado hatuna majengo ya kutosha, tuna azma ya kujenga Mahakama Kuu kila Mkoa, lakini bado hatuna uwezo huo. Sasa lazima bajeti ya Mahakama itazamwe na mimi nataka niseme kwamba, nimefurahi sana, sasa tunae *Chief Court Administrator*, cheo ambacho ni kikubwa kidogo kuliko Katibu Mkuu wa kawaida wa Wizara. Huyu aliyeteuliwa sasa, binafsi ni mtu mmoja mchapa kazi sana na nina hakika atasimamia masuala haya kwenda kupambana na Hazina, kuendesha Miradi na kuisimamia na kuhakikisha kwamba kama Mahakama itajengwa basi inajengwa inakamilika. Kwa sababu sasa hivi tunasimamia sisi wenyewe, sisi ni Wanasheria, *we are legal professionals,* hatujui mambo ya pesa sana, hata wale Makandarasi wanaweza wakatulalia, lakini sasa tuna Mtawala, mtu anayejua nini kutawala, nini pesa, nini *manpower* na anajua mambo ya kufanya. Tuna hakika Mheshimiwa Katanga, atakuwa mtu wa manufaa sana katika kubadilisha utendaji kazi wa Mahakama zetu na masuala haya yatatusaidia sana tutakapokuwa na Mahakama za kutosha, Mahakimu wa kutosha, *well trained,* basi usikilizaji wa kesi uta-*improve* na haki itazidi kutendeka na *at the end of the day* somo letu kubwa hapa ni kutoa haki kwa watu wote na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa kuna vitendo vya rushwa katika Mahakama, mimi siweze kukataa, Mahakama zinaendeshwa na watu; na Mahakimu na watu wanaofanya Mahakamani ni watu *very powerful,* watu wana nguvu sana na sisi wananchi wa kawaida kwa kawaida tunaogopa sana kuingizwa Mahakamani.

Ukiingia Mahakamani pale mtu wa kawaida unatetemeka, jambo ambalo ulitakiwa useme siyo, unaweza ukasema ndiyo, ukajikuta unaingizwa kwenye hatia unafungwa au unatozwa faini. Kwa hiyo, kama atatokea mtu akakwambia unataka nikusaidie bwana, nikumalizie jambo lako fanya kitu fulani, mara nyingi unafanya. Sisemi Waheshimiwa Wabunge, maana ninyi ni weledi, welewa, mtakataa kufanya lakini watu wengi nawafahamu, akiambiwa kati ya kupelekwa Mahakamani au kutoa shilingi laki moja, atatoa laki moja, anaogopa kuburuzwa Mahakamani. Kwa hiyo, suala la rushwa lipo katika Mahakama zetu kwa sababu Mahakama iko katika nafasi hiyo. Tunapambana nalo sana na nataka niseme, Jaji Mkuu tuliyenae sasa, Mheshimiwa Mohamed Chande, jambo hili analichukia na anapambana nalo sana na anaongoza pale Mahakama katika kupambana na jambo hili. Mara zote watu ambao wamefahamika kufanya mambo haya, wamechukuliwa hatua za kinidhamu ama za Kisheria. (*Makofi*)

Mahakama kuwa na vifaa vya kisasa; hili limezungumzwa na Mheshimiwa Sylvester Koka, Mbunge wa Kibaha na amezungumza kuhusu Mahakama ilivyokuwa chakavu; ni kweli Mahakama zetu ni chakavu, nyingi tuliziriithi kutoka *Local Authorities* na ndiyo maana sasa hivi tunawaomba watu wa *Local Government* tufanye kazi pamoja. Kwa mfano, katika hii Mikoa minne mipya, tumeomba Serikali wanapojenga Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, wajenge na *Regional Police Commander's Office*, wajenge na Mahakama na nyumba ya Hakimu. *(Makofi)*

Tunadhani katika Mikoa hii minne mipya, mambo haya yatatekelezwa na ikifikia hatua hiyo ikishaingia katika

mfumo mzima wa Serikali itakuwa vizuri. Sasa hivi tatizo ni kwamba, Mahakama imewekwa pembeni, iliambiwa ni mhimili unaojitegemea kaeni pembeni, kwa hiyo, mara nyingi wakawa wanasahauliwa, lakini sasa tunaingiza kwenye *mainstream,* tuna Mtawala ambaye ni Mfanyakazi wa Serikali, ataweza kuyafanya mambo haya. Nimeulizwa hapa kwamba, katika kujenga hizo Mahakama, wajenge pia na Magereza, lakini hili la Magereza sitaki kulisemea, atakuja kulisemea Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi atakapowasilisha Hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kila Mkoa iwe na Mahakama nalo limesemwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe na Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki. Wote wamesema jamani kila Mkoa uwe na Mahakama Kuu; nasema na sisi ndiyo azma yetu, tunaazimia kila Mkoa upate Mahakama Kuu ili haki iweze kutendeka na wananchi wapate haki yao katika ngazi angalau ya Mkoa. Hatuwezi kusema kila Wilaya, lakini kwa Dar es Salaam pale, tumeamua tutaweka Mahakama Kuu Wilaya ya Kinondoni, Temeke na Ilala. Tutaweka Mahakama Kuu katika Wilaya hizo kwa sababu zile ni kubwa, *almost* sawa na Mikoa. Nia hasa ni kuweka Mahakama Kuu katika kila Mkoa. Kwa kuanzia tutaanza na angalau hizo za Temeke, Ilala na Kinondoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ombi hapa kutoka kwa Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki amesema, tuanzishe Mahakama ya Rufani kwa upande wa Zanzibar ambapo itarahisisha shughuli za upande wa Zanzibar na pia utaratibu wa kuwalipa posho inayoridhisha kwa waajiri wa Zanzibar kwa kazi kubwa

wanazofanya za Mahakama ya Rufaa. Mimi nasema huu ni ushauri mzuri, sisi ni nchi mmoja, ni Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama ya Rufaa ni Chombo cha Muungano, haitakuwa vibaya hata kidogo kulifikiria wazo hili na kulitekeleza, lakini nasema tumelipokea na bahati nzuri kwa utaratibu wa sasa, wenzangu wa Mahakama wapo hapa hapa, basi tutalizungumza, ikiwezekana tutalitekeleza kwa wakati unaofaa, ni jambo zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ameuliza Mahakama imetenga pesa kwa ajili ya ujenzi ya Mahakama ya Bunda? Ndiyo, Mahakama ya Bunda itajengwa, muhame sasa kutoka kwenye nyumba ya Mheshimiwa Steven Wasira ambako ndiko Mahakama ilipo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya *ICT* au TEHAMA kwenye masuala ya Utawala wa Mahakama na utoaji haki; hili limeletwa na Mheshimiwa January Makamba, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, anatuhimiza tutumie Tehama kwenye masuala ya Utawala wa Mahakama na utoaji haki. Mimi nakubaliana nae na ndiyo maana nikasema kwa kuanzia tunataka kuanza kufanya *tele-justice* na tutawashirikisha wao kama Wizara katika utaratibu huu, watatusaidia sana, najua wanao wataalamu, amezungumza maneno mengi kweli hapa ya kitaalamu, lakini yote siyajui mimi nasema tunataka kutumia TEHAMA katika utoaji haki ili kurahisisha na kuwezesha haki kupatikana kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na swali la Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu, Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi anasema, anapenda kujua kama Mahakama za Mwanzo, Ngadu, Ukimbu na

Mwamagembe zitakarabatiwa katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Jibu ni kwamba, napenda nimhakikishie Mheshimiwa kuwa, Mahakama hizo zitakarabatiwa katika Mwaka huu wa Fedha wa 2012/2013, ila Mahakama ya Wilaya ya Manyoni itakarabatiwa kadiri tutakapopata fedha hapo baadaye. *(Makofi)*

Lipo tatizo na hili nililizungumzia Kisera, lipo tatizo la upatikanaji wa nakala za hukumu kutoka kwenye Mahakama zetu kwa watu ambao wako Magerezani wanakata rufaa; mara nyingi umetokea uchelewaji wa kupata nakala hizi. Tatizo kubwa hapa, unalitazama katika namna mbili; moja, kuna utumiaji wa teknolojia. Zipo Mahakama za Mwanzo mpaka leo hii bado zinatumia kitu kinachoitwa *type writer. Type writer* ile ukipiga pale inabidi baadaye unapiga kwenye kitu kinachoitwa *stencil* mpaka halafu ndiyo unakwenda kuburuza. Sasa teknolojia hiyo imepitwa sana, ndiyo maana mtazamo wetu ni kuingiza teknolojia mpya kabisa kuanzia kule chini mpaka huko juu na inawezekana kabisa.

Kwa sababu mimi mwenyewe ni mfano mzuri, katika Wilaya yetu ya Nachingwea, simu iliyokuwepo kabla ya ujio wa simu hizi za mkononi, ilikuwa ni simu ambayo kwanza unazungusha hivi, halafu *operator* wa pale Nachingwea anakujibu *hallow, hallow, hallw* unasemaje? Unasema naomba Dar es Salaam namba kadhaa na yeye anampigia mtu wa Lindi, mtu wa Lindi anapiga Dar es Salaam, halafu wewe ni kama ka-*extension* tu pale. Tulishatoka pale sasa hivi tupo kwenye simu za viganjani. Hizi zingine hatukupitia sisi, tuliruka moja kwa moja. Kwa hiyo, nasema kama iliwezekana kule na huku inawezekana tukaondokana na *type writer*, tukaenda mpaka kwenye

*tele-justice.* Nasema hii inawezekana na hndiyo ndoto yangu mimi. *(Makofi)*

Watakaposema *Chikawe Two,* kama alivyosema Mheshimiwa pale, basi tulikuja na hili, mabadiliko ambayo yatasaidia kuboresha huduma katika Mahakama zetu na katika sekta nzima ya utoaji haki.

Mheshimiwa John John Mnyika, alitaka Serikali itoe maelezo Bungeni ni kwa nini Mfuko wa Mahakama haukupokea kiwango kilichopangwa na Bunge cha shilingi bilioni 20 badala yake umepokea shilingi bilioni 14.7, ikawa chini ya asilimia 75 lakini juu ya asilimia 74? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa masuala ya bajeti, nataka niseme, labda siyo Wizara hii tu pengine Wizara zote hizi, aliyepata nyingi sana alipata asilimia 90. Huyo ndiyo alipata, ni nadra kupata asilimia 100, ndiyo maana hii ni bajeti, makisio, tunakisia mipango na mipango Waswahili mnasema siyo matumizi. Mipango ni mipango na matumizi ni kitu kingine. Tunapanga 100 tunatumia 70, ndiyo tulizopata. Ninashukuru hapa asilimia hii chini ya 75 siyo mbaya, lakini je, tumefanyia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, asilimia hii tumepunguza kesi nyingi sana kwa kutumia pesa hizi shilingi bilioni 14. Mfuko wa Mahakama umechukua kila kitu kinachopelekwa katika Mfuko ule, wanakaa wenyewe wanapanga kwa kuangalia *Strategic Plan* zao, wapi tupeleke pesa zaidi na wapi tuache. Tumewapa fuko lile, wanakaa nalo wanapanga, sisi tunaenda kutazama tunasema, *hands off eyes on,* tunawatazama, lakini hatuwagusi kwamba fanyeni hivi, hapana. Tunasema

jamani, bajeti ya mwaka huu mnapata hizi shilingi bilioni 90, basi angalieni ninyi kulingana na *Strategic Plan* yenu na *Work Plan* zenu, mnataka kufanya vitu gani katika mwaka huu, vipangeni, tuvipate, sisi tutakuwa tunatazama kama mnavifanya basi hatutawaingilia. *After all,* huu ni Mhimili ambao haupaswi kuingiliwa vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndivyo tunavyofanya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika, mimi niseme hali hii imetokana na hii *Cash Budget* tuliyokuwa nayo. Tulichokipata ndiyo hiki na sidhani kama ipo Wizara itakayokwambia imepata asilimia 100 ya bajeti yake. Hata ile bajeti ndogo kabisa ya Wizara ya Afrika Mashariki ya shilingi bilioni tatu, sina hakika kama wamepata zote. Wanapogawa wanagawa *Pro rata* kwa asilimia, kila mtu anapata asilimia kadhaa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika, tushukuru tumepata tulichokipata, lakini kazi tuliyoifanya ni kubwa, tumepunguza sana kesi katika Mahakama zetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa limezungumzwa hapa na Mheshimiwa Profesa Kahigi, kuhusu matumizi ya Lugha ya Kiswahili. Mheshimiwa Mustapha Akunaay na yeye amezungumzia hili, lakini yeye alizungumza lile la adhabu mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niyazungumze yote kwa pamoja. Hili la kutumia Kiswahili katika Mahakama zetu siyo *impossible,* lakini inabidi twende taratibu tufikie hapo. Sasa hivi tunapowafundisha vijana wetu wanaosoma Sheria, tunatumia Lugha ya Kiingereza. Vitabu wanavyotumia ni vya Kiingereza. Sasa inawezekana wote sisi ni Waswahili na tunajua kiswahili, lakini zipo *terminologies* za Kilatini kidogo ngumu, inabidi tufanye kazi, tunaweza kufika pale na

tutafika, nina hakika kabisa ipo siku tutakapoweka *focus* yetu kwenye kubadilisha tutafika katika matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa nasema twende taratibu tusije tukavuruga, maana unaweza ukaenda kasi ukavuruga kila kitu. Hapa tuna-*deal* na haki za wananchi, haki za binadamu, ukizivuruga hizo, kwa kweli hata ile *your raisontente,* ile sababu ya wewe kuwepo hapa haipo. Wewe uko hapa kulinda haki za watu, halafu wewe ndiyo unaenda kuzivuruga; na unaweza ukazivuruga kwa kutoa uamuzi mdogo tu kwamba, kuanzia leo kila kitu kwa Kiswahili, ukakosa watu wa kufanya hiyo kazi, utakuwa umevuruga. Nasema ni ushauri mzuri sana, sisi tunaupokea, tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la adhabu mbadala la Mheshimiwa Akunaay ni wazo zuri. Nasi mwaka jana tulikuwa na dhima kwamba, tutumie zaidi adhabu mbadala na mpaka sasa bado tunaendelea tunataka hivyo. Tutumie adhabu mbadala, badala ya kupeleka watu wote gerezani, siyo vizuri, haipendezi wala haitakiwi. Kwa hiyo, tutatumia adhabu mbadala, Sheria zinaturuhusu, vifungo vya nje, watu watapewa adhabu za kwenda kufanya *community work, community service,* kwenda kufyeka majani katika Viwanja vya Bunge, wakisimamiwa, halafu wanarudi majumbani kwao. Tena nafikiri itapunguza sana matendo ya uhalifu, maana unajiona kila asubuhi na tai yako unaenda kufyeka majani, unasimamiwa na Afisa pale, unafyeka majani Viwanja vya Bunge, hutapenda kurudia hilo kosa ulilolifanya. Kwa hiyo, nafikiri adhabu mbadala tunai-*encourage* na sisi tunaikubali tunataka

tuifanye, kuliko hili la kujenga magereza zaidi na kuwafunga watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli, ninayo mengi mno ya kuzungumza hapa, lakini nimalizie machache tu. Mheshimiwa David Kafulila, alizungumzia kwamba, tatizo Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Nguruka, Wilaya ya Kigoma, kukosa uadilifu, ulevi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelichukukua, nimewakabidhi wenyewe wataenda kumkagua, maana wale Mahakakimu wanasimamiwa na wakubwa zao, kwa hiyo, wataenda kumkagua, wakiyakuta hayo, atachukuliwa hatua. Kwa vile Mheshimiwa wewe umesema, mimi ninaamini unachokisema ni kweli. Kwa hiyo, sisi tutalifuatilia hili kwa karibu sana, tumchukulie hatua. Hatuwezi kuwa na Hakimu ambaye hafuati maadili ya kazi. Hii ni kazi ambayo ina maadili ya juu sana. Huwezi kuwa na Hakimu mlevi, sasa anaingia Mahakamani anafanya nini? Anatoaje hukumu? Anasikilizaje kesi? Lazima atakuwa na kasoro. Kwa hiyo, nasema hili tunalipokea na tunalichukulia kwa nguvu zote kama ulivyolisema. Tutaona ni jinsi gani huyo bwana atachukuliwa hatua za kinidhamu inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na kama nilivyosema, nina marundo hapa ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Nataka niwahakikishieni kuwa, maoni haya yote nimeyapokea na mimi na watu wangu katika Wizara tutayafanya kazi moja tu, tutayashughulikia haya, tuone yale ambayo tunaweza kuyatekeleza kwa haraka tuyafanye, yale ambayo yanachukua *medium term*

tuyachukulie *medium term,* yale ya *long term* tutafanya hivyo.

Ninasema ninawashukuru sana kwa maoni yenu, najua wote mmeyatoa kwa nia moja tu ya kujaribu kuboresha Sekta hii ya Sheria, Sekta hii ya Utoaji Haki ili wananchi wetu waweze kupata haki yao kwa haraka ama kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kukushukuru wewe na Wenyeviti wenzio, Spika na Naibu Spika, kwa kutuongoza vizuri ndani ya Bunge hili na kuzingatia Kanuni kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni, hoja imetolewa na imekwisha kuungwa mkono. Naomba sasa nimwite Katibu kwa hatua inayofuata; Katibu.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge sasa linaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Sera na Utaratibu wa Kiti ni ule ule. Umuhimu wa Waheshimiwa Wabunge kujikita kwenye Sera ni jambo la utaratibu katika Kamati ya

Matumizi. Kwa hiyo, naomba nikumbushe suala hilo na nitaendelea nao kwa mujibu wa utaratibu na Mwongozo wa Spika.

Naomba nimwite Katibu atuongoze.

**Fungu 8 - *Constitutional Review Commission***

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* ... Sh. 27,505,471,000

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, nilihoji juu ya posho…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, Kifungu gani?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Fungu la 210300, vilevile 220700.

**MWENYEKITI:** Ni moja tu Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa mujibu wa utaratibu tuliobadilisha Kanuni wakati wa Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, nenda kwenye hoja moja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zinahusiana zote zinahusu kitu kimoja.

**MWENYEKITI:** Enhee, hebu twende.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Vifungu 210300, 220700 na 221000, vinahusu Posho za Tume ya Katiba. *Personnel Allowances, Rental Expenses* na *Travel-in-Country,* kwenye Randama ya Tume zote hizo ni posho. Tumeuliza na ninaomba nipatiwe majibu hapa,

posho zote hizo jumla ni shilingi bilioni 14.6, kati ya shilingi bilioni 34 takriban ambayo ni Bajeti ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ili Bunge hili lipitishe kitu linachokijua; gharama ya kila Mjumbe wa Tume na Mjumbe wa Sekretarieti na hawa Watumishi wengine; hizi posho bilioni ngapi hizi nataka niambiwe. Nilimwuliza Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati tulipokuwa Dar es Salaam naye aliahidi kutoa hizo taarifa za gharama ya kila Mjumbe wa Tume kwa Kamati nzima ya Katiba na Sheria tutakapofika Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana asubuhi nimemwuliza akaniambia atanipa. Mpaka leo, hicho alichoahidi kwamba atatupa hajatupa. Nataka tujue hizi gharama za kila kichwa kimoja Tume ya Katiba ni kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Lissu. Kwanza kabisa, naomba nikanushe kwamba, *Rental Expenses* siyo posho; *Rental Expenses* hizi ni kwa ajili ya kugharimia gharama za pango la nyumba kwa ajili ya Wajumbe na Watumshi wengine na jumla yake ni watu 57 ambao wanatoka nje ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ametaka kujua ni kwa nini hatujampatia nyaraka mbalimbali. Pia ametaka kujua kiwango cha posho wanachokipata Watumishi wengine wa Sekretarieti ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri, ameelezea katika majumuisho yake, kiwango cha malipo ya posho ni siri ya mwajiri na mwajiriwa. Ahsante.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub Vote 1001,* Kifungu 210300. Ninataka kufahamu, Tume hii ya Katiba, imeanza kufanya kazi na inazunguka, wanalipana posho na vitu vingine. Fedha, tunazipitisha leo; hizo fedha walizoanza kuzunguka zilipitishwa lini; kwa sababu Fungu hili ni jipya na wanaendelea kuzunguka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nijue walikuwa wanalipwa kupitia Fungu gain kwa sababu kwenye Bajeti ya Mwaka jana hizi fedha hazikuwepo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, siyo suala la Sera, nitalijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilipitishwa na Bunge lako Tukufu katika Bajeti ya Mwaka jana chini ya Wizara ya Fedha, zikawa *ring fenced* kwa ajili ya shughuli hii kwa sababu tulijua itatokea.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (1), naomba kuchukua na kutumia Madaraka ya Kiti, kuliongezea Bunge nusu saa zaidi ili Waheshimiwa Wabunge, waweze kuendelea na hoja iliyoko mbele yetu na kutufikisha mahali ambapo tunaweza kufanya maamuzi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni, sitawahoji na hivyo kwa mujibu wa Kanuni hiyo, tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

Kif. 1002 - *Finance and Account Unit* ..... ..... Sh. 108,732,000
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit* .... .... ...... ..... .... Sh. 90,488,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ....... Sh. 170,244,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Information Communication and Technology* .... .... .... .... ......... ...... ....... .... Sh. 714,000,000
Kif. 1006 - *Communications and Outreach* ..... Sh. 2,611,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 - *Review Coordination Unit* .... ..... Sh. 2,744,653,000

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu 1007, Kasma 221200 - *Communications & Information.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma hii ndiyo ambayo inahusu Programu ya Utoaji wa Elimu kwa Umma. Kwa misingi ya fikra za mwanzoni za Sheria, Programu ya Elimu, ilikuwa kwenye awamu tatu lakini katika hatua ya sasa awamu ya kwanza ni kabla ya kukusanya maoni, awamu ya pili ni wakati wa kukusanya maoni. Kwa kuwa Tume ilichelewa kuanza kazi, ilianza kazi tarehe 1 mwezi Mei na sasa ipo katika kukusanya maoni; ningependa uhakika kutoka kwa Serikali, iwapo kifungu hiki ambacho kimetengewa shilingi bilioni mbili *plus,* pamoja na kwamba, zoezi la kukusanya maoni linaendelea; je, Tume itatoa vilevile maoni kwenye maeneo ambayo haijakwenda bado kabla ya kwenda kutoa maoni badala ya utaratibu wa sasa wa elimu kutolewa wakati huo huo maoni yanakusanywa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii tulitaka iwe huru na ni Tume Huru; imekaa imejipangia mkakati wake, imejipangia jinsi gani itatenda kazi. Nasema kama ni wazo anataka tulipeleke, tutalipeleka, lakini wao walivyojipangia ndiyo hivyo wanavyofanya. Wazo ni zuri, tutalipeleka kwao walitizame, waone kama pengine ni busara watangulie kwanza kwenda kutoa elimu, halafu baadaye wakatoe maoni au wanadhani pengine wakifanya hivyo, wananchi watakuwa wamesahau, siku wanafika wanakuta wameshasahau kitu walichofundishwa juzi. Yote hayo nafikiri tukiwapelekea Tume, wataangalia jinsi gani ya kufanya. Hii ni Tume Huru, tuiache iwe huru.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

**Fungu 12 - *Judiciary Service Commission***

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* …Sh. 1,337,451,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … …. …. …… Sh. 46,990,600
Kif. 1003 - *Procurement Management Unit* ... ... Sh. 9,405,000
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* …. …. ….. ….. ….. Sh. 38,607,600
Kif. 1005 - *Recruitment, Appointment &*
... ...... ...... ..... ..... ..... .... *Confirmation* Sh. 370,004,000
Kif. 1006 - *Ethics and Discipline Section* … …. ….. ….Sh. 129,694,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*.. ... Sh.2,329,207,800

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo 220900 - *Training Foreign.* Kifungu hiki hakijatengewa fedha na naamini kabisa Ofisi ya Mwanasheria inastahili pia kupeleka Wanasheria waka nje ya nchi ili waweze kujifunza kupata *exposure* kutoka kwa Wanasheria wengine. Je, ni kwa nini kifungu hiki hakijapatiwa fedha?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu ya ukomo wa bajeti.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ningependa kupata maelezo kwenye *Sub Vote 1001,* Kasma ya 221000 – *Travel-in-Country*; naona ime-*shoot* sana mwaka huu. Napenda napate maelezo ni kwa sababu gani?

**MWANASHERIA MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mlivyosikia ni kwamba, tuna nia ya kuongezea wananchi wetu weledi kwenye masuala ya mikataba.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* … … … … … Sh.572,030,300

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Planning Division*… … … … … … … .... Sh.664,738,600

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma 221000 – *Travel-in-Country*. Mwaka wa Fedha wa 2011/2013 ilikuwa takriban shilingi 99,360,000, lakini mwaka huu ime-*double* ikafika shilingi 180,300,000. Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ni kwa ajili ya kugharamia safari za kikazi za ndani kwa ajili watumishi wetu; na kwa kuwa tutafungua ofisi nyingine mpya mikoani, tunatarajia kufanya ziara za mara kwa mara na tutakuwa tunaenda mahakamani katika mikoa mingine, ndiyo maana safari zitaongezeka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*… … …… … …… .... Sh.453,306,500

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 – *Government Communication Unit*… … .. Sh.241,627,900

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub Vote 1005,* kifungu 230400 kinazungumzia *Routine Maintenance and Repair of Vehicles and Transportation Equipment*. Katika *Vote* hii inaonesha sifuri; je, Idara hii ina magari? Je, matengenezo ya magari watategemea nini kwa sababu haijatengewa fedha yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama hizi zitagharamiwa katoka kwenye kifungu cha Idara ya Utawala.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 – *Legal Registry Unit*... ... ... ...... ... ...... Sh.283,210,400

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma 220900 - *Training Foreign.* Napenda kujua kwa nini imekuwa *amount* ndogo ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza ni kutokana na ukomo wa bajeti, kwa hiyo, unafanya mipango kutokana na kiwango cha fedha ulichonacho.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nilikuwa nataka kupata maelezo kwenye kifungu hicho hicho Kasma 229900 - *Other Operating Expenses,* ime-*shoot* sana kutoka milioni nne mpaka milioni 31 na tumeona fungu hili lina matumizi mengine mbalimbali sasa tungepata maelezo ya ziada.

**MWENYEKITI:** 229900.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, kuna wakati Serikali imekuwa ikishtaki au kushtakiwa. Vilevile katika taratibu za kisheria kuna kitu wanaita *attestation* na wewe kama

Mwanasheria Mkuu wa Serikali huwezi ukajifanyia *attestation* wewe mwenyewe. Kwa hiyo, gharama hizi ni kwa ajili ya kugharamia huduma za kisheria ambazo tunazipata katika Ofisi za Mawakili wengine wa Kujitegemea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 – *Procuremnent Management Unit*… …… Sh.353,309,300
Kif. 1008 – *Research and Library Service Unit*… …… … Sh.270,192,500
Kif. 1009 – *Management Information System Unit* … … … …. ... .... .... .... .... .... ..... ...... Sh.457,958,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 – *Legislative Drafting*… … … … … … … Sh.1,309,336,700

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Sub Vote 2003, Item 210100 - Basic Salaries - Pensionable Posts.* Tunaona imeongezeka kwa kiasi kikubwa sana ukilinganisha na sehemu nyingine ambapo ilikuwa shilingi milioni 271.8 hadi kufikia 371.8. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba maelezo hapo kwamba, imeongezeka kwa kasi zaidi uki-*compare* na sehemu nyingine.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Fedha hizi zimeongezeka kwa sababu Idara hii ya Mwandishi Mkuu wa Sheria inatarajia kuajiri watumishi wengine wapya. Kwa hiyo ni wazi kabisa ni lazima kifungu hiki kitaongezeka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 – *Civil Litigation and Arbitration Division* …… … ... .... .... .... .... .... ..... ..... Sh.1,239,248,400

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo ya kutosha kwenye Kasma 220900 - *Training Foreign*. Kitengo hiki kimetengewa fedha nyingi sana, lakini ukiangalia *training domestic* kimetengewa fedha wakati kama wangeweza kupata *training* hapa nchini petu ingeweza kujumuisha watu wengi sana kuliko kupeleka *training* nje ya nchi na hiki kifungu kimetengewa fedha nyingi sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni kwa sababu ya *ticket* na posho za watu wanaokwenda kusoma na tunapeleka hawa watu sehemu nyingine duniani.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwa nataka ufufunuzi kuhusiana na Kasma 221100 - *Travel Out of Country*, ambayo imepungua kutoka shilingi milioni 197 mwaka uliopita mpaka shilingi milioni 80 hivi sasa na hii ni Idara ya *Civil Litigation and Arbitration Division* na kumekuwepo na *complains* kidogo kwamba sehemu ya kesi za Serikali na Taasisi zake zilizoko nje ya nchi,

zinaendeshwa na makampuni binafsi; kesi kubwa kubwa za muda mrefu kama za *IPTL* na *DOWANS* na nyinginezo. Sasa ningependa kupata ufafanuzi tu, ku-*drop* kwa kiwango cha pesa kwenye fungu la safari za kesi za nje, ongezeko la *Private Sector,* makampuni ambayo yanafanya hii kazi.

Je, kifungu cha safari hakitaathirika kwa sababu ya kupungua kwa kiwango cha pesa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilieleza awali, unapanga kutokana na hela uliyonayo, kwa hiyo, hata safari pia kiwango kitakuwa kutokana na uwezo wa kifedha tutakaokuwa nao, lakini kitagharamia tiketi na hati za kusafiria, yaani *visa.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 – *Treaties and Contracts Division*… …… … Sh.1,299,881,300

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – *Constitutional Affairs and Human Right* … …… … ... ... .... ... .... .... .... ..... Sh.1,064,112,900

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma ya 221200 - *Communications and Information*, imeongezeka zaidi ya mara tatu, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atupe maelezo kidogo.

**MWENYEKITI:** Sema ni *amount* gani hiyo iliyokuwa zaidi ya mara tatu.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Ni *Sub Vote 4001*, Kasma 221200 - *Communications and Information;* Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 ilikuwa 960,000, lakini sasa hivi tunaona ipo zaidi ya mara tatu na imefikia shilingi 3,600,000. Naomba maelezo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni gharama za simu za ofisini.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 – Kurugenzi ya Mashtaka**

Kif. 2002 – *Public Prosecutions Division*…………….. Sh.2,424,047,800
Kif. 2004 – *Zonal Office Arusha*……… ……… ……… Sh.794,021,500
Kif. 2005 – *Zonal Office Dodoma*……… ……… ……... Sh.434,393,900
Kif. 2006 – *Zonal Office Dar es Salaam*………………. Sh.1,319,091,300
Kif. 2007 – *Zonal Office Iringa*…… …… ……… ………. Sh.269,990,600
Kif. 2008 – *Zonal Office Moshi*……………………………. Sh.391,070,200
Kif. 2009 – *Zonal Office Kagera*… …… …… …… ….. Sh.332,332,400
Kif. 2010 – *Zonal Office Mbeya*… …………………..... Sh.439,335,800

Kif. 2011 – *Zonal Office Mtwara*………………………. Sh.308,783,800
Kif. 2012 – *Zonal Office Mwanza* ....…………………. Sh.682,494,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sauti zenu sizisikii.

Kif. 2013 – *Zonal Office Ruvuma*…………………………. Sh.278,504,400
Kif. 2014 – *Zonal Office Sumbawanga*………………….. Sh.211,373,800
Kif. 2015 – *Zonal Office Tabora*………………………….... Sh.541,218,800
Kif. 2016 – *Zonal Office Tanga*…………………………… Sh.469,767,600
Kif. 2017 – *Zonal Office Shinyanga*…………………….. Sh.310,279,900
Kif. 2018 – *Zonal Office Singida*………………………… Sh.170,975,200
Kif. 2019 – *Zonal Office Lindi*…………………….....……... Sh.136,845,400
Kif. 2020 – *Zonal Office Mara*……………...…………….. Sh.241,953,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*……… …….. Sh.0
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*………… ……………. Sh.0
Kif. 2002 – *Court of Appeal Dar es Salaam*……….. Sh.85,415,911,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mnasema?

**MBUNGE FULANI:** Amepotea.

**MWENYEKITI:** Tuko Fungu Namba 40 – Mahakama. Tulikuwa ukurasa 226, sasa tupo ukurasa 227. Katibu hebu anza tena ukurasa 226.

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*…… ……… .. Sh.0
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*……… ……….. … …. Sh.0
Kif. 2002 – *Court of Appeal Dar es Salaam*……….. Sh.85,415,911,000

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nipo kwenye kifungu 220700 - *Rental Expenses*. Naomba niulize lingine ambalo haliko kwenye vifungu sasa la 220700, linalohusu *Rental Expenses*. Nataka kujua leo tumesikia jinsi ambavyo mahakama inadaiwa, Majaji wanakaa kwenye nyumba za kupanga ambazo

hazijalipiwa na hili fungu la *rental expenses* kwa mwaka huu ni sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile …

**MWENYEKITI:** Ni swali moja tu Mheshimiwa Tundu Lissu, naomba uheshimu Mwongozo wa Kiti. Unakata kujua kwa nini fungu hilo halijatengewa fedha, kwa hiyo, ukirudi kwenye hoja nyingine hutendi haki kwangu kama Kiti wala Kanuni zangu wala kwa taratibu za Bunge. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Mwaka huu wa Fedha, Mfuko wa Mahakama ndiyo umeanza rasmi; kwa hiyo, pesa zote zipo hapa kwenye bilioni 85.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hatukusikii.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Mwaka huu wa Fedha, Mfuko wa Mahakama ndiyo unaanza rasmi na pesa zote zipo hapa kwenye Mfuko, shilingi bilioni 85 ambazo zitapangiwa matumizi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*…..Sh. 8,550,002,700
Kif. 1002 - *Finance and Accounts*……………… ……..Sh. 129,665,600

Kif. 1003 - *Policy and Information Services*…………Sh. 440,847,400
Kif. 1004 - *Internal Audit* ……………………….. ……….Sh. 63,103,300
Kif. 1005 - *Government Communication Unit*………..Sh.44,569,500
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit* …………Sh.75,947,000
Kif. 1007 - *Management Information Unit*………… Sh. 92,557,200
Kif. 2004 - *Public Legal Service Unit*. …… …. ... .... Sh. 127,742,000
Kif. 2005 - *Legal Reform Unit* …… … ……… …. ... .... ..... ..... Sh. 0
Kif. 4001 - *Constitutional Affairs*…… ……… … …. Sh. 20,136,300

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumalize haya mafungu madogo kabisa tukija kwenye Mshahara wa Waziri iwe kazi rahisi zaidi. Tunaenda Fungu 55.

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*........ Sh.1,465,815,740

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*…………………….. Sh.150,822,400

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu Kidogo Namba 221000 – *Travel-In-Country.* Kifungu hiki kimepewa *zero*, Tume hii ya Haki za Binadamu moja ya tatizo kubwa ambalo wanapata wanashindwa kusafiri na kuwafuata wananchi maeneo walipo kwa ajili ya kuwasaidia katika matatizo yanayotokea. Hapa kumewekewa *zero,* ningependa kupata maelezo ni kwa nini hawajatengewa hata shilingi kwa ajili ya kusafiri na wapo Dar es Salaam hawana *branches* nyingi nyingine, lakini pia hakuna vyombo vya kusafiria na pia hawajatengewa hela yoyote kwa ajili ya kusafiri? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali, ukomo wa bajeti ulikuwa mdogo sana kwenye Tume hii, lakini baada ya punguzo ambalo tulilifanya kupitia ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Tume hii ilifanikiwa kupata nyongeza ya shilingi bilioni 1.4. Kwa kuwa mitambo ya Hazina ilikuwa imeshafungw, ndiyo maana tulishindwa kukitengea fedha. Mara mitambo itakapofunguliwa, basi kitapata fedha zake, kwa sababu sasa hivi wana nyongeza ya *1.4 billion.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*………………………… Sh. 110,355,200

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Legal Services*……… …… ……… ………Sh. 245,723,400

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma 220700. Naomba kufahamu kwa nini hawakutenga *rental expenses* kwa mwaka huu wa fedha?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Leticia, *Sub Vote 1004, Item 220700* hapa ni *rental expenses,* siyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia tunaomba urudie.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *Sub Vote 1004,* Kasma 220700 inasema, *rental expenses,* lakini kwa mwaka huu wa fedha hakuna kiasi chochote kilichotengwa chini ya *legal services*. Naomba kuelewa kwa nini hazikutengwa fedha?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinapata fedha baada ya Tume hii kuongezewa fedha ambazo tulikuwa tumezitoa kwenye Tume ya Katiba na kuongeza *about 1.45 million* na wao wataweza kuzitia sasa hapa na ku-*mention.* Hii itaweza ku-*meet* hizo *rental expenses.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 – *Procurement Unit*…………………………...Sh. 1,407,114,400

Kif. 1006 – *Management, Information System Unit*….Sh. 186,115,200
Kif. 2001 – *Administrative Justice* ……………………….Sh. 705,128,400
Kif. 2002 – *Human Rights* ………………………………. .Sh. 431,390,760
Kif. 2003 – *Research and Documentation* … … …..Sh. 159,476,800
Kif. 2004 – *Public Education and Training*…… …… ...Sh. 181,397,000
Kif. 3001 – *Zanzibar Office* ……….. …… … ….. Sh. 199,156,700

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 - *Administration and HR. Management*… Sh. 3,409,248,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji, nimebakiwa na dakika kumi kufika saa 2.15, muda nilioongeza wa nusu saa umeshakwisha na kwa mujibu wa kanuni sasa tunaingia katika kupitisha mafungo yote kwa ujumla wake.

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kif. 1003 - *Planning Division* ... ... ... .... ..... ... ... ... ... .... .... Sh.0
Kif. 3001 - *Civil Litigation & Arbitration Division*… .... ..... ...... .. Sh. 0
Kif. 3002 - *Treaties and Contracts Division* … … … .Sh. 700,000,000

*(Vifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 - Kurugenzi ya Mashtaka**

Kif. 2002 - *Public Prosecution Division*……………..Sh.2,989,224,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*…Sh. 17,213,116,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001 - *Administration and HR. Management*……Sh. 624,000,000
Kif. 1003 - *Policy and Information Services*…………Sh. 2,817,727,000
Kif. 2005 - *Legal Reform Unit*…… ……… ……… … … .... .... . .Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* … … … .. Sh. 0
Kif. 1004 - *Legal Services*……… ……….. ……….. …… ….. Sh. 0
Kif. 1006 - *Management Information Unit*… …… …… … … Sh. 0
Kif. 2001 - *Administrative Justice*…… …… … …… …… …… Sh. 0
Kif. 2002 - *Human Rights* …… ……… …… …… ... Sh. 200,000,000
Kif. 2003 - *Research and Documentation* … … … … … … Sh. 0
Kif. 2004 - *Public Education and Training*… …… …… … … .....Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*……Sh. 616,350,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa naomba niwatakie kila la kheri Waheshimiwa Mawaziri, wakafanye kazi zao vyema ili kuweza kulisaidia Taifa letu na hasa katika mchakato huu mzito tunaoingia kwenye nchi yetu wa Mabadiliko ya Katiba.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nirudi kwenye mwongozo lakini nianze kwa kurejea maagizo ya Mheshimiwa Naibu Spika mchana. Labda niongezee maneno machache katika kusisitiza mwongozo huo kwa kurejea pia maombi ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, akiendelea kunukuu Hotuba iliyowekwa mbele ya Meza na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa *Order Paper,* tuliona kwamba Hati zilizotakiwa kusomwa leo miongoni mwa zote kulikuwa na Hati ambayo ilitakiwa isomwe na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu, ambaye aliiwasilisha.

Kwa mujibu wa Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuombwa mwongozo, alimwagiza Mheshimiwa Tundu Lissu, itakapofika kipindi hiki cha jioni aje na *addendum* ya kuondoa *paragraph* namba mbili iliyopo katika ukurasa wa tisa. Kwa mujibu pia wa Kanuni Namba 64(1), Mheshimiwa *AG* pia aliomba mwongozo nimwombe Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa sababu ya kukiuka Kanuni Namba 64(1)(a), vilevile aondoe maneno ambayo yapo kwenye kifungu cha 9(2), ukurasa wa 18. Pia kwangu mimi kama Kiongozi ambaye naongoza Kiti hiki, kwa kusisitiza mahusiano ya kuheshimu Mihimili tuliyonayo, inayofanya kazi katika Taifa letu, tuna Mhimili wa Bunge kama Chombo ambacho kina

hadhi na heshima kubwa; kuna Mhimili mwingine wa Mahakama na ukiangalia hoja ambayo inatakiwa iondolewe inaihusu Mahakama kwa kuteua Majaji ambao ni Watumishi wa Mahakama Kuu.

Kwa hiyo, labda kwa dakika moja, nikuombe Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa heshima na taadhima ya Bunge hili, uondoe kifungu cha paragraph ya pili kwenye ukurasa wa tisa ili Bunge hili libakie na maneno mengine ya Kambi ya Upinzani. Libaki na heshima yake kwa maana ya kuheshimu Mhimili wa Mahakama Kuu, kuheshimu uteuzi na wadhifa wa Mheshimiwa Rais katika uteuzi huo wa Majaji wetu, lakini pia kuwatendea haki Majaji wetu kwa kutokuendelea kuvunja Kanuni Namba 64(e), kujadili mwenendo wa Majaji hao ndani ya Bunge kinyume na utaratibu kama ilivyoelekezwa na kuletwa ombi hilo na Mheshimiwa *AG*.

Mheshimiwa Tundu Lissu, naomba nikupe dakika moja ya kuondoa kifungu hicho lakini kama hukiondoi nisingependa maelezo, naomba useme unakiondoa ama hukiondoi kusudi nitoe mwongozo unaofuata.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana, ninashangazwa sana na utaratibu ambao unataka kutumika hapa ambao haupo kwenye kanuni wala haupo mahali popote. Kwa mujibu wa taratibu zetu, yaani Kanuni hizi, kama kulikuwa na jambo ambalo kuna mtu hakulipenda, nimesema kitu ambacho siyo cha kweli kwa mfano alitakiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) aombe utaratibu, kuhusu utaratibu, ili nikae anielekeze kwamba nilichosema kinakwenda kinyume na Kanuni. Huo

ndiyo utaratibu wa Kanuni hizi; hilo ni jambo la kwanza na hiyo haikufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kama nilikuwa nimesema kitu kisichokuwa cha kweli, nimesema uongo, utaratibu wa Kanuni upo juu ya kusema uongo, upo kwenye kanuni ya 63. Kanuni ya 63 yote inazungumzia kutosema uongo Bungeni na kitu gani kinatakiwa kifanyike hatua kwa hatua, hiyo haijafanyika. Natakiwa nifute tu bila kujali Kanuni za Bunge hili na mimi kwenye masuala ya Kanuni, tutagombana sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Kanuni hazijafuatwa, walioomba mwongozo hawajafuata Kanuni na Kiti chako hakijafuata Kanuni, kuniambia nifute kitu bila kutoa maelezo yanayotakiwa kwa mujibu wa Kanuni ni kutaka na mimi nishikiriki kwenye kukanyaga Kanuni za Bunge hili Tukufu na kwenye hilo sitakuwa tayari.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimshukuru Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa kunipa msimamo wake, lakini naomba nimwelekeze pia kwenye Kanuni Namba 63 anayosema imekiukwa, inayomtaka mtu anayetaka kupewa maelezo ya uhakika yeye mwenyewe athibitishe maelezo haya.

Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, wakati Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria alipokuwa anajibu hoja hapa na wakati *AG* anajibu hoja vile vile alisema na kueleza wazi mbele ya Bunge hili na ninafikiri Waheshimiwa Wabunge wote inabidi tuchukue *Hansard* tuipitie; alisema wazi na Mheshimiwa Waziri ameliweka wazi na *AG* kwamba, utaratibu katika uteuzi wa

Majaji hawa ulifuatwa na baada ya kuthibitisha kwamba hiki kilichoandikwa hapa siyo sahihi, *AG* alifuata utaratibu wa Kikanuni na kukuomba Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa sababu kile ambacho kipo huku unachosema sicho na wewe ukidai una taarifa ndiyo kwa heshima na taadhima aliomba sana uondoe hiki kitu kwa sababu maneno haya uliyasema na hasa pale uliposisitiza kwamba, *vetting* haikufuatwa.

Mwanasheria Mkuu aliongeza Kanuni nyingine Namba 64(e), Mheshimiwa Tundu Lissu unaijua; inawakataza Wabunge kuzungumzia mienendo ya Rais, lakini mienendo ya Majaji. Sasa Kanuni hii wala haihitaji Mheshimiwa *AG* athibitishe namna gani kwa sababu kwenye Hotuba hii imeelezwa wazi umejadili mwenendo wa Majaji kwa kueleza yale yaliyoelezwa hapa. Ukitaka kusoma nitaisoma lakini nadhani tusiendelee kupoteza muda kwani kila mtu anayo taarifa hii na anajua kilichoandikwa.

Mheshimiwa Lissu umesema kitu kingine kizuri sana kwamba, haya yote yaliyofanyika leo hayajawekwa kwa mujibu wa Kanuni, hayajapangwa humu. Mimi natumia sasa Kanuni, ninaamuru mambo haya kufanyika kwa mujibu wa Kanuni Namba (2); Mheshimiwa Tundu Lissu, wewe ni Mwanasheria unaelewa, nina Kanuni Namba (2) inayosema hivi; wewe unasema kwamba mambo haya hayajawekwa Kikanuni na hayamo katika Kanuni.

Ngoja niendelee Mheshimiwa Tundu Lissu!

Kanuni Namba (2) inaniambia kwamba, iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti yoyote katika Kanuni hizi, Spika ataamua utaratibu wa kufuatwa katika

jambo ama shughuli hiyo kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge, pamoja na mila na desturi za uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na uamuzi huo utaingizwa katika Kitabu cha Maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye wa uendeshaji wa shughuli za Bunge.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Tundu Lissu, ukilitazama jambo hili toka asubuhi, aliposimama Mbunge wa Karagwe, yeye alichoomba hapa ni kumwomba Naibu Spika atueleze, hakusema kwamba umesema uongo. Yeye alitaka Naibu Spika atueleze hivi ni halali kwa Bunge hili kujadili mwenendo wa Mhimili mwingine. Hiyo ndiyo ilikuwa hoja ya msingi iliyotangulia toka asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nafikiri nisipoteze mud, inawezekana kabisa hapa tunachanganyana Kikanuni na Kimaamuzi, nadhani kwa mujibu wa Kanuni hii hii nilipeleke jambo hili kwenye Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na niiombe Kamati hiyo ninayoisema hapa ipitie mwenendo wa shughuli hii yote leo hapa Bungeni, ipitie Taarifa za *Hansard* katika Bunge hili, ipitie yaliyoandikwa na mtiririko wote wa mwongozo katika Kiti na Bunge Zima kwa ujumla wake leo na ilishauri Bunge kupitia katika Kiti hiki nini ni haki na hatima ya kufanya katika jambo hili.

Nadhani tukifanya hivyo, tunaweza kuwa tunajenga heshima ya Mhimili wetu wa Bunge katika kufanya maamuzi na kushughulikia mambo mengine yote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu na nitaomba basi nimwagize Mwenyekiti wa Kamati hiyo afanye haraka ili haya mambo tuwe tunaelekezana na kuyafikisha vizuri, tuweze kuishi kwa maana ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili kwa usalama.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa mwongozo huo, nina matangazo yafuatayo:-

Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa, kesho tarehe 14 Julai, 2012, Siku ya Jumamosi, kutakuwa na Kikao cha Kamati kupitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2012. Kikao hicho kitafanyika kuanzia saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa C.

Nina tangazo lingine, tunaendelea kukumbushwa kwamba, ile Semina ya Chuo Kikuu Huria itafanyika kesho saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa. Huyu aliyeandika saa kumi haja-*specify* kama ni saa ya Kiingereza au ya Kiswahili; tunaombwa kuhudhuria.

Ninalo tangazo lingine la michezo kesho hiyo hiyo Jumamosi, jioni kutakuwa na mchezo wa kirafiki kati ya Timu ya *Bunge Sports Club* na Timu ya *Albino United* kutoka Dar es Salaam. Kwa hiyo, wachezaji wote, Kamati ya Ufundi, wahudhurie mazoezi mepesi kesho saa 12 asubuhi na mechi itafanyika jioni kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyoletewa hapa Mezani kwangu. Baada ya kumaliza kutoa mwongozo huo na kumaliza kazi nzito ambayo

tumekuwa nayo leo, ninawashukuru sana kwa ushirikiano. Ninaomba niahirishe shughuli hizi za Bunge.

*(Saa 2.23 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 16 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*